JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU TAARIFA YA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNE, 2014

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi
Mtaa wa Samora /Ohio,
S. L .P 9080,
Simu: +255 (022) 2115157/8,
Nukushi: +255 (022) 2117527,
Barua pepe: ocag@nao.go.tz,
Tovuti: www.nao.go.tz,
**Dar es Salaam.**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Barabara ya Samora, S.L.P. 9080, Dar es Salaam.
Simu ya Upepo: 'Ukaguzi' D'Salaam, Simu: 255(022)2115157/8, Tarakishi: 255(022)2117527, Barua pepe: ocag@nao.go.tz,
tovuti: www.nao.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na.FA.27/249/01/2013/2014 **Tarehe:26 Machi 2015**

Mh. Dkt. Jakaya M. Kikwete,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
S.L.P. 9120,
Ikulu,
**1 Barabara ya Baraka Obama,**
**11400 DAR ES SALAAM.**

**Yah: Kuwasilisha Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabuza Serikali juu yaTaarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka ulioishia tarehe 30Juni, 2014**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa 2005) na Kifungu cha 34 (1)(c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

Ninayo heshima kubwa kuwasilisha ripoti kuu ya ukaguzi ya mwaka inayohusu taarifa za fedha za serikali kuu za mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2014 kwa taarifa na hatua zako muhimu.

Katika ripoti hiyo, nimetoa mapendekezo yenye lengo la kujenga ambayo kama yatatekelezwa yanaweza kupunguza matukio ya ukiukwaji wa taratibu na kwa kiasi kikubwa kuboresha uwajibikaji wa watendaji wa Serikali katika masuala ya fedha.

Nawasilisha.

Prof. Mussa Juma Assad
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**Mdhibiti Na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,**
**Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

***Ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano***

Madaraka na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameelezwa kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa 2005) na kufafanuliwa zaidi katika Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

**Dira**
Kuwa kituo cha ufanisi katika Ukaguzi wa Hesabu za Serikali na Taasisi za Umma.

**Dhima**
Kutoa huduma ya ukaguzi wa hesabu yenye tija ili kuimarisha uwajibikaji nathamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

**Katika kutoa huduma zenye ubora, ofisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:**

**Uadilifu:** sisi ni asasi adilifu inayotoa huduma kwa namna isiyo na upendeleo.

**Ubora:** sisi ni wanataaluma wanaotoa huduma zenye ubora kwa kuzingatiaviwango kubalifu vya Ukaguzi

**Uaminifu:** tunahakikisha kuwa na kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatiautawala wa sheria.

**Mtazamo wa watu:** tunatazama na kukazia zaidi katika matarajio ya wadauwetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia mteja na kuwa nawatumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.

**Uvumbuzi:** sisi ni asasi ambayo wakati wote inahamasisha utamaduni wakupokea na kuendeleza mawazo mapya kutoka ndani na nje ya asasi.

**Matumizi bora ya rasilimali**: sisi ni asasi inayothamini na kutumia rasilimali zaumma ilizokabidhiwa kwa umakini mkubwa.

**Tunaifikia adhma yetu kwa kufanya yafuatayo:**
- Kuchangia usimamizi bora wa fedha za umma kwa kuhakikisha kwamba wateja wetu wanawajibika kwa rasilimali walizokabidhiwa;
- Kusaidia kuboresha ubora wa huduma za jamii na kusaidia ubunifu katika kufanya matumizi bora ya rasilimali za umma;
- Kutoa ushauri wa kiufundi kwa wateja wetu juu ya mapungufu yaliyoko katika mifumo ya uendeshaji wa shughuli zao
- Kufanya ukaguzi shirikishi baina yetu na wateja wetu katika mchakato mzima wa ukaguzi; na
- Kuwapatia mafunzo sahihi wakaguzi wetu, vitendea kazi vya kutosha na motisha ili kuhakikisha uhuru wakati wakitekeleza majukumu yao.

## YALIYOMO

Mdhibiti Na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ................................iv

Dira na Dhima ............................................................................ v

VIFUPISHO ...............................................................................xi

DIBAJI .................................................................................. xxvii

SHUKRANI...............................................................................xxx

MUHTASARI ...........................................................................xxxi

SURA YA KWANZA........................................................................ 1

UTANGULIZI NA MAMBO YA JUMLA ................................................. 1

1.0 Utangulizi ............................................................................. 1

1.1 Mamlaka na Umuhimu wa ukaguzi............................................... 1

1.2 Viwango na taratibu zilizotumika kutoa taarifa ............................. 4

1.3 Idadi ya wakaguliwa ................................................................. 5

1.4 Majukumu ya kisheria ya Asasi zinzokaguliwa ............................... 8

1.5 Taarifa za Fedha ...................................................................... 9

SURA YA PILI ...........................................................................10

HATI ZA UKAGUZI.......................................................................10

2.0 Utangulizi ............................................................................10

2.1 Maana ya hati ya ukaguzi .........................................................10

2.2 Aina za hati za ukaguzi ............................................................10

2.3 Aya yenye masuala ya msisitizo na aya yenye masuala mengine .........12

2.4 Mchanganuo wa hati za ukaguzi kwa Serikali Kuu kwa

mwaka 2013-14 ........................................................ 13

2.6 Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa miaka mitano iliyopita (2009/10 - 2013/14) ........................................................ 16

SURA YA TATU ........................................................ 20

UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA ........................................................ 20

3.0 Utangulizi ........................................................ 20

3.1 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi

yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kila fungu ........................................................ 20

3.2 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa ripoti jumuifu .................. 21

3.3 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ..................... 22

SURA YA NNE ........................................................ 24

MAKUSANYO YA MADUHULI NA MCHANGANUO WA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO ........................................................ 24

4.0 Utangulizi ........................................................ 24

4.1 Ukusanyaji wa maduhuli na mchanganuo wa matumizi .................... 24

4.3 Masuala Kuhusu Mpango Wa Kubakiza Makusanyo .......................... 36

SURA YA TANO ........................................................ 38

HESABU ZA TAIFA ........................................................ 38

5.0 TAARIFA YA HESABU ZA MAJUMUISHO ........................................ 38

5.1 Ukaguzi wa Taarifa za Hesabu za Majumuisho .............................. 38
5.2 Ukaguzi Mamlaka ya Mapato Tanzania .......................................... 43
5.3 Ofisi ya Msajili wa Hazina ............................................................. 57
5.4 Ukaguzi wa Deni la Taifa ............................................................... 64
5.5 Ukaguzi wa Awali wa Malipo ya Mafao ya Wastaafu ........................ 73
SURA YA SITA ....................................................................................... 79
MFUMO WA UTHIBITI WA NDANI ............................................................ 79
6.0 Utangulizi ....................................................................................... 79
6.1 Mambo muhimu yatokanayo na tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani. ..... 79
SURA YA SABA ....................................................................................... 89
USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA ................................ 89
7.0 Utangulizi ....................................................................................... 89
7.1 Usimamizi wa rasilimali watu ......................................................... 89
7.2 Usimamizi wa mishahara ................................................................ 89
SURA YA NANE ...................................................................................... 99
WAKALA WA SERIKALI NA TAASISI NYINGINE ........................................ 99
8.0 Utangulizi ....................................................................................... 99
8.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Wakala za Serikali ..................................... 99
8.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Mifuko Maalum ya Serikali ....................... 115
8.3.Matokeo ya Ukaguzi wa Taasisi nyingine za Serikali ....................... 116
8.4 Ukaguzi wa Vyama Vya Siasa .......................................................... 119

SURA YA TISA........ 121

USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA ........ 121

9.0 UTANGULIZI........ 121

9.1 Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.7 ya 2011 na Kanunizake za Mwaka 2013........ 121

9.2 Mapungufu yaliobainika katika ukaguzi wa Manunuzi........ 121

**SURA YA KUMI**........ 139

USIMAMIZIWAMATUMIZI........ 139

10.0 UTANGULIZI ........ 139

10.1 Mapungufu katika Usimamizi wa matumizi ........ 139

SURA YA KUMI NA MOJA ........ 153

USIMAMIZI MALI NA MADENI ........ 153

11.0Utangulizi ........ 153

11.1 Ukaguzi wa Usimamizi wa Mali........ 153

11.2 Ukaguzi wa madeni kwa mwaka 2013/2014 ........ 167

SURA YA KUMI NA MBILI........ 171

12.0 UKAGUZI MAALUM........ 171

12.1Utangulizi ........ 171

SURA YA KUMI NA TATU ........ 187

HITIMISHO NA MJUMUISHO WA MAPENDEKEZO ........ 187

13.0 UTANGULIZI........ 187

## Orodha ya Majedwali


Jedwali 1: *Matokeo ya hati za Ukaguzi kwa Miaka Mitano*......................................xxxiii
Jedwali 2: *Mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kisheria*......................................................................1
Jedwali 3: *Idadi ya Wakugliwa*......................................................................6
Jedwali 4: *A*ina za hati za ukaguzi......................................................................11
Jedwali 5: Aya yenye masuala ya msisitizo na aya yenye masuala mengine......................................................................12
Jedwali 6: *Mchanganuo wa hati za ukaguzi-2013/14*......................................................................13
Jedwali 7: *Muhtasari wa mwenendo wa bajeti kwa miaka mitatu* ......................................................................26
Jedwali 8: Inaonyesha uchambuzi wa bajeti ......................................................................28
Jedwali 9: Uwiano wa fedha zilizoidhinishwa kwa matumizi ya kawaida dhidi Makisio......................................................................29
Jedwali 10: *Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida na matumizi halisi*......................................................................30
Jedwali 11: *Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya maendeleo dhidi Makisio.* ......................................................................31
Jedwali 12: *Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya maendeleo dhidi Matumizi halisi.*......................................................................32
Jedwali 13: *Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya maendeleo dhidi Matumizi halisi.*......................................................................34
Jedwali 14: *Muhtasari wa Mpango wa* kubakiza makusanyo ......................................................................37
Jedwali 15: Jumla ya makusanyo kwa mwaka 2013/14......................................................................44
Jedwali 16: Ufanisi wa ujumla katika makusanyo ya mapato Tanzania ......................................................................46
Jedwali 17: Muhtasari wa kesi zilizo katika Bodi ya Rufaa za Kodi na Mahakama ya Rufaa Tanzania......................................................................48
Jedwali 18: Muhtasari wa kesi zilizo katika Bodi ya Rufaa za Kodi na Mahakama ya Rufaa Tanzania......................................................................50
Jedwali 19: Misamaha iliyotolewa kwa wanufaika wasiostahili ......................................................................53
Jedwali 20: Misamaha kutolewa mara mbili kwenye ankara moja......................................................................55
Jedwali 21: *Ukuaji wa Deni la Taifa katika Kipindi cha Miaka 5*......................................................................65
Jedwali 22: Mseto wa Deni la Ndani......................................................................67
Jedwali 23: Mseto wa Deni la Ndani......................................................................70
Jedwali 24: Idadi ya Majalada ya Wastaafu......................................................................75
Jedwali 25: *Mafao ya Wastaafu yaliyozidishwa*......................................................................75

Jedwali 26: Mafao ya Wastaafu yaliyopunjwa ....... 75
Jedwali 27: *Mapungufu katika ufanisi wa kitengo cha ukaguzi wa ndani.* ....... 79
Jedwali 28: Mapungufu katika Utendaji wa Kamati ya Ukaguzi ....... 81
Jedwali 29: Mapungufu katika kuzuia Vihatarishi ....... 83
Jedwali 30:*Udhaifu wa Uliojitokeza kwenye Mifumo ya Teknolojia ya habari* ....... 84
Jedwali 31: Mapungufu yaliobainikia katika tathimini ya udanganyifu. ....... 86
Jedwali 32: Mchanganuo wa mapungufu yaliojitokeza katika mifumo ya ndani kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ....... 86
Jedwali 33: Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi ambao hawapo kwenye utumishi wa Umma ....... 90
Jedwali 34: Watumishi 473 ambao hawajathibitishwa ....... 92
*Jedwali 35: Taasisi ambazo watumishi wake wanapata mshahara chini ya kiwango kilichopitishwa kisheria.* ....... 93
Jedwali 36: Mishahara isiyolipwa ambayo haikuingizwa katika Akaunti husika ....... 95
Jedwali 37: Watumishi waliostaafu ambao hawakuweza kurudi nyumbani ....... 96
Jedwali 38: *Orodha ya balozi zenye wastaafu* ....... 97
Jedwali 39: Muhtasari wa Mapungufu yaliyojitokeza ....... 104
Jedwali 40: Wakala Wenye Mali zisizothaminiwa ....... 106
Jedwali 41: Ardhi na Nyumba zisizo na hati miliki ....... 107
Jedwali 42: Mali zisizotumika ....... 108
Jedwali 43: Orodha ya Madeni Yasiyolipwa ....... 109
Jedwali 44: Wakala wenye Madeni Yasiyolipwa ....... 110
Jedwali 45: Madeni Yanayotegemea Maamuzi ya Matukio ....... 112
Jedwali 46: Malipo yasiyokuwa na Viambatisho ....... 113
Jedwali 47: Orodha ya Wakala walio na Masurufu yasiyorejeshwa ....... 114
Jedwali 48: Wakala wa Serikali walio na Ukosefu wa Watumishi ....... 114
Jedwali 49: Muhtasari wa Makosa yaliyojitokeza – Mifuko Maalum ....... 115
Jedwali 50: Matokeo ya Ukaguzi Katika Taasisi Nyingine ....... 117
Jedwali 51: Hapa chini ni muhtasari wa aina ya maoni ya ukaguzi niliyotoa kufuatia kaguzi za vyama vya siasa kwa kipindi mwaka ulioishia 30 Juni 2010, 2011, 2012 na 2013. ....... 120
Jedwali 52: Taasisi zilizofanya Manunuzi nje ya Mpango wa Manunuzi wa Mwaka ....... 123

Jedwali 53: Taasisi zilizofanya Manunuzi bila idhini ya Bodi ya Zabuni ....... 124
Jedwali 54: Manunuzi yasiyo kuwa na ushindani ....... 125
Jedwali 55: Mapokezi ya vifaa visivyofanyiwa ukaguzi ....... 126
Jedwali 56: Utunzaji Usioridhisha wa Kumbukumbu za Manunuzi ....... 127
Jedwali 57: Ununuzi wa bidhaa na huduma bila ya kuwepo kwa Mikataba ....... 128
Jedwali 58: Manunuzi kwa kutumia Masurufu ....... 129
Jedwali 59: Manunuzi bidhaa na huduma toka kwa wazabuni wasioidhinishwa ....... 130
Jedwali 60:Bidhaa zilizolipiwa hazikupokelewa ....... 131
Jedwali 61: Tathmini ya PPRA Uzingatiaji Sheria na Kanuni za Manunuzi ....... 133
Jedwali 62: Mapungufu yaliyojitokeza katika Wizara na Idara za Serikali zilizokaguliwa ....... 134
Jedwali 63: Taarifa ya Mhakiki Mali ....... 137
Jedwali 64: Orodha ya *Taasisi zenye hati za malipo zinazokosekana:* ....... 141
Jedwali 65: Taasisi zilizohusika na kufanya manunuzi bila kudai risiti za kielektroniki ....... 143
Jedwali 66: Taasisi zenye masurufu yasiyorejeshwa kwa muda mrefu ....... 147
Jedwali 67: Malipo zaidi ya kiasi kinachostahili ....... 149
*Jedwali 68: Ulinganisha wa matumizi yasiyo na faida kwa miaka miwili* ....... 151
Jedwali 69:*Ulinganifu wa malipo yasiyokusudiwa kwa miaka miwili:* ....... 151
Jedwali 70: Taasisi ambazo zina vyombo vya moto ambavyo zimeegeshwa bila matengenezo. ....... 153
*Jedwali 71: Taasisi ambazo hazikutenganisha ardhi na majengo.* ....... 154
Jedwali 72: Mali ambazo hazikuonyeshwa katika taarifa za fedha. ....... 156
Jedwali 73: Mali zisizoshikika ambazo hazikuonyeshwa katika taarifa za fedha ....... 156
Jedwali 74:Taasisi ambazo hazina nyaraka za umiliki wa ardhi na majengo. ....... 158

Jedwali 75: Taasisi ambazo taarifa zake za mali zinatofautiana na taarifa iliyopo katika rejista ya mali za kudumu....................................................159
Jedwali 76: Taasisi ambazo rejista ya mali za kudumu haziendani na wakati..........................................................................................................159
Jedwali 77: Taasisi ambazo rejista ya mali za kudumu haziendani na wakati ..........................................................................................160
Jedwali 78: Nyumba za serikali ambazo ziko katika hali mbaya ...............................161
Jedwali 79: Taasisi zilizonunua mali za kudumu ambazo hazitumiki..........................................................................................................163
Jedwali 80: Taasisi zenye vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye vitabu. ..........................................................................................................164
Jedwali 81: Taasisi ambazo zina mapungufu katika usimamizi wa vifaa ..........................................................................................................166
Jedwali 82: Taasisi zenye kesi zinazoendelea..............................................................168

# Vielelezo

Kielelezo 1: Mbinu za Ukaguzi ..........3
Kielelezo 2: Utaratibu Ukaguzi kwa mwaka 2013/14 ..........5
Kielelezo 3: Muundo wa Wakaguliwa ..........6
Kielelezo 4: Dondoo ya mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Serikali Kuu kwa mwaka uliomalizika 2013/14 ..........8
Kielelezo 5: Majukumu ya kisheria ya wakaguliwa ..........9
Kielelezo 6: mchanganuo wa hati zilizotolewa na aina zakekwa mwaka wa fedha-2013/14 ..........14
Kielelezo 7: Inaonesha mlinganisho (Kwa taasisi) wa Hati za ukaguzi zilizotolewa kwa mwaka wa fedha- 2013/14 ..........15
Kielelezo 8: Mwenendo wa Hati za ukaguzi zilizotolewa kwa miaka mitano iliyopita..........17
Kielelezo 9: Chati inayoonesha Mwenendo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa miaka mitano iliyopita..........18
Kielelezo 10: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa Miaka iliyopita ..........21
Kielelezo 11: Taarifa hizi pia zinaweza kuonekana kwenye chati hapa chini ..........35
Kielelezo 12: Makusanyo halisi kwa kila Idara kwa mwaka 2013/14 ..........45
Kielelezo 13: Mseto wa Deni la Taifa..........65
Kielelezo 14: Ukuaji wa Deni la Taifa katika Kipindi cha Miaka 5 ..........66
Kielelezo 15: Mseto wa Deni la Nje ..........68
Kielelezo 16: Chati ya zenye mapungufu katika ufanisi wa kitengo cha ukaguzi wa ndani ..........80
Kielelezo 17: Taasisi zenye mapungufu katika Kamati za Ukaguzi ..........82
Kielelezo 18: Mapungufu katika tathimini ya Vihatarishi katika taasisi za Serikali Kuu ..........83
Kielelezo 19: Taasisi zenye udhaifu kwenye Mifumo ya Udhibiti wa Teknolojia ya Habari ..........85
Kielelezo 20: Asilimia ya mapungufu katika mifumo ya ndani ..........87
Kielelezo 21: Mapungufu katika Mafungu,Wakala na Taasisi nyingine za Serikali ..........88
Kielelezo 22: Mchanganuo wa Mapato ya wakala kutoka Serikalini na Mapato ya Ndani ..........100

Kielelezo 23: Mchango wa Mapato kwenye wakala kutoka Serikalini na Mapato ya Ndani 2013/2014 ........ 101
Kielelezo 24: Mwenendo wa malipo yaliyo na nyaraka pungufu ........ 140
Kielelezo 25: Malipo ambayo Hati za malipo zinakosekana ........ 141
Kielelezo 26: Malipo Katika vifungu visivyostahili ........ 144
Kielelezo 27: Malipo yaliyofanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa ........ 146
Kielelezo 28: Masurufu yasiyorejeshwa kwa muda mrefu ........ 148
Kielelezo 29: Mwenendo wa malipo zaidi ya kiwango stahiki ........ 150

**Viambatisho**

Kiambatisho 1: Hati za Ukaguzi kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 zilizotolewa kwa Mafungu ya Serikali kuu (Votes)........206
Kiambatisho 2: Hata za Ukaguzi kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 zilizotolewa kwa Wakala wa Serikali(Agencies) ........209
Kiambatisho 3: Hati za Ukaguzi kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 zilizotolewa kwa Taasisi nyingine (Other Institutions) ........211
Kiambatisho 4: Hati za Ukaguzi kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 zilizotolewa kwa Ofisi za Balozi ........213
Kiambatisho 5: Hoja zilizosalia ........215
Kiambatisho 6: Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya taarifa ya jumla ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ........219
Kiambatisho 7: Utekelezaji wa mapendekezo ya kamata ya kudumu ya bunge ya hesabu za serikali........253
Kiambatisho 8: Fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa kwa Wizara, idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa dhidi ya bajeti iliyoidhinishwa ........264
Kiambatisho 9: Fedha za Maendeleo zilizotolewa kwa Wizara, idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa dhidi ya bajeti iliyoidhinishwa........272
Kiambatisho 10: Kampuni ambazo Serikali ina ubia au umiliki hisa za asilimia 50........279
Kiambatisho 11: Misamaha ya kodi kwa Taasisi mbalimbali........280
Kiambatisho 12: Miradi iliyofadhiliwa na Mikopo ya nje ........281
Kiambatisho 13: Michango isiyowasilishwa ........286
Kiambatisho 14: Orodha ya Mafungu yenye mapungufu ya mifumo ya ndani........287
Kiambatisho 15: Orodha ya Taasisi ambazo zina mapungufu ya mifumo ya ndani ........290
Kiambatisho 16: Orodha ya Wakala wa Serikali ambazo zina mapungufu ya mifumo ya ndani........291
Kiambatisho 17: Upungufu wa Idadi ya Watumishi wa Umma........292
Kiambatisho 18: Nafasi za watumishi zilizoachwa wazi zaidi ya miezi sita ........294
Kiambatisho 19: Mapungufu katika Utekelezaji wa Mikataba na Miradi ........296
Kiambatisho 20: Taarifa ya Mhakiki Mali 2013/2014........298
Kiambatisho 21: Hati za malipo zenye nyaraka pungufu ........304
Kiambatisho 22: Malipo katika vifungu vya bajeti visivyostahili........305
Kiambatisho 23: Matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa ........306

Kiambatisho 24: Matumizi yasiyokuwa na manufaa ......................................................... 307
Kiambatisho 25: Fedha kutumika kwa shughuli zisizokusudiwa ........................................ 308
Kiambatisho 26: Orodha ya madeni kwa miaka miwili 2012/2013 na 2013/2014 ........................................................................................................ 309
Kiambatisho 27: Orodha ya taasisi zilizopata hati zenye shaka pamoja na sababu za msingi za kupata hati hizo kwa mwaka 2013/14 ............................................... 312
Kiambatisho 28: Utegemezi wa Wakala katika Ruzuku ya Serikali ..................................... 316
Kiambatisho 29: Bajeti na Mapato halisi ya ndani ya Wakala ............................................ 318
Kiambatisho 30: Ruzuku ya Matumizi Mengineyo ............................................................... 321
Kiambatisho 31: Ruzuku ya Maendeleo ya Wakala ............................................................. 323

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| **AAG** | Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali |
| **AccGen** | Mhasibu Mkuu wa Serikali |
| **ADC** | Chama cha ADC |
| **ADS** | Sekta ya Utawala |
| **ADEM** | Wakala wa Maendeleo ya Elimu |
| **ACBF** | Taasisi ya Kujenga Uwezo Afrika |
| **AfDB** | Benki ya Maendeleo ya Afrika |
| **AFROSAI** | Shirika la Taasisi Kuu za Ukaguzi Kanda ya Afrika |
| **AFROSAI-E** | Shirika la Taasisi Kuu za Ukaguzi kwa nchi zinazoongea kiingereza |
| **AFP** | Chama cha Wakulima Tanzania |
| **AGR** | Ripoti Kuu Ya Mwaka Ya Mdhibiti Na Mkaguzi Mkuu Wa Hesabu Za Serikali |
| **AGITF** | Mfuko wa Pembejeo za Kilimo |
| **AMCOS** | Chama Cha Ushirika Cha Kuuza Mazao ya Kilimo |
| **ATCL** | Shirika la Ndege la Tanzania |
| **APP** | Mpango wa Manunuzi wa Mwaka |
| **APPT** | Chama cha APPT Maendeleo |
| **ASA** | Wakala wa Mbegu |
| **APRM** | Mpango wa kujitathimini wan chi za Afrika |
| **BOQ** | Mchanganuo wa gharama za Ujenzi |
| **BoT** | Bank kuu ya Tanzania |
| **CAG** | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali |
| **CCM** | Chama cha Mapinduzi |
| **CCTV** | Kamera na Runinga za Ulinzi |

| | |
|---|---|
| **CCK** | Chama cha Kijamii (CCK) |
| **CDTI** | Chuo cha Maendeleo ya jamii |
| **CEO** | Mtendaji Mkuu |
| **CHAUMA** | Chama cha Ukombozi wa Umma |
| **CHAUSTA** | Chama cha Haki na Ustawi |
| **CHADEMA** | Chama cha Demokrasia na Maendeleo |
| **CG** | Serikali Kuu |
| **CKL – Net** | Mtandao wa Habari Tanzania |
| **CRDB** | Benki ya CRDB |
| **CUF** | Chama cha Wananchi |
| **CS-DRMS** | Jumuiya ya Madola-Mfumo wa kunakili na kusimamia Madeni |
| **DAG** | Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali |
| **DART** | Mpango wa Mabasi yaendayo kasi Dar es Salaam |
| **DDCA** | Wakala wa Uchimbaji na Ujenzi wa Visima na mabwawa |
| **DDH** | Hospitali Teule za Wilaya |
| **DGAM** | Idara ya Mhakiki Mali |
| **DMO** | Afisa wa Kukusanya Madeni |
| **DP** | Chama cha Demokrasia |
| **DSA** | Uchambuzi wa ustahimilivu wa Madeni |
| **DW** | Mkurugenzi wa Wanyama Pori |
| **EFD** | Mashine ya Kutoa Risiti za Mauzo |
| **e GA** | Wakala wa Serikali Mtandao |
| **ESCB** | Mradi wa Kujenga Uwezo Katika Uzalishaji wa Nishati |
| **EPS** | Sekta ya uchumi na Uzalishaji |
| **FETA** | Wakala wa Mafunzo ya Uvuvi |
| **GBEs** | Taasisi za Kibiashara za Serikali |

| | |
|---|---|
| **GCLA** | Wakala wa maabara ya Kemia Tanzania |
| **GIZ** | Shirika la Maendeleo ya Ujerumani |
| **GN** | Tangazo la Serikali |
| **GoT** | Benki Kuu ya Tanzania |
| **GPSA** | Wakala wa Manunuzi ya Serikali |
| **GST** | Wakala wa Utafiti wa Miamba Tanzania |
| **H.E** | Mtukufu |
| **HCMIS** | Mfumo wa taarifa za rasilimali watu |
| **IACB** | Chuo cha Sanaa Bagamoyo |
| **IALSD** | Taasisi ya Uongozi ya Afrika Kwa Maendeleo Endelevu |
| **IFAC** | Shirikisho la Wahasibu la Kimataifa |
| **IFMS** | Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha |
| **IFRS** | Viwango vya Kimataifa vya utunzaji wa hesabu |
| **IJA** | Chuo cha Utawala wa Mahakama Lushoto |
| **INTOSAI** | Shirika la kimataifa la Taasisi kuu za Ukaguzi |
| **IPSAS** | Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma |
| **ISA** | Viwango vya Ukaguzi vya Kimataifa |
| **ISCF** | Mfuko wa Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika |
| **ISSAIs** | Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Taasisi za Umma |
| **IT** | Teknolojia ya Habari |
| **JNIA** | Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere |
| **JKT** | Jeshi la Kujenga Taifa |
| **LDF** | Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo |
| **LGA** | Mamlaka ya Serikali za Mitaa |
| **LGTI** | Chuo cha Serikali za Mitaa(Hombolo) |
| **LITA** | Wakala cha Mafunzo ya Mifugo |
| **LPO** | Mikataba midogo ya Manunuzi |

| | |
|---|---|
| **LRMS** | Mfumo wa kusimamia malipo ya kodi za ardhi |
| **LST** | Shule ya Sheria Tanzania |
| **MAFSC** | Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika |
| **MCS** | Mfuko wa Maendeleo ya Maji |
| **MDAs** | Wizara, Idara na Wakala |
| **MDEF** | Mfuko wa Kusaidia maendeleo ya Madini |
| **MFAIC** | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa |
| **MoF** | Wizara ya Fedha |
| **MoHSW** | Wizara ya afya na ustawi wa jamii |
| **MSD** | Bohari ya Madawa |
| **MTEF** | Mkakati wa Matumizi wa Muda wa Kati |
| **NA** | Akaunti za Taifa |
| **NAIVS** | Mpango wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo |
| **NAO** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi |
| **NAOT** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania |
| **NCCR - MAGEUZI** | Chama cha NCCR Mageuzi |
| **NDRF** | Mfuko wa Maafa wa Taifa |
| **NDS** | Mkakati wa Deni la Taifa |
| **NFRA** | Wakala wa hifadhi ya chakula ya Taifa |
| **NFA** | Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale |
| **NHIF** | Mfuko wa Bima ya Afya |
| **NHBRA** | Wakala wa Utafiti wa Shirika La Nyumba Tanzania |
| **NIDA** | Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa |
| **NLD** | Chama cha NLD |
| **NM-AIST** | Chuo cha Sayansi na Teknologia cha Nelson Mandela |
| **NSSF** | Mfuko wa Taifa wa hifadhi za jamii |

| | |
|---|---|
| **NRA** | Chama cha NRA |
| **OSHA** | Wakala wa usalama na afya makazini |
| **OPRAS** | Upimaji wa utendaji kazi wa wazi wa watumishi |
| **PA** | Mashirika ya Umma |
| **PA&S** | Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalumu |
| **PAA** | Sheria ya Ukaguzi wa Umma |
| **PAC** | Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu |
| **PAR** | Kanuni za Ukaguzi za Umma |
| **Para** | Aya |
| **MKURABITA** | Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na BiasharaTanzania |
| **PBRF** | Mfuko wa Mendeleo ya Haki za Wazalishaji wa Miti Tanzania |
| **PCCB** | Taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa |
| **PCT** | Shirikisho la Pharmacia Tanzania |
| **PE** | Taasisi inayofanya Manunuzi |
| **PFA** | Kanuni za Fedha za Umma |
| **PFMRP** | Maboresho ya Usimamizi wa fedha za Umma |
| **PFR** | Kanuni za Fedha za Umma |
| **PMIS** | Mifumo ya manunuzi ya Umma |
| **PMG** | Mlipaji Mkuu wa Serikali |
| **PMO-RALG** | Ofisi ya Waziri Mkuu-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **PMU** | Kitengo cha Usimamizi wa manunuzi |
| **PO-PSM** | Ofisi ya Raisi Utumishi |
| **PPA** | Sheria ya Manunuzi ya Umma |
| **PPE** | Mali, Mitambo na Vifaa |
| **PPF** | Mfuko wa hifadhi ya Mashirika ya Umma |
| **PPP** | Ushirikiano waSekta binafisi na Sekta za Umma |
| **PPR** | Kanuni za manunuzi ya Umma |

| | |
|---|---|
| **PPRA** | Mamlaka ya Udhibiti wa manunuzi ya Umma |
| **PSAs** | Makubaliano ya kugawana Uzalishaji |
| **PSPF** | Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma |
| **PWPF** | Mfuko wa Ifadhi ya wanyama pori |
| **PWTI** | Chuo cha Wanyama pori Pasiansi |
| **RAS** | Katibu Tawala Mkoa |
| **REA** | Wakala wa Umeme Vijijini |
| **RFB** | Bodi ya Barabara |
| **RPC** | Kamanda wa Polisi wa Mkoa |
| **RS** | Sektretariate ya Mkoa |
| **RITA** | Wakala wa uandikishaji wa vizazi na Vifo |
| **SAU** | Chama cha Sauti ya Umma |
| **SDU** | Kitengo cha Maendeleo ya Mifumo |
| **Sect.** | Kifungu |
| **SES** | Sekta ya Uhuduma |
| **Shs.** | Fedha ya Tanzania |
| **SNAO** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Sweden |
| **SOS** | Sekta ya kijamii |
| **SPD** | Mkutano wa kimataifa wa SMART Partnership |
| **SSRA** | Mamlaka ya kudhibiti Mifuko ya Jamii |
| **TAA** | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege |
| **TADEA** | Chama cha TADEA |
| **TaESA** | Wakala wa ajira Tanzania |
| **TANROADS** | Wakala wa Barabara Tanzania |
| **TASUBA** | Taasisi ya Sanaa Bagamoyo |
| **TATC** | Kituo cha Kuunda Mitambo na Magari Tanzania |

| | |
|---|---|
| **TB** | Bodi ya Zabuni |
| **TBA** | Wakala wa Majengo |
| **TCRA** | Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania |
| **TCLA** | Tanzania Chemistry Laboratory Agency |
| **TFS** | Wakala wa Huduma za Misitu |
| **TFF** | Mfuko wa kuifadhi Misitu Tanzania |
| **TEMESA** | Wakala wa Ufundi wa Mitambo,magari na umeme |
| **TGLA** | Wakala wa Mafunzo ya Kimataifa |
| **TGFA** | Wakala wa ndege za Serikali |
| **TIA** | Taasisi ya Uhasibu Tanzania |
| **TIN** | Namba ya Mlipa Kodi |
| **TIC** | Kituo cha Uwekezaji Tanzania |
| **TLP** | Chama cha TLP |
| **TMA** | Mamlaka ya Hali ya Hewa |
| **TMAA** | Wakala wa Madini Tanzania |
| **TNMC** | Chama cha Wakunga na Manesi |
| **TPA,** | Mamlaka ya Bandari |
| **TPSC** | Chuo cha Utumishi wa Umma |
| **TRA** | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| **TSSU** | Kitengo cha Huduma za Kiufundi |
| **TTSA** | Wakala wa Mbegu Tanzania |
| **TVLA** | Wakala wa Maabara ya Mifugo |
| **TWPF** | Mfuko wa uhifadhi wa Wanyama pori |
| **URT** | Serikali ya Jamhuri ya Muungo wa Tanzania |
| **UPDP** | Chama cha UPDP |
| **UDP** | Chama cha UDP |

| | |
|---|---|
| **UMD** | Chama cha UMD |
| **UN** | Umoja wa Mataifa |
| **USAID** | Shirika La Msaada la Marekani |
| **VAH** | Hospitali binafisi za Kujitolea |
| **VAT** | Kodi ya Ongezeko la thamani |
| **VT** | Fungu |
| **WMA** | Wakala wa Mizani na Vipimo |
| **WDF** | Mfuko wa Maendeleo wa wanawake |
| **WDMI** | Chuo cha Maendeleo ya Maji |
| **WETCU** | Chama cha Walimaji wa Tumbaku Magharibi |

## Dibaji

Nina furaha kubwakuwasilishataarifa yangu ya kwanzaya ukaguziwa Serikali Kuu(Wizara, Idara, Wakala na Taasisizinazojitegemea) nikiwakamaMdhibitina Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zaJamhuri ya Muungano waTanzaniatangukuteuliwa na MheshimiwaDr.JakayaM.Kikwete,Rais waJamhuri ya Muungano waTanzania.



**Prof Mussa.J.Assad**

Kazi hii ya ukaguzi imefanyika katika mazingira ya kuwa Serikali ina wajibu wa kuwapatia huduma wananchi wake kutokana na kodi wanazo lipa pamoja na rasilimali nyingine za nchi. Wakati huo huo, Taasisi hizi za serikali kuu zinawajibika kwa ajili ya usimamizi na utendaji,kuhusiana na ukusanyaji na matumizi ya rasilimali katika kutoa huduma .

Taarifa hii ya Ukaguzi inasaidia kujenga mazingira na matarajio kutoka kwa watumishi wa Wizara,Idara na Sektretarieti za Mikoa ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, kimaadili na kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za utumishi.

Katika Mwaka wa fedha uliopita Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa ziliaandaa taarifa za fedha kwa kutumia Viwango vya kimataifa vya kihasibu katika sekta vya umma kwa msingi wa fedha usio taslimu (accrual basis of accounting). Kutumia Viwango vya kimataifa vya kihasibu katika sekta ya umma vya msingi wa fedha usiyo taslimu pamoja Mfumo mpya wa kielektroniki wa Malipo Serikalini (Epicor version 9.05), imelazimu watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kuwajengea uwezo kuhusu mifumo hii mipya ili kuweza kufanya ukaguzi katika mazingira ya kutumia kompyuta.

Taarifa hii ya Ukaguzi inawasilishwa kwa Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu 34(1)(c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka, 2008.

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (2) (c) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano na hesabu zinazosimamiwa na Katibu wa Bunge.

Chini ya Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha kwa Rais kila ripoti anayotoa chini ya Ibara 143(2)(c). Baada ya kupokea ripoti hizo, Rais ataagiza wanaohusika waziwasilishe ripoti hizo mbele ya Kikao cha kwanza cha Bunge ndani ya siku saba baada ya kuanza kwa kikao.

Uhuru wa kiutendaji wa ofisi yangu kwa kiasi kikubwa umeimarika baada ya kuanza kutumia Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na 11 ya mwaka, 2008. Hata hivyo, kulingana na viwango vya kimataifa maboresho zaidi yanahitajika hasa kwa upande wa kupanga mishahara na ajira za watumishi wa ofisi yangu ili kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba kwa ufanisi zaidi.

Ni vyema kutambua kuwa wakati ofisi yangu inatoa taarifa kuhusu ukiukwaji wa sheria, taratibu na kanuni mbalimbali na udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani kwenye taasisi za Umma na hasa Serikali Kuu, lakini wajibu wa kuhakikisha kuwepo kwa mifumo thabiti ya udhibiti wa ndani ni jukumu la Maafisa Masuuli.

Bunge na watanzania kwa ujumla wanatarajia kupata uhakikisho kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na taarifa za fedha na usimamizi wa rasilimali katika Serikali Kuu pia ufanisi na ubora na usimamizi wa mipango iliyowekwa. Kwa njia ya ukaguzi, ofisi inachangia katika kutoa mapendekezo kuhusu uimarishaji na uboreshaji wa sekta ya Umma. Kwa msingi huu, Serikali Kuu na Ofisi yangu kila mmoja ana mchango katika kujenga imani kwa umma katika usimamizi wa rasilimali za umma. Ingawa majukumu ya ofisi yangu na yale ya taasisi za umma yanatofautiana, hata hivyo matarajio ya usimamizi bora wa rasilimali yanafanana.

Ili kukidhi matarajio ya Wabunge na Umma wa watanzania kwa mapana zaidi, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufanya uchambuzi wa njia bora zaidi za kufanya ukaguzi na kuongeza wigo wa masuala yanayokaguliwa na hivyo kuimarisha utendaji wa uwajibikaji katika sekta ya Umma. Aidha, tunahakikisha ukaguzi wetu unalenga kuyapa kipaumbele maeneo muhimu ili kuchangia maendeleo katika sekta ya Umma. Kwa kuwa kazi ya ukaguzi ni chachu katika usimamizi wa fedha, tutaendelea kujadili masuala yanayoathiri utawala/uongozi katika sekta ya umma, hasa katika utoaji wa taarifa za usimamizi wa fedha na masuala ya utawala bora.

Natarajia kuwa Bunge litaona taarifa hii kuwa ni muhimu katika kuhakikisha Serikali inatekeleza jukumu lake la usimamizi wa fedha za Umma na utoaji wa huduma kwa Watanzania. Hivyo, nitafurahi kupata maoni kutoka kwa watumiaji wa ripoti hii jinsi gani nitaweza kuboresha taarifa yangu kwa siku zijazo.



Profesa Mussa Juma Assad
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali**

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
**Dar es Salaam,**

**Machi, 2015**

## Shukrani

Napenda kutoa shukarani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dr. Jakaya M. Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kunituea kuwa Mdhibiti na Mkaguzi wa hesabu za Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.Nashukuru sana kwa uteuzi huu wa kikatiba na ninahakika nitafanya kazi hii kwa uadilifu na weledi wa hali ya juu.

Napenda, kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wakurugenzi, Watendaji Wakuu na wafanyakazi wote wa Taasisi za Serikali kuu zilizokaguliwa, kwa ushirikiano walioutoa kwa wakaguzi wakati wa zoezi zima la ukaguzi. Vilevile ninapenda kuwashukuru sana wafanyakazi wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kujitolea kwao na uvumilivu waliouonyesha katika kukamilisha taarifa ya ukaguzi, hii imeniwezesha kutekeleza jukumu la kikatiba la kuwasilisha taarifa kabla ya tarehe 31/03/2015 kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.Nawashukuru watu wote, taasisi na wadau mbalimbali waliofanikisha kwa namna moja au nyingine uandaaji wa taarifa hii.

Pia, napenda kuwashukuru wajumbe wa kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuu, kwa maoni yao mazuri, maelekezo na mapendekezo wakati wa mijadala na Maafisa Masuuli. Bunge kupitia kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuu inajukumu la kutoa uhakika na uthibitisho wa namna fedha za umma zilivyotumika.Tunalipa umakini mkubwa jukumu la kamati katika kusimamia uwajibikaji katika kuwezesha uelewa wa pamoja wa mamlaka ya mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za Serikali miongoni mwa wadau wote wa ndani na nje ya nchi.

Napenda pia kutambua kazi iliyofanywa na Idara cha Usimamizi wa Mali(Division of Government Assets Management) za Serikali ilio chini ya Wizara ya Fedha kwa kuandaa na kuwasilisha taarifa ya uhakiki wa mali uliofanyika kwenye baadhi ya Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa kwa mwaka wa fedha 2013/14 na kuonyesha mambo mengi ambayo kwa kiasi kikubwa yalijitokeza kwenye ripoti yangu ya mwaka. Napenda kutambua kazi iliyofanywa na Kitengo hiki ambayo nimeona ni vyema nikaijumuisha kwenye ripoti yangu.

Nina kila sababu ya kuwashukuru wadau wetu wengine ikiwa ni pamoja na Waziri wa Fedha, Mlipaji Mkuu wa Serikali; na Mamlaka ya Ununuzi wa Umma(PPRA) walio chini ya Wizara ya Fedha kwa ushirikiano nautoaji wa taarifa muhimu zilizohitajika kwa ajili ya maandaliziya ripoti hii. Pia

napenda kumshukuru Mpiga chapa kwa kuharakisha uchapaji wa ripoti hii na kuweza kuiwasilisha kwa wakati.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa wafadhili hasa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden, Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Kimataifa la Misaada la Maendeleo la Sweden, Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Kusimamia na Kuboresha Sekta ya Fedha za Umma (PFMRP), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Misaada la Ujerumani (GIZ), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Serikali ya China na wale wote wanaotutakia mema ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha Ofisi yangu. Michango yao katika kukuza rasilimali watu, mifumo ya teknolojia ya habari na mali (vitendea kazi) imekuwa na manufaa makubwa katika kufanikisha shughuli zetu.

Mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu; napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kazi nzuri aliyofanya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali aliyestaafu Ndugu Ludovick S. L. Utouh.Nasema asante sana kwa yote uliyofanya katika kuboresha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.

Naahidi utumishi uliotukuka kwa taifa katika kipindi hiki cha kusimamia uwajibakaji katika mapato na matumizi ya rasilimali za umma.Muhtasari

## Utangulizi

Muhtasari huu unaainisha kwa kifupi hoja mahususi zilizojadiliwa kwa kina katika sura husika za ripoti hii zinazohitaji kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, na Menejimentiza taasisi za Serikali Kuu husika ili kuhakikisha kunakuwa na tija na ufanisi katika utendaji wa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa.Ripoti hii inajumuisha matokeo ya ukaguzi ambayo yalionekana kukwamisha utendaji wa Serikali Kuu na Sektretarieti za Mikoa yaliyotokana na taarifa za Ukaguzi.Kwa ujumla ripoti hii inahusisha masuala ambayo yalionekana ya muhimu na ambayo yanahitaji hatua za haraka.Masuala hayo kwa ufupi ni kama ifuatavyo:

i) **Mwenendo wa jumla wa hati za Ukaguzi**

Ukaguzi wa taarifa za fedha ulifanyika kwa Wizara na idara za Serikali sitini (60), Sekretarieti za Mikoa ishirini na tano (25) na Balozi thelathini na nne (34) kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2014.Vile vile katika taarifa hii nimejumuisha matokeo ya ukaguzi kwa Wakala Wa Serikali (32), Mifuko maalumu kumi na mbili (12), Taasisi nyinginezo kumi na tatu (13) pamoja na vyama vya siasa. Muhtasari wa matokeo muhimu ya ukaguzi yamejumuishwa katika taarifa hii na taarifa za kina kwa menejimenti ambazo zilitumika kutengeneza taarifa hii zimetolewa kwa barua kwa Maafisa Masuuli wote husika. Matokeo na hati za ukaguzi kwa miaka mitano zilizotolewa ni kama inavyoonekana katika jedwali Na 1 hapa chini:

**Jedwali 1:** *Matokeo ya hati za Ukaguzi kwa Miaka Mitano*

| | Hati za Ukaguzi | Hati inayoridhisha | | Hati yenye shaka | | Hati isiyoridhisha | | Hati Mbaya | | Jumla ya wakaguliwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Total | % | Total | % | Total | % | Total | % | |
| Miaka | 2009/10 | 78 | 76% | 21 | 21% | 2 | 2% | 1 | 1% | 102 |
| | 2010/11 | 99 | 93% | 8 | 7% | 0 | 0% | 0 | 0% | 107 |
| | 2011/12 | 103 | 95% | 5 | 5% | 0 | 0% | 0 | 0% | 108 |
| | 2012/13 | 85 | 73% | 30 | 26% | 1 | 1% | 1 | 1% | 117 |
| | 2013/14 | 166 | 94% | 9 | 5% | 1 | 1% | 0 | 0% | 176 |

**Hati isiyoridhisha ilitolewa kwa taarifa za Hesabu Jumuifu za Fedha za Taifa**

Sababu kuu ya kutolewa kwa hati isiyoridhisha kwa hesabu hizi ni kama ifatavyo:

- Taarifa za Hesabu za Majumuisho kwa kipindi kinachoisha 30 Juni, 2014, zimejumuisha taasisi za umma zenye vipindi tofauti vya ufungaji wa hesabu na kile cha serikali kinyume na Kanuni ya 6 ya IPSAS, Aya ya 47.
- Taasisi nyingi za umma zimekuwa zikitumia kanuni mbalimbali za uhasibu katika kuwasilisha hesabu. Wakati Serikali Kuu, ambaye ndie mmiliki wa taasisi hizo imekuwa ikitumia Kanuni za Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS Accrual basis of accounting) inapoandaa hesabu zake, bado baadhi ya taasisi kama vile Shirika la Magazeti Tanzania (TSN), Benki ya Posta, Mamlaka ya Bandari na nyinginezo zimekuwa zikitumia kanuni za IFRS kwenye kuwasilisha taarifa zao.
- Mapitio ya Hesabu za Majumuisho ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yamebaini kwamba kuna taasisi za umma ambazo hazikujumuishwa. Taasisi ambazo hazikujumuishwa ni Unit Trust of Tanzania (UTT), Suma JKT, Tanzania Nurses and Midwife Council (TNMC), na Mamlaka ya Usajili wa Leseni za Biashara (BRELA). Kutokuwepo kwa taasisi hizi za umma

kwenye hesabu za majumuisho kunaharibu uwasilishwaji wa uhalisia wa taarifa za hesabu.

Kwa ujumla, mwaka huu kuna ongezeko kubwa la hati zinazo ridhisha ukilinganisha na miaka iliyopita. Taasisi zilizopata hati inayoridhisha zimeongezeka kutoka 73% mwaka jana hadi 93%. Taasisi zilizopata hati yenye shaka zimepungua kwa asilimia 26%hadi asilimia 6%

**ii) Utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita**

Ufuatailiaji makini wa mapendekezo ya ukaguzi husaidi kupatikana kwa thamani halisi ya ukaguzi.Nimefanya ufuatiliaji juu ya utekelezaji wa mapendekezo yangu katika taarifa za Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa. Katika Wizara na Idara za Serikali, kulikuwa na hoja 2,228 zilizotolewa kwa Wizara na Idara 85, Ofisi za Balozi 34 na Sekretariati za Mikoa 25. Kati ya mapendekezo 2,228, mapendekezo 846 (38%) yametekelezwa kikamilifu, 653 (29%) yalitekelezwa kwa sehemu na 681 (31%) hayakutekelezwa na mapendekezo 48 (2%) yalipitwa na wakati.Kutokana na asilimia 38% ya hoja kutekelezwa kikamilifu hii inaonesha kuwa Kasi ya utekelezaji wa mapendekezoniliyotoa sio ya kuridhisha.

Katika ukaguzi wa mwaka jana, taarifa yangu ilikuwa na masuala Ishirini na mbili (22) ambayo yalihitaji majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali. Nimepokea majibu kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ambapo hoja kumi na tano (15) zimefungwa huku hoja saba bado zinasubiri majibu.

Katika ripoti hii ya ukaguzi jumla ya mapendekezo 26 hayajatekelezwa ambayo yanahitaji jitihada za serikali kufanyia kazi.Hii inaonesha ongezeko la mapendekezo 4 sawa na asilimia 18% ikilinganishwa na Ukaguzi wa Mwaka wa fedha uliopita.Taarifa hizi zimeelezwa kwa kina katika sura ya tatu.

iii) **Utekelezaji wa Mapendekezo ya kamati ya bunge ya hesabu za Serikali Kuu**

Katika taarifa hii ya ukaguzi kuna jumla ya mapendekezo kumi (10) yaliotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ambayo hayajatekelezwa. Mapendekezo saba yalitolewa kwa miaka ya nyuma na mapendekezo matatu yametolewa mwezi Januari, 2015. Tarehe 28/1/2015 wizara ya fedha ilitoa majibu ya repoti ya PAC iliyowasilishwa bungeni Mwezi Januari, 2015. Ufuatiliaji wa mapendekezo ya kamati ya bunge ya hesabu za Serikali kuu bado unaendelea.Taarifa hizi zimeelezwa kwa kina katika sura ya tatu.

iv) **Kuchelewa kutolewa kwa fedha**

Kumekuwa na ucheleweshaji katika kutolewa kwa fedha kutoka Hazina na kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hii imesababisha kuchelewa kwa utekelezaji au kutotekelezwa kabisa kwa miradi iliyokusudiwa kutekelezwa na kupelekea kuongezeka kwa gharama za miradi zaidi ya ilivyopangwa awali na kupelekea halikadhalika kuwepo kwa kiasi kikubwa cha fedha zisizotumika mwishoni mwa mwaka. Katika kipindi cha mwaka wa fedha uliomalizika, fedha za maendeleo kiasi cha TZS.1,888,911,542,533 hazikutolewa sawa na asilimia (38%) wakati kiasi cha TZS.19,229,865,085 sawa na asilimia (1%) cha fedha iliyotolewa hakikutumika. Kiasi cha TZS.400,259,001,766 za akaunti ya matumizi ya kawaida hakikutolewa wakati kiasi cha TZS.8,279,275,815 cha fedha iliyotolewa sawa asilimia 0.09% hakikutumika.

Fedha za maendeleo kiasi cha TZS.1,259,031,558,670 sawa na 40.01% ya fedha zilizotolewa kwa Wizara na Sekretarieti za Mikoa na fedha za matumizi ya kawaida kiasi cha TZS.2,187,509,171,733 sawa na 23% ya fedha zilizotolewa kwa Wizara na Sekretarieti za Mikoa zilitolewa katika robo ya nne ya mwaka wa fedha. Taarifa hizi zimeelezwa kwa kina katika sura ya nne ya taarifa hii.

v) **Mapungufu katika Hesabu Jumuifu**

Nimebaini kuwa Serikali imekuwa ikiandaa hesabu kwa kujumuisha hesabu kutoka taasisi mbalimbali za serikali ambazo zimekuwa zikitumia miongozo tofauti ya uandaji wa hesabu pamoja na kufunga hesabu tarehe tofauti. Mapungufu haya yanapatikana kwenye sura ya tano ya taarifa hii.

vi) **Usimamizi usioridhisha wa uwekezaji wa Serikali na maslahi mengine**

Nimebaini kuwepo kwa kudorora kwa uwekezaji wa serikali katika taasisi mbalimbali na hata kupelekea thamani yahisa za serikali kupungua au kuwa katika hatari ya kuisha kabisa. Hii imesababisha Serikali Kushindwa kuongeza mtaji zaidi wakati inapohitajika kama ilivyojidhihirisha katika hisa za Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Biashara (NBC 1999 Ltd.), Shirika la Ndege (ATCL), TAZARA, TTC na Shirika la Reli (TRL) ambayo yote kwa namna moja au nyingine yamekumbwa na uhaba wa mtaji.

vii) **Mamlaka ya Mapato Tanzania**

Makisio ya makusanyo ya kodi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania yaliyokuwa yameidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014 yalikuwa TZS 10,914 billioni ambapo kiasi cha TZS 9, 996 bilioni kilikusanywa. Hata hivyo, upembuzi kuhusiana na ukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha ukaguzi unaonyesha kiwango cha makisio hakikuweza kufikiwa kwa asilimia 8.4. kutokufikia kwa makisio kumekuwepo kwa miaka minne iliyopita ukiacha mwaka 2011/2012.

Kufuatia hili, usimamizi wa fedha umekuwa ni sehemu muhimu katika usimamizi wa matumizi ya umma. Kutokana na kupungua kwa fedha zinazotolewa, kumesababisha serikali na taasisi zake kushindwa kutekeleza kazi kama ziliyoidhinishwa. Kama kumekuwa na usahihi wa makaridio ya makusanyo, ingekuwa rahisi kuwa na mikataba ya ufanisi kwa upande wa TRA ili kufikia

malengo hayo. Hatukuweza kupata ushahidi kama mikataba ya ufanisi inazingatiwa.

Ukiacha hilo, kuna changamoto zingine kama; ucheleweshwaji wa kusikiliza rufaa za kesi za kodi, matumizi mabaya ya misamaha ya kodi, mapungufu katika ukusanyaji ushuru wa forodha, mapungufu katika sheria za kodi zilizopo na mapungufu katika ukadiriaji wa kodi. Haya yote yanachangia katika kukwamisha ukusanyaji wa mapato. Masuala haya kwa kirefu yameelezwa katika ukurasa wa tano wa ripoti hii.

Hata hivyo, kuna mambo ya haraka yanayoweza kufanyika ili kuziba mianya katika ukusanyaji wa mapato na kuongeza ufanisi. Kwa mfano, inafahamika kwamba serikali inafanya biashara kwa kiasi kikubwa na sekta binafsi, lakini wafanyabiashara wengi hawazingatii sheria ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) inayowataka kutumia mashine za kiielekroniki katika kutoa stakabadhi za mauzo (EFD receipts). Kama Serikali ikiamua kwamba Serikali na Taasisi zake zote zisinunue bidhaa au huduma yoyote kutoka kwa wafanyabiashara wasiotoa stakabadhi za kielekroniki, ninaamini utii wa sheria hii ungeongezeka na hivyo kuongeza makusanyo ya kodi ya ongezeko la thamani na kodi nyinginezo.

Kuna maeneo mengine ambayo TRA haijajikita sana katika kukusanya kodi. Moja ya maeneo haya ni mapato yatokanayo na pango. Maendeleo katika ujenzi wa majengo ni eneo linalokuwa kwa kasi katika kipindi cha miaka 20 iliyopita. Orodha ya wamiliki wa majengo haijawahi kuandaliwa wala kutumika na TRA kukusanya mapato na chanzo hiki. Hivyo, ni muhimu suala hili kupewa kipaumbele na Serikali.

**viii) Tathimini ya mfumo wa udhibiti wa ndani**

Katika taarifa hii nimejumuisha mapungufu mbalimbali yaliobainika katika mifumo ya udhiti ya ndani yaliojitokeza wakati wa ukaguzi na kujumuisha katika taarifa yangu.Mifumo ya ndani ni

eneo muhimu linalohitaji kuboreshwa katika utendaji wa taasisi za serikali kuu. Nilibaini kuwa kamati ya Ukaguzi na Vitengo vya ukaguzi wa Ndani vilifanya kazi chini ya kiwango kutokana na uhaba wa watumishi, rasilimali na mapungufu katika muundo wa kamati za ukaguzi. Nilibaini kwamba Wizara/Idara za Serikali na Sekretarieti za mikoa hazikuwa na Sera inayoongoza matumizi ya Teknolojia ya Habari iliyoandikwa na kutolewa kwa watumiaji wote wa vifaa vya kompyuta, pia nilibaini kutokuwepo mpango wa kufufua huduma iwapo majanga yakijitokeza. Maelezo ya kina kuhusu udhibiti wa ndani yanapatikana sura ya sita ya taarifa hii.

**ix) Udhaifu katika Usimamizi wa rasilimali watu na taarifa za Mishahara**

Katika kupitia usimamizi wa rasilimali watu na mishahara ,nilibaini mapungufu yafuatayo:Malipo ya mishahara yalifanyika kwa watumishikatika wizara,idara na Sekretarieti za Mikoa ambao hawapo katika utumishi wa umma,upungufu wa watumishi 9,670 katika Wizara na Idara ,Sekretarieti za Mikoa na balozi,baadhi Watumishi wa umma kukaimu nafasi zilizoachwa wazi kwa muda zaidi ya miezi sita, Watumishi wa umma kutothibitishwa kazini kwa muda mwafaka, watumishi katika Wizara na Idara , na Sekretarieti za Mikoa kupokea mishahara chini ya kiwango kinachoruhusiwa kisheria, fedha za mishahara isiyolipwa hazikupelekwa katika akaunti husika,kulipwa posho na kodi ya pango kwa maofisa waliostaafu kazi katika balozi tano za Tanzania nje ya nchi na ambao hawakuwa na mkataba wa kisheria wa ajira.Taarifa hizi zimeelezwa kwa kina katika sura ya saba.

**x) Mapungufu katika Utendaji wa Wakala za Serikali**

Katika taarifa mwaka wa fedha 2013/2014 nimejumuisha sura inayoelezea mapungufu mbalimbali yaliojitokeza kwenye wakala (ambazo kwa idadi ni 37), mifuko maalumu na taasisi nyingenezo za serikali. Ukaguzi unaonesha kuwa kuna mapungufu katika kuzingatia sheria mbalimbali katika taasisi hizi. Mapungufu mengi yameainishwa katika sura ya nane yakionesha ukosefu wa uadilifu kutozingatia au upotoshaji wa sheria na kanuni. Mapungufu

yaliojitokeza yanajumuisha,malipo yasiokuwa na viambatanisho vya kutosha,malimbikizo ya madeni,mapato yatokanayo na madeni hayakukusanywa,fedha za maafa hazikusimamiwa vizuri,kukosekana kwa hati za viwanja na nyumba.Undani wa taarifa hii umeelezewa kwenye sura ya nane.

**xi) Mapungufu katika Manunuzi na usimamizi wa mikataba**

Licha ya, Serikali kuendelea na juhudi katika kuimarisha sheria na taratibu za manunuzi katika ofisi zote za umma kwa kutekeleza mapendekezo yangu ya nyuma na mapendekezo yaliyotolewa na Mamlaka ya udhibiti wa Manunuzi ya umma. Hata hivyo, bado kuna baadhi ya Wizara, Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa ambazo hazifuati kikamilifu mahitaji yaliyomo katika sheria ya Ununuzi wa Umma katika kuidhinisha zabuni, usimamizi wa mikataba, kutozingatiwa mpango wa manunuzi, utunzaji wa nyaraka za manunuzi usioridhisha katika kitengo cha manunuzi, kutofanyika uteuzi wa kamati ya tathmini, kamati ya ukaguzi bidhaa na kamati mapokezi. Maelezo ya kina kuhusu mikataba na manunuzi ya bidhaa na huduma yanapatikana sura ya tisa ya taarifa hii.

**xii) Mapungufu katika usimamizi wa Matumizi**

Katika mwaka huu wa fedha nimebaini mapungufu mbalimbali katika usimamizi wa matumizi ya fedha za serikali katika maeneo yafuatayo; Malipo ya kiasi cha TZS. 39,117,335,237 yaliofanyika bila ya kuwepo viambatisho vya kutosha Katika malipo haya yanajumuisha ( Hati za malipo hazikupatikana wakati wa ukaguzi,Risiti za kielectroniki hazikuambatanishwa na Malipo yasiyoambatanishwa na risiti),Malipo yaliyofanyika kwenye vifungu visivyostahili TZS.1,833,544,597,Matumizi yaliofanyika nje ya bajeti yenye thamani ya TZS. 4,956,081,490,masurufu ya muda mrefu yasiyorejeshwa TZS.291,558,029; Malipo ya zaidi TZS.440,721,740;Malipo yasiokuwa na manufaa TZS. 924,558,029,Malipo yaliofanywa kwa kazi zisizokusudiwa TZS.1,562,946,574;Mapungufu haya yameelezewa kwa kina kwenye sura ya kumi.Katika ukaguzi wa matumizi ya risiti za

kielektroniki nilibaini kuwa makampuni binafisi hayatoi risiti za kielektroniki hii ilipelekea malipo yenye thamani ya TZS.4,419,662,152 kutokuwa na risiti hizo.

**xiii) Usimamizi wa Mali**

Usimamizi wa mali za umma ni eneo lenye changamoto nyingi linalohitaji mpango mkakati kwa ajili ya kutekeleza lengo husika. Kama ilivyobainishwa katika sura ya kumi na moja Mapitio ya usimamizi wa mali na madeni kwenye taasisi za serikali kuu ulibaini mapungufu yafuatayo:magari na pikipiki ambazo zimeegeshwa bila matengenezo katika taasisi 11 kwa mwaka huu wa fedha, ikilinganishwa na taasisi 17 kwa mwaka wa fedha uliopita,taasisi nane (8) zilitoa taarifa ya ardhi na majengo lakini taasisi hizi hazikuwa na hati miliki ambazo zinathibitisha umiliki wa mali hizo, nyumba 29 katika balozi za Tanzania nje ya nchi ambazo ziko katika hali mbaya zinahitaji matengenezo, viwanja katika Ubalozi wa Tanzania Maputo Msumbiji,Lilongwe Malawi na Moroni Comoro havijaendelezwa na mapungufu mbalimbali katika usimamizi wa vifaa katika taasisi 11.

**xiv) Mapungufu katika usimamizi wa madeni**

Katika ukaguzi wa madeni nilibaini,malimbikizo ya madeni katika Wizara na idara zake 59 na Sekretarieti za Mikoa 23 yenye jumla ya TZS.772,508,290,161ikiwa ni ongezekolaTZS.272,979,513,582 sawa na asilimia 55% ikilinganishwa na kiasi cha TZS.499,528,776,579 katika mwaka wa fedha uliopita(ulioishia 30 Juni 2013). Nilibaini matumizi ambayo hayakulipwa mwaka wa fedha uliopita hayakuingizwa kwenye bajeti ya mwaka huu unaofuata katika mzunguko wa bajeti wa wizara. Hii itapelekea kuongezeka kwa madeni kutokana na fedha za bajeti za mwaka husika kutumika kulipia madeni ya kipindi kilichopita. Katika hali ya kipekee madeni yalihusisha madeni ya matibabu katika hospitali za India yanayofikia Rupia 605,014,043 sawa na TZS.16,940,393,204 hadi kufikia mwezi Januari,2015.

Mbali na hilo kulikuwa na kesi 83 katika taasisi 12 dhidi ya makampuni na watu mbalimbali zenye jumla ya kiasi cha TZS.599,473,932,835 zilikuwa bado zinasubiri maamuzi ya mahakama wakati ambapo kesi zingine zilikuwa zina zaidi ya miaka kumi na hakukuwa na taarifa za mahakamajuu ya tarehe zakusikilizwa. Taarifa hizi zimeelezwa kwa kina katika sura ya kumi na moja.

**xv) Ukaguzi Maalumu**

Katika mwaka 2013/2014 nimefanya kaguzi maalum nane (8). Taarifa zimeandaliwa na kutolewa kwa mamlaka husika. Hata hivyo, maelezo ya ukaguzi maalum uliofanyika yanapatikana katika sura ya kumi na mbili ya taarifa hii. Muhtasari wa masuala ya msingi kutokana na ukaguzi maalum ni kama inavyooneka hapa chini:

- Ukaguzi maalum wa mfumo mzima wa manunuzi, uagizaji kutoka nje ya nchi, mapokezi na usambazaji wa pembejeo za kilimo katika sekta ya kilimo cha tumbaku chini ya WETCU – Tabora ulibaini kuwa wazabuni walipewa zabuni bila ya kuwasilisha maombi ya zabuni na pia zabuni hazikuidhinishwa na bodi ya zabuni.kulikuwa na utunzaji hafifu wa kumbukumbu pamoja na ukiukwaji mkubwa wa taratibu za kiuhasibu. Pia, nimebaini kuwepo mgongano wa maslahi katika mchakato mzima wa manunuzi ya zabuni.

- Katika ukaguzi maalum wa ujenzi wa jengo la kumbi za watu mashuhuri katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam katika kipindi cha mwaka 2006/2007 hadi 2011/2012nilibaini mapungufu kadhaa ambayo ni;Mkataba wa ujenzi haukupatikana wakati wa ukaguzi.Katika taarifa yake, mthamini Mkuu wa majengo ya Serikali amebainisha kwamba thamani ya jengo hilo hadi Mwezi Mei, 2014 ni sawa na TZS3,072,000,000 tofauti na TZS12 billioni zilizotolewa taarifa.Niligundua manunuzi ya TZS 916, 917,145 yalifanyika kinyume na Sheria ya Manunuzi ya Umma.

- Ukaguzi maalum ulifanyika kwenye Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa kimataifa kuhusu matatizo yanayozikumba balozi za Tanzania ulifanyika kwa miaka ya fedha 2010/2011,2011/2012 and 2012/2013 ulibaini kuwa,bajeti za balozi ziliandaliwa bila kuzingatia mahitaji halisi ya balozi,ukomo wa bajeti haukuzingatia matumizi kama ya umeme na mafuta ya magari,fedha za maendeleo kutotosheleza na kutotenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya serikali yaliyopo Balozini.

- Katika Ukaguzi maalum juu ya utekelezaji wa mikataba ya ujenzi wa mradi wa usambazaji maji Chalinze – Awamu ya pili nilibaini;mikataba kutokamilika kwa muda uliopangwa,kutopatikana kwa taarifa ya upembuzi yakinifu haukufanyika,kasoro mbalimbali katika usanifu wa mradi na michoro,malipo kufanyika bila ya kuonesha kazi zilizofanyika,miundombinu ya maji kukabidhiwa bila kufanyiwa majaribio na malipo ya ziada kutokana na ucheleweshaji wa malipo TZS.3,897,283,923.

- Ukaguzi maalum wa fedha zilizotumiwa na Wizara mbalimbali kuchapisha hotuba za bajeti baada ya kuidhinishwa na bunge la bajeti kwa mwaka 2011/2012 na 2012/2013 ulibaini kuwa jumla ya TZS.2,545,517,366.79zilitumika kugharimia machapisho ya hotuba za bajeti za wizara 21 na taasisi 5 katika kipindi cha mwaka 2011/2012 na 2012/2013. Nilibaini piakutokuwepona sheriazinazoelekeza matangazo ya bajeti kwenye vyombo vya habari.

- Ukaguzi maalum katika fungu 98 – Wizara ya Ujenzi kuhusu uhalali wa fedha TZS.252,975,000 za ujenzi wa barabara.Ilibainika kuwataarifa iliyowasilishwa ya mradi wa ujenzi wa barabara Na 4168 wa TZS.252,975,000 haukuwa sahihi kwani fedha zilitumika kulipia madeni ya wakandarasi.

- Nilifanya ukaguzi maalum wa taarifa za fedha za Mkutano wa kimataifa wa global 2013 Smart Partnership Dialogue ambapo Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ilikuwa mwenyeji .Ukaguzi huu ni kwa ajili ya kipindi cha miezi kumi na nane kuanzia Julai 2012 hadi Januari 2014 nakubaini manunuzi yenye thamani ya TZS.614,626,341 yalifanyika nje ya mpango wa manunuzi uliopitishwa. Kutozingatiwa kwa bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya manunuzi ya tiketi za usafiri wa ndege pia vifaa kununuliwa baada ya mkutano kuisha.

- Ukaguzi maalum wa mradi wa matrekta na zana za kilimo wa SUMA JKT kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2010 hadi Aprili, 2014 ulibaini kuwakampuni ya ESCORT LTD ilipewa tenda ya kuuza matrekta, pampu za umwagiliaji, zana za kilimokwa USD 40,000,000 wakati mzabuni alikuwa ameomba kwa gharama ya USD 35,526,411.48 na hivyo kusababisha ziada ya ya USD 4,473,588.52 ambazo hazikuwa na maelezo. Manunuzi ya matrekta 2,114 pamoja na zana za kilimo 4,450 yalifanyika bila ya kufuata taratibu za manunuzi. Pia nilibaini hasara ya TZS 261,029,531 iliyotokana na kunyofolewa vipuri kwenye matrekta matano na zana za kilimo 16(power tillers)

**Mhutasari wa Mapendekezo**

Katika ukaguzi wa mwaka 2013/2014 natoa mapendekezo yafuatayo kwa matumizi bora ya rasilimali za taifa na utoaji wa huduma bora kwa jamii.

**Utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita**

Serikali ikishirikiana na maafisa masuuli wa taasisi husika wanatakiwa kuweka bidii ya kutosha ili kufanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa.Kuna umuhimu wa kuboresha mifumo ya ndani.Hii inatokana na mapungufu yaliyojitokeza kusababishwa na mifumo dhaifu.Maafisa masuuli wanashauriwa kuanda mpango mkakati wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kuweza kutekeleza mapendekezo hayo kwa wakati.

**Ucheleweshaji wa kutolewa kwa fedha**
Ili kukabiliana na changamoto ya fedha zilizoidhinishwa kutototolewa kwa wakati, nashauri Serikali kuandaa makisio ya matumizi ya mwaka yanayoendana na makusanyo ya mapato ili kuzuia kutolewa kwa kiasi kikubwa cha fedha mwishoni mwa mwaka wa fedha. Kwa kufanya hivyo, inatarajiwa kwamba shughuli zilizopangwa zitatekelezwa kama zilivyopangwa.

**Mapungufu katika usimamizi wa uwekezaji wa Serikali (Msajili wa Hazina)**
Napendekeza kuwa, serikali itenge kiasi cha fedha cha kutosha kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato pamoja na gawio analopata Msajili wa Hazina kutoka kwenye makampuni mbalimbali ili kuweza kulinda uwekezaji wake katika makampuni pamoja na kubuni sehemu nyingine za uwekezaji.Vilevile, napendekeza serikali kufanya thamini ya uwekezaji mara kwa mara kwenye kampuni mbalimbali ili kuweza kubaini mafanikio ya uwekezaji huo.

**Mapungufu katika Hesabu Jumuifu**
Nashauri serikali kuhakikisha mfumo wa kihasibu wa taasisi zake unakuwa mmoja ili kuweza kuendana na Viwangovya kimataifa vya uandaaji wa hesabu vile vile kuunganisha hesabu za taasisi zake zote ili kuonesha hali halisi ya hesabu za majumuisho.

**Mapungufu katika Misamaha ya Kodi na Matumizi ya Mashine za elektroniki**
Ninapendekeza Serikali iimarishe mfumo wa udhibiti na usimamizi wa misamaha ya kodi inayotolewa na menejimenti ya TRA iimarishe mfumo wa ukaguzi na uchunguzi kupunguza migogoro kuhusiana na ulipaji wa kodi. Pia, kuwe na kikao cha kimkakati kujadili maeneo maalumu na njia za kukuza ukusanyaji wa mapato pamoja na kushughulikia rufaa za kesi za kodi nchini.

Mamlaka ya Mapato Tanzania kutoza wafanyabiashara wasiotumia mashine za kielektroniki. Serikali itoe miongozo kwa taasisi zake kuacha kufanya biashara na wazabuni wasiotoa risiti za kielektroniki.

**Usimamizi wa rasilimali watu na taarifa za Mishahara**
Serikali inashauriwa kuhakikisha kuwakasoro hii haitokei na Maafisa Masuuli wote kuhakikisha mishahara iliyolipwa kwa wasio watumishi wa umma inarudishwa kutoka kwa watumishi hao na kuwasilishwaHazina,Sekretarieti yaajira ya Utumishi wa Umma kuhakikishaajira yawafanyakazi wapyana uthibitisho wa watumishi wanaokaimu nafasi zilizoachwa wazi unafanyika ili kuongeza ubora katika utoaji wa huduma kwa jamii,Wizara,Idara na Sekretarieti za Mikoa zirekebishe taarifa za wafanyakazi wake wote katika mfumo wa malipo ya mshahara(LAWSON), Maafisa Masuulikuimarisha mfumo waudhibiti wa ndani juu ya mikopoya wafanyakazi, maafisa wastaafukatika balozi za Tanzania warudishwe nyumbani mara baada ya kustaafu na nafasi zao kujazwa maramoja.

**Wakala wa Serikali, mifuko maalumu na taasisi nyingine**
Idara za serikali zinashauriwa kulipa madeni yote wanayodaiwa na wakala wa serikali pamoja na taasisi nyingine. Maafisa masuhuli wanashauriwa kuzingatia sheria na miongozo mbalimbali ili kuboresha uwajibikaji na uwazi katika wakala, mifuko maalumu na taasisi nyingine.

**Mapungufu katika Manunuzi na Usimamizi wa mikataba**
Kwa kuzingatia muhtasari wa matokeo ya ukaguzi katika ripoti hii natoa ushauri kwa menejimenti na Taasisi za Serikali Kuukuhakikisha zinaifuata kikamilifu Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013. Nguzo kuu za mchakato wa manunuzi (Afisa Masuhuli, Kitengo cha Manunuzi, Bodi ya Zabuni, kamati ya tathimini pamoja naidarazinazohitaji) kufanya kazi bila kuingiliana kama ilivyoainishwa kwenye sheria ya umma ya mwaka 2011. Maafisa masuhuli pamoja na kitengo cha manunuzi kuhakikisha mpango wa manunuzi wa mwaka unafuatwa na manunuzi yanafanyika kwa idhini ya bodi ya zabuni.Vifaa na bidhaa vinafanyiwa ukaguzi kabla ya kupokelewa.Vile vile taasisi za

serikali kuu kuzingatia sheria ya manunuzi katika ushindanishi wa bei pamoja na upatikanaji wa wazabuni.

**Mapungufu katika Usimamizi wa Mali**
Serikali inashauriwa kuhakikisha kwamba mali zote zinalindwa na mali ambazo zimechakaa na haziwezi kufanyiwa matengenezo zinaondolewa ili kuzuia uwezekano wa kupata hasara kwa baadae, Wizara, idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na balozi zote zipate hati za umiliki wa mali za serikali walizonazo, matengenezo ya majengo ya ubalozi yafanyike ili kuzuia uharibifu zaidi wa majengo na viwanja vya serikali katika balozi husika viendelezwe.

**Usimamizi wa Madeni**
Ninapendekeza kwa serikali Kuhakikisha fedha zinatolewa kama zilivyopitishwa katika bajeti ili kupunguza limbikizo kubwa la deni ambalo linaweza kusababisha madai kuongezeka.

**Madeni ambayo kuthibitika kwake kunategemea maamuzi ya tukio/mahakama**
Maafisa masuhuli kwa kushirikiana na ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali nawashauri kufuatilia kwa karibu mashauri au kesi mbalimbali zilizopo mahakamani ili kukamilika kwa wakati ili kupunguza gharama kwa serikali.Kuweka makisio katika bajeti kwa zile kesi ambazo serikali inaweza kushindwa na kuepuka maamuzi yanayoweza kupelekea kujitokeza kwa malalamiko/au kesi mahakamani na kuongeza udhibiti wa madeni.

**Mapungufu katika usimamizi wa Matumizi**
Bodi za ushauri za wizara pamoja na maafisa masuuli wanatakiwa kuzingatia kuwa matumizi yote ya serikali yanatakiwa kuwa na viambatanisho vya kutosha ili kuweza kuboresha usimamizi wa matumizi na ufuatiliaji wa matumizi ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali.

**Ukaguzi Maalumu**
- AMCOS zinashauriwa kuzingatia sheria ya manunuzi ya umma na kanuni zake katika manunuzi yote. Serikali ifanye uchunguzi pamoja

na kuviagiza vyombo vyake vya kichunguzi kwaajili ya kuwachukulia hatua stahiki wahusika wote.

- Nashauri kuwa uendelezaji wowote katika viwanja vya ndege ufanyike kwa makini ili kuleta ufanisi katika utendaji. Serikali inapaswa kuwa na mfumo wa udhibiti wa ndani ulio imara hususani wa mali zinazopatikana. Mfumo wa nyaraka na kumbukumbu unapaswa kuboreshwa ili kuhakikisha ukamili, uadilifu na upatikanaji wa taarifa.

- Naishauri Serikali kuongeza bajeti ya balozi nje ya nchi ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yake.

- Serikali kuingia mikataba ambayo fedha za kutosha zimetengwa katika utekelezaji wa miradi.Michoro ya kazi za ujenzi inatakiwa kupitiwa na wataalamu kabla ya kuidhinisha ujenzi ili kuhakikisha kazi bora inafanyika.Serikali itoe kazi kwa wakandarasi kulingana na uwezo wa usajili wao.Michoro kwa miradi kama ule wa Chalinze uhakikiwe na wataalam kabla ya kazi kutangazwa.

- Serikali iandae mwongozo kwa taasisi zake namna ya kutangaza bajeti ikishapitishwa na bunge.

- Matangazo ya zabuni za Serikali yaendane sambamba na kiasi cha bajeti kilichotengwa katika mwaka husika. Wizara ikishirikiana na TANROADS kuboresha kitengo cha uhasibu katika utunzaji sahihi wa malipo kwa wakandarasi pamoja na usuluhishi wa madeni ya ukandarasi na rejista ya madeni.

- Menejimenti ya SUMA JKT iboreshe mifumo ya ndani ikiwa ni pamoja na kuzingatia sheria za manunuzi.

## SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI NA MAMBO YA JUMLA

### 1.0 Utangulizi

Sura hiiinatoataarifa ya jumla kuhusumchakato wa ukaguzi,hitaji la kisheriala kufanyaukaguzi namahusianokati yaMkaguzi nawakaguliwa.

### 1.1 Mamlaka na Umuhimu wa ukaguzi

Mamlakaya kisheria yanampa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuuwa Hesabu za Serikali kuanzisha nakufafanua kusudi, jukumu na mawanda ya shughuliza ukaguzikatikaJamhuri ya Muungano waTanzania.

### 1.1.1 Mamlaka ya Ukaguzi

Kwa mujibu waIbara ya 143 yaKatiba yaJamhuri ya Muungano waTanzaniaya mwaka 1977(iliyofanyiwa marekebisho) na kifungu cha10cha Sheriaya Ukaguzi wa UmmaNa.11 ya mwaka 2008, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuuwa Hesabu za Serikali nimkaguziwa wamapatoyote ya Serikalina matumizi.Mamlakayake Kisheria nikama yalivyo katika **Jedwali Na.2**hapa chini.

Jedwali 2: *Mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kisheria*

| Vigezo | Mamlaka |
|---|---|
| Ibara ya 143 (2) (C) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 | Inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kufanya ukaguzi na kutoa taarifa ya ukaguzi angalau mara moja kila mwaka kwa mujibu wa taarifa za fedha zilizoandaliwa na Maafisa Masuuli wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Taarifa za fedha za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na taarifa za fedha za Bunge. |
| Ibara ya 143 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na kila mtumishi wa Serikali aliyeruhusiwa na yeye atakuwa na haki ya kuchunguza vitabu, taarifa za akaunti, ripoti na hati nyinginezo zote zinazohusika na aina yoyote ya akaunti iliyotajwa katika ibara ndogo (2). |

| | |
|---|---|
| Kifungu Na. 10 (2) (a) chaSheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11, 2008 | Inamhitaji Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kujiridhisha kwamba taarifa za fedha zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya uhasibu vilivyokubalika kama inavyotakiwa na sheria husika. |
| Kifungu Na. 34 cha Sheria ya Ukaguzi ya Umma Na.11, 2008 na Kanuni. 88 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma, 2009 | ▪ vinahitaji Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu baada ya uchunguzi wa taarifa zote za fedha kuandaa na kuwasilisha Ripoti Jumuifu ya mwaka<br>▪ Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atawasilisha ripoti Jumuifu ya mwaka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ifikapo tarehe 31 Machi kila mwaka na taarifa hiyo kufikishwa na Waziri katika Bunge ndani ya siku saba ya kikao kijacho cha Bunge. |

*Chanzo:Katibaya Jamhuri ya Muunganoya 1977,Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008&Kanuni za Ukaguzi wa Ummaya mwaka 2009*

### 1.1.2 Umuhimu waUkaguzi

Sehemu hiiinatoamaelekezo yalengo la ukaguzi, madhumuni, mbinu, wigo/mawanda na viwango vya ukaguzi.

#### 1.1.2.1 Lengo la Ukaguzi

Lengo kuu lakufanya ukaguzini kumwezeshaMdhibiti na Mkaguzi Mkuukutoamaoni huru ya ukaguzikuhusiana nahesabu zaWizara,Idara, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Mapato TanzanianaHesabu Jumuifu za Taifakwamwaka ulioishia Juni 30, 2014.

Pia,kuthibitisha kamataarifa za fedhazimetayarishwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu katika sekta ya Umma visivyo vya msingi wa taslimu (IPSASaccrual basis of accounting).

#### 1.1.2.2 Mbinu za Ukaguzi

Ukaguzihuu ulijumuisha kupitia taarifa mbalimbali za uhasibu pamoja na taratibu nyingineili kukidhimalengo ya ukaguzi. Taratibu zilizotumika ni kama zinavyoonekana katika **KielelezoNa.1** hapo chini:

**Kielelezo 1: Mbinu za Ukaguzi**




*Chanzo: Taarifa za ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2013/14*

### 1.1.2.3 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi huu ulifanyika kwa kufanya tathminiya ufanisi wauhasibuna mifumo ya udhibitiwa ndani juu yashughuli mbalimbali zataasisi zaSerikali Kuu.Ukaguzi ulifanywakwa misingi yasampuli, Kwa hiyomatokeo ya ukaguzi huu kwa kiasi kikubwa yalitegemea kumbukumbu za taarifa nanyaraka tulizoomba na kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Kamamkaguzi, si jukumu langu la msingihasakutafutaudanganyifu namakosa, hivyo basi, ukaguziwangu hauwezikutegemewakufichuamambo yotehayo.Hata hivyoukaguzi wanguulipangwakwa njia ya kuwezakujiridhisha kwamba kama kungekua na makosamakubwa katika taarifa za fedhayanayotokana nakukiukwa kwa taratibuikiwa ni pamoja naudanganyifu ningeweza kuzibaini.Wajibuwa kuchunguza, kuzuia dosari nakuwekamfumothabiti waudhibiti wa ndanini jukumu la Menejimenti ya taasisi husika.

## 1.2 Viwango na taratibu zilizotumika kutoa taarifa

Sehemu hii inaeleza juu ya viwango na taratibu za ukaguzi zilizotumika wakati wa ukaguzi wa mwaka wa fedha 2013/14.

### 1.2.1 Viwango vilivyotumika wakati wa ukaguzi

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (INTOSAI), Shirika la Asasi Kuu za Ukaguzi Afrika(AFROSAI), na Shirika la Asasi Kuu za Ukaguzi Afrika –Nchi zinazozungumza Kiingereza (AFROSAI-E). Ushirikiano na taasisi nyingine kuu za Ukaguzi (SAI) imewezesha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) kuwa na eneo kubwa la kujifunza na kubadilishana uzoefu na utaalamu wa ukaguzi katika sekta ya umma.

Ukaguzi huu ulifanyika kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Asasi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs) viliyotolewa na Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (INTOSAI), ili kutoa uhakika kama taarifa za fedha ni sahihi na hazina makosa makubwa.

### 1.2.2 Taratibu zilizotumika kutoa taarifa

Ufanisi wa ukaguzi wangu hutegemea sana mawasiliano mazuri na menejimenti ya wakaguliwa. Mawasiliano ni muhimu katika mchakato mzima wa ukaguzi ambao unahusisha hatua zifuatazokwa muhtasari, **KielelezoNa.2**hapa chini kinaonyesha hatua ukaguzi zinazotumika katika ukaguzi wa Serikali Kuu.

**Kielelezo 2: Utaratibu Ukaguzi kwa mwaka 2013/14**




*Chanzo: Taarifa za ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2013/14*

## 1.3 Idadi yawakaguliwa

Sehemu hii ya ripotiinaelezaidadi yawakaguliwakwamwaka wa fedha ulioishia2013/14pamoja nampangilio wa Ofisi ya Ukaguzi ya Taifa.

### 1.3.1 Idadi yawakaguliwa

Katika kipindi cha mwaka2013/14, jumla yawakaguliwa176chini yaSerikali Kuuwalikaguliwa; wakaguliwahawa jumlayao na asilimia zao ni kama kwawanavyoonekana katika **Jedwali Na.3na kielelezoNa.3** hapa chini.

**Jedwali 3:** ***Idadi ya Wakugliwa***

| Muundo na Idadi ya Wakaguliwa kwa mwaka wa Fedha 2013/14 | | |
|---|---|---|
| | **Jumla** | **Asilimia** |
| Wizara & S/Mikoa | 87 | 39.7 |
| Balozi | 34 | 22.5 |
| Taasisi nyingine | 23 | 16.6 |
| Wakala | 32 | 21.2 |
| **Jumla** | **176** | **100** |

***Chanzo: Taarifa za ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2013/14***

**Jedwali Na.3**: hapo juu inayohusu muundo wawakaguliwakwa mwaka wa fedha2013/14 inaweza pia kuonekana kwa **Kielelezo Na.3** hapo chini.

**Kielelezo 3: Muundo wa Wakaguliwa**




***Chanzo: Taarifa za ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2013/14***

Pamoja na hayo, sikufanikiwa kufanya ukaguzi wa Wakala mbili za Serikali kwa sababu tofauti kama nilivyoainisha hapa chini.

- Mamlaka ya Usajili waBiashara na Leseni(BRELA)–Hesabu zake hazikuwasilishwa kwa sababu ya mataatizo katika mfumo wa uhasibu,(EPICOR).
- Shirika la Maendeleo laKigamboni(KDA) –Hesabu zake hazikuwasilishwa kwa sababu halijaanza utendaji tangu lilipoanzishwamwaka2012.

Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania(TFDA) –Hesabu zake zimekamilika na kukaguliwa na taarifa yake imejumuishwa katikaRipoti ya mwaka ya Mashirika ya Ummana Taasisinyingine kwa mwaka2013/14.

### 1.3.2 Mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Ofisi ya Taifa ya Ukaguziinafanya kazi zake za ukaguzi kwa mpangilio watimuza ukaguzizinazoongozwa naviongozi wa timuna kusimamiwa naMkaguzi Mkuuwa njewa Hesabu (CEA) ambaye anatoa taarifa kwaMsaidizi wa MkaguziMkuu(AAGs). Imekuwamuhimukuwagawanya wakaguliwawetu katikamaeneomadogoyanayoitwaSektayanaongozwa naMsaidizi wa MkaguziMkuu (AAGs)ambaye anatoa taarifa kwaNaibuMkaguziMkuu (DAGs), ambaye anatoa taarifa moja kwa moja kwaMdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Dondoo yampangilio wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Serikali Kuu ni kama inavyoonekanakatika **KielelezoNo.4**hapa chini:

**Kielelezo 4: Dondoo ya mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Serikali Kuu kwa mwaka ulioshia 2013/14**




## 1.4 Majukumu yakisheriaya Asasi zinazokaguliwa

Majukumuya kisheria yaasasi inayokaguliwakatika maandaliziya taarifa ya fedhana kuwasilishataarifa hizo yanaweza kufafanuliwakwa msaada wa**KielelezoNa.5** hapa chini.

**Kielelezo 5: Majukumu ya kisheria ya wakaguliwa**




***Chanzo***: *Sheria ya fedha ya Umma Na.6,2001 na Kanuni zake za Mwaka 2009, Waraka wa Kihasibu Na.11 wa mwaka 2012/13*

## 1.5 Taarifa za Fedha

Taarifa kamili za fedha zinazoandaliwa kwa mujibu wa viwango vya Kimataifa vya Uhasibu wa Sekta ya Umma kwa misingi ya fedha isiyo taslimu inajumuisha taarifa zifuatazo:

i. Mizania ya Hesabu;
ii. Taarifa ya mapato na matumizi/ Taarifa ya ufanisi wa fedha;
iii. Taarifa yamabadiliko ya mtaji;
iv. Taarifa ya mtiririko wa fedha;
v. Taarifa ya uwiano wabajeti nakiasi halisi cha matumizina
*vi.* Sera zaUhasibu namaelezo yataarifa za fedha.

## SURA YA PILI

## HATI ZA UKAGUZI

### 2.0 Utangulizi

Ni wajibu wangu kikatiba kutoa uhakika kwa wadau wa taasisi zilizo chini ya Serikali Kuu kama taarifa zao za fedha zimeandaliwa kwa kufuata viwango vya kimataifa vya uandaaji wa taarifa za fedha za umma kuhusu mizania ya hesabu ya taasisi husika katika tarehe husika, hali ya fedha na mtiririko wake katika kipindi kinachohusika.

### 2.1 Maana ya hati ya ukaguzi

Hati ya ukaguzi inatoa maoni ya kama taarifa za fedha zimeandaliwa, zimezingatia masuala yote muhimu, kulingana na mifumo inayokubalika ya uandaaji wa taarifa za fedha. Maoni hayo ya ukaguzi ni lazima yaoneshe kama taarifa husika za fedha zimetoa ufafanuzi wa kutosha kumwezesha mtumiaji wa taarifa hizo kuzielewa ama la.

Maoni ya mkaguzi katika taarifa za fedha:

- Yanasaidia kuzifanya taarifa za fedha kuaminika zaidi;**hata hivyo**
- Hayatoi uhakika wa kufanikiwa kwa taasisi siku za usoni, na
- Hayatoi dhamana kwamba taasisi iko huru dhidi ya ubadhilifu.

### 2.2 Aina za hati za ukaguzi

Kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Taasisi za Umma (ISSAIs), **JedwaliNa.4**lifuatalo linafafanua aina za hati za ukaguzi.

## Jedwali 4: *A*ina za hati za ukaguzi

| Hati ya ukaguzi | Mazingira inayotolewa | Hali halisi kwa mwaka 2013/14 |
|---|---|---|
| Hati inayoridhisha *(ISSAI 1700.16)* | Taarifa za fedha zimeandaliwa kwa kuhusisha masuala yote muhimu, kulingana na mifumo ya uandaaji wa taarifa za fedha iliyokubalika kimataifa. | Jumla ya taasisi 166 sawa na asilimia 94 zimepata hati inayoridhisha; angalia **Jedwali Na.6Kiambatisho 1-4** |
| Hati yenye shaka *(ISSAI 1705.7)* | Taarifa za hesabu zilizoandaliwa zinaonyesha kukwazwa kwa mawanda ya ukaguzi kunakotokana aidha na uongozi wa taasisi husika au na hali ambayo ipo nje ya uwezo wa mkaguzi na endapo kukwazwa huko kuna madhara makubwa lakini sio muhimu; au kuna kiasi kikubwa cha kutokukubaliana na uongozi wa taasisi kaguliwa aidha kutokana na kuwa na taarifa ambazo hazijitoshelezi kwenye taarifa za fedha au kurekodi vitu kwenye taarifa za fedha kinyume na inavyotakiwa. | Jumla ya taasisi 9 sawa na asilimia 5 zimepata Hati yenye shaka; angalia J**edwali Na.6Kiambatisho1-4** |
| Hati isiyoridhisha *(ISSAI 1705.8)* | Hati hii inatolewa pale ambapo mkaguzi amejiridhisha kuwa, taarifa zilizoandaliwa na kukaguliwa zina makosa makubwa na yenye athari kubwa, likiangaliwa kosa moja moja au kwa ujumla wake. Makosa hayo yanaweza yakawa yametokea kutokana na; kutokukubaliana na uongozi wa taasisi husika aidha kwa kuwa na taarifa ambazo hazijitoshelezi kwenye hesabu au kurekodi vitu kwenye taarifa za fedha kinyume na inavyotakiwa. Kutokukubaliana huko kunapelekea taarifa za fedha kupoteza uhalisia wake na hivyo kutoaminiwa kwa ujumla wake. Kwa hali hiyo mkaguzi anahitimisha kuwa taarifa zilizoandaliwa hazionyeshi hali halisi ya shughuli zilizofanywa na hivyo hazikuzingatiwa viwango vya kimataifa vya uandaaji wa taarifa hizo. | hati ya ukaguzi isiyoridhisha ilitolewa kwa Hesabu Jumuifu za Taifa |
| Aya ya Hati mbaya *(ISSAI 1705.9;10)* | Hati mbaya hutolewa pale ambapo mkaguzi ameshindwa kupata nyaraka za kutosha wakati wa ukaguzi ili kuweza kutoa hati sahihi na kujidhihirisha kuwa, madhara yanayoweza kutokea kutokana na mapungufu ambayo hajaweza kuyagundua yanaweza yakawa makubwa na ya muhimu sana. Katika hali hii mkaguzi anakataa kutoa hati ya ukaguzi. | Hakuna taasisi iliyopata hati mbaya. |

Chanzo: *ISSAI &Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2013/2014*

## 2.3 Aya yenye masuala ya msisitizo na aya yenye masuala mengine

Aya yenye masuala msisitizo pamoja na aya yenye masuala mengine, kama ilivyo kwenye **Jedwali Na.5**Nimeweka aya ya mausala ya msisitizo kwenye ripoti zangu kwa wakaguliwa ili kuwaeleza masuala ambayo, ingawaje yameripotiwa sahihi kabisa kwenye taarifa za fedhani ya muhimu sana na ni ya msingi kwa watumiaji kutoa maelezo zaidi waweze kuzielewa taarifa hizo.

**Jedwali 5: Aya yenye masuala ya msisitizo na aya yenye masuala mengine**

| Aya yenye masuala ya msisitizo | Aya yenye masuala mengine |
|---|---|
| • Uwalakini kutokana na madai ya kisheria ambapo haijulikani matokeo ya madai hayo yanaweza kuathiri hesabu za mwisho<br>• Pale ambapo kuna kiasi kikubwa cha kutooana au kuchanganyana kati ya yaliyomo kwenye ripoti ya mwaka ya wakaguliwa na taarifa za fedha, au kati ya ufafanuzi uliopo kwenye taarifa za fedha na taarifa zenyewe za fedha ambapo yalihitaji kurekebishwa lakini uongozi wa taasisi husika haukufanya hivyo.<br>• Masuala muhimu yalioneshwa kwenye taarifa za fedha na muhimu sana kwa watumiaji wa taarifa katika kuelewa hesabu hizo | • Endapo kumegundulika kiasi kikubwa cha udanganyifu kwenye taarifa nyingine za mwaka (other information in the annual report) ambapo ilihitaji kurekebishwa lakini uongozi wa taasisi husika haukufanya hivyo.<br>• Masuala yanayohusiana na kutokuwepo na; kamati makini na zenye ufanisi za ukaguzi au kamati hizo kutokuwepo kabisa, vitengo vya ukaguzi wa ndani kutokidhi haja au kutokuwepo kabisa na kutokuwepo vitengo vya manunuzi makini na vyenye ufanisi,<br>• Hali ya kutozingatia sheria na kanuni ambazo zimeleta athari ndogo |

Chanzo: *Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs)*

Katika mwaka huu wa ukaguzi,jumla ya taasisi 29 ilipata hati safi zenye maswala msisitizo au maswala mengine. Kama ilivyo kwenye **Jedwali Na. 6 na Viambatanisho Na. 1-4**

## 2.4 Mchanganuo wa hati za ukaguzi kwa Serikali Kuu kwa mwaka 2013-14

Hati za ukaguzi zilizotolewa kwa mwaka 2013-14 kwa upande wa Serikali kuu ni kama unavyoainishwa katika **Jedwali Na. 6**hapa chini:

**Jedwali 6:** ***Mchanganuo wa hati za ukaguzi-2013/14***

| | Hati | inayoridhisha | | Hati yenye Shaka | | Hati isiyoridhisha | | Hati mbaya | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Jumla | % | Jumla | % | Jumla | % | Jumla | % | |
| Idara | Wizara & S/Mikoa | 79 | 91% | 7 | 8% | 1 | 1% | 0 | 0% | 87 |
| | Balozi | 34 | 100% | 0 | 0% | 0 | 0% | 0 | 0% | 34 |
| | Taasisi zingine | 21 | 91% | 2 | 9% | 0 | 0% | 0 | 0% | 23 |
| | Wakala | 32 | 100% | 0 | 0% | 0 | 0% | 0 | 0% | 32 |
| | **Jumla** | 166 | 94% | 9 | 5% | 1 | 1% | 0 | 0% | 176 |

**Chanzo:***Taarifa za mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali-2013/14*

Mchanganuo wa hati za ukaguzi za taasisi za Serikali kuu kwa mwaka 2013/14 ulioneshwa kwenye **Jedwali Na.6** unafafanuliwa zaidi na **Kielelezo Na.6** hapa chini:

**Kielelezo 6: mchanganuo wa hati zilizotolewa na aina zakekwa mwaka wa fedha-2013/14**




Chanzo: *Taarifa za mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali-2013/14*

**Kielelezo No.6** hapo juu kinaonesha kwamba, kwa mwaka 2013/14, Taasisi za Serikali Kuu zimeboresha uandaaji na uwasilishaji wa taarifa zao za fedha. Bado ipo fursa ya kuimarisha namna ya uandaaji na uwasilishaji taarifa za fedha kwa mujibu wa miongozo na viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha.

Mchanganuo zaidi wa hati za ukaguzi za taasisi za Serikali kuu kwa mwaka 2013/14 (kwa makundi) ulioneshwa kwenye **Jedwali Na.6** unafafanuliwa na **Kielelezo Na.7** hapa chini;

**Kielelezo 7: Inaonesha mlinganisho (Kwa taasisi) wa Hati za ukaguzi zilizotolewa kwa mwaka wa fedha- 2013/14**




**Chanzo:** *Taarifa za mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali-2013/14*

Katika **Kielelezo No. 7** hapo juu kinaonesha kwamba, balozi na wakala wa serikali zinaongoza katika uandaaji na kuwasilishwa taarifa za fedha kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya uandaaji wa taarifa za fedha ikifuatiwa na Wizara na taasisi nyingine.

## 2.5 Vigezo vya hati yenye shaka

Kulingana na jedwali Na. 6 hapo juu,kulikuwa na Taasisi tisa (9) zilizopata hati yenye shaka. Taasisi hisi ni pamoja na Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera, Geita, Iringa, Mwanza, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Mambo ya Ndani, Idara ya Deni la Taifa, Chuo cha Wanyamapori Pasiansi na Baraza la Famasia

Tanzania. Orodha ya Taasisi hizi pamoja na vigezo vya hati yenye shaka viko **kiambatisho Na. 27.** Pia hesabu jumuifu za Taifa zilipata hati isiyoridhisha kutokana na vigezo vifuatavyo:

- Taarifa za Hesabu za Majumuisho kwa kipindi kilichoishia 30 Juni, 2014, zimejumuisha taasisi za umma zenye vipindi tofauti vya ufungaji wa hesabu na kile cha serikali kinyume na Kanuni ya 6 ya IPSAS, Aya ya 47.
- Taasisi nyingi za umma zimekuwa zikitumia kanuni mbalimbali za uhasibu kwenye kuwasilisha hesabu. Wakati Serikali Kuu, ambaye ndie mmiliki wa taasisi hizo imekuwa ikitumia Kanuni za Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS Accrual basis of accounting) inapoandaa hesabu zake, bado baadhi ya taasisi kama vile Shirika la Magazeti Tanzania (TSN), Benki ya Posta, Mamlaka ya Bandari na nyinginezo zimekuwa zikitumia kanuni za IFRS kwenye kuwasilisha taarifa zao.
- Mapitio ya Hesabu za Majumuisho ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yamebaini kwamba kuna taasisi za umma ambazo hazikujumuishwa. Taasisi ambazo hazikujumuishwa ni Unit Trust of Tanzania (UTT), Suma JKT, Tanzania Nurses and Midwife Council (TNMC), na Mamlaka ya Usajili wa Leseni za Biashara (BRELA). Kutokuwepo kwa taasisi hizi za umma kwenye hesabu za majumuisho kunaharibu uwasilishwaji wa uhalisia wa taarifa za hesabu.

Kwa ujumla, mwaka huu kuna ongezeko kubwa la hati zinazo ridhisha ukilinganisha na miaka iliyopita. Taasisi zilizopata hati inayoridhisha zimeongezeka kutoka 73% mwaka jana hadi 94%. Taasisi zilizopata hati yenye shaka zimepungua kutoka asilimia 26%hadi asilimia 5%.

## 2.6Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa miaka mitano iliyopita (2009/10 - 2013/14)

Mwenendo wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2009/10 hadi mwaka wa fedha 2014/15 kwenye taasisi za Serikali Kuu zinaweza kuchambuliwa kama zinavyoonekana katika **Kielelezo Na8**

Kielelezo 8: Mwenendo wa Hati za ukaguzi zilizotolewa kwa miaka mitano iliyopita

| | | 2009/10 | | | | | 2010/11 | | | | | 2011/12 | | | | | 2012/13 | | | | | 2013/14 | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati isiyoridhisha | Hati Mbaya | Jumla | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati isiyoridhisha | Hati Mbaya | Jumla | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati isiyoridhisha | Hati Mbaya | Jumla | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati isiyoridhisha | Hati Mbaya | Jumla | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati isiyoridhisha | Hati Mbaya | Jumla |
| Hati za Ukaguzi | Wizara & S/Mikoa | 49 | 19 | 2 | 1 | 71 | 67 | 8 | 0 | 0 | 75 | 73 | 3 | 0 | 0 | 76 | 56 | 28 | 0 | 1 | 85 | 79 | 7 | 1 | 0 | 87 |
| | Balozi | 29 | 2 | 0 | 0 | 31 | 32 | 0 | 0 | 0 | 32 | 30 | 2 | 0 | 0 | 32 | 29 | 2 | 1 | 0 | 32 | 34 | 0 | 0 | 0 | 34 |
| | Taasisi zingine | 0 | - | - | - | 0 | 0 | - | - | - | 0 | 0 | - | - | - | 0 | 0 | - | - | - | 0 | 21 | 2 | 0 | 0 | 23 |
| | Wakala | 0 | - | - | - | 0 | 0 | - | - | - | 0 | 0 | - | - | - | 0 | 0 | - | - | - | 0 | 32 | 0 | 0 | 0 | 32 |
| | Jumla | 78 | 21 | 2 | 1 | 102 | 99 | 8 | 0 | 0 | 107 | 103 | 5 | 0 | 0 | 108 | 85 | 30 | 1 | 1 | 117 | 166 | 9 | 1 | 0 | 176 |
| % | Wizara & S/Mikoa | 69% | 27% | 3% | 1% | 100% | 89% | 11% | 0% | 0% | 100% | 96% | 4% | 0% | 0% | 100% | 66% | 33% | 0% | 1% | 100% | 91% | 8% | 1% | 0% | 100% |
| | Balozi | 94% | 6% | 0% | 0% | 100% | 100% | 0% | 0% | 0% | 100% | 94% | 6% | 0% | 0% | 100% | 91% | 6% | 3% | 0% | 100% | 100% | 0% | 0% | 0% | 100% |
| | Taasisi zingine | - | - | - | - | - | 0% | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | 91% | 9% | 0% | 0% | 100% |
| | Wakala | - | - | - | - | - | 0% | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | 100% | 0% | 0% | 0% | 100% |
| | Jumla | 76% | 21% | 2% | 1% | 100% | 93% | 7% | 0% | 0% | 100% | 95% | 5% | 0% | 0% | 100% | 73% | 26% | 1% | 1% | 100% | 94% | 5% | 1% | 0% | 100% |

**Chanzo:** *Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesbu za Serikali kwa miaka 2009/10, 2010/11, 2011/12, 2012/13 & 2013/14*

Uchambuzi wa mwenendo wa hati za ukaguzi kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2009/10 hadi 2014/15 zinaweza kutolewa kwa kutumia **kielelezo Na.9** pamoja na mwelekeo wa mwenendo kama inavyokana hapa chini.

Kielelezo 9: Chati inayoonesha Mwenendo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa miaka mitano iliyopita




***Chanzo:** Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesbu za Serikali kwa miaka 2009/10, 2010/11, 2011/12, 2012/13 & 2013/14*

Uchambuzi kama unavyoonekana katika jedwali Na.6, na mwelekeo wa mwenendo katika Kielelezo Na.8 hapo juu inaonesha kwamba:

a) **Hati Safi**: kuna uhusiano na mwenendo chanya kati ya hati safi zilizotolewa na idadi ya miaka ya fedha kuanzia mwaka 2009/10 hadi 2013/14. Hii ina maana kwamba, idadi ya Hati Safi katika Serikali Kuu inaongezeka kadri miaka inavyoongezeka.

b) **Hati yenye Shaka:** Kwa mwaka 2013/14 Hati zenye shaka zimepungua kutoka 30 hadi 9 ikilinganishwa na idadi ya Hati zenye shaka zilizotolewa katika kipindi cha mwaka 2012/13.

Kwa ujumla, kutokana na uchambuzi hapo juu mwenendo wa hati za ukaguzi kwa kipindi cha miaka mitano, inaweza kuonekana kuwa, kuna mafanikio katika kuandaa hesabu kwa taasisi za Serikali Kuu ambazo zipo katika kipindi cha mpito cha utekelezaji wa maandalizi ya hesabu kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma visivyo vya misingi ya Taslimu (IPSAS accrual basis of accounting)

# SURA YA TATU

# UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA

## 3.0 Utangulizi

Surahii inatoamatokeoya tathminijuuya utekelezajiwa mapendekezoyaliyotolewa kwa miaka ya nyuma kwa kila fungu na ripoti ya jumla ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Piaufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC).

Inatoa Muhtasari wa maoni ya Ukaguzi pamoja na tathmini ya hatua za utekelezaji za Wizara, Idara, Wakala na Sektretarieti za Mikoa zilizofanywa katika kutekeleza maoni yangu.

## 3.1 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kila fungu

Ufuatiliaji ulifanywa kutathmini hali ya wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa ripoti ya kila fungu umeonyesha kuwa Wizara, Wakala na Idara 30, Balozi 23 na Sekretarieti za Mikoa 23 zina hoja ambazo hazijajibiwa na zile ambazo zimejibiwa bila kukamilika ni TZS 1,292,399,778,599JP¥17,089,499,858, £79,568, €221,968 and US$ 57,662,248 Orodha kamili inayoonyesha kiasi halisi katika kila fungu imeambatanishwaa katika **Kiambatisho Na. 5** cha ripoti hii.

Mchanganuo unaonesha kuwa Wizara na Idara 89 na Sekretarieti za Mikoa 25zilikuwa na jumla ya mapendekezo 2,228 kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo zilihitaji utekelezaji kutoka kwa Maafisa Masuuli.Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ni kama ilivyoelezwa katika **Kielelezo Na. 9:**

Kielelezo 10: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa Miaka iliyopita




***Chanzo: taarifa kwa menejimenti za wizara, Idara, Balozi na Sekretarieti za Mikoa kwa mwaka 2013/2014***

Kwa ujumla, utekelezaji wa maoni ya ukaguzi umekuwa wa kasi ndogo na uliokosa mikakati mizuri ya utekelezaji. Ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa mali za umma, nashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha wanatekeleza mapendekezo ya ukaguzi kwa wakati ili kupunguza kujirudia rudia kwa hoja za ukaguzi.Maafisa Masuuli waandae mpango kazi wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi pamoja na majibu ya hoja za ukaguzi ndani ya siku 21 toka siku ambayo ripoti jumuifu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ilipowasilishwa bungeni na kuwasilishwa kwa Mlipaji Mkuu wa serikali na nakala kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

## 3.2 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa ripoti jumuifu

Majibu ya serikali kwa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwenye ripoti ya jumla ya mwaka 2012/2013 yaliwasilishwa kwa

mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kupitia barua yenye kumbukumbu namba C/DE.85/229/01/72 ya tarehe 30 Agosti, 2014.Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 inahitaji Mlipaji Mkuu wa Serikali kuwasilisha nakala ya majibu jumuifu ya serikali na mpango kazi wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali katika ripoti ya jumla ya mwaka wa fedha 2012/2013 alitoa mapendekezo ya ukaguzi 22 kwa serikali.katika mwaka huu, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ametoamapendekezo ya ukaguzi 28 kwa serikali, ikiwa ni ongezeko la mapendekezo sita ukilinganisha na mwaka uliopita.
Utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoka kwa Serikali ni kama inavyoonekana kwenye **Kiambatanisho Na. 6** cha ripoti hii.

## 3.3 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC)

Kifungu cha 40 cha sheria ya ukaguzi wa umma na. 11 ya mwaka 2008 inahitaji Mlipaji Mkuu wa Serikali na Maafisa Masuhuli kuzingatia hoja na mapendekezo ya Kamati ya kudumu ya bunge ya hesabu za serikali wakati wa kutoa majibu kwa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali aliwasilisha hoja na mapendekezo ya kamati kwa taarifa za fedha za serikali kuu kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2013 bungeni mwezi Januari, 2015na serikali kutoa majibu tarehe 28 Januari, 2015. Utekelezaji wa mapendekezo ya kamati ya kudumu ya bunge ya hesabu za serikali ni kama inavyoonekana kwenye **kiambatanisho 7** cha ripoti hii.

Natambua mchango wa kamati ya kudumu ya bunge ya hesabu za serikali, kwa hatua ambazo imekuwa ikizichukua hususan kwa mapendekezo niliyokuwa nikitoa katika ripoti zangu, kwa jinsi hiyo nimeweza kutekeleza majukumu yangu ya kisheria na kwa ufanisi.

Ni muhimu mambo yote yaliyoibuliwa pamoja na mapendekezo yaliyotolewa na kamati ya kudumu ya bunge ya hesabu za serikali yakatekelezwa kwa umakini kwa kuwekwa katika mpango kazi unaotekelezeka.

Kwa kutekeleza mapendekezo ya kamati ya kudumu ya bunge ya hesabu, serikali itakuwa kwenye nafasi ya kuongeza ukusanyaji wa mapato, kudhibiti bajeti na matumizi, hivyo kuleta uwajibikaji katika rasilimali za taifa.

# SURA YA NNE

# MAKUSANYO YA MADUHULI NA MCHANGANUO WA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO

## 4.0 Utangulizi

Sehemu hiiinaeleza juu ya mtazamo mzima wa bajeti ya nchi kwa ujumla na vyanzo vyafedha za bajetiikilinganishwa navyanzovilivyoidhinishwa vya mapato, fedha zilizotolewa zamatumizi ya kawaida namatumizi ya maendeleo na fedha za mpango wa bakizo kwa mwaka 2013/14.

## 4.1 Ukusanyaji wa maduhuli na mchanganuo wa matumizi

Makisio ya mapato na matumizi ya Serikali huidhinishwa kwa misingi ya fedha taslimuna hutumika kwa mwaka wa fedhakuanzia tarehe 1 Julaihadi 30 Juni.Bajetiiliyoidhinishwa na Bungehujumuisha shughuli zotendani yaSerikali yaJamhuri ya Muungano waTanzania.Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha2013/2014ilikuwaSh.18,248.98 bilioni.

## 4.2 Masuala muhimu niliyobainisha kuhusiana na Usimamizi wa Fedha za Umma

Sehemu hii ya ripotiinatoakwa muhtasarimatokeo ya ukaguziwa ukusanyaji wa mapatona fedha nyingine zilizogharamia matumizi katika bajeti,utekelezaji wa bajeti,fedha zilizotolewa nakiasikilichotumikwa kwa Serikali Kuu kwa mwaka2013/14.

### 4.2.1 Maelezo ya jumla yaukusanyaji wa mapatoya utendaji

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 jumla ya makisio ya mapato ya Serikali yalifikia kiasi cha Sh.18,248.98 bilioni ikijumuisha matumizi ya kawaida Sh.12,574.95 bilioni na Sh.5,674.03 bilioni kwa ya ajili ya matumizi ya Maendeleo.

Vyanzo vya mapato ya kugharamia bajeti hiyo ni pamoja na Kodi ya mapato, Mapato yasiyo ya Kodi, Fedha za gawio kutoka kwa

wawekezaji (Finance Income), mikopo ya ndani na nje na fedha za Misaada toka kwa wahisani.

Jumla ya mapato halisi ya makusanyo kutoka vyanzo mbalimbali yalifikia kiasi cha TZS.16,304.29 bilioni hivyo, kushindwa kufikia lengo la ukusanyaji kwa jumla ya TZS.1,583.54 bilioni sawa na asilimia 8.85 bila kujumuishwa kwa mapato kutoka vyanzo vya Serikali za Mitaa.

Kati ya mapato yote yaliyokusanywa kiasi cha TZS.12,491.66 bilioni kilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kiasi cha TZS.3,578.67 bilioni kwa Matumizi ya maendeleo. Hata hivyo, kiasi cha TZS.4,747.66 bilioni kilitolewa katika robo ya nne ya mwaka. Fedha hizi ziligawiwa kwa Wizara ,Idara, na wakala za Serikali, kiasi cha TZS.3,928.84 bilioni, Sekretarieti za Mikoa TZS.43.996 bilioni na Serikali za Mitaa zilipata TZS.774.82 bilioni.

Katika mwaka wa fedha 2013/2014 mapato halisi yaliyokusanywa kutokanana kodi yalikuwa TZS.9,289 bilioni (ikiwa ni asilimia 89) ikilinganishwa na lengo la TZS.10,412.94 bilioni, hivyo kutofikia lengo kwa kiasi cha TZS.1,123.94 bilioni  sawa na asilimia 11 ya Makisio idhinishwa.

Mapato yasiyotokana na kodi,zilikusanywa jumla ya TZS.532 bilioni (83%) ikilinganishwa na lengo la TZS.639.68 bilioni hivyo kushindwa kufikia lengo kwa kiasi cha TZS.107 bilioni sawa na asilimia 17 ya Makisioyaliyoidhinishwa.

Mapato halisi kutoka fedha za gawio (Finance Income)zilikuwa TZS.108.71 bilioni (88%) ikilinganishwana lengo la TZS.123.75bilioni, ambapo kiasi cha TZS.15.04 bilioni sawa na asilimia 12 ya Makisio hakikupokelewa.

Mikopo ya ndani ilikuwa TZS.3,289.41 bilioni dhidi Makisioidhinishwa ya TZS.1,699.86 bilioni hivyo kukopa zaidi kwa

kiasi cha TZS.1,589.55 bilioni sawa na asilimia 94zaidi ya Makisio ya yaliyopitishwa.

Mikopo ya Nje na Msaada ya wahisani katika 2013/14 jumla ya TZS.3,084.93 bilioni zilipatikana dhidi ya Makisioyaliyoidhinishwa ya TZS.5,011.6bilioni. Misaada kutoka nje kiasi cha TZS.1,926.67 bilioni ambayo ni asilimia 38 ya Makisioyaliyopitishwa hayakupokelewa.Mwenendo waukusanyaji wa mapatokwa miaka mitatu mfululizokwa muhtasari nikamaunavyoonekana katika**Jedwali Na.7**hapo chini.

Jedwali 7: *Muhtasari wa mwenendo wa bajeti kwa miaka mitatu(Kiasi katikaBilioniTZS)*

| **2013/2014** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Aina ya mapato** | Makisio yaliyoidhinishwa TZS | Mapato Halisi TZS | Tofauti (Pungufu)/Zaidi | Asilimia ya kutofikia lengo (%) |
| Mapato ya ndani (Kodi) | 10,412.94 | 9,289.00 | (1,123.94) | (10.79) |
| Mapato ya vyanzo visivyotokana na Kodi | 639.68 | 532.24 | (107.44) | (16.80) |
| Mapato yatokanayo na gawio (Finance Income) | 123.75 | 108.71 | (15.04) | (12.15) |
| Mikopo ya Ndani | 1,699.86 | 3,289.41 | 1,589.55 | 93.51 |
| Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani | 5,011.60 | 3,084.93 | (1,926.67) | (38.44) |
| **Jumla** | **17,887.83** | **16,304.29** | **(1,583.54)** | **(8.85)** |
| **2012/2013** | | | | |
| **Aina ya Mapato** | Makisio yaliyoidhinishwa TZS | Mapato Halisi TZS | Tofauti (Pungufu)/Zaidi | Asilimia ya kutofikia lengo (%) |
| Mapato ya ndani (Kodi) | 8,432.29 | 8,052.29 | (380.01) | (4.51) |
| Mapato ya vyanzo visivyotokana na Kodi | 644.58 | 419.56 | (225.02) | (34.91) |
| Mapato yatokanayo na gawio (Finance Income) | 72.26 | 61.59 | (10.66) | (14.76) |
| Mikopo ya Ndani | 1,632.00 | 2,492.71 | 860.71 | 52.74 |
| Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani | 4,410.81 | 3,992.17 | (418.64) | (9.49) |
| **Jumla** | **15,191.94** | **15,018.33** | **(173.62)** | **(1.14)** |
| **2011/2012** | | | | |
| **Aina ya Mapato** | Makisio yaliyoidhinishwa TZS | Mapato Halisi TZS | Tofauti (Pungufu)/Zaidi | Asilimia ya kutofikia lengo (%) |
| Mapato ya ndani (Kodi) | 6,229 | 6,415 | 186 | 2.99 |
| Mapato ya vyanzo visivyotokana na Kodi | 693 | 720 | 27 | 3.93 |
| Mapato yatokanayo na gawio (Finance Income) | 205 | 208 | 3 | 1.59 |
| Mikopo ya Ndani | 1,204 | 1,639 | 435 | 36.13 |
| Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani | 5,195 | 3,168 | (2,027) | (39.02) |
| **Jumla** | **13,526** | **12,150** | **(1,375)** | **(10.17)** |

*Vyanzo:Taarifa ya ukaguzi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania,taarifa ya ukaguzi ya Deni la Taifa, Taarifa ya ukaguzi yaWizara yafedhaza2013/2014na Taarifa ya jumla ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali yamwaka 2012/2013.*

Mwenendo wa makisio ya mapato yatokanayo na kodi katika mwaka wa fedha 2013/2014 yameongezeka kwa asilimia 24 na ikilinganishwa na asilimia 67 ya makisio katika mwaka wa fedha 2012/2013 na 2011/2012 kwa mtiririko huo, Hata hivyo kumekuwako na ongezeko katika ukusanyaji wa mapato halisi kwa asilimia 15 na asilimia 45 ikilinganishwa na mapato yaliyokusanywa katika mwaka wa fedha 2012/2013 na 2011/2012 kwa mtiririko huo.

Katika mwaka wa fedha 2013/2014 makisio ya mapato yasiyotokana na kodi yalipungua kwa asilimia 0.8 na asilimia 8 ikilinganishwa na Makisio ya mwaka wa fedha 2012/2013 na 2011/2012 kwa mtiririko huo. Hata hivyo, makusanyo halisi ya mapato yasiyo ya kodi yaliongezeka kwa asilimia 27 na yalipungua kwa asilimia 26 ikilinganishwa na makusanyo halisi katika mwaka wa fedha 2012/2013 na 2011/2012 kwa mtiririko huo.

Makisio ya mapato yatokanayo na Fedha za gawio (Finance Income) katika mwaka wa fedha 2013/2014 yaliongezeka kwa asilimia 71 na kupungua kwa asilimia 40 yakilinganishwa na Makisio yaliyopitishwa katika mwaka wa fedha 2012/2013 na 2011/2012 kwa mtiririko huo. Mapato ya fedha halisi yaliongezeka kwa asilimia 77 na kupungua kwa asilimia 48 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2012/2013 na 2011/2012 kwa mtiririko huo.

Fedha halisi kutoka katika mikopo ya ndani iliongezeka kwa asilimia 32, huku mikopo ya nje na misaada ya wahisani ikipungua kwa asilimia 23 katika mwaka wa fedha 2013/2014 wakati ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2012/2013.

Pamoja na ukweli kwamba, Makisio ya mapato yaliongezeka na mapato halisi kuongezeka kwa mwaka wa fedha 2013/2014, ufanisi katika utelekezaji wa bajeti haukuwa nzuri kwani malengo mengi hayakufikiwa hasa katika ukusanyaji wa mapato ya ndani. Kwa maana ya mapato yatokanayo na kodi na yale yasiyotokana na kodi.

Mapato yatokanayo na Fedha za gawio na yale yasiyotokana na Kodi yamekua yakipanda na kushuka mwaka hadi mwaka. Kutotimiza malengo katika ukusanyaji wa mapato inaathiri utekelezaji wa bajeti. Mwenedo wa bajeti unaoonesha kupanda na kushuka kwa makisio na mapato ni kama unavyookana katika **Jedwali Na.8**hapo chini

Jedwali 8: Inaonyeshauchambuzi wa bajeti(Kiasi katikaBilioniTZS)

| Aina ya Mapato | Makisio yaliyoidhishwa TZS 2013/14 (A) | 2012/13 (B) | 2011/12 (C) | D Tofauti (A - B) | E Tofauti (A - C) | % D | % E |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mapato ya ndani (Kodi) | 10,412.94 | 8,432.29 | 6,228.84 | 1,980.65 | 4,184.10 | 23.49 | 67.17 |
| Mapato kutoka vyanzo visivyotokana na Kodi | 639.68 | 644.58 | 692.74 | (4.90) | (53.06) | -0.76 | -7.66 |
| Mapato yatokanayo na gawio (Finance Income) | 123.75 | 72.26 | 204.87 | 51.49 | (81.13) | 71.26 | -39.60 |
| Mikopo ya Ndani | 1,699.86 | 1,632.00 | 1,204.26 | 67.86 | 495.60 | 4.16 | 41.15 |
| Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani | 5,011.60 | 4,410.81 | 5,195.18 | 600.79 | (183.58) | 13.62 | -3.53 |
| **Jumla ya Makisio** | **17,887.83** | **15,191.94** | **13,525.90** | **2,696** | **4,362** | | |
| **Aina ya Mapato** | **Mapato Halisi TZS 2013/14** | **2012/13** | **2011/12** | **D Tofauti (A - B)** | **E Tofauti (A - C)** | **% D** | **% E** |
| Mapato ya ndani (Kodi) | 9,289 | 8,052 | 6,415 | 1,237 | 2,874 | 15.36 | 44.81 |
| Mapato ya vyanzo visivyotokana na Kodi | 532 | 420 | 720 | 113 | (188) | 26.86 | -26.07 |
| Mapato yatokanayo na gawio (Finance Income) | 109 | 62 | 208 | 47 | (99) | 76.50 | -47.77 |
| Mikopo ya Ndani | 3,289 | 2,493 | 1,639 | 797 | 1,650 | 31.96 | 100.65 |
| Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani | 3,085 | 3,992 | 3,168 | (907) | (83) | -22.73 | -2.63 |
| **Jumla ya Mapato** | **16,304** | **15,018** | **12,150** | **1,286** | **4,154** | | |

*Vyanzo:Taarifa ya ukaguzi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania,taarifa ya ukaguzi ya Deni la Taifa, Taarifa ya ukaguzi yaWizara yafedhaza2013/2014na Taarifa ya jumla ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali yamwaka 2012/2013.*

### 4.2.2Uwiano wa fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa kwa Wizara, idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa dhidi ya bajeti iliyoidhinishwa.

Makisio ya matumizi ya kawaida yaliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kwa Wizara, Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa yalikuwa TZS.9,959.81 bilioni ambayo inaonyesha ongezeko la TZS.1,359.93 bilioni sawa na asilimia 16 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2012/2013 ya TZS.8,599.88 bilioni.

Mapitio ya hesabu za Wizara na Sekretarieti za Mikoa zilibainisha kuwa TZS.9,559.55 kilipokelewa kama matumizi ya kawaida ikiwa ni asilimia 96 ya Makisio yaliyoidhinishwa, hivyo, kiasi cha TZS.400.26 bilioni hakikutolewa sawa na asilimia 4 ya Makisio yaliyoidhinishwa kwa matumizi ya kawaida.
Hata hivyo, kuna ongezeko katika fedha iliyotolewa la TZS.1,275.14 bilioni sawa na asilimia 15 ikilinganishwa na fedha zilizotolewa mwaka fedha 2012/2013. Fedha zilizotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2012/13 ilikuwa TZS.8,284.42 bilioni dhidi ya bajeti ya TZS.8,599.88 bilioni kupelekea kiasi cha TZS.315.46 bilioni sawa na asilimia 4 ya Makisio pitishwa kutotolewa.

Fedha za matumizi ya kawaida ambazo hazikutolewa katika mwaka wa fedha 2013/14 ziliathiri utekelezaji wa shughuli za kawaida za Wizara na Sekretarieti za Mikoa. Uwiano huu unaweza kuonekana katika **jedwali Na.9** kama linavyoonekana hapa chini. Maelezo zaidi yapo katika **kiambatisho Na.8**

Jedwali 9: Uwiano wa fedha zilizoidhinishwakwa matumizi ya kawaida dhidiMakisio: (Kiasi katikaBilioniTZS).

| Mwaka wa fedha | Makisio yaliyoidhinishwa | Fedha zilizotolewa | Tofauti |
|---|---|---|---|
| 2013/14 (A) | 9,959.81 | 9,559.55 | 400.26 |
| 2012/13 (B) | 8,599.88 | 8,284.42 | 315.46 |
| 2011/12 (C) | 9,214.89 | 8,687.23 | 527.66 |
| Tofauti (A - B) | 1,359.93 | 1,275.14 | |
| Tofauti (A - C) | 744.93 | 872.32 | |

***Chanzo:** Hesabu za Wizara na Sekretarieti za Mikoa zilizokaguliwa*

### 4.2.3 Uwiano wa fedha za matumizi ya kawaida kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na matumizi halisi katika Wizara, Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa.

Matokeo ya ukaguziyanaonyesha kuwa zilitumika jumla ya TZS.9,551.28bilioni kwa matumizi ya kawaida kwamwaka wa fedha2013/2014, dhidi ya TZS.9,559.55bilioni zilizotolewa hivyo kupelekea kiasi cha TZS.8.28bilioni sawa na asilimia0.09ya fedhailiyotolewa kutotumika.

Katika mwaka wa fedha 2013/2014 matumizi halisi yaliongezeka kwa kiasi cha TZS.1,302bilioni ikilinganishwa namatumizi halisikatika mwaka wa fedha2012/2013. Uwiano huu unaweza kuonekana katika **jedwali Na.10** kama linavyoonekana hapa chini. Maelezo zaidi yapo katika **kiambatisho Na.8**

Jedwali 10:*Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida na matumizi halisi(Kiasi katikaBilioniTZS)*

| Mwaka wa Fedha | Fedha zilizotolewa | Matumizi Halisi | Fedha zisizotumika |
|---|---|---|---|
| 2013/14 (A) | 9,559.55 | 9,551.28 | 8.28 |
| 2012/13 (B) | 8,284.42 | 8,249.28 | 35.14 |
| 2011/12 (C) | 8,687.23 | 8,685.28 | 1.96 |
| Tofauti (A - B) | 1,275.14 | 1,302.00 | |
| Tofauti (A - C) | 872.32 | 866 | |

*Chanzo: Hesabu za Wizara na Sekretarieti za Mikoa zilizokaguliwa*

Kwa ujumla kwa mwaka wa fedha 2013/2014, matumizi ya kawaida yaliongezeka ukilinganisha na miaka miwili iliyopita kama inavyoonekana katika Jedwali hapo juu.

### 4.2.4 Uwiano wa fedha za maendeleo zilizotolewa kwa Wizara, idara za Serikali na Sekretariati za Mikoa dhidi ya bajeti iliyoidhinishwa.

Makisio kwa matumizi ya Maendeleo yaliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2013/2014 yalikuwa TZS.5,035.94 bilioni ambayo

inaonyesha ongezeko la bilioni TZS.810.47 sawa na asilimia 19 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2012/2013 ya TZS.4,225.48bilioni.

Mapitio ya hesabu za Wizara na Sekretarieti za Mikoayamebainisha TZS.3,147.03 bilioni zilitolewa kama matumizi ya maendeleo ikiwa ni asilimia 63 ya makisio yaliyoidhinishwa.Hivyo, TZS.1,888.91 bilioni hazikutolewa sawa na asilimia 38 ya makisioyaliyoidhinishwa.

Hata hivyo, fedha za maendeleo zilizotolewa katika mwaka 2013/2014 zilikuwa pungufu kwa TZS.100.49 bilioni ikilinganishwa na fedha zilizotolewa mwaka 2012/2013 kwa ajili ya maendeleo.Uwiano huu unaweza kuonekana katika J**edwali Na.11**kama linavyoonekana hapa chini. Maelezo zaidi yapo katika **kiambatisho Na.9**

Jedwali 11: *Uwiano wa fedha zilizotolewakwa matumizi ya maendeleo dhidiMakisio: (Kiasi katikaBilioniTZS).*

| Mwaka wa fedha | Makisio yaliyoidhinishwa | Fedha zilizotolewa | Tofauti |
|---|---|---|---|
| 2013/14 (A) | 5,035.94 | 3,147.03 | 1,888.91 |
| 2012/13 (B) | 4,225.47 | 3,247.53 | 977.95 |
| 2011/12 (C) | 4,311.01 | 3,384.43 | 926.58 |
| Tofauti (A - B) | 810.47 | (100.49) | |
| Tofauti (A - C) | 724.93 | (237.40) | |

***Chanzo: Hesabu za Wizara na Sekretarieti za Mikoa zilizokaguliwa***

Jumla ya Fedha za Maendeleo kiasi cha TZS.3,247.53 bilioni zilitolewa katika mwaka wa fedha 2012/2013 ikilinganishwa na bajeti iliyokuwa imeidhinishwa ya TZS.4,225.474 bilioni,hivyokiasi cha TZS.977.94 bilioni sawa na asilimia 23 hazikutolewa.

Fedha za maendeleoambazo hazikutolewa mwaka 2013/14 ziliathiriutekelezaji washughuli za maendeleopia huongeza malimbikizoya matumiziyanayodaiwa namakandarasinakuanzakulimbikiza ribaambayo inakuwamzigokwa Serikalikatika siku za usoni.

### 4.2.5Uwiano wa fedha za maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na matumizi halisi katika Wizara, Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa.

Matokeo ya ukaguziyanaonyesha kuwafedha za maendeleo toka katikamfuko mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha2013/14 zilikua jumla ya kiasi cha TZS.3,147.03bilioniambapomatumizi halisiyalikuwaTZS.3,127.8bilioni na kusababishakutotumikakwa kiasi cha TZS.19.23bilioni sawa na asilimia0.61 ya fedha zilizotolewa.

Matumizi ya fedha za maendeleo pia yalipungua kwa kiasi cha TZS.75.30bilioni ikilinganishwa namatumizi ya mwaka2012/2013.Uwiano huu unaweza kuonekana katika **jedwali Na.12**kama linavyoonekana hapa chini. Maelezo zaidi yapo katika **kiambatisho Na.9**

Jedwali 12: *Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya maendeleo dhidi Matumizi halisi: (Kiasi katika Bilioni TZS).*

| Mwaka wa Fedha | Fedha zilizotolewa | Matumizi Halisi | Fedha zisizotumika |
|---|---|---|---|
| 2013/14 (A) | 3,147.03 | 3,127.80 | 19.23 |
| 2012/13 (B) | 3,247.53 | 3,203.10 | 44.43 |
| 2011/12 (C) | 3,384.43 | 3,376.30 | 8.14 |
| Tofauti (A - B) | (100.49) | (75.30) | |
| Tofauti (A - C) | (237.40) | (248.49) | |

*Chanzo:Hesabu za Wizara na Sekretarieti za Mikoa zilizokaguliwa*

Matumizi ya Fedha za Maendeleo yanaonyesha kupungua kwa ujumla katika mwaka wa fedha 2013/14 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2012/13. Hata hivyo, kiasi cha TZS.1,259.03 bilion kilitolewa kwenye robo ya nne ya mwaka wa fedha 2013/2014 hivyo kuweza kuathiri mpango mzima wa matumizi.

**Mapendekezo**
Kuimarisha na kuboresha mifumo ya kiuchumi na kuhakikisha maendeleo imara ya kiuchumi, kunahitaji kuzingatia sheria, Kanuni na nyaraka mbalimbali zinazotolewa na Serikali ili kuweza kuongeza ufanisi katika utendaji na hatimaye kuchangia kuongeza mapato ya Serikali ili kufikia malengo yanayowekwa.

Ufanisi katika ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita inaonyesha kuongezeka kwa wastani. Serikali inatakiwa kuchukua hatua madhubuti katika eneo hili, ikiwa ni pamoja na, kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kusimamia utekelezaji wa sheria zinazohusiana na ukusanyaji wa mapato kama sheria ya inayosimamia ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mfumo wa kielektroniki 'EFD' na kurekebisha mfumo wa bajeti ili uweze kutekelezwa kufikia malengo.

Serikali inashauriwa kuandaa bajeti inayotekelezeka na ipeleke fedha kwenye Wizara, Idara za Serikali na Sekretariati za Mikoa kama zilivyoidhinishwa na bunge. Hali hii itasaidia ufanisi wa bajeti kwa kiasi kikubwa na kupunguza uhamisho wa fedha wa mara kwa mara kati ya mafungu mbali mbali. Pia, Serikali inashauriwa iboreshe viashiria vya mapato ya ndani na nje pamoja na kuwasiliana na wadau wa maendeleo ili watimize kwa wakati ahadi zao na kutoa fedha za misaada kwa wakati.

### 4.2.6 Uwiano wamapato yasiyotokana na kodi dhidi ya bajeti iliyoidhinishwa

Bajetiiliyoidhinishwa kwa ajili yamapato yasiyotokana na kodikatika Wizara na Idara za Serikali (MDA) Sekretarieti za Mikoa na Balozikwa mwaka wa fedha2013/2014ilikuwa TZS.639,631

milioni; TZS.49milioni naTZS.17,152 milioni kwa mtiririko huo. Makusanyo halisiyalikuwaTZS.532,221 milioni, TZS.14 milioni na TZS.21,069milioni kwa Wizara na Idara za Serikali (MDA), Sekretarieti za Mikoa na Balozi.

Kulikuwa na mapungufu katika ukusanyaji ambapo Wizara na Idara zake walishindwa kufikia lengo kwa TZS.107,410milioni sawa na asilimia17ya makisio,Balozizilivuka lengo kwaTZS.3,917milionisawa na asilimia23juu ya makisio wakatiSekretarieti za Mikoa zilishindwa kufikia lengo kwa TZS.35milioni sawa naasilimia71ya makisio yaliyoidhinishwa.

Aidha, bajetiiliyoidhinishwa ya mwaka 2012/2013 kwa ajili yamapato yasiyotokana na kodikwa ajili Wizara na Idara za Serikali (MDA), Sekretarieti za Mikoa na Baloziilikuwa kiasi cha TZS.644,515 milioni,TZS.65 millioni na TZS.15,968 milioni.Makusanyo halisi ya mapato yalikuwaTZS.461,138 milioni,TZS.2,128 milioni na TZS.19,918 milioni kwaWizara na Idara za Serikali (MDA), Sekretarieti za Mikoa (RS) na Balozi. Maelezo zaidi yapo katika **Jedwali Na.13** hapa chini.

Jedwali 13: *Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya maendeleo dhidi Matumizi halisi: (Kiasi katika Bilioni TZS).*

| | | Idara | Makisio Idhinishwa | Makusanyo Halisi | Ziada/ Pungufu | % ya halisi dhidi ya makisio | % ya halisi dhidi ya yasiyokusanywa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Miaka | 2013/14 | Wizara | 639,631 | 532,221 | (107,410) | 83.21 | (16.79) |
| | | S/Mikoa | 49 | 14 | (35) | 28.93 | (71.07) |
| | | Balozi | 17,152 | 21,069 | 3,917 | 122.84 | 22.84 |
| | 2012/13 | Wizara | 644,515 | 461,138 | (183,377) | 71.55 | (28.45) |
| | | S/Mikoa | 65 | 2,128 | 2,063 | 3,273.85 | 3,173.85 |
| | | Balozi | 15,968 | 19,918 | 3,950 | 124.74 | 24.74 |
| | 2011/12 | Wizara | 342,176 | 361,334 | 19,158 | 105.60 | 5.60 |
| | | S/Mikoa | 65 | 8,130 | 8,065 | 12,507.69 | 12,407.69 |
| | | Balozi | 13,503 | 21,413 | 7,910 | 158.58 | 58.58 |

***Chanzo:Hesabu za Wizara na Sekretarieti za Mikoa zilizokaguliwa***

Kielelezo 11: Taarifa hizi pia zinaweza kuonekana kwenye chati hapa chini (Kiasi katika TZS milioni)




*Chanzo:Hesabu za Wizara na Sekretarieti za Mikoa zilizokaguliwa*

Mwenendo wa mapato yasiyotokana na kodi umekuwa ukitofautiana mwaka hadi mwaka na ufanisi wake umekuwa ukipanda na kushuka kwa Wizara na Idara zake na Sekretarieti za Mikoa. Ofisi za Balozi zimekuwa zikifanya vizuri mwaka hadi mwaka kama inavyoonekana kwenye chati hapo juu.

Ingawa makisio ya mapato yasiyo ya kodi yamekuwa yakitofautina kwa kiwango kidogo makusanyo yake halisi yamekuwa yakiongezeka sana mwaka hadi mwaka kitu ambacho kinaonyesha mapato zaidi yanaweza kupatikana kutoka chanzo hiki kama hatua madhubuti zikichukuliwa na Serikali katika kusimamia sheria zinazohusu ukusanyaji wa mapato, hii ni pamoja na matumizi ya mfumo wa kukusanyia mapato wa kieletroniki (EFD) katika ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi.

Sekretarieti za Mikoa zimeonyesha kushuka kwa mapato mwaka hadi mwaka kwa kipindi cha miaka mitatu kama mwenendo huo unavyoonekana hapo kwenye chati juu.

Serikali inashauriwa kuchua hatua zaidi katika kukusanya mapato yasiyo ya kodi hasa katika ngazi za Wizara. Idara za Serikali na Wakala wa Serikali chini ya wizara mama zisimamiwe vizuri na wizara husika ili kuweza kufikia malengo waliyojiwekea kwani mapato yasiyo ya kodi husaidia katika kugharimia matumizi ya kawaida.

## 4.3 Masuala Kuhusu Mpango Wa Kubakiza Makusanyo

Sehemu hii inatoa taarifa juu ya mambo yaliyojitokeza katika ukaguzi wa mwaka 2013/14 kuhusu mpango wa Serikali kubakisha fedha katika chanzo kilichokusanya kwa makubaliano (retention scheme).

### 4.3.1 Kushindwa kurejesha pesa za Mpango wa kubakiza makusanyo TZS 32.74 bilioni

Serikali inamakubaliano nabaadhiWizara, Idara zake naWakala kuweka makusanyo yao yote kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kisha asilimia iliyokubalika yamapato hayo hurejeshwa kwa Wizara au Idara husika chini ya mpango wa kubakiza makusanyo.

Wizarahizoni pamoja na;Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Elimu naMafunzo yaUfundi, Wizara ya Nishati na Madinina Wizara yaMaendeleo ya Jamii,Jinsia na Watoto.

Zoezi la ukaguzi katika Wizara na Idara zake limebainikwamba kiasi chaTZS.32.74bilionizikiwa fedha za mpango wa mabakizo hazikurejeshwa kwenye Wizara na Idara husika ambazo ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazikiasi chaTZS.23.07bilioni na Idara ya Uhamiaji kiasi chaTZS.9.67bilioni. Muhtasari wake ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na.14** hapa chini.

Jedwali 14:*Muhtasari wa Mpango wa* kubakiza makusanyo *(Kiasi katika TZS bilioni)*

| Wizara/ Idara | Makisio idhinishwa | Makusanyo Halisi | Asilimia ya mabakizo | Kiasi cha kubakiza | Kiasi kilichopelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali | Kiasi kilichobakizwa/kilichorejeshwa | Kiasi kisichorejeshwa | Asilimia isyokusanywa (Zaidi)/Pungufu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Aridhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | 100.05 | 47.89 | 100 | 47.89 | 47.89 | 25 | 23.07 | 52.13 |
| Nishati na Madini | 220.00 | 176.05 | 96 | 169.01 | 176.05 | 169 | | 19.98 |
| Maliasili na Utalii | 84.45 | 73.28 | 37 | 27.11 | 45.81 | 27 | - | 13.23 |
| Kitengo cha Zimamoto na Uokoaji | 35.38 | 19.96 | 37 | 7.38 | 19.96 | 7 | - | 43.60 |
| Mambo ya Ndani-Jeshi la Polisi | 17.99 | 25.17 | 33 | 8.31 | 25.17 | 8 | - | (39.86) |
| Idara ya Uhamiaji | 84.19 | 87.33 | 47 | 41.05 | 87.33 | 31 | 9.67 | (3.74) |
| Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto | 1.58 | 1.02 | 93 | 0.95 | 0.07 | 1 | - | 35.55 |

***Chanzo:Hesabu za Wizara na Sekretarieti za Mikoa zilizokaguliwa***

Isipokuwa Wizara ya Mambo ya Ndani -Jeshi la Polisina Idara ya Uhamiaji waliokusanya zaidi ya malengo, Wizara nyingine zilizo chini yampango wa kubakiza makusanyo zilishindwa kufikia malengokwa kati ya asilimia13.23na asilimia52.13kama kuonekana **Jedwali Na.15** hapo juu.

Serikali inatakiwakutekelezampango huu wa kubakiza makusanyo kwa kurejeshafedha kwaWizara na Idara husika kulingana namakusanyo yaona kwa uwiano waliokubaliana. Kurejesha makusanyo kwa wakati itawezesha Wizara na Idara husikakutekelezamalengo yaoambayo kwa upande mwingine itaongezamakusanyosiku zijazo.

Wizara na Idarachini yampangokubakiza makusanyo wanahimizwa kukusanya mapato yasiyo ya Kodina kukidhilengo walilojiwekea kwa mwaka.

## SURA YA TANO

## HESABU ZA TAIFA

### 5.0 TAARIFA YA HESABU ZA MAJUMUISHO

Sura hii ninaelezea masuala ya msingi yaliyojiri kutokana na ukaguzi wa Hesabu za Taifa. Hesabu hizi ni pamoja na; Hesabu za Majumuisho, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Msajili wa Hazina (Treasury Registrar), Deni la Taifa, na Kitengo cha Ukaguzi wa Awali cha Malipo ya Pensheni.

### 5.1 Ukaguzi wa Taarifa za Hesabu za Majumuisho

#### 5.1.1 Utangulizi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianza rasmi kutumia Viwango vya uandaaji Kimtaifa wa Hesabu za Umma (IPSAS) visivyo vya taslimu (accrual basis) wakati wa kuandaa Taarifa za Hesabu kuanzia 1 Julai, 2012. Hivyo basi, serikali iliandaa Hesabu za Majumuisho kwa kuzingatia kanuni za IPSAS katika mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2013.

Hata hivyo, serikali ilifanikiwa kujumuisha taarifa za hesabu za Serikali Kuu pekee, na kuacha hesabu za Serikali za Mtaa na Taasisi za Umma (Government Business Enterprises).

Mwaka huu, serikali imejumuisha taasisi zake zote isipokuwa Suma JKT, Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC), na Mamlaka ya Usajiri wa Leseni za Biashara (BRELA).

#### 5.1.2 Uandaaji wa Taarifa za Hesabu za Majumuisho

Kufuatia uamuzi wa serikali kurasmisha matumizi ya Kanuni za Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS accrual basis of accounting) kuanzia tarehe 1 Julai, 2012, serikali inalazimika kuandaa taarifa ya hesabu zake na za taasisi inazomiliki kulingana na Kanuni Na.6 za IPSAS na Kifungu cha 25 cha Sheria za Fedha, 2001 (marekebisho 2004).

Pamoja na nia ya dhati ya serikali ya kuboresha uwazi na uwajibikaji, ujumuishwaji wa taasisi za umma kwenye Taarifa za Hesabu za Majumuisho umeendelea kukumbwa na changamoto kadha wa kadha katika utekelezaji. Changamoto hizo ni pamoja na:

#### 5.1.2.1 Kujumuishwa kwa Taasisi zenye kutumia Kanuni za Uhasibu Tofauti

Taasisi nyingi za umma zimekuwa zikitumia kanuni mbalimbali za uhasibu kwenye kuwasilisha hesabu. Wakati Serikali Kuu, ambaye ndie mmiliki wa taasisi hizo imekuwa ikitumia Kanuni za Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS Accrual basis of accounting) inapoandaa hesabu zake, bado baadhi ya taasisi kama vile Shirika la Magazeti Tanzania (TSN), Benki ya Posta, Mamlaka ya Bandari na nyinginezo zimekuwa zikitumia kanuni za IFRS kwenye kuwasilisha taarifa zao.

Hivyo, kutokuwepo kwa usuluhishi wa kanuni za kiuhasibu kati ya zile za serikali na taasisi zake inapelekea taarifa za hesabu za majumuisho kuandaliwa na taarifa zisizo wiana. Hali hii inatia shaka kwenye uhalisia wa hesabu za majumuisho.

Hali kadhalika, nimebaini uwepo wa sera mbalimbali za kiuhasibu katika taasisi za umma. Kujumuishwa kwa taasisi zenye sera tofauti pasipo kufanyiwa usuluhishi inapelekea kuleta uwalakini wa uhalisia wa taarifa za hesabu za Majumuisho.

Napenda kushauri watendaji katika taasisi za umma kuhakikisha kwamba wanazifanyia usuluhishi kanuni zao za kiuhasibu ili kuendana na IPSAS, kanuni zinazotumika serikalini. Mwisho zaidi, napendekeza serikali kuandaa sera na miongozo ya kiuhasibu itakayotumiwa na taasisi zote za Umma.

#### 5.1.2.2 Kutofanyiwa Marekebisho Ufungaji wa Hesabu za Taasisi zenye Vipindi Tofauti

Taarifa za Hesabu za Majumuisho kwa kipindi kinachoisha 30 Juni, 2014, zimebainisha kujumuishwa kwa taasisi za umma zenye vipindi tofauti vya ufungaji wa mahesabu na kile cha serikali kinyume na Kanuni ya 6 ya IPSAS, Aya ya 47.

Vilevile, nimebaini kwamba serikali haikufanyia maboresho vipindi vya ufungaji taarifa za hesabu za taasisi zake ili kuleta uwiano. Muhtasari wa taasisi za umma zenye ufungaji wa hesabu katika vipindi tofauti na serikali unaonekana katika **Kiambatanisho 10.**

Natambua uwepo wa Mwongozo wa Hazina Na. 11 wa mwaka wa fedha 2014/2015 uliotolewa tarehe 9 Januari, 2015 ukizitaka taasisi zinazomilikiwa na serikali kufunga hesabu zake kulingana na kipindi cha ufungaji wa hesabu za serikali. Pia, Mwongozo wa Hazina Na. 12 wa mwaka wa fedha 2014/2015 nao ulizitaka idara na taasisi zote za serikali kuzingatia Kanuni sahihi za hesabu za majumuisho katika taasisi za umma.

Kuna haja ya serikali kufuatilia kwa ukaribu jitihada zake ili kuhakikisha kwamba taasisi za umma zinafunga hesabu zao katika vipindi sawa ili kupunguza muda unaotumika kufanya masahihisho ya hesabu zao.

Kutokana na hali hii, naishauri serikali isimamie miongozo inayotolewa ili taasisi zote za umma zifunge hesabu zake mwishoni mwa mwaka wa serikali, na pia kupunguza changamoto zinazoweza kutokea wakati wa kusuluhisha vipindi tofauti vya hesabu.

#### 5.1.2.3 Uandaaji wa Hesabu za Majumuisho kwa kutumia Taarifa ambazo Hazijakaguliwa

Taarifa ya Hesabu za Majumuisho huwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi mwezi mmoja baada ya taarifa za hesabu kutoka wizara na idara zake, serikali za mitaa na tawala za mikoa pamoja na

halmashauri. Hivyo, ni wazi kwamba ukaguzi wa taarifa za hesabu za majumuisho huanza wakati taarifa za wizara, idara, tawala za mikoa, halmashauri na serikali za mitaa bila kusahau taasisi za umma mbalimbali zikiendelea kufanyiwa ukaguzi.

Utaratibu huu unapelekea taarifa za majumuisho kujumuishwa kwa kutumia hesabu ambazo hazijakaguliwa, na hata kufanyiwa marekebisho. Mwishowe, inaleta changamoto kwenye kufanya marekebisho/masahihisho yaliyojitokeza ndani ya hesabu za majumuisho na hatimaye inashindikana kufanya hivyo.

Hivyo basi, changamoto hii inapelekea hesabu za majumuisho kugubikwa na tofauti kubwa kati ya taarifa zake na zile hesabu za serikali na taasisi zake moja moja. Hatimaye, taarifa za Hesabu za Majumuisho zinaweza kutokuwa sahihi.

Napendekeza serikali kupitia upya tarehe ya uwasilishwaji wa hesabu za majumuisho kwa kuifanyia maboresho kifungu cha 25 cha Sheria ya Fedha, 2001 (marekebisho 2004) ili tarehe ya kuwasilishwa hesabu za majumuisho iwe miezi 7 baada ya serikali kufunga mwaka.

### 5.1.2.4 Kuandaa Hesabu za Majumuisho za Serikali kwa Kutumia Mfumo Unaojiendesha

Kimsingi, Hesabu za Majumuisho zinaandaliwa kwa kutumia taarifa za hesabu za serikali, taasisi zake, wabia, na wakala huku zikizingatia taratibu zilizowekwa na kanuni za uhasibu. Wakati wa uandaaji wa hesabu za majumuisho, taarifa za hesabu za serikali na taasisi zake zinajumuishwa hatua kwa hatua, na pia kujumuisha vitu vinavyofanana ndani ya mizania za mali, madeni, mapato na matumizi.

Nilipitia utaratibu mzima wa kuandaa hesabu za majumuisho na kubaini kwamba mfumo wa kihasibu unaotumika haujawezeshwa kujumuisha taarifa mbalimbali za hesabu. Hali hii inapelekea taarifa za hesabu kutoka taasisi mbalimbali na zile za serikali

kuingizwa bila kutumia mfumo wa komputa. Serikali imekuwa ikifanya hivyo kwa kuingiza takwimu moja moja kwenye kurasa zilizodahiliwa za 'Microsoft Excel'. Kwa kutumia utaratibu huu wa kujumuisha, usalama wa takwimu zinazojumuishwa na Excel unakuwa mashakani, huku ukichukua muda mrefu, na pengine kuwa na kasoro nyingi.

Japokuwa kumekuwa na changamoto katika hesabu za majumuisho hasa kwenye taasisi za serikali ambazo hazitumii Mfumo wa Malipo wa Epicor, bado kuna uwezekano wa Serikali Kuu pamoja na Serikali za Mitaa kuandaa hesabu za majumuisho kwa kutumia mfumo unaojiendesha na hapo baadae kujumuishwa kwenye taasisi zote.

Mfumo wa kisasa unaojiendesha wenyewe wakati wa kufanya hesabu za majumuisho utapunguza kwa kiasi kikubwa dosari pamoja na makosa na hivyo kuwezesha kutambua na kuboresha masahihisho ili kuonyesha salio sahihi wakati wote.

Napendekeza kwa serikali ifikirie kufanya maboresho kwenye mfumo wa Epicor ili kuweza kujumuisha taarifa za fedha za Serikali Kuu na za Mitaa. Vile vile naishauri serikali iandae mwongozo ambao utatumiwa na Taasisi za Serikali wakati wa majumuisho.

#### 5.1.2.5 Kushindwa Kujumuisha Uwekezaji wa Serikali kwa Wabia na Wakala (Associates)

Serikali ina ubia katika kampuni 4 huku ikimiliki hisa za asilimia 50 na pia ina uwakala katika kampuni 27 ambako inamiliki kati ya asilimia 20 hadi 50 kama inavyoainishwa kwenye **Kiambatanisho 10.**

Kanuni ya 7 na 8 inaitaka serikali kuzingatia misingi ya ubia na uwakala wa uwekezaji wake. Kanuni hizi zinatoa mwongozo ni jinsi gani serikali inapaswa kujumuisha taarifa ya hesabu za ubia na uwakala wake katika Hesabu za Majumuisho.

Badala yake, nimebaini kwamba serikali haijumuishi ubia na uwakala wake katika Hesabu zake. Kutokuingizwa kwa wabia na wakala wa serikali katika hesabu za majumuisho kunaweza kupelekea taarifa za fedha za Majumuisho kutokuelezea hali halisi.

Napendekeza kwamba serikali ijumuishe ubia na uwakala wake katika taarifa za hesabu zake kwa kuzingatia umiliki wake.

#### 5.1.2.6 Kushindwa KujumuishaTaarifa za Fedha

Mapitio ya Hesabu za Majumuisho ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yamebaini kwamba kuna taasisi za umma ambazo hazikujumuishwa. Taasisi ambazo hazikujumuishwa ni Unit Trust of Tanzania (UTT), Suma JKT, Tanzania Nurses and Midwife Council (TNMC), na Mamlaka ya Usajili wa Leseni za Biashara (BRELA). Kutokuwepo kwa taasisi hizi za umma kwenye hesabu za majumuisho kunaharibu uwasilishwaji wa uhalisia wa taarifa za hesabu.

Napendekeza serikali kufanya jitihada za maksudi ili kujumuisha hesabu zote za taasisi zake.

## 5.2 Ukaguzi Mamlaka ya Mapato Tanzania

### 5.2.1 Utangulizi

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Na.11 ya mwaka 1995 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na.8 ya mwaka 1996 ikiwa na majukumu ya kusimamia na kukusanya mapato ya kodi kwa niaba ya Serikali.

Mamlaka inatengeneza aina mbili za Taarifa za Hesabu ambazo ni zile za Mapato na Taarifa ya Hesabu ya Matumizi. Taarifa ya Hesabu za Matumizi inaandaliwa kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya Taarifa za Fedha (IFRS) wakati zile za Mapato zinaandaliwa kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya kihasibu katika Sekta ya Umma kwa misingi ya fedha taslimu.

### 5.2.2 Mchanganuo wa Makusanyo ya Mapato

Sehemu hii inatoa taarifa fupi ya matokeo ya mapato ya Tanzania, mchanganuo linganifu wa makusayo ya mapato katika nchi za Afrika Mashariki, na inatoa taarifa fupi ya kodi zisizokusanywa bado ambazo masuala yake bado yako mahakamani na mwisho ni mapendezo yangu kuhusu masuala ya kodi.

### 5.2.3 Matokeo ya Makusanyo ya Mapato Tanzania

Katika mwaka wa ukaguzi niliona kwamba Mamlaka ya Mapato ilikusanya jumla ya Shilingi bilioni 9,996 dhidi ya malengo yaliyowekwa ya Shilingi bilioni 10,914 hali inayoonyesha upungufu katika ukusanyaji kwa shilingi bilioni 918 ambazo ni sawa na asilimia 8. ya jumla ya makisio au malengo. **Jedwali Na. 15** lifuatalo linaonyesha jumla ya makusanyo ya mapato toka Tanzania bara na visiwani:

**Jedwali 15:** Jumla ya makusanyo kwa mwaka 2013/14

| TZS Bilioni | Lengo | Makusanyo halisi | Tofauti | asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Mapato ya Ndani | 1,975.41 | 1,745.49 | (229.92) | (11.64) |
| Walipakodi wakubwa | 4,690.24 | 4,491.64 | (198.61) | (4.23) |
| Forodha na Ushuru wa Bidhaa | 4,248.17 | 3,759.52 | (488.65) | (11.50) |
| **Jumla (Pasipo kodi za vocha)** | **10,913.82** | **9,996.64** | **(917.18)** | **(8.40)** |

**Chanzo: Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa mwaka 2013/14**

Kwa ujumla makusanyo yote katika idara zote tatu hayakufikia malengo kwa mwaka huu. Hata hivyo, idara ya walipakodi wakubwa ndiyo iliyokusanya kwa kukaribia lengo.Idara hii ilishindwa kufikia lengo la asilimia 4.23 ikilinganishwa na idara ya Forodha and Ushuru wa Mapato asilimia 11.50 na asilimia 11.64 idara ya kodi za ndani.

**Kielelezo Na. 11** kinachofuata kinaonyesha kwamba idara ya walipakodi wakubwa ilikusanya asilimia 45 ya makusanyo halisi ambayo ndiyo sehemu kubwa kuliko zote ikifuatiwa na Idara ya Forodha yenye asilimia 38 na kodi za ndani asilimia 17 ambayo ndiyo ya chini zaidi ya zote.

**Kielelezo 12: Makusanyo halisi kwa kila Idara kwa mwaka 2013/14**




### 5.2.4 Ufanisi wa Kodi na mwelekeo wa Mapato

Mwelekeo wa makusanyo ya mapato kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, kwa wastani, ulikuwa chini ya makadirio yaliyoidhinishwa isipokuwa katika mwaka 2011/2012 ambapo makusanyo halisi yalivuka makadirio kwa asilimia 4. Ingawa kulikuwa na mwelekeo wa ongezeko la ufanisi wa mapato (uwiano wa kodi dhidi ya zao la jumla la ndani (GDP)) kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita hadi kufikia asilimia 16.9 katika mwaka 2013/2014, huu uwiano wa kodi dhidi ya zao la ndani bado ulikuwa chini ya asilimia 19.9 ya kilichotarajiwa na Mamlaka kufikiwa mwaka 2018.

Ingawa Mamlaka haikufikia lengo, imerikodi ongezeko katika uwiano wa kodi na zao la ndani kwa takribani asilimia 1 ikilinganishwa na zao la asilimia 16 la mwaka mmoja uliopita. **Jedwali Na. 16** hapo chini linaonyesha mwelekeo wa makusanyo kwa kipindi cha miaka mitano:

Jedwali 16: Ufanisi wa ujumla katika makusanyo ya mapato Tanzania (milioni TZS)

| **Mwaka** | **2009/10** | **2010/11** | **2011/12** | **2012/13** | **2013/14** |
|---|---|---|---|---|---|
| Lengo | 4,919,169 | 5,721,831 | 6,329,413 | 7,978,158 | 10,957,001 |
| Makusanyo halisi | 4,516,674 | 5,443,592 | 6,586,585 | 7,912,304 | 10,026,659 |
| Uwiano kati ya lengo na makusanyo halisi | 92% | 95% | 104% | 99% | 92% |
| **zao la jumla la ndani (GDP) (Tax/GDP)** | | | | | |
| **Tanzania** | | | 15.80% | 16.00% | 16.90% |
| **Kenya** | | | | | 22.10% |
| **Rwanda** | | | | | 14.90% |
| **Uganda** | | | | | 13.30% |
| **Burundi** | | | | | 13.60% |

**Chanzo: Takwimu za Mamlaka ya Mapato Tanzania, 2014**

Kutokana na uchambuzi wa malengo dhidi ya makusanyo, makusanyo halisi ikilinganishwa na asilimia ya makadirio yalikuwa ni asilimia 96 kwa wastani kwa muda wa kipindi cha miaka mitano iliyopita ambayo ni chini ya malengo, lakini kumbukumbu za makusanyo ya mwaka huu zinaonekana kuwa ndogo zaidi kwa kipindi chote kwani kiasi kisicho kusanywa kilifikia kiwango cha juu cha asilimia 8.

Sababu zilizotolewa na TRA ni kuwa maamuzi ya serikali kusitisha ukusanyaji wa kodi katika kadi za simu na ushuru katika kusafirisha fedha kwa njia ya simu umekuwa na matokeo hasi katika ufanisi wa Mamlaka ya Mapato katika ukusanyaji wa kodi kwani vyanzo hivyo vipya vilikuwa tayari ni vigezo vilivyotumika

katika makadirio ya mwaka 2013/14. Hili linasababisha wasiwasi wangu juu ya mfumo wa utambuzi wa vyanzo vya kodi, ukadiriaji wa mapato na usimamizi kuhusiana na kodi hizo.

Kwa upande mwingine, mchanganuo linganifu wa ufanisi wa kodi kwa nchi zote za Afrika Mashariki inaonyesha kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania iko katika nafasi ya pili nyuma ya Kenya na kwamba Mamlaka inafanya vizuri katika uwiano wa zao la kodi dhidi ya zao la ndani la jumla zaidi ya Rwanda, Uganda, na Burundi. Kwa kuzingatia mwelekeo linganifu wa Kenya, ninaonelea kwamba, ufanisi wa kodi wa Tanzania kwa pande zote mbili za zao halisi na zao lengwa, zinaacha fursa ya maboresho zaidi kwa kuongeza juhudi katika ukusanyaji wa mapato.

Kwa hiyo, ninapendekeza kwa Serikali kuhakikisha hatua za utekelezaji katika kukusanya kodi zinapewa kipaumbele kuepusha vipingamizi katika kukunyaji kodi kwa siku zijazo na Mamlaka iweke juhudi ili kuboresha ufanisi wake.

### 5.2.5 Kesi za muda mrefu katika bodi ya rufaa ya kodi na Mahakama TZS.1,716 bilioni

Wakati wa ukaguzi wangu, nilibaini kwamba Mamlaka ya Mapato ina kesi zilizoko katika bodi ya rufaa na Mahakama ya rufaa za kodi kwa muda mrefu zenye jumla ya shilingi bilioni 1,716.23 ambazo kiasi cha shilingi bilioni 261.19 zimekwama katika Mahakama ya Rufaa na kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 1,455.04 kinasubiri maamuzi katika bodi ya rufaa za kodi kama taarifa inavyoonekana hapa chini kwenye **Jedwali Na. 17:**

Jedwali 17: Muhtasari wa kesi zilizo katika Bodi ya Rufaa za Kodi na Mahakama ya Rufaa Tanzania

| S/N | Mwaka | Bodi ya rufaa za kodi | | Mahakama ya rufaa Tanzania | | Jumla Kuu | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (USD) | (SHS "000") | (USD) | (SHS "000") | (USD) | (SHS "000") |
| 1 | 2002 | - | 24,519,199 | - | - | - | 24,519,199 |
| 2 | 2003 | - | 7,051,800 | - | - | - | 7,051,800 |
| 3 | 2004 | 15,008,720 | 26,912,582 | - | - | 15,008,720 | 26,912,582 |
| 5 | 2005 | 11,502,492 | 2,482,708 | - | 21,355,407 | 11,502,492 | 23,838,115 |
| 6 | 2006 | - | 1,671,961 | - | 234,295 | - | 1,906,256 |
| 7 | 2007 | - | 35,356,744 | 7,999,826 | 2,879,720 | 7,999,826 | 38,236,464 |
| 8 | 2008 | 10,000 | 14,333,378 | - | 17,118,181 | 10,000 | 31,451,559 |
| 9 | 2009 | - | 70,925,132 | - | - | - | 70,925,132 |
| 10 | 2010 | 1,505,426 | 132,931,042 | - | 1,576 | 1,505,426 | 132,932,618 |
| 11 | 2011 | 215,211,223 | 18,715,164 | - | 80,386,487 | 215,211,223 | 99,101,650 |
| 12 | 2012 | 13,446,396 | 111,823,457 | 1,702,971 | 25,317,358 | 15,149,367 | 137,140,815 |
| 13 | 2013 | 315,059,470 | 2,048,313 | 26,042,542 | 50,981,458 | 341,102,012 | 53,029,770 |
| | Total | **571,743,727** | **448,771,480** | **35,745,340** | **198,274,481** | **607,489,066** | **647,045,961** |
| | Kiwango cha kubadili fedha kilichotumika | | | | | **SHS.1760/USD** | **1:01** |
| | Mapato ya kodi yaliyokwama katika kesi kwa "000" | | | | | **1,069,180,757** | **647,045,961** |
| A | Jumla ya mapato yaliyokwama katika kesi (SHS Billions) | | | | | **1,716.23** | |
| B | Bajeti ya mwaka 2013/14 (SHS billions) | | | | | **18,249** | |
| C | Sehemu ya mapato ya kodi kwa asilimia ya bajeti (A/B *100) | | | | | **9%** | |
| D | Zao la jumla la ndani kwa mwaka 2013/14 (SHS Billions) | | | | | 55,619.08 | |
| E | Sehemu ya mapato ya kodi kwa asilimia ya zao la ndani (GDP) (A/D*100) | | | | | 3% | |

Kwa ujumla, jedwali hapo juu linaonyesha mapato yaliyokwama katika rufaa ni asilimia kumi (10%) ya jumla ya makadirio ya makusanyo na asilimia tatu ya zao la jumla la ndani (GDP), ya mwaka 2014/2015. Hivyo thamani ya kodi inayobishaniwa katika bodi ya rufaa ya kodi na mahakama ya rufaa za kodi iko juu na serikali inapata gharama katika kuendesha kesi hizi kwa muda mrefu, na hasara kwenye mapato pale mrufani atakapo filisika kabla ya kesi kuamuliwa.

Hivyo napendekeza kwamba(a) usikilizwaji wa kesi hizi ufanyike haraka na Mahakama (b) Kwa suluhisho la kudumu, napendekeza kwa serikali kuunda kamati huru ya kusikiliza rufani, na (c) menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kuongeza nguvu na kuboresha mchakato wa ukaguzi na uchunguzi ili kupunguza malalamiko kati ya Mamlaka na walipakodi.

### 5.2.6 Usimamizi wa misamaha na ukusanyaji wa Kodi

Sehemu hii ineleza mambo makuu mawili katika usimamizi wa misamaha ya kodi na ukusanyaji wa mapato Tanzania. Sehemu ya kwanza ineleza mambo ya misamaha ya kodi na sehemu ya pili inajumuisha mambo ambayo ninaona ni muhimu kutolewa taarifa katikia ripoti yangu.

#### 5.2.6.1Misamaha ya kodi kwa mwaka wa ukaguzi TZS.1,834.097 Bilioni

Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Mapato ilitoa misamaha ya kodi kwa ajili ya shughuli maalum zilizoainishwa kama vile uwekezaji katika bidhaa za mtaji kwa kipindi maalum cha wakati ili kuvutia uwekezaji kutoka nje ya nchi na kukuza sera maalum za kiuchumi kama vile kuhamasisha uwekezaji katika sekta maalum, kuendeleza uhusiano na mataifa mengine kwa kutoa misamaha kwa shughuli za kidiplomasia na kwa sababu za kibinadamu.

Misamaha hii hutolewa kulingana na matakwa ya sheria na kanuni zilizopo. Hakika Misamaha hii ni halali lakini ikitolewa bila udhibiti wa kutosha, mapungufu katika sheria zilizopo, njama na vitendo vya matumizi mabaya ya misamaha na ukosefu wa mfumo wa kutosha wa usimamizi yote haya hutoa fursa inayopelekea upotevu usio wa lazima wa mapato ya kodi kwa kupitia misamaha ya hiyo kodi.

Taarifa za Fedha za Mamlaka ya Mapato kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2014 zinaonyesha misamaha ya kodi yenye jumla ya shilingi bilioni 1,834.097 (3.3% ya zao la ndani la jumla (GDP)) ikiwa ni misamaha iliyotolewa kwa taasisi mbalimbali na watu binafsi (2012/13: TZS 1,515.607 bilioni). Mwenendo unaonyesha ongezeko la TZS.318.49 bilionisawa 21% ya kiasi kilichoripotiwa katika mwaka wa fedha uliopita.

Endapo kiasi hiki cha TZS. 1,834.097 bilioni kilichosamehewa kingekusanywa, makusanyo yote yangekuwa TZS.11,724.07 bilioni badala ya TZS.9,889.97 bilioni ambacho ni Zaidi ya lengo

lililokadiriwa la shilingi10.809 bilioni. Mwelekeo wa ongezeko, unaleta matokeo hasi katika makusanyo kwa ujumla. Maelezo ya misamaha kwa wanufaika yanaonyeshwa katika **kiambatanisho Na. 11 cha ripoti hii.**

### 5.2.6.2Mchanganuo linganishi wa Misamaha ya Kodi

Uwiano wa misamaha ya kodi na zao la ndani la jumla uliongezeka toka asilimia 2.10 mwaka 2009/2010 hadi asilimia 4.39 katika mwaka 2011/2012 kabla ya kushuka hadi asilimia 3.13 na 3.30 katika miaka ya 2012/2013 na 2013/2014 kwa mtiririko huo. Jedwali Na. 7 hapo chini linaonyesha kwamba kiasi cha misamaha ya kodi kwa wastani wa asilimia 3.0 ya zao la ndani la jumla kwa miaka mitano iliyopita.**Jedwali Na18** hapa chini linaonesha.

Jedwali 18: Muhtasari wa kesi zilizo katika Bodi ya Rufaa za Kodi na Mahakama ya Rufaa Tanzania

| **Mwak (Milioni TZS)** | Pato la mwaka(Nominal GDP) | Jumla ya misamaha ya kodi | Asilimia ya Misamaha ikilinganisha na pata la Taifa (Exemptions to GDP In %) |
|---|---|---|---|
| **2009/10** | 31,316,224 | 653,652.50 | 2.10% |
| **2010/11** | 35,026,679 | 1,016,320.30 | 2.90% |
| **2011/12** | 41,125,313 | 1,806,203.60 | 4.39% |
| **2012/13** | 48,385,100 | 1,515,607.40 | 3.13% |
| **2013/14** | 55,619,077 | 1,834,097.36 | 3.30% |

***Chanzo: Tarifa za fedha za Mamlaka na takwimu, 2010-2014.***

Kutokana na mchanganuo hapo juu, kiasi cha misamaha ya kodi cha asilimia ya pato la Taifa la jumla (GDP) kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kilikuwa asilimia 3 ya GDP, kwa wastani, ambacho bado kiko juu ikilinganishwa na lengo la asilimia moja ya pato la Taifa au asilimia tano ya makusanyo yote. Misamaha hiyo kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita ilifikia kiwango cha juu kabisa cha asilimia 4 ya GDP katika mwaka wa 2011/12 kikifuatiwa na asilimia 3 ya GDP katika mwaka huu wa ukaguzi. Hata hivyo, mapitio yangu yalionyesha kwamba hakuna mwongozo uliokubalika wa kisera ulioweka kiwango cha misamaha ya kodi ambacho nchi ingezingatia wakati wote.

Ongezeko la misamaha ya kodi limeamsha hamasa kwa umma na wadau wengine juu ya kiwango, matumizi na matokeo ya mihamaha ya kodi katika uchumi wa nchi. Kuna mtazamo kuwamakusanyo yaliyosamehewa kupitia misamaha ya kodi yako juu, huzorotesha uchumi wa nchi; na kwa wawekezaji misamaha ya kodi si kigezo muhimu katika maamuzi ya uwekezaji. Wengine wanaonelea kuwa kuna matumizi mabaya ya misamaha ya kodi. Kutokana na kilio hiki cha jamii, Rais na kamati ya hesabu za serikali (PAC) ya bunge waliitaka Ofisi yangu kufanya ukaguzi kwenye misamaha ya kodi kwa lengo la kuthibitisha kama misamaha ya kodi inatolewa kwa kuzingatia mfumo wa sheria zinazotawala katika misamaha ya kodi, matumizi mazuri ya misamaha hiyo na kama misamaha hiyo ina matokeo chanya katika uchumi wa nchi na kuishauri serikali juu usimamizi mzuri wa misamaha.

Yafuatayo ni mambo muhimu yaliyotokana na ukaguzi wa misamaha ya kodi kwa miaka ya 2011/2012 na 2012/2013 .:

**a) Mafuta ya msamaha kutumiwa na kampuni nyingine TZS.22,325,178,728**

Mapitio ya matumizi ya mafuta ya msamaha katika kampuni za madini yalionyesha kuwa kampuni mbili za Geita Gold Mines na Resolute Tanzania Limited, zilihamisha mafuta ya msamaha kwa kampuni nyingine zisizo na misamaha hiyo. Jumla ya thamani ya mafuta yaliyokuwa na msamaha wa kodi ya TZS. 22,325,178,728 yalihamishwa ambapo TZS. 22,305,069,488 yanahusu Geita Gold Mines Ltd na TZS. 20,109,240 yanahusu Resolute Tanzania Limited. Uhamishwaji wa mafuta hayo kwenda kwa kampuni isiyo na misamaha hiyo ni kinyume na tangazo la serikali Na. 480 lililochapishwa tarehe 25 Oktoba, 2002. Tangazo hili la serikali linataka kusitishwa kwa misamaha kama mafuta ya msamaha yatatolewa kwa matumizi mengine au kuhamishwa, kuuzwa au kutolewa kwa namna yoyote ile kwa mtu asiyestahili misamaha hiyo.

Ninapendekeza kwa menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kurejesha kodi ya mafuta yanayosafirishwa kwa wakandarasi waliopewa kazi na mkandarasi mkuu ya kiasi cha TZS.22,305,069,488 kwa M/s Geita Gold Mines na TZS.20,109,240 kwa Resolute Tanzania Limited, na M/s Geita Gold Mines Ltd

.Piaawasilishe kwa wakaguzi repoti ya matumizi kwa mwezi Apri,l 2013 ambayo hayakutolewa wakati wa ukaguzi

**b) Matumizi mabaya ya Misamaha yaliyofanywa na Kiliwarrior Expedition Ltd TZS. 392,701,602**

Katika miaka ya fedha ya 2011/12 na 2012/13 Kiliwarrior Expedition Ltd ya S.L.P 12339, Arusha mwenye hati ya misamaha Na. 030863 na 030863-1 aliingiza magari ishirini na nane (28) yenye msamaha wa kodi wa TZS. 465,235,220.

Ziara ya wakaguzi ilibaini kuwa kampuni hiyo ilikuwa na magari mawili tu moja likiwa na namba za usajili T721 AFM lilinunuliwa tarehe 10/01/2005 na lingine lenye namba ya usajili T461 AUU lilinunuliwa tarehe 30/04/2008; yote mawili yakiwa si miongoni mwa magari yaliyoingizwa na kusamehewa kodi katika kipindi hicho cha ukaguzi.

Zaidi ya hayo, uongozi wa Mamlaka ya Mapato Mkoa wa Arusha alitoa maelezo kuwa baadhi ya magari yaliyoingizwa yalisajiliwa na kutumiwa na watu wasiostahili msamaha huo. Mamlaka ilizuia utoaji wa usajili mpya wa leseni za magari matano (5) na iliweza kuokoa kodi ya TZS 72,533,618 kati ya TZS.465,235,220 na kubakia ya TZS 392,701,602. Hata hivyo, suala kuu ni kwa nini Mamlaka haikuweza kuzuia uandikishaji wa magari kwa watumiaji wasiokuwa waagizaji wa magari hayo. Kwa maoni yetu, udhaifu katika mazingira ya mifumo ya udhibiti (Mfumo wa Usimamizi wa misamaha ya kodi) na njama(collusion) ndio sababu zilizopelekea wafanyabiashara wasio waaminifu kutumia vibaya misamaha ya kodi kwa manufaa yao binafsi na hivyo kudhoofisha malengo ya kiuchumi ya motisha wa misamaha hiyo.

**c) Misamaha iliyotolewa kwa wanufaika wasiostahili TZS. 53,399,565**

Kilimakyaro Mountain Lodge Limited ilipewa hati ya msamaha Na. 031753 kwa lengo la kupanua mradi wa nyumba ya kulala wageni wiliyani Karatu, mkoani Arusha katika shamba Na. 2531 lililoko katika kijiji cha Changarawe. Mapitio ya misamaha yalionyesha kuwa kampuni hiyo iliingiza nchini magari matatu kwa ajili ya mradi huo yenye jumla ya msamaha wa kodi wa TZS. 72,641,973 kama inavyoonyeshwa katika **Jedwali Na. 19** hapa chini:

Jedwali 19: Misamaha iliyotolewa kwa wanufaika wasiostahili

| Na | Tarehe | Namba ya Usajili | Gari iliyoagizwa | Namba ya Chassis | Namba ya Usajili | Misamaha (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 29/12/11 | R120526 | BMW X5 iliyotumika | WBAZW4209 0L465446 | T647BYB | 39,145,405.60 |
| 2 | 22/06/12 | R057812 | Toyota Land Cruiser Prado iliyotumika | JTEBZ29J10 0012725 | T630CBB | 14,254,160.40 |
| 3 | 14/03/13 | R026995 | Hyundai Santa mpya | KMHSU81CSD U072516 | T680CHX | 19,242,406.80 |
| | | | **Jumla** | | | **72,641,972.80** |

Ziara yetu katika eneo la mradi haikukuta magari husika, hata hivyo, Menejimenti ya kampuni iliifahamisha timu ya ukaguzi kuwa kampuni iliingiza nchini gari mpya moja aina ya Hyundai Santa ambayo wakati wa ziara ilikuwa Jijini Dar es Salaam na kwamba menejimenti ya kampuni haijui chochote kuhusiana na magari mengine mawili. Hivyo, serikali ilipoteza mapato ya jumla ya TZS 53, 399, 565 kwa kupitia misamaha ya kodi ilitolewa kwa mfaidika asiyejulikana kwa kuingiza nchini magari ya BMW X5 na Land Cruiser Prado.

Naishauri menejimenti ya Mamlaka ya Mapato (a) kuchunguza na kukusanya kodi za magari mawili kisha ifungue mashtaka kwa wahalifu waliohusika (b) iimarishe mazingira na mfumo wa udhibiti dhidi ya magari yaliyosamehewa kodi kwa kuhakikisha kwamba magari yaliyosamehewa kodi hayasajiliwi kwa jina jingine lisilo la muagizaji aliyepata msamaha huo wa kodi.

### 5.2.7 Mambo mengine yanayohusu usimamizi wa makusanyo ya Mapato

#### 5.2.7.1 Kukosekana kwa ushahidi wa kuondolewa nchini mali zilizoingizwa kwa muda zenye kodi ya jumla ya TZS.835,974,894,955

Mapitio ya mfumo wa kutunzia taarifa za Forodha, "Asycuda ++" kwa mwaka 2013/2014 umeshindwa kuthibitisha uondokaji wa mizigo 6,316 iliyoingizwa nchini kwa muda kutoka nchi mbalimbali

kinyume na kifungu 117(3) cha sheria ya kusimamia ushuru wa forodha ya Afrika Mashariki (EACCMA) ya mwaka, 2004. Mizigo hiyo iliyoingizwa kwa muda ina kodi yenye jumla ya TZS. 835, 974,894,955. Mali na mitambo mingine inayoingizwa nchini kwa muda inaweza kutumika nchini kinyume na matakwa ya sheria na hivyo kuikosesha Serikali mapato.

Naishauri Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (a) kufanya uchunguzi juu ya bidhaa na vifaa vilivyoingizwa kwa muda kwa lengo la kukusanya kiasi cha kodi husika na (b) kuweka udhibiti imara utakaowezesha kusimamia maingizo yote ya muda na utakao hakikisha kuwa bidhaa hizo hazitumiki hapa nchini.

**5.2.7.2Kutokusanywa kwa Ada ya Mchakato wa Forodha *(Customs Processing Fees)* TZS. 511,501,388**

Katika mwaka wa fedha 2013/2013 nilibaini kuwa Kampuni ya Gesi ya Uingereza *(BG Company))* ambayo inajihusisha na utafutaji wa gesi na mafuta huko Mtwara haijalipa Ada ya Mchakato wa Forodha *(Customs Processing Fees)* yenye jumla ya TZS. 511,501,388.09. Kutolipa kwa Ada ya Mchakato wa Forodha kunasababisha ukosefu wa mapato hivyo kuathiri Serikali pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania katika kufikia malengo yake

Hivyo naishauri menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania Kuchunguza kampuni zote za gesi na madini ili kujihakikishia kuwa kampuni hizo zinalipa ada za mchakato wa forodha na kukusanya kiasi ambacho hakijalipwa.

**5.2.7.3Nafuu maalum ya kodi iliyotolewa mara mbili kwenye Ankara moja USD 326,078 (sawa na TZS.540,598,195)**

Mapitio ya misamaha maalum ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) yalibainisha kuwa kampuni ya Swala Oil and Gas (T) Ltd ilipewa misamaha maalum ya VAT mara mbili kupitia ankara ya USD 163,039 kila moja wakati wa manunuzi ya mradi wa “20 Seismic - Seismic Data line” Kwa kutumia ankara kifani moja Na. 478 ya 30 Septemba, 2013.

Ilionekana kuwa mfumo wa kupitia wa viambatisho vya misamaha maalum ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ilikuwa hautoshi na hivyo kupelekea hali hii isiyo ya kawaida. Hivyo basi, kiasi cha Dola za Kimarekani 163,039 kilitolewa kwa kampuni hii kinatakiwa kurudishwa. **Jedwali Na. 20** linaonyesha misamaha iliyopokelewa kwa kutumia ya ankara yenye namba 478.

Jedwali 20: Misamaha kutolewa mara mbili kwenye ankara moja

| **Na** | **Namba ya usajiri** | **18% VAT** | ***Ankara namba*** | ***Muuzaji*** |
|---|---|---|---|---|
| 18/10/2013 | 115-280-066 | 163,039 | 478 | Polaries Seismic(T) Ltd |
| 10/10/2013 | 115-280-066 | 163,039 | 478 | Polaries Seismic(T) Ltd |
| **Jumla** | | **326,078** | | |

Hivyo, nashauri kwamba menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ikusanye Dola za kimarekani 163,039 ambazo zilitolewa kwa kampuni ya Swala Oil and Gas (T) Ltd na kuhakikisha kuwepo kwa udhibiti stahiki utakaozuia jambo kama hili kujirudia.

#### 5.2.7.4 Kodi iliyokokotolewa inayosubiri kukusanywa TZS.33,149,386,548

Mapitio ya daftari la uchunguzi wa kodi uliofanywa na Idara ya Uchunguzi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mwaka 2013/14 na taarifa hiyo kupelekwa ofisi za mikoa kwa ajili ya ukusanyaji, inaonyesha kodi iliyokokotolewa ya TZS. 33,149,386,548. Hali hii ilionekana katika sampuli ya ofisi za mikoa ya kodi iliyotembelewa ya Kinondoni, Ilala, Temeke na Mwanza.

Hata hivyo, kiasi hicho cha kodi bado hakijakusanywa hadi wakati wa ukaguzi Novemba, 2014. Kutokusanya kodi iliyokokotolewa kwa muda mrefu kunatokana na mfumo dhaifu wa ukusanyaji wa kodi katika ofisi za mikoa za Mamlaka ya Mapato Tanzania.

**5.2.7.5 Kodi iliyokokotolewa pungufu ya kiasi halisi kwa TZS.28,531,795,324 na $329,149 (sawa na TZS.29,077,484,868)**

Wakati wa ukaguzi wa mwaka 2013/14 nilibaini kodi iliyokokotolewa pungufu ya kiasi kilichopaswa kulipwa kwa TZS.28,531,795,324 na USD.329,149.

Nilikokotoa kodi kwenye sampuli ya majalada, nyaraka na taarifa za malipo na kufanya mapitio ya taarifa za Mamlaka ya Mapato Tanzania na kubaini kuwa maafisa wa kodi walikokotoa kodi pungufu. Kwa maoni yangu ukokotoaji wa kodi ulio pungufu ya kiasi halisi kinachopaswa kulipwa kunatokana na kutokuwepo kwa mfumo wa kutosha wa upitiaji makadirio ya kiasi cha kodi na hivyo kupelekea kuinyima serikali mapato yake halali.

**5.2.7.6 Faini iliyotozwa bila kukusanywa kwa kutotumia mashine za kielekitroniki (EFD) TZS.368,900,000**

Kifungu Na. 20 cha Kanuni za mashine za kielekitroniki *"Electronic Fiscal Device"* (EFD) za mwaka 2012 kinamtaka mtu yeyote anayetakiwa kutumia mashine za kielekitroniki (EFD) na ameshindwa kufanya hivyo kwa sababu zilizo nje ya matakwa ya Kanuni, kulipa faini isiyopungua Sh. 3,000,000 au kutumikia kifungo cha muda usiozidi miezi kumi na miwili, au vyote kwa pamoja.

Mapitio ya taarifa za utendaji za kila mwezi ulibaini kuwa faini ya TZS. 440,793,600 ilitozwa kwa wafanyabiashara ambao walishindwa kutumia mashine za kielekitroniki (EFDs) kutolea stakabathi ambapo jumla ya TZS. 71,893,600 tu zililipwa sawa na asilimia 16, na hivyo kufanya bakaa ya TZS. 368,900,000 bado kulipwa.

Kwa maoni yangu, kushindwa kukusanya tozo hizo za adhabu kunaweza kuhamasisha kutotumika kwa mashine hizo kwa watu wanaotakiwa kuzitumia na ni ishara ya upungufu katika harakati za ukusanyaji wa tozo hizo katika ofisi za mikoa.

Menejimenti ya Mamalaka ya Mapato Tanzania ihakikishe inatoza na kukusanya adhabu toka kwa wafanyabiashra wasio tumia mashine za kielekitroniki (EFDs) na kuhakisha kuwepo kwa mfumo wa ukusanyaji wa adhabu hizo kwa wakati ili kuongeza idadi ya wanaozingatia sheria.

## 5.3 Ofisi ya Msajili wa Hazina

### 5.3.1 Utangulizi

Ofisi ya Msajili wa Hazina (TRO) ilianzishwa kwa Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu) Sura ya 370 ya mwaka, 2002 (marekebisho 2010). Msajili wa Hazina amepewa mamlaka ya kumiliki na kusimamia uendeshaji wa mashirika ya umma na shughuli za wafanyabiashara, na mashirika ambayo serikali ina hisa.Msajili wa Hazina analo jukumu la kusimamia na kuishauri Serikali kuhusu uwekezaji katika mashirika na taasisi za umma.

Hivyo basi, Ofisi ya Msajili wa Hazina inalo jukumu la kusimamia mitaji ya serikali kwenye uwekezaji ndani ya Mashirika ya Umma na ya Binafsi ambako serikali inamiliki hisa kwa niaba ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika aya zifuatazo nitawasilisha hoja kuhusiana na usimamizi wa uwekezaji wa serikali na pia hoja za kiutawala ndani ya mashirika ya umma.

#### 5.3.1.1Usimamizi Usiotosheleza Kwenye Uwekezaji wa Serikali na Vipaumbele Vyake

Wakati wa ukaguzi wa taarifa za hesabu 2013/14 nimebaini kupungua kwa uwekezaji wa serikali na vipaumbele vyake katika mashirika na taasisi nyingine na wakati mwingine kupungua kwa hisa zake na hata mwishowe kuwa hatarini kupoteza hisa hizo. Hii inatokana na Serikali kuchelea kuongeza mtaji kwenye mashirika na taasisi inazowekeza wakati ilipohitajika kufanya hivyo kama inavyodhiirishwa hapa chini;

a) Mnamo mwaka 2012, kwenye Mkutano wa Mwaka wa Benki ya Afrika (AfDB), Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na wanahisa wenzeke zilikubaliana kimsingi kuongeza

mtaji wa hisa ili kufikia Dola za Kimarekani 32.05 milioni ambazo zilipangwa kulipwa kwa awamu.

Hata hivyo, nimebaini kwamba katika mwaka wa fedha 2013/14 serikali ilichelewa kulipa awamu ya pili ya hisa 2,967 zenye thamani ya Dola za Kimarekani 2.66 milioni. Hali hii ilipelekea serikali kupoteza hisa zake hizo.

b) Hisa za Serikali kwenye Benki ya Taifa ya Biashara (NBC, 1999 Limited) ziko hatarini kupotea baada ya serikali kushindwa kutumia haki yake ya kununua hisa zaidi (exercise 'share call option') zenye thamani ya TZS.22.53 bilioni ifikapo tarehe 31 Machi, 2015. Uhitaji wa kununua hisa zaidi ndani ya NBC umesababishwa na benki kutokidhi Uwiano wa Mtaji (Capital Adequacy Ratio) katika kuendesha shughuli zake kama ilivyoelekezwa na benki kuu.

Kuchelea kwa serikali kuongeza hisa zake kunatokana na serikali kutokuwa na fungu la bajeti kwa ajili ya utekelezaji huu katika mwaka wa fedha 2012/13. Vivyo hivyo, serikali imeendelea kutokutenga fungu la bajeti katika mwaka wa fedha 2013/14 kwa ajili ya kununua hisa hizo na hivyo kuipelekea Kamati ya hesabu za Serikali ya Bunge kuingilia kati juu ya kigugumizi cha serikali mnamo Novemba, 2014.

Hali hii hapo juu imechangiwa na makubaliano ya kuongeza mtaji kati ya Serikali na ABSA (ambao ndio wanahisa wakubwa ndani ya NBC 1999 Limited). Makubaliano hayo yalitokana na kupungua kwa Uwiano wa Mtaji wa NBC kuliko viwango vilivyowekwa na Benki Kuu. Serikali inajikuta katika wakati mgumu inapotakiwa kununua hiza zaidi (share call option) kutokana na kutokuwa na fedha na hivyo kujikuta inaelekea kupoteza umiliki wa hisa zake ndani ya NBC.

Mapitio yangu ya taarifa ya Msajili wa Hazina iliyotolewa mwezi Novemba, 2014 umebaini kwamba kushuka kwa mtaji wa benki umetokana na mapungufu ya wa menejimenti ya NBC ambayo iko chini ya ABSA.

Hata hivyo, matokeo ya mapungufu menejimenti yanajikuta yakiiathiri Serikali na hivyo kuonyesha kwamba hali kama hii inaweza kujitokeza pia katika mashirika mengine endapo suluhisho la kudumu halitapatikana hivi karibuni.

c) Kwa upande mwingine, mashirika mengine serikali kama vile Shirika la Ndege (ATCL), TAZARA, Shirika la Reli (TRL) yamekuwa yakiendeshwa kwa ruzuku ya serikali na kugubikwa na uhaba wa mtaji hususan shirika la Reli ambalo limekuwa likinusuriwa kwa kupata msaada toka serikalini. Japokuwa hali ya mashirika haya kwa sasa hivi inaweza kujengewa hoja tofauti, lakini michango yao katika ustawi wa nchi ni mkubwa mno.

Katika kesi hizi zote zilizotajwa, kukosekana kwa mfuko wa uwekezaji uliotayari Serikali ilishindwa kufanya vizuri na Ofisi ya Msajili wa Hazina (TRO) pia. Kwa hali hii, wanahisa katika makampuni mengine yanayofanana wanaweza kujaribiwa kuangalia hali hii ya ukomo wa bajeti ya Serikali na kuchagua kubadili mitaji wakiona Serikali ipo katika hali ngumu kibajeti ili waweze kuondokana na umiliki wa Serikali katika makampuni yao. Hivyo kwa maoni yangu kukosekana kwa fedha za uwekezaji kunazuia mikakati ya marekebisho ya mashirika ya kibiashara ya Serikali (GBE) na inapelekea hisa kushuka thamani katika makampuni ambapo Serikali inataka kuwekeza.

### 5.3.2 Ushiriki hafifu wa Msajili wa Hazina katika Mikutano Mkuu wa Mwaka

Wakati wa ukaguzi wangu nilibaini kuwa, Msajili wa Hazina hakushiriki vya kutosha katika Mikutano Mkuu wa Mwaka (AGMs) wa makampuni ambayo Serikali ina hisa chache na hakuwa na sera na taratibu tayari wa kufuatilia, kupendekeza na kulinda hisa Serikali ikiwa ni pamoja na maslahi ya Serikali katika uwekezaji usiokua na tija. Kwa maoni yangu, kutokana na kukosekana kwa

uwakilishi wa kutosha wa Serikali katika makampuni haya, Serikali inakosa nafasi ya kuchangia maamuzi muhimu ambayo yanaweza kuwa na athari juu ya umiliki wa uwekezaji na maslahi ya mengine.

Katika jukumu la Msajili wa Hazina kusimamia uwekezaji, nilifanya pia tathmini ya uwezo wa kifedha ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ofisi na kubaini kuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina inategemea sana Ruzuku ya serikali ambayo daima ni ndogo kuweza kusimamia uwekezaji mkubwa wa Serikali ambao unafikia kiasi cha TZS. 19,367.47 Bilioni hadi kufikia tarehe 30 Juni 2014. Ofisi ya Msajili wa Hazina pia hukusanya gawio, makusanyo mengine madogo madogo na michango kutoka makampuni chini ya utawala wake ambapo kiasi cha TZS.108.71 bilioni zilizokusanywa katika mwaka wa fedha 2013/14, lakini mapato hayo hayakufanyika msaada Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa sababu haipo katika mpango wa mabakizo (Retention Scheme) kwa sasa, na kwa hiyo makusanyo yote ni yaliwasilishwa mfuko mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, uwezo wa Ofisi ya Msajili wa Hazina katika kutekeleza mamlaka yake ni mdogo.

Ukosefu wa fedha za uwekezaji wa Serikali na mapungufu niliyoyataja hapo awali, yanaifanya Ofisi ya Msajili wa Hazina kushindwa kufanya lolote pale ambapo makampuni ambayo Serikali ina maslahi yanapotaka kubadili mitaji yao. Mapungufu haya ya fedha yanaweka maslahi  ya Serikali na uwekezaji katika makampuni hayo kuwa katika hatari kubwa sana ya kupotea au kumezwa na hatimaye kupoteza maslahi yote ya kimkakati ya serikali na nchi kwa ujumla. Kwa maoni yangu, ili Serikali iweze kujikwamua na changamoto nilizobainisha katika usimamizi wa uwekezaji wake katika hisa na maslahi mengine hatua zifuatazo ni muhimu kuchukuliwa:

a) Serikali kuanzisha mfuko wa uwekezaji kutokana na mapato inayopokea kutokana fedha za gawio na mapato mengine mbalimbali ili kujijengea mfuko kwa ajili ya uwekezaji wakati

wowote na makampuni ambayo serikali ina hisa au haja ya kubadili mtaji au kushiriki katika fursa nyingine ya uwekezaji ambayo Serikali inaweza kutaka kuwekeza. Kwa hali hii, Serikali inaweza kuruhusu Ofisi ya Msajili wa Hazina kubakia na makusanyo yake yote kwa kipindi maalum (kusema labda miaka mitano) na hivyo kuendeleza kupitia mapendekezo mengine hapa chini.

b) Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuanzisha mpango wa mabakizo kwa ajili ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kuwezesha uanzishwaji wa mfuko wa uwekezaji. Mpango huu pia unaweza kutumika kama kipimo cha utendaji cha Ofisi ya Msajili wa Hazina ambayo itawezesha Serikali kutathmini uwezo wa Msajili katika kuhamasisha mapato kutokana na uwekezaji wake.

c) Ofisi ya Msajili wa Hazina mara kwa mara hupitia utendaji wa uwekezaji na mikakati ya makampuni ambayo Serikali ina hisa chache ili kujua uwepo wa uwekezaji huo kwa Serikali. Kutokana na mapendekezo ya Mwaka ya ripoti ya wawekezaji wenye hisa chache, Ofisi ya Msajili wa Hazina inaweza kuja na mkakati wa kuendelea kuwepo au kutoka kwa makampuni haya ambao utalinda maslahi ya Serikali na ya umma kwa ujumla.

d) Ofisi ya Msajili wa Hazina ianzishe mfumo wa kuhakikisha kwamba Serikali inawakilishwa vizuri na kushiriki katika kufanya maamuzi ya makampuni ambayo Serikali ina hisa kwa manufaa ya umma. Hii itasaidia kuhakikisha Serikali inashiriki vya kutosha katika Mikutano Mkuu wa Mwaka na mikutano mingine ya kufanya maamuzi.

### 5.3.3 Usimamizi wa Madeni chini ya TRO

Nimepitia majukumu ya kifedha ya ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni 2014. Nia ni kutathmini utayari wa ofisi kuchukua majukumu mapya ambayo awali yalikua chini ya Wizara ya Fedha na aliyekua msimamizi wa makapuni hayo "Consolidated Holding Corporation". Pia nilipitia jinsi ofisi

ilivyoweza kusimamia mikopo na dhamana iliyotolewa na Serikali kwa Mashirika ya Umma, madaftari ya mikopo na kumbukumbu za uwekezaji katika Taasisi za Serikali na uwezo wa kulipa madeni yake.

Pia nilibaini kuwa dhamana nyingi zilizoshindwa kurejeshwa na madeni mengi yasiyotokana na uwekezaji ambayo Serikali ina mkataba nayo hatimaye yalihamishiwa Ofisi ya Msajili wa Hazina. Madeni yanayotokana na fidia, pensheni na maamuzi ya Mahakama yasiyohusiana na uwekezaji yalihamishiwa Ofisi ya Msajili wa Hazina kutoka Wizara ya Fedha. Pia, dhamana zilizokwisha muda wake ambazo kimsingi ni deni la Taifa hazikuweza kuhamishiwa katika idara sahihi ambayo inasimamia madeni ya Taifa .

Pia, nilibaini kuwa madeni yote yasiyo ya uwekezaji ambayo hayahudumiwi na Ofisi ya Msajili wa Hazina, yalihudumiwa kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali. Madeni hayo jumla yake ilifikia kiasi cha TZS 721.28 bilioni ukiondoa dhamana zilizokwisha muda wake kiasi cha Dola za Kimarekani (USD) 61.7107 milioni. Hivyo napata wasiwasi na uwezo wa Ofisi ya Msajili wa Hazina kushughulikia madeni makubwa ambayo hayahusiani na kazi ya msingi ya Ofisi hiyo wala hayaendani na bajeti ya Msajili wa Hazina. Kwa maoni yangu asili ya madeni haya yanastahili kuwekwa chini ya ofisi ya Deni la Taifa. (Idara ya Usimamizi wa Madeni) Kwa msingi huu, napendekeza hatua zifuatazo kuchukuliwa:

- Serikali irekebishe na kuweka madeni katika mafungu yasiyo ya uwekezaji na dhamana zilizopita muda wake kisha kuyahamishia Ofisi ya Deni la Taifa ili kuiwezesha Serikali kuanda usimamizi na muundo wa ulipaji wake. Hili linaweza kufanyika kwa Serikali kutoa dhamana (bonds) ambazo zitatumika kama chombo kwa ajili ya kurekodi na kulipa madeni hayo chini fungu sahihi.

- Ofisi ya Msajili wa Hazina ipitie taarifa za madeni yake na kuandaa bajeti ya kutosha kila mwaka ili kulipa madeni yake

yaliyobaki ambayo yanahusiana na uwekezaji pale yanapohitajika kulipwa. Hii itaepusha mkusanyiko zaidi wa madeni.

### 5.3.4 Usimamizi wa Makampuni ya Serikali yanayoendeshwa Kibiashara na Mamlaka ya Msajili wa Hazina

Tathmini yangu ya mamlaka, uwezo na majukumu ya Msajili wa Hazina nilibaini kuwa kuna Sheria mbalimbali ambazo zina uhusiano na usimamizi wa vyombo Serikali vinavyoendeshwa kibiashara (GBEs), mashirika ya umma, uwekezaji na uuzaji wa mali za Serikali. Kwa maoni yangu kuwepo kwa sheria nyingi kunajenga matatizo katika usimamizi wa uwekezaji.

Kwa upande wa utawala, nilibaini udhaifu mkubwa ikiwa ni pamoja na kutozingatiwa kwa misingi ya utawala hasa katika uteuzi wa Bodi ya Wakurugenzi na Mtendaji Mkuu. Baadhi ya Bodi bado zina wabunge na wafanyakazi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina .Jambo hili jambo linaleta mgongano wa maslahi na linakiuka utendaji wa utawala bora. Wakati mwingine, Wizara Mama huingilia kati utendaji na Utawala wa Kampuni ya Serikali yanayoendeshwa Kibiashara. Kwa maoni yangu, Wizara Mama ilitakiwa tu kusimamia maswala ya Sera na uratibu na wabunge wabaki na jukumu la ungalizi.

Kwa misingi hiyo, nashauri hatua zifuatazo kuchukuliwa ili kuwezesha utawala bora kwa makampuni yanayomilikiwa na Msajili wa Hazina.

a) Serikali kuharakisha zoezi la kutunga Sheria ya Msajili wa Hazina ili kumwezesha Msajili wa Hazina kukabiliana na masuala ya utendaji na Utawala na Wizara Mama kubakia na jukumu la uangalizi tu.

b) Nasisitiza mapendekezo yangu niliyotoa katika ripoti ya Ukaguzi ya Mashirika ya Umma na Taasisi nyingine kwa mwaka wa fedha 2012/13 kwamba, Wabunge na wafanyakazi wa Msajili wa Hazina

wasiwe wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi katika Shughuli za Serikali ili kuepuka mgongano wa maslahi na kuboresha uwajibikaji wa makampuni kupitia Bodi yao ya Wakurugenzi na Wizara mama kutoingilia kati katika shughuli na utawala wa Makampuni ya Serikali yanaendeshwa Kibiashara.

Naamini kuwa kama Serikali itatekeleza mapendekezo haya, uwezo mkubwa wa makampuni yanayomilikiwa Serikali na taasisi utafunguliwa.

## 5.4 Ukaguzi wa Deni la Taifa

### 5.4 .1Utangulizi

Deni la Taifa linatafsiriwa na Wizara ya Fedha kama madeni ambayo Serikali Kuu na idara zake zinawajibika kuyalipa. Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada ya Serikali ya mwaka 1974 (iliyorekebisha 2004) ndio sheria inayoongoza uendeshaji wa shughuli za deni la taifa. Kulingana na vifungu namba 3 na 6 vya sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada ya Serikali, 1974 Waziri wa Fedha ndiye mwenye dhamana ya kukopa na kutoa dhamana kwa niaba ya Serikali.

### 5.4.2 Mseto wa Deni la Taifa

Deni la Taifa kufikia tarehe 30 Juni, 2014 lilikuwa TZS.26,487.4 bilioni. Mseto wa deni la taifa unajumuisha deni la Ndani lenye thamani ya TZS.7,144.5 bilioni na deni la Nje lenye thamani ya TZS.19,342.9 bilioni kama inavyoonyeshwa katika **Kielelezo Na.12** chini;

**Kielelezo 13: Mseto wa Deni la Taifa**




Katika mwaka huu wa fedha, jumla ya TZS.6,374.3bilioni zilipokelewa kutoka kwa wafadhili wakati TZS.3,240.1 sawa na asilimia 17.8 ya makisio ya makusanyo ya fedha taslimu.

Deni la taifa limekuwa likiendelea kukua kila mwaka kutokana na kuwepo kwa nakisi ya mapato ya serikali na matumizi, ubadilishwaji wa hati za ukwasi kugharamia bajeti ya serikali, na pia ukopaji kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Jedwali hili hapa chini, laonyesha ukuaji wa deni la taifa katika kipindi cha miaka 5 iliyopita.

Jedwali 21: *Ukuaji wa Deni la Taifa katika Kipindi cha Miaka 5*

| | **2009/10** | **2010/11** | **2011/12** | **2012/13** | **2013/14** |
|---|---|---|---|---|---|
| Deni la Ndani, TZS bilioni | 2,254 | 3,707 | 4,076 | 5,775 | 7,144.50 |
| Deni la Nje, TZS bilioni | 7,858 | 10,735 | 12,430 | 15,634 | 19,343 |
| **Jumla ya Deni la Taifa, TZS bilioni** | 10,112 | 14,442 | 16,506 | 21,409 | 26,487 |

Kielelezo 14: Ukuaji wa Deni la Taifa katika Kipindi cha Miaka 5




Chanzo: *Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa – VT 22*

### 5.4.3 Mseto wa Deni la Ndani

Mseto wa deni la ndani unajumuisha dhamana zinazouzwa sokoni, na zisizouzwa zenye ukomo tofauti kama vile dhamana za muda mrefu na hati fungani. Mwishoni mwa mwaka wa fedha, Juni 2014, Deni la ndani lilifikia TZS.6,986.5 bilioni ikilinganishwa na kiasi cha TZS.5,775.1 bilioni zilizofikiwa mwishoni mwa Juni, 2013. Deni la ndani limeongezeka kwa TZS.1,211.5 bilioni sawa na asilimia 21 ya nyongeza ya deni la ndani lililorekodiwa.

Ongezeko la deni la ndani limetokana na serikali kushindwa kufikia malengo ya ukopeshwaji katika soko la nje hivyo kulazimika kukopa zaidi katika soko la ndani. Sababu nyingine iliyopelekea deni kukua ni ubadilishwaji wa hati za ukwasi(liquidity papers) kugharamia matumizi ya serikali. Vivyo hivyo, makusanyo ya mapato kuendelea kutokidhi matumizi nayo

imeipelekea serikali kuendelea kukopa kwa kutumia Hati fungani na za dhamana za muda mrefu ili kugharamia bajeti ya serikali.

Katika soko la ndani, benki za kibiashara zimekuwa zikiongoza kwa kumiliki sehemu kubwa ya deni kwa kiwango cha asilimia 51.5. Taasisi za kibenki za kibiashara zimekuwa zikikuza uwekezaji katika deni la ndani kwa kipindi cha miaka 3 mfulilizo. Katika mwaka wa fedha 2013/14, benki za kibiashara zilikuwa zinamiliki asilimia 51.5 ya deni la ndani na huku Benki Kuu ikimiliki asilimia 21.1 ya deni kama inavyoonyeshwa katika **jedwali Na 22 hapa chini:**

Jedwali 22: **Mseto wa Deni la Ndani**

| Wakopeshaji | 2011//12 | | 2012/13 | | 2013/14 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | TZS, Bilioni | Asilimia | TZS, Bilioni | Asilimia | TZS, Bilioni | Asilimia |
| Benki Kuu ya Tanzania | 1,172.8 | 25.8 | 1,443.5 | 24.9 | 1,571.8 | 21.1 |
| Benki za Kibiashara | 2,100.2 | 46.2 | 2,771.6 | 48.0 | 3,679.4 | 51.5 |
| Mifuko ya Hifadhi, TZS | 704.6 | 15.5 | 808.4 | 14 | 1,078.8 | 15.1 |
| Bima | 254.6 | 5.6 | 288.7 | 5.5 | 500.1 | 7 |
| Wadau Wengineo | 250.0 | 5.5 | 346.4 | 5.6 | 242.9 | 3.4 |
| Taasisi zisizokuwa za Kibenki | 3.6 | 1.4 | 115.4 | 2 | 71.4 | 1 |
| | **4,485.9** | **100%** | **5,774.2** | **100%** | **7,144.5** | **100%** |

**Chanzo:** ***MKUKUTA na Hesabu za Mwaka Fungu 22***

Napenda kutoa rai kwa serikali kuboresha soko la upili (Secondary Market) ili kuwezesha amana zinazonunuliwa katika soko la awali (Primary) ziweze kuuzwa na kununuliwa. Umiliki wa asilimia 51.5 za mabenki ya kibiashara kwenye deni la ndani unachangia kuadimika kwa mitaji na hivyo kupelekea hiyo mitaji michache inayopatikana kuwa ghali. Isitoshe, wawekezaji binafsi

wanashindwa kununua dhamana za serikali kutokana na kutokuwa na uhakika wa kuziuza katika soko la upili

### 5.4.4 Mseto wa Deni la Nje

Hadi tarehe 30 Juni 2014 Deni la nje lilikuwa TZS 19,342 bilioni sawa na asilimia 73.1% ya deni la Taifa .Sehemu kubwa ya mseto wa Deni la Taifa inatokana na Deni la Nje. Mseto wa deni unajumuisha mikopo kutoka mashirika ya kimataifa, mikopo ya bidhaa ndani na nje, mikopo ya kibiashara, nchi wahisani na taasisi za kimataifa.Deni hili liliongezeka kwa TZS 3,708.6 bilioni sawa na 23.7% ikilinganishwa na deni la nje la TZS 15,634.2 la mwaka 2012/2013.Hata hivyo Jumla ya TZS 3,084.9 bilioni zilipokelewa kutoka nje ikilinganishwa na bajeti ya TZS 3,855.2 bilioni.Mlinganisho wa Madeni ya nje kwa aina tofauti ya vyanzo ni kama ilivyo katika **Kielelezo Na 14**hapa chini.

**Kielelezo 15: Mseto wa Deni la Nje**




Uchambuzi wangu umebaini kwamba sehemu kubwa ya fedha za mkopo kutoka nje zilielekezwa kwenye miradi ya maendeleo sambamba na malengo ya MKUKUTA.

Ukaguzi wangu umebaini kwamba ongezeko la deni la nje limechangiwa na ukopaji kutoka Mashirika ya Kimataifa kama vile IDA ambako tumepokea jumla ya TZS.1,641.2 kwa ajili ya miradi ya maendeleo na ya kijamii ikiwemo Nishati na Gesi (TZS.165.9 bilioni), Sekta ya Usafiri (TZS.271.3 bilioni), Sekta ya Maji (TZS.210.7 bilioni), Mradi wa Kupunguza Umaskini (TZS.140.5 bilioni) na miradi mingineyo.

Vile vile serikali ilipokea TZS.93.9 bilioni kutoka nchi wahisani, EXIM benki 918.4 bilioni, na TZS.431.4 bilioni kutoka kwenye benki za kibiashara. Fedha hizo zilielekezwa katika miradi ya bomba la gesi, TZS.510.8 bilioni,Gesi Asilia ya SongoSongo, TZS.239.8, Ukarabati wa Chuo cha Muhimbili, TZS.24 bilioni, na miradi mingineyo.

Mikopo kutoka kwenye benki za kiabiashara ilielekezwa katika Makubaliano ya Muda ya Mkopo (Term Facility Agreement Credit) kutoka benki ya Credit Suisse (TZS.406.8 bilioni), HSBC benki TZS.12.5 bilioni, Danske benki TZS.12.1 bilioni ambazo zilipelekwa kuboresha miradi ya maendeleo kama vile barabara ya Tanzania – Zambia, mtambo wa kufua umeme MW60 huko Nyakato, Mwanza. Uchambuzi zaidi wa pesa zilizopokelewa na miradi iliyofadhiliwa umeonyeshwa kwenye **Kiambatanisho 12.**

### 5.4.5 Kutoingizwa Dhamana za Serikali katika Mseto wa Deni

Nimebaini kwamba serikali imekuwa ikitoa udhamini wa mikopo kwa kwa taasisi za kijamii kama vile Mamlaka ya Vitambulisho (NIDA), na Bunge. Hata hivyo, udhamini wa mikopo hiyo umekuwa ukiendelea pasipo kuingizwa katika Deni la taifa.

Vilevile, serikali imekuwa ikifanya malipo ya mikopo kwa taasisi zilizokiuka masharti ya udhamini. Mikopo hiyo bado imeendelea kutoingizwa katika hesabu za mseto wa deni la taifa.

Kwa mtizamo wangu, aina ya udhamini huu kwa hali halisi ya kiuchumi ndani ya taasisi hizi unastahili kuwa mkopo halisi kwa serikali na hivyo uhusishwe ndani ya hesabu za fungu 22 – Deni la Taifa.

### 5.4.6 Kukosekana kwa usuluhishi wa malipo kati ya Serikali na Benki Kuu

Uhakiki wa malipo ya Serikali kwenda Benki Kuu kwa ajili ya kulipia gharamazaUkwasi(liquidity Management costs) pamoja na riba inayotozwa Serikali kwenye Nakisi yake katika kipindi chamwaka 2012/13 na 2013/14 umebaini kuwepo kwa tofauti ya TZS.20,615,511,725ambayo haijaweza kufanyiwa usuluhishi. Tofauti hii imeonekana kutokana na uwepowa tofauti kwenye hati za madai kutoka Benki Kuu ikilinganishwa na malipoyanayohakikiwa na Serikali na kulipwa.

Nimeelezwa kwamba, Mhasibu Mkuu wa Serikali amekuwa akifanya uhakiki wa hati zamalipo na kisha kulipa kiasi anachoona ni halali pasipo kumshirikisha mdeni wake,Benki Kuu. Tofauti ya madai inaonyeshwa katika jedwali lifuatalo hapa chini;

**Jedwali 23: Mseto wa Deni la Ndani**

| | **Hati ya Madai kutoka Benki Kuu TZS (milioni)** | **Uhakiki Kutoka Serikalini TZS (milioni)** | **Kiwango Kilicholipwa na Serikali TZS (milioni)** | **Tofauti ambayo haijasuluishwa, TZS (milioni)** |
|---|---|---|---|---|
| | **A** | **B** | **C** | **A-B** |
| Gharama za Uendeshwaji wa Ukwasi | 41,746.8 | 30,793.8 | 30,793.8 | 10,952.9 |
| Tozo ya Nakisi ya Serikali mwaka 2011/12 na 2012/13 | 62,232.4 | 53,223.5 | 50,000.0 | 9,008.8 |
| Tozo ya Nakisi ya Serikali mwaka 2012/13 na 2013/14 | 44,301.1 | 43,647.7 | 30,000.0 | 653.7 |
| **Jumla** | | | | **20,615.5** |

Nashauri idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kufanya usuluhisho ya hati zote za madai pindi zinapoletwa na Benki Kuu. Endapo kutatokea tofauti, maridhiano yafanyike ili kuondoa tofauti hizo kabla ya kufanya malipo.

### 5.4.7 Tathmini ya Utendaji wa Dhamana za Serikali katika Soko la Ndani

Kulingana na Mpango wa Utoaji wa Dhamana za Serikali wa mwaka 2013/2014 ulioandaliwa na Kamati ya Maendeleo ya Masoko ya Dhamana, serikali ilipanga kukopa TZS.1,904 bilioni (Thamani ya Uso) kutoka soko la ndani ili kugharamia bajeti ya serikali pamoja na gharama ya kurudisha dhamana sokoni. Serikali ilipanga kukopa kwa kuuza hati fungani zenye wastani wa Thamani ya Uso (Face Value), TZS.618.6 ambazo ni asilimia moja ya Pato la Taifa. Ukomo wa ukopaji huu uliridhiwa baina ya Serikali na Chombo cha Kusimamia Sera ya Dhamana (Policy Support Instrument) kwa uangalizi wa IMF. Pia, serikali ilipanga kutumia kiasi cha TZS.1,286 bilioni ili kukomboa dhamana za serikali. Hata hivyo, nimebaini mapungufu yafuatayo wakati wa utekeleza wa Mpango:

**a) Tofauti za Kimsingi katika Kugharamia Hati za Muda Mfupi**

Aya ya 3.0 ya Mpango wa Utoaji wa Dhamana za Serikali wa mwaka 2013/2014 inabainisha kwamba serikali ilipanga kuuza Hati Fungani zenye Thamani ya Uso, TZS.997 bilioni. Hata hivyo, kufikia mwezi Mei serikali tayari ilishauza Hati fungani zenye Thamani ya Uso TZS.2,262 na hivyo kupelekea ongezeko la asilimia 125 kwenye ukopaji.

Jumla ya Hati fungani zenye thamani ya TZS.1,680 bilioni ziliuzwa kwa ajili ya kulipia dhamana za serikali zilizoisha muda. Kiwango hicho ni kikubwa kuliko kile kilichopendekezwa katika Mpango wa Utoaji wa Dhamana za Serikali (takribani mara mbili zaidi). Isitoshe, Hati za Ukwasi zenye thamani ya (face value)TZS.580.9 zilibadilishwa na kisha kurudishwa sokoni ili kugharamia bajeti ya serikali.

**b) Ukopaji wa Ndani kuvuka Ukomo**

Serikali ilikubaliana na ukomo wa kukopa ndani ya soko la ndani wa asilimia 1 ya Pato la Taifa. Ukomo huu ni mwendelezo wa Program ya Shirika la Fedha Duniani (PSI - IMF) kuzisaidia nchi zenye uhitaji wa fedha kwa kukopa ndani ya

soko la ndani pasipo kuleta athari za kiuchumi. Ukomo huu unaendana sambamba na Mpango wa Utoaji wa Dhamana za Serikali 2013/14 ambapo serikali ilipaswa kukopa kwa kuuza dhamana zisizodi TZS.618.6 bilioni katika soko la ndani.

Hata hivyo, mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa bajeti inaonyesha kwamba serikali ilikopa zaidi ya asilimia 58 ya ukomo kwa kuuza dhamana zenye thamani ya TZS.967.7 bilioni. Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ilinieleza kwamba ukomo huu ulifanyiwa marekebisho na kuongezwa, japo sikuweza kupata vielelezo thabiti juu ya mabadiliko ya ukomo.

**c) Ukopaji wa Ndani Uliozidi Malengo**

Serikali ilipanga kukopa kwa kuuza dhamana zenye Thamani (face value) ya TZS.1,904 bilioni kwenye soko la ndani kwa ajili ya kuendesha bajeti ya serikali na pia kugharamia dhamana zilizokomaa na hivyo kurudishwa sokoni.

Badala yake, serikali iliuza dhamana zenye thamani ya TZS.3,169 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 66.4. Ongezeko la ukopaji huu lina athari kubwa katika utekelezaji wa bajeti yote kwani serikali inalazimika kutenga pesa zaidi kwa ajili ya kugharamia dhamana hizi kwa kulipa riba na gharama nyingine ambazo hazikuwa katika bajeti.

**d) Ukosefu wa Uwiano Sawia wa Ukomo katika Dhamana za Serikali**

Muundo wa Dhamana za Serikali katika Deni la Ndani umegubikwa na wingi wa dhamana za muda mfupi. Kulingana na Mpango wa Utoaji wa Dhamana za Serikali wa mwaka 2013/2014 ulioandaliwa na Kamati ya Maendeleo ya Masoko ya Dhamana, serikali ilipanga kuuza dhamana za muda mrefu. Nia hasa ilikuwa kuiwezesha serikali kuleta uwiano sawia wa muundo wa dhamana zake katika soko na hivyo kuipunguzia gharama za kulipa dhamana hizo katika vipindi vya pamoja.

Hata hivyo, nimebaini kwamba serikali iliuza zaidi Hati fungani pamoja na Dhamana za muda mfupi, miaka 2, na hivyo kuendelea kuiongezea serikali gharama za ulipaji katika vipindi vifupi. Hali hii ni kinyume na Mpango wa Utoaji wa Dhamana za Serikali na pia kinyume na Mkakati wa Taifa wa Deni, 2002 (National Debt Strategy, 2002).

Napenda kuishauri serikali kuongeza ushindani katika soko la ndani la dhamana za serikali na hivyo kuongeza ushawishi wa ununuzi wa dhamana za muda mrefu.

## 5.5 Ukaguzi wa Awali wa Malipo ya Mafao ya Wastaafu

Sehemu hii ya ripoti inawasilisha mambo ya msingi yaliyojitokeza kwenye ukaguzi wa awali wa Malipo ya Mafao ya Wastaafu (Pensheni) katika kipindi cha mwaka 2013/14.

### 5.5.1 Utangulizi

Ukaguzi wa awali wa malipo ya mafao ya wastaafu unafanyika kwa kuzingatia ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 (marekebisho, 2005) na Kifungu cha 29 na 5 (a) cha Sheria ya Ukaguzi No. 11 ya mwaka 2008 ambayo inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kujiridhisha na kuruhusu malipo yafanyike kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali na kuhakikisha kwamba ibara ya 136 ya Katiba imezingatiwa.

Hivyo ni muhimu kufanya ukaguzi wa awali kwenye malipo yote ya Serikali ambayo sio rahisi kuyatabiri na kutengewa fedha za matumizi katika bajeti ya mwaka 2013/14.

### 5.5.2 Lengo la kufanya Ukaguzi wa Awali

Sababu kuu ya kufanya ukaguzi wa awali ni kusimamia usahihi wa malipo ya Mafao ya Wastaafu ili kuweza kubaini/kugundua mapema kasoro zinazoweza kujitokeza ili kuwawezesha wastaafu kulipwa mafao sahihi. Vile vile ukaguzi wa awali unasaidia kunusuru malipo ambayo yanaweza kufanyika kimakosa kwa mstaafu asiyestahili.

Kwa upande mwingine, ukaguzi wa awali unalenga kuhakikisha kwamba Sheria za Mafao, kanuni na taratibu za utumishi wa umma, Muundo (aina) wa utumishi (scheme of service), mawasiliano, na Ngazi za mishahara zinazingatiwa.

### 5.5.3 Mawanda ya Ukaguzi

Hoja za ukaguzi na mapendekezo yake ndani ya ripoti hii haihusishi watumishi wa umma ambao mafao yao yanashughulikiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Watumishi wa Umma (PSPF).

Ukaguzi wa awali wa malipo ya Mafao ya Wastaafu umefanyika katika maeneo yafuatayo:

- Watumishi wa umma, watoa huduma mchanganyiko, wanajeshi na viongozi wengine, walimu, na maafisa usalama.
- Malipo ya kimkataba kwa viongozi wa kisiasa, wageni toka nje, wastaafu waliorejeshwa kwenye utumishi, na raia waliopewa ajira wakiwa na umri wa miaka zaidi ya 45
- Kiinua mgongo kwa watumishi wasiokuwa na mafao, na pia
- Malipo kwa viongozi wa juu, na askari polisi

### 5.5.4 Ufafanuzi wa Hoja za Ukaguzi na Mapendekezo

Hoja kuu zilizojiri katika ukaguzi wa awaliwa malipo ya Mafao ya Wastaafu pamoja na mapendekezo yake kwa mwaka wa fedha 2013/14 unaonyeshwa katika sehemu ya ripoti hii kama ifuatavyo:

#### 5.5.4.1 Utekelezaji wa Mwaka (Ufanisi wa Kiutendaji)

Katika kipindi cha mwaka 2013/14, Ofisi ya Ukaguzi ilianza ukaguzi ikiwa na majalada 70 yaliyotokana na ukaguzi wa kipindi cha mwaka 2012/13.

Kipindi hiki, majalada ya wastaafu 4,738 yaliletwa kwa ajili ya kukaguliwa. Majalada 4,764 yalikaguliwa na kuidhinishwa, majalada 200 sawa na asilimia 5 yalirejeshwa kwa Maafisa Masuuli wahusika kwa ajili ya masahihisho, na majalada 44 yalikuwa bado yakiendelea na ukaguzi wakati wa kufunga mwaka wa fedha 30 Juni, 2014 kama inavyoonyeshwa katika **jedwali Na 24** hapa chini:

Jedwali 24: Idadi ya Majalada ya Wastaafu

| Maelezo | Majalada |
|---|---|
| Idadi ya majalada 1 Julai, 2013 | 70 |
| Majalada yaliyopokelewa | 4,738 |
| Jumla ya Majalada kwa Ukaguzi | **4,808** |
| Majalada Yaliyokaguliwa | 4,764 |
| **Majalada Yaliyobaki 30Juni, 2014** | **44** |

### 5.5.4.2 Ukokotoaji Usio Sahihi wa Mafao ya Wastaafu

Ukaguzi wangu wa malipo ya majalada ya Mafao ya Wastaafu umebaini kwamba baadhi ya malipo ya wastaafu yalikokotolewa isivyo sahihi. Kati ya majalada 4,764 ya wastaafu yaliyokaguliwa, malipo ya majalada 355 yalibainika yamezidishwa kwa kiasi chaTZS.982,514,159huku majalada 283 yakiwa yamepunjwa malipo ya TZS.281,456,311 kama inavyoonyeshwa katika **Jedwali 25**na **Jedwali 26**hapa chini:

Jedwali 25: *Mafao ya Wastaafu yaliyozidishwa*

| S/N | Maelezo | Idadi ya Kesi | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | Kipindi kilichozidishwa | 156 | 458,289,494 |
| 2 | Mishahara iliyozidishwa | 101 | 313,598,270 |
| 3 | Makosa katika Ukokotoaji | 26 | 89,761,932 |
| 4 | Mapunjo NSSF | 43 | 48,217,808 |
| 5 | Mapunjo katika madeni/Mikopo | 29 | 72,646,655 |
| | **Jumla** | **355** | **982,514,159** |

Jedwali 26: Mafao ya Wastaafu yaliyopunjwa

| S/N | Maelezo | Idadi ya Kesi | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | Kipindi kilichozidishwa | 191 | 156,020,781 |
| 2 | Mishahara iliyozidishwa | 63 | 38,313,356 |
| 3 | Makosa katika Ukokotoaji | 20 | 79,852,140 |
| 4 | Mapunjo NSSF | 8 | 7,127,076 |
| 5 | Mapunjo katika madeni/Mikopo | 1 | 142,959 |
| | **Jumla** | **283** | **281,456,312** |

Uchambuzi huu hapo juu unadhihirisha umuhimu wa ukaguzi wa awali katika malipo ya Mafao ya Wastaafu, kwani pasipo kufanyika serikali ingepoteza jumla ya TZS.701,057,848. Hivyo basi, uokoaji wa fedha hizo ni mojawapo ya mchango wa Ofisi yangu. Pia,

ukaguzi wa awali umeweza kuelezea athari zinazoweza kuletwa na Maafisa Masuuli ambazo zingeweza kuigharimu Serikali na Wastaafu endapo ukaguzi usingefanyika.

#### 5.5.4.3 Ucheleweshwaji Usiokuwa na Tija katika Kuandaa Mafao ya Wastaafu

Ukaguzi wangu wa malipo ya awali ya Wastaafu, umebaini baadhi ya malipo ya wastaafu yamekuwa yakichelewa kuwasilishwa PSPF na waajiri. Ucheleweshwaji huu umepelekea baadhi ya wastaafu kushindwa kuandaliwa malipo yao na pia kuigharimu Serikali tozo(Penalty). Kwa maoni yangu, fedha za adhabu na ugumu wa maisha wanaoupata wastaafu vingeweza kuepukika endapo michango ya watumishi ingekuwa ikiwasilishwa katika muda muafaka.

Changamoto nyingine inayopelekea mafao ya wastaafu kuchelewa ni kutokana na baadhi ya waajiri kuwasilisha nyaraka za mafao ambazo hazijitoshelezi na hivyo kutofautiana na ukokotoaji unaofanyika wakati wa uhakiki. Hali hii inapojitokeza, Ofisi yangu imekuwa ikiwaagiza waajiri kuleta nyaraka zilizokosekana na hivyo wakati mwingi zoezi zima kugubikwa na ucheleweshaji.

Kutokana na mapungufu ya kiutendaji, napenda kuishauri Serikali kufanya yafuatayo;

- Wizara ya Fedha ichukue jukumu la kufanya zoezi la kutambua michango yote iliyocheleweshwa na ile ambayo muda wake wa kuwasilishwa umepitiliza kuhakikisha kwamba imelipwa kutoka kwenye Wizara na idara zake, Taasisi na Mashirika ya Umma. Hii itapelekea waajiri kurudia makisio ya bajeti.
- Mlipaji Mkuu wa Serikali na Maafisa Masuuli kuhakikisha kwamba vitengo ambavyo viko chini ya mamlaka zao vinawasilisha michango ya watumishi katika mifuko ya Hifadhi ili kuepuka ucheleweshwaji pamoja na adhabu.
- Watumishi wanaoandaa malipo ya mafao wazingatie kanuni na taratibu za ukokotoaji kwa kuhakikisha kwamba nyaraka zote muhimu zimeambatanishwa

#### 5.5.4.4 Malikimbizo ya Michango kutokana na Taarifa zenye makosa za Waajiriwa TZS.299,978,036

Waraka wa Serikali wenye kumbu. Namba EC/AG/120/08/64 wa tarehe 14 Mei, 2009 unawataka waajiri wote kuhakikisha kwamba wanaingiza taarifa sahihi za watumishi kwenye mtandao wa malipo ya mishahara na pia makato/michango yote ya kisheria inawasilishwa kwenye mifuko ya Hifadhi katika wakati muafaka. Vilevile, Maafisa Masuuli ambao watasababisha uchelewaji wa michango hiyo watabeba majukumu ya kulipa adhabu zote zitakazotokana na ucheleweshaji wa michango.

Nimebaini kwamba kuchelewa kuwasilisha michango ya watumishi kumepelekea serikali kulimbikiza deni la TZS.299.9 bilioni katika kipindi cha mwisho wa mwaka kama inavyoonyeshwa kwenye **Kiambatisho 13**. Malimbikizo haya yalitokana na kutowasilisha michango kwa wakati na Maafisa Masuuli na michango iliyokatwa kutoka kwenye mishahara tofauti na mishahara sahihi iliyolipwa na mchangiaji.

Majadiliano na uongozi ulibaini kwamba ucheleweshaji wa uwasilishaji wa michango ya mafao kisheria unatokana na kutojazwa taarifa sahihi za watumishi kwenye mfumo wa LAWSON. Kwa mantiki hiyo basi, ujazaji usio sahihi wa taarifa za watumishi unaofanywa na Maafisa Masuuli unapelekea serikali kuingia kwenye gharama zisizostahili na pia kuwanyima watumishi stahiki zao za mafao wanapostaafu.

Napenda kuwashauri Maafisa Masuuli wajaze taarifa sahihi za watumishi katika mfumo wa LAWSON na kuwasilisha michango ya watumishi katika muda muafaka.

#### 5.5.4.5 Maandalizi ya Bajeti yasiyo Halisi ya Kitengo cha Mafao (Pensheni)

Makisio ya bajeti ya Kitengo cha Mafao kwa mwaka 2013/14 yalikuwa TZS.278.7 bilioni, huku matumizi halisi yakiwa TZS.265.0 bilioni na hivyo kupelekea kiasi cha TZS.13.6 bilioni kushindwa kutumika sawa na asilimia 4.9.

Kwa upande mwingine, nimebaini kwamba katika mwaka wa fedha kitengo cha mafao kimetengewa bajeti ya TZS.462.7 bilioni na hivyo kuleta tofauti ya TZS.184 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 66 ukilinganisha na makisio ya bajeti ya kipindi kilichopita.Mapitio zaidi ya taratibu za maandalizi ya bajeti katika kitengo cha Pensheni yamebaini mapungufu yafuatayo:

- Jeshi la Polisi ndio taasisi pekee ya serikali inayoleta taarifa za watumishi wake kwa ajili ya maandalizi ya bajeti.
- Kukosekana kwa taratibu za mawasiliano rasmi kati ya kitengo cha mafao na idara za serikali
- Kuandaa bajeti ya kipindi kinachofuata kwa kuweka nyongeza katika bajeti iliyopita.

Kwa muktadha huu, ni maoni yangu kwamba makisio ya mafao ya wastaafuyamekuwa yakifanyika pasipo kuzingatia uhalisia kutokanana kukosekana kwa taarifa muhimu kutoka kwa idara za serikali ukiachilia Jeshi la Polisi. Istoshe, ongezeko la asilimia 66 ya makisio ya bajeti ya mwaka 2014/15 halijaweza kujengewa hoja/uthibitisho/uhalali.

Naishauri serikali kuboresha mfumo wa maandalizi ya bajeti na kuwezakuingiza taarifa za watumishi kutoka idara zote husika.

## SURA YA SITA

## MFUMO WA UTHIBITI WA NDANI

### 6.0 Utangulizi

Sura hii inaainisha hoja za ukaguzi kutoka katika taasisi zilizo katika Serikali Kuu zinazohusiana na mambo mbalimbali yaudhibiti wa ndaniikiwa ni pamoja na; utendajiwa Kamati za Ukaguzi, utendaji kazi wa kitengo cha ukaguzi wa ndani, Udhibiti wa jumla wa mfumo wa Teknolojia ya Habari, mchakato wa kutathmini viatarishi pamoja udhibiti na uzuiaji udanganyifu

### 6.1 Mambo muhimu yatokanayo na tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani.

Ufuatao ni muhtasariwa matokeoya ukaguzi wa mwaka2013/14:

#### 6.1.1 Udhaifu katika utendaji wa kitengo cha ukaguzi wa ndani.

Kanuni Na.28(1) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 inahitaji Maafisa Masuuli wa kila taasisi chini ya Serikali Kuu kuanzisha na kuendeleza kitengo cha Ukaguzi wa ndani.

utendaji wa kitengo cha Ukaguzi wa ndani katika taasisi zilizo chini ya Serikali Kuukwa mwaka2013/14 matokeo yake kwa Muhtasari ni kama yanavyoonekana katika **jedwali Na.27**hapa chini.

Jedwali 27: *Mapungufu katika ufanisi wa kitengo cha ukaguzi wa ndani*.

| | Mapungufu yaliyobainishwa kutokana na ukaguzi |
|---|---|
| Ufanisi katika kitengo cha ukaguzi wa ndani | Baadhi ya vipengele vya ukaguzi havikukaguliwa na wakaguzi wa ndani |
| | Upungufu wa watumishi katika kitengo cha Ukaguzi wa ndani |
| | Mapendekezo ya wakaguzi wa ndani kutokufanyiwa kazi na menejimenti |
| | Kutokutumika kwa mkataba kwa wateja wa ukaguzi wa ndani uliopitishwa |
| | Upungufu wa fedha katika kusaidia kazi za kitengo cha ukaguzi wa ndani katika kufanya kazi zao kwa ufanisi. |
| | Kitengo kinakosa vitendea kazi kama vile kompyuta na magari |

*Chanzo: Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2013/2014*

**Kielelezo Na.15** kinaonyesha asilimia ya mapungufu katika utendaji kazi wa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani yaliyoonekana

katika taasisi tofauti zilizo chini ya Serikali Kuu, ambapo;-asilimia 64 ya mapungufu yote yalitoka katika mafungu (Votes), asilimia 14 katika wakala wa Serikali, asilimia 14 kutoka katika balozi na asilimia 7 ya mapungufu yalitoka katika taasisi nyingine.

**Kiambatisho Na.14-16** kinaonyesha kwa kina orodha ya taasisi zenye mapungufu katika ufanisi wa kitengo cha ukaguzi wa ndani.

Kielelezo 16: Chati ya zenye mapungufu katika ufanisi wa kitengo cha ukaguzi wa ndani




***Chanzo:Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2013/2014***

Kutokana na kielelezo Na.17 hapo juu, ninapendekezwa kwamba Serikali Kuu iboreshe ufanisi katika vitengo vya ukaguzi wa ndani. Nashauri pia ihakikishe kuwa kuna rasilimali watu za kutosha, fedha pamoja navitendea kazi.

### 6.1.2Mapungufu katikaUtendajiwa Kamati za Ukaguzi

Kanuni ya 30ya Kanuni ya Fedhaza Umma, 2001inahitajikila chombochini yaSerikali Kuukuwa nakamati ya ukaguzi.

Wakati wa mapitioya utendaji waKamati za Ukaguzikatika vyomboSerikali Kuu kwa mwaka2013/14, mapungufu yafuatayoyalibainikakama yanavyoonekana katika **Jedwali Na.29** hapa chini.

**Jedwali 28:Mapungufu katikaUtendajiwa Kamati ya Ukaguzi**

| | |
|---|---|
| Utendaji wa Kamati Za Ukaguzi | Kutoandaliwa kwa taarifa ya mwaka ya Kamati za Ukaguzi |
| | Kutofanyika kwa vikao vya kila robo mwaka na kukosekana kwa mihutsari ya vikao |
| | Mikakati ya mwaka na mipango mikakati kutothibishwa na kamati za ukaguzi |
| | Kutomwalika Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwenye vikao vya Kamati za ukaguzi |
| | Baadhi ya Taasisi bado hazina Kamati za Ukaguzi |
| | Muundo wa Kamati za Ukaguzi bado una mapungufu |
| | Kamati za Ukaguzi kutopitia Hesabu za Taasisi |

***Chanzo:*** *Hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2013/14*

**KielelezoNo.16** kinaonyesha madhaifu yaliyobainika katika ukaguzi wa Kamati za Ukaguzi kwenye vyombo mbalimbali vya Serikali Kuu kwa asilimia ambapo, asilimia 69 ya madhaifu hayo yameonekana katika Mafungu (Votes), asilimia 21 ni kutoka Wakala wa Serikali, asilimia 5 kutokaBalozi na asilimia 5 kutokataasisi nyingine.Maelezo zaidi yanayoonesha madhaifu katikaKamati za Ukaguzi yanapatikana katika**KiambatishoNo.14-16**

**Kielelezo 17: Taasisi zenye mapungufu katika Kamati za Ukaguzi**




***Chanzo: Hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2013/14***

Kutokana na **Kielelezo Na.16** hapo juu nashauri, Serikali Kuukuimarisha utendaji waKamatizake za Ukaguzi upande wa Mafungu (Votes). Utoaji wanyarakana mashartina kuongezamikutano ya kawaida, mawasiliano na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikalipamoja nakufuatamahitaji ya kisheriajuu ya uanzishwajina muundo wawanachama wakamati za ukaguzininashauri vitekelezwe.

### 6.1.3 Mapungufu katika udhibiti wa Vihatarishi

Udhibiti wa vihatarishi ni sehemu ya jukumu la taasisi husika ili kuweza kufikia malengo yake. Udhibiti huu unajumuisha kuelewa madhumuni ya taasisi, kubainisha na kufanyia kazi vihatarishi vinavyoonekana kuathiri malengo ya taasisi pamoja na kutengeneza mipango ya baadaye itakayo saidia kuondoa vihatarishi vilivyobainika.

Katika ukaguzi wa mwaka huu mapitio ya vihatarishi yalifanyika katika taasisi za Serikali kuu (Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa) na mapungufu yaliobainika ni kama yalivyoainishwa kwenye **Jedwali Na.29**

**Jedwali 29: Mapungufu katika kuzuia Vihatarishi**

| | **Mapungufu katika kuzuia vihatarishi** |
|---|---|
| Utaratibu wa Kuzuia Vihatarishi | Mpango mkakati wa kuzuia Vihatarishi haukuandaliwa |
| | Rejista ya Vihatarishi haikuandaliwa |
| | Sera ya kuzia vihatarishi haikuandaliwa |
| | Tathimini ya Vihatarishi kutofanyika mara kwa mara |
| | Muundo wa kuzuia vihatarishi haukuandaliwa |

*Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi kwa Menejimenti kwa mwaka wa fedha 2013/2014*

**Kielelezo Na.17** Inaonesha mapungufu katika tathimini ya vihatarishi yanatokana na taasisi za serikali kuu ambapo; asilimia 72% ya mapungufu ya vihatarishi yametoka kwenye Mafungu,asilimia 19% kutoka kwenye Wakala,asilimia 3% kutoka kwenye balozi na asilimia 6% kutoka kwenye taasisi nyingine. Taasisi zilizohusika zimeoneshwa kwenye **Kiambatanisho 14-16**

Kielelezo 18: Mapungufu katika tathimini ya Vihatarishi katika taasisi za Serikali Kuu




***Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi kwa Menejimenti kwa mwaka wa fedha 2013/2014***

Kama inavyooneka kwenye **Kielelezo Na.17** hapo juu nashauri taasisi za Serikali Kuu kuboresha tathimini ya Vihatarishi katika Mafungu (Votes).

### 6.1.4 Changamoto Kwenye Mfumo wa Teknolojia ya Habari

Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha ni mfumo wa usimamizi wa fedha ambao unatumiwa na Serikali ya Tanzania na ambao umeunganishwa na mfumo wa EPICOR ili kukidhi mahitaji ya kuchakata taarifa za fedha.

Mapitio yalifanyika ili kutambua ufanisi katika udhibiti wa mfumo wa teknolojia ya habari katika uendeshaji wa Taasisi mbalimbali kwenye Serikali kuu na uwezo wa mifumo ya udhibiti kufikia malengo ili kuweza kubaini iwapo mifumo iliyopo inafanya kazi kwa ufanisi tarajiwa Jedwali Na 30 hapa chini.

Jedwali 30: *Udhaifu wa Uliojitokeza kwenye Mifumo ya Teknolojia ya habari*

| | **Mapungufu yaliyojitokeza kwenye Ukaguzi** |
|---|---|
| Mifumo ya udhibiti wa Teknologia ya Habari | Kutokuwepo kwa mfumo wa kurudisha huduma kama kukitokea janga litakalopekea kupotea kwa taarifa |
| | Kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa kuweka kumbukumbu na kurudisha katika hali ya kawaida mifumo muhimu ya iliyoharibika. |
| | Mfumo wa zamani na mfumo mpya kutumika kwa wakati mmoja. |
| | Upungufu wa watumishi kwenye kitengo cha Mifumo ya kompyuta |
| | Mipango ya Mafunzo kwa mifumo ya TEHAMA haijaimarishwa |
| | Baadhi ya Moduli za EPICOR hazitumiki – Utunzaji wa Mali na Mali zilizoko gharani |
| | Kamati ya Kusimamia mikakati ya teknolojia ya habari na kamati kuu ya usimamizi wa TEHAMA kutoanzishwa. |
| | Kutokuwepo kwa sera maalum ya Mifumo ya Habari |
| | Kutokuwepo kwa mipango ya muda mrefu ya uimarishaji wa mifumo ya habari |
| | Kutokuwepo na mifungamano kati ya mifumo mbalimbali ya komputa inayotumiwa kuchakata habari. |
| | Programu za kuzuia virusi (ant virus) hazihuishwi mara kwa mara |
| | Vizimia moto na jenereta la dharura havipo |
| | Kutokuwepo na ulinzi wa kutosha kwenye jengo sehemu zenye mifumo ya komputa |
| | Kutokuwepo na Makubaliano ya Viwango vya Kutoa huduma na watoa huduma za mitandao |
| | Mifumo ya uhasibu kuendelea kuwa ya kizamani isiyotumia Kompyuta |

*Chanzo:* Taarifa za Ukaguzi za Taasisi husika

**Jedwali Na.30** linaonyesha asilimia za changamoto zilizoonekana kwenye mifumo ya udhibiti wa Teknologia ya Habari kutoka kwenye taasisi mbalimbali za Serikali Kuu, ambapo asilimia 68 ya makosa yametokea kwenye Wizara, asilimia 17 kutoka kwenye Wakala wa serikali kuu, asilimia 13 kutoka kweye balozi na asilimia 2 ya udhaifu ilikuwa ni kutoka taasisi nyingine za serikali

Kielelezo 19: Taasisi zenye udhaifu kwenye Mifumo ya Udhibiti wa Teknolojia ya Habari




**Chanzo:** ***Taarifa za Ukaguzi wa Hesabu kwa Mwaka 2013/2014***

Kutokana na **Kielelezo Na 18;** Ninapendekeza kuwa Taasisi zote za Serikali Kuu ziwe na Mwongozo wa Teknolojia ya Habari utakao wezesha kuunganisha Maamuzi ya Mipango ya Muda Mrefu ya Mifumo ya Habari, Mipango ya Kuwekeza ya Taasisi husika na Mipango mipana na muda mrefu ya Taasisi yote kwa ujumla.

### 6.1.5 Mapungufu katika kuzuia udanganyifu

Malengo ya kufanya tathmini ya viashiria vya udanganyifu lilikuwa ni kuwahakikishia wadau mbalimbali kuwa taasisi za serikali kuu(Wizara,Idara, na Sekretarieti za Mikoa) zina miundo madhubuti katika kuzuia na kupambana na udanganyifu pamoja na kugundua maeneo ya kuboresha.

**Jedwali Na.32** hapa chini linaonesha mapungufu yaliyobainika wakati wa tathimini ya viashiria vya udanganyifu katika taasisi saba za Serikali kuu.**Kiambatanisho Na 14-16**kinaonesha taasisi husika.

Jedwali 31: Mapungufu yaliobainikia katika tathimini ya udanganyifu.

| | |
|---|---|
| Tathimini ya Udanganyifu | Mpango wa kuzuia udanganyifu haujaandaliwa |
| | Hakuna utaratibu ulioandaliwa kwaajili ya kutambua na kuzui viashiria vya Udanganyifu |
| | Kugushi na kuongeza bei ya Michanganuo ya gharama ya ujenzi(Mfano manunuzi ya vifaa vya hospitali) na ubadhirifu wa mali za hospitali |

*Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi kwa Menejimenti ya mwaka wa fedha 2013/14*

**Muhtasari**

Mapitio ya mifumo ya ndani katika taasisi za Serikali kuu yalifanyika katika maeneo ya Utendaji wa kamati ya Ukaguzi, Utendaji katika kitengo cha Ukaguzi wa Ndani,Mapungufu katika Udhibiti wa Vihatarishi,Mapungufu katika Mazingira ya Usimamizi wa Teknolojia ya Habari,Mapungufu katika kuzuia udanganyifu.

Jedwali **Na.32** hapa chini linaonesha mapungufu yaliojitokeza kwenye mifumo ya ndani katika taasisi za Serikali Kuu katika ukaguzi wa mwaka huu.

Jedwali 32: Mchanganuo wa mapungufu yaliojitokeza katika mifumo ya ndani kwa mwaka wa fedha 2013/2014

| | Na | Eneo la Tathimini | Fungu | Wakala | Balozi | Taasisi | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mapungufu** | 1 | Mapungufu katika Kamati za Ukaguzi | | 9 | 2 | 2 | 43 |
| | 2 | Mapungufu katika Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani | 27 | 6 | 6 | 3 | 42 |
| | 3 | Mapungufu katika usimamizi wa Teknologia | 31 | 8 | 6 | 1 | 46 |
| | 4 | Mapungufu katika Udhibiti wa Vihatarishi | 22 | 6 | 1 | 2 | 31 |
| | 5 | Mapungufu katika kuzuia udanganyifu. | 7 | 0 | 0 | 0 | 7 |
| | Jumla | | **117** | **29** | **15** | **8** | **169** |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Asilimia | 1 | Mapungufu katika Kamati za Ukaguzi | 70% | 21% | 5% | 5% | 25% |
| | 2 | Mapungufu katika Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani | 64% | 14% | 14% | 7% | 25% |
| | 3 | Mapungufu katika usimamizi wa Teknologia | 67% | 17% | 13% | 2% | 27% |
| | 4 | Mapungufu katika Udhibiti wa Vihatarishi | 71% | 19% | 3% | 6% | 18% |
| | 5 | Mapungufu katika kuzuia udanganyifu. | 100% | 0% | 0% | 0% | 4% |
| | **Jumla** | | **67%** | **17%** | **9%** | **5%** | **100%** |
| | *Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi kwa Menejimenti kwa mwaka wa fedha 2013/14* | | | | | | |

Mchanganuo katika Jedwali **Na.32** hapo juu wa mapungufu yaliojitokeza wakati wa tathimini ya mfumo wa ndani katika taasisi za serikali kuu yanaweza kuelezewa kwenye Pai Chati Kielelezo Na.19 (Asilimia ya mapungufu ya mifumo ya ndani) na Kielelezo Na.20 (Asilimia ya mapungufu ya mifumo ya ndani kama ilivyotokea kwenye taasisi).

Kielelezo 20: Asilimia ya mapungufu katika mifumo ya ndani




*Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi kwa Menejimenti kwa mwaka wa fedha 2013/2014*

**Chati Na.19** hapo juu kinaonesha mapungufu ya mifumo ya ndani kama ilivyotokea kwenye Kamati ya Ukaguzi, kitengo cha ukaguzi wa ndani pamoja na usimamizi wa teknolojia unafanya asilimia 78% ya mapungufu yote, wakati asilimia 22% inatokana na,Mapungufu katika Udhibiti wa vihatarishi (18%) na mapungufu katika kuzuia udanganyifu (4%)

Taasisi za serikali kuu zinatakiwa kuimarisha kamati za ukaguzi wa ndani, Kitengo cha ukaguzi wa ndani, pamoja na mifumo ya tekinolijia kwa mujibu wa sheria na taratibu.

**Kielelezo 21: Mapungufu katika Mafungu,Wakala na Taasisi nyingine za Serikali**




*Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi kwa Menejimenti kwa mwaka wa fedha 2013/2014*

Chati Na.20 inaonesha mapungufu ya mifumo ya ndani katika taasisi za Serikali kuu ambapo asilimia 69% ya mapungufu yametoka katika Mafungu, asilimia 17% kutoka kwenye Wakala, asilimia 9% kutoka kwenye balozi mbalimbali nje ya nchi na asilimia 5% yametokana na taasisi nyingine za serikali.

Naishauri serikali kuboresha mifumo ya ndani ili utendaji kazi wake uweze kuaminiwa na wadau mbalimbali.

## SURA YA SABA

## USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA

### 7.0 Utangulizi

Sehemu hii ya ripotiinaonyesha ukaguziuliofanywa juu yarasilimali watu na usimamiziwa mishaharakwa taasisi zaSerikali Kuu kwa mwaka2013/14.

### 7.1 Usimamizi wa rasilimali watu

Ukaguzi wa rasilimali watu ni mchakato wakukaguasera, taratibu,nyaraka, mifumo, na utendaji wa kila siku wa usimamizi rasliimali watu katika taasisi husika. Kwa ujumla, ukaguzi wa rasilimali watu ni mapitio yamifumoya mwajiri iliyo rasmi na isiyo rasmina taratibu zake ili kuweza kupima kama zinakidhi mahitaji yake ya sasa na ya baadae, na kama zinatoa kinga ya kutosha kutokana nadhima ya kisheria.

### 7.2 Usimamizi wa mishahara

Katika ukaguzi wa mishahara, mkaguzi anakagua nyaraka zote zinazohusiana na mishahara,kuthibitishanakubainisha mapungufukati yamishahara na kumbukumbu za watumishi, wafanyakazi ambao kumbukumbu za mishahara hazijakamilika, makato ambayo yanatofautiana na michango, n.k. Udhibiti wa mfumo wa ndanikuhusu mishahara ni lazima ujitosheleze ili kuhakikisha usahihi wataarifa,kugundua na kuzuiaudanganyifu.

### 7.3 Masuala muhimuyaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa usimamizi wa rasilimali watu na mishahara

Ufuatao ni muhtasari wa masuala yaliyojitokeza katika ukaguzi wa Wizara, Wakala, Idara za Serikali, balozi za Tanzania nchi za nje na Sekretarieti za Mikoa:

### 7.3.1 Malipo ya mishahara kwawafanyakazi ambaohawapo kwenye utumishi wa UmmaTZS.141,387,963

Nilibainisha malipo ya mishahara kiasi cha TZS. 141,387,963 kutoka katika taasisi saba(7) kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.33**hapachini yaliyohusisha watumishi waliomaliza muda wao, waliofukuzwa na walioacha kazi ambao hawakugundulika na kuondolewa kwenye orodha ya mishahara kwa wakati baada ya muda wao wa utumishi kufikia ukomo kinyume na Sheria ya Umma kwa wastaafu (Public Service Retirement Benefit Act Na.2 of1999),kifungu Na. 17.

Jedwali 33: Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi ambaohawapo kwenye utumishi wa Umma

| Na. | Fungu | Wizara, idara na Sekretarieti za Mikoa | Kiasi (TZS.) |
|---|---|---|---|
| 1) | 52 | Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii | 74,475,500 |
| 2) | 83 | Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga | 24,150,992 |
| 3) | 37 | Ofisi ya Waziri Mkuu | 13,584,400 |
| 4) | 79 | Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro | 10,635,414 |
| 5) | 86 | Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga | 10,371,205 |
| 6) | 93 | Idara ya huduma za Uhamiaji | 6,216,050 |
| 7) | 51 | Wizara ya Mambo ya ndani | 1,954,400 |
| | | **Jumla** | **141,387,963** |

***Chanzo: Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2013/2014***

Ninapendekeza kwambaMaafisa Masuuli wa taasisi za serikali hapo juuwahakikishe mishahara iliyolipwa kwa hao watumishi ambao hawapo katika utumishi wa umma inarejeshwa na kuwasilishwa Hazina.

### 7.3.2 Upungufu wa watumishi 9,668

Wakati wa ukaguzi wa raslimali watu kutoka katika Wizara na Idara 9,Sekretarieti za Mikoa 14 na balozi 6, idadi ya watumishi waliotakiwa katika ikama ilikuwa 18,027, lakini nilibainiwatumishiwaliopo kazini ni 8,359 na kusababisha upungufu wa watumishi wa umma 8,359 sawa na asilimia 54 ya ikama.

Upungufu huu wa watumishi unaathiri utendaji waSerikalikatika utoaji wa huduma. Mchanganuo wa upungufu wa watumishi ni kama unavyoonekana katika **Kiambatisho 17.**

Uhaba wa wafanyakaziunaathiri utendaji wa taasisi husika katika suala la utoajiwa hudumakwa jamii; hivyo basi, ninapendekeza Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na ofisi ya Rais manajimenti ya utumishi wa umma kuhakikishawafanyakazi wapyawanajazanafasi zilizo waziili kuongezautoaji wa huduma borakwa jamii.

### 7.3.3 Watumishi wa Umma kukaimu katikanafasi zilizoachwawazi kwa zaidi ya miezisita

Kanuni D24(3)ya Kanuni za KudumuzaUtumishi wa Umma2009 (Standing Orders for the Public Service of 2009) inataka mtumishi kutokukaimunafasi iliyoachwa wazi kwakipindi cha zaidi ya miezisita.Hata hivyo,Ukaguzi wa usimamizi wa rasilimali watukatika Sekretarietiza Mikoa mitano(5), Balozi mbili na Idara za Serikalitatu(3) nilibaini kwamba,maafisa 28 wamekaimu katika nyadhifa mbalimbali kwa muda wa zaidi ya miezi sita kinyume na utaratibu bila ya kuthibitishwa.

Kukaimu kwa muda mrefu hakukubaliani na kanuniya utawala bora kwa taasisi husika. Mchanganuo wa nafasi zilizoachwa wazi zinazoshikiliwa na maafisa ambao hawajathibitishwa zinaonekana katika **kiambatisho 18**

Ninapendekeza Serikali kuhakikisha kwamba taasisi husika kushirikiana na Ofisi ya Rais -Menejimenti ya Utumishi wa Umma inawathibitisha maafisa wenye sifawanaokaimu nafasi zilizoachwa wazi au kuteua maafisa wapya wenye sifa katika nafasi hizo.

### 7.3.4 Watumishi wa umma kutokuthibitishwa kwa wakati

Kulingana na Kanuni ya D 45 ya Kanuni za Kudumu zaUtumishi wa Umma ya Mwaka, 2009 inayohusu uthibitisho wa uteuzi kwa mara ya kwanza inasema kwamba"(1) mtumishi wa umma anayo haki ya kuthibitishwa katika cheo chakebaada ya kipindi cha majaribio kuisha iwapo mwenendo na utendaji wake vinaridhisha. (2)Akishathibishwa, kipindi cha majaribio kwa mtumishi wa umma kitakwisha na atakuwa kwenye ajira ya kudumu na mafao ya uzeeni chini ya masharti yasheria za pensheni''

Sehemu ya II,Kifungu cha.6(1) (b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, 2002, kinasema, KilaKatibu Mkuu,Mkuu wa Idaraza Serikali,Katibu Tawala wa Mkoana Mkurugenzi waMtendaji wa Serikaliza Mitaa watakuwa namamlakakatika uteuzi,uthibitishona kusimamia nidhamu yawatumishi wa ummaisipokuwa walewalioteuliwa na Rais.

Hatahivyo,katika sampuli ya Sekretarieti za Mikoa nilizochagua,nilibainisha watumishi473ambao ajira zao hazikuthibitishwa, ingawakipindi chamajaribio kilikuwa kimekwishakama inavyoonekana katika **jedwali Na.34**hapa chini.

Jedwali 34: Watumishi 473 ambao hawajathibitishwa

| Na. | Fungu | Jina | Watumishi wasiothibitishwa |
|---|---|---|---|
| ***1*** | 80 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara | 268 |
| ***2*** | 70 | Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha | 115 |
| ***3*** | 77 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mara | 90 |
| | | **Jumla** | **473** |

***Chanzo:****Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2013/2014*

Kutothibitishwa kwa watumishi wa umma kazini kwa wakati baada ya muda wa majaribio kupita, inavunja moyo wa utendaji kazi kwa watumishi husika, hivyo ninapendekeza Serikali ihakikishe Wizara, Idara za Serikali, Wakala wa Serikali na Sekretarieti za Mikoa zinakuwa na taarifa sahihi za watumishi wote na kuziingiza

katika mfumo wa LAWSON ikiwa ni pamoja na kuwathibitisha kazini wale ambao hawajathibishwa na wana sifa za kuthibitishwa.

### 7.3.5 Watumishi wa umma kupokea mishahara chini ya kiwango kinachokubalika kisheria

Kifungu cha 3 katika Sheria ya kurejesha Madeni Na.7 ya mwaka 1970(Debt Recovery Act) kinataka watumishi wa umma kutopokea chini ya theluthi moja (1/3) ya pato lake la mishahara.

Pia,kanuni Na. F.12 ya Kanuni za Kudumu zaUtumishi wa Umma ya mwaka 2009, inaelekeza kwamba malipo ya mishaharachiniya kiwango kilichowekwa niusumbufu kiuchumi kwawafanyakazi.

Aidha,barua yenyeKumb.No.C/CE.45/271/01/1/87 ya 19/03/2009 inatoa ukomokama ilivyopitishwa naOfisi ya Rais -Menejimenti ya Utumishi waUmma(yaani1/3ya Pato laMshahara).

Katika ukaguzi wangu nilibaini jumla ya wafanyakazi314 kutoka katika Wizara na Idara zake tisa (9) na Sekretarieti za Mikoa mitatu (3)walilipwamishahara yaochini ya kiwango kinachoruhusiwakisheria na Ofisi ya Rais -Menejimenti ya Utumishi waUmma kama inavyoonekana katika **jedwali Na.35**hapa chini.Katika suala hiliwafanyakaziwanaishi kwa mishahara iliyo chini ya kiwango kilichopitishwa kwa mujibu wa sheria, kitu ambacho kinaweza kuwavunja moyo na kutoa huduma chini ya kiwango.

*Jedwali 35: Taasisi ambazo watumishi wake wanapata mshahara chini ya kiwango kilichopitishwa kisheria.*

| Na. | Fungu | Wizara, idara na Sekretarieti za Mikoa | Idadi ya watumishi ambao wanaopata mshahara chini ya kiwango kilichopitishwa kisheria |
|---|---|---|---|
| 1) | 29 | Huduma za Magereza | 99 |
| 2) | 93 | Idara ya Uhamiaji | 73 |
| 3) | 39 | Jeshi la Kujenga Taifa | 35 |
| 4) | 77 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mara | 27 |
| 5) | 52 | Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii | 24 |
| 6) | 46 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi | 19 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7) | 70 | Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha | 8 |
| 8) | 86 | Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga | 8 |
| 9) | 34 | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa | 6 |
| 10) | 50 | Wizara ya Fedha | 6 |
| 11) | 21 | Hazina | 5 |
| 12) | 91 | Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya | 4 |
| | | **Jumla** | **314** |

*Chanzo: Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2013/2014*

Ninaishauri serikali kuhakikisha kwamba taasisi husika zinafuata kiwango kilichowekwa kisheria na watumishi wanapata mikopo kulingana na viwango vya mishahara yao.

Pia, natoa wito kwa MaafisaMasuuli husika kuimarisha mfumo waudhibiti wa ndani juuya mikopoya wafanyakazi . mtumishi aombe mkopo mpya baada ya kumaliza kulipa malimbikizo ya madeni na pia maafisa masuuliwaongeza matumizi yaMfumo wa Kuratibu Rasilimali Watu (LAWSON) ili kutatua tatizo hili na kushughulikia kiutawala wanaoshindwa kulipa madeni yao.

### 7.3.6 Mishahara isiyolipwa ambayo haikuingizwa katikaAkauntihusika TZS.121,844,254

Waraka wa Uhasibu Na.3 kwa mwaka 2013/2014 wenye kumbukumbu Na. EB/AG/485/01/VOL.III/57wa tarehe28 Mei 2014 unawataka Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa mishaharaisiyolipwa inaingizwa katika akaunti Namba.9921141201 iliyopo Benki Kuu yaTanzania. mishahara hiiinahitajika kupelekwa kwenye akauntikupitia mfumo wa kutuma pesa wa benki kwa benki (TISS) na kwa wale ambaohawatumiiTISS; baruaya uhamishowa fedha inatakiwa kutumika.

Ukaguzi katika wizara, idara na Sekretarieti za Mikoa zilizochaguliwa ulibaini wizara moja na Sekretarieti za Mikoa mbili za NjombenaRukwa ambazo zilikuwa na mishahara isiyolipwaya kiasi chaTZS121,844,253.81 ambayo haikurejeshwa Hazina kulingana na waraka hapo juu.Mchanganuo wa Mishahara isiyolipwa ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na.36**hapa chini:-

Jedwali 36: Mishahara isiyolipwa ambayo haikuingizwa katikaAkauntihusika

| Na. | Fungu | Jina | Kiasi(TZS) |
|---|---|---|---|
| 1. | 49 | Wizara ya Maji | 92,166,972 |
| 2. | 89 | Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa | 19,830,953 |
| 3. | 54 | Sekretarieti ya Mkoa wa Njombe | 9,846,329 |
| | | **Jumla** | **121,844,254** |

*Chanzo: Taarifa za hesabu zilizpkaguliwa kwa mwaka 2013/2014*

Kutowasilishwa kwamishahara isiyolipwakwa muda mrefukunaweza kusababishamatumizi mabaya ya fedha hizo.Hii ni ukiukwaji wa maelekezo namiongozo iliyotolewa naWizara ya Fedha (kupitia kwa mlipaji mkuu wa serikali).Serikali inashauriwa kuhakikisha kuwaMaafisa Masuuli wote wanazingatia maelekezo namiongozo inayotolewa na Wizara ya Fedha.Mishahara isiyolipwa iwasilishwe Hazinabila kuchelewa.

### 7.3.7 Taarifa za mishahara zinaonyesha tarehe za kuzaliwa za watumishi wa umma zisizo sahihi

Kulingana na kanuniC (1) ya Kanuni za Kudumu zaUtumishi wa Umma za mwaka 2009, taarifa kamili na zilizo sahihi za mtumishi wa umma ni lazima zitunzwe katika Ofisi ya Rais -Menejimenti ya Utumishi waUmma na katika makao makuu ya ofisi husika ya mtumishi wa umma.

Ukaguzi uliofanyika wa sampuli za Sekretarieti za Mikoa mbili na Wizara moja kuhusuMfumo wa Uratibu Rasilimali Watu (LAWSON) na mafaili binafsi ya wafanyakazi kwa mwaka wa fedha uliomalizikaJuni 30, 2014, katika Wizara ya Afyana Ustawi wa Jamii(Fungu 52) naSekretarieti ya Mkoa wa Mwanza ulibainiwatumishi sabini na saba (Wizara ya Afyana Ustawi wa Jamii) na wawili (Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza) ambao tarehe zao za kuzaliwa zilionyesha kuwa wamezaliwa tarehe 1Februari,1900. Hii ina maana kwambatarehe ya kustaafukwa wafanyakazihawaingekuwa 02/01/1960.

Pia, mapitio ya taarifa za mishahara katika Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha (Fungu 70) ilibaini kuwa tarehe za kuzaliwa za watumishi tisa (9) hazikuwa sahihi kutokana na ukweli kwamba watumishi wawili walionekana katika taarifa zilizopo kwamba wamezaliwa mwaka 1900 wakati watumishi saba (7) walionekana wameajiriwa chini ya miaka 18 kinyume na kifungu cha 5 (3) cha Sheria ya Mahusiano Kazini ya mwaka 2004 (Labor Relation Act) ambacho kinazuia ajira ya watoto. Kwa maana hiyo hakukuwa na ushahidi kwamba watumishi walioajiriwa walikidhi vigezo vya ajira nakumbukumbu za watumishi hao hazikuingizwa kwa usahihi katika mfumo.

Ninapendekeza kwa Serikali kuhakikisha kwamba taarifa sahihi za watumishi wote wa ummazinaingizwa kwa usahihi katika mfumo wa wa utaratibu raslimali watu ili kuepusha watumiaji kutoelewa taarifa hizo.

Pia,Afisa Masuuli wote wanashauriwa kuhakikisha kwamba kumbukumbu za wafanyakazi katika ofisi zao husika zinafanana na taarifa za mishahara zilizopo Hazina.

### 7.3.8 Ukosefu wa fedha za kusafirisha watumishi wa ubalozi waliostaafu na mali zao

Kati ya balozi za Tanzania 34 nilizokagua, balozi nne zilikuwa na wastaafu wanne ambao walishindwa kurudi nyumbani kwa sababu ya uhaba wa fedha za kuwasafirisha pamoja na mali zao kinyume na Kanuni za Kudumu zaUtumishi wa Umma, Kanuni J8 (I), kiambatisho J /I, na kanuni Na. 71 (1) ya Kanuni za Huduma za Nje (Tanzania Foreign Service Regulations) naTangazo katika Gazeti La Serikali Na. 394la18/10/2013.Balozi hizo ni kama zinavyoonekana katika **Jedwali Na.37** hapa chini:

Jedwali 37: Watumishi waliostaafu ambao hawakuweza kurudi nyumbani

| Na. | Fungu | Jina la ubalozi | Tarehe ya kustaafu/ kipindi |
|---|---|---|---|
| 1 | 2001 | Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa | Februari 22, 2014 |
| 2 | 2003 | Ubalozi wa Tanzania Cairo | Machi 4 ,2014 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | 2004 | Ubalozi wa Tanzania Kinshasa | 28/03/2014 |
| 4 | 2008 | Ubalozi wa Tanzania Maputo | Miezi 19 mpaka Feb. 2015 |

***Chanzo: Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2013/2014***

Nashauri Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuandaa bajeti inayokidhi mahitaji yagharama za usafirishaji wa watumishi wastaafu na mali zao baada ya kustaafu.

### 7.3.9 Malipo ya posho na kodi ya nyumba kwa watumishi waliostaafu wasio na mikataba TZS.543,796,737.35

Sampuli ya Balozinnezilizochaguliwa zilikuwa zina maafisa wanaofanya kazi bilamikatabahalali ya ajirahivyo kiasi chaTZS543,796,737.35zililipwakamaposho na kodi ya pango kwa watumishi hao baada ya kustaafu.

Maafisa hawawastaafu walibakia wakifanya kazi bila ya kuwa na mikataba kwa kuwa serikali ilikuwa na uhaba wa fedha kwa ajili ya kulipiagharama za kuwarudisha nyumbani baada ya kufikiaumri wa kustaafu.**Jedwali Na.38** linaonyesha orodha zabalozi zenye wastaafu ambao hawajarejea nyumbani baada ya kustaafu.

Jedwali 38:*Orodha ya balozi zenye wastaafu*

| Na. | Jina/Fungu | Tarehe ya kustaafu | Kiasi(TZS) |
|---|---|---|---|
| 1. | Ubalozi wa Tanzania Kinshasa (Fungu 2004) | Alistaafu 28/03/2014 (Posho ya miezi 10) | 130,868,872 |
| 2. | Ubalozi wa Tanzania Kinshasa (Fungu 2004) | Alistaafu 28/03/2014 (kodi ya pango kwa miezi 10) | 41,225,000 |
| 3. | Ubalozi wa Tanzania Maputo (Fungu 2008) | Mstaafu ana miezi 19 tangu alipostaafu mpaka wakati wa ukaguzi (Februari ,2015)<br><br>Ubalozi umeingia gharama ya dola za kimarekani 124,165.16 sawa na shilingi za kitanzania 204,101,448.35 kama malimbikizo yake wakati amestaafu.<br>Kiasi hiki ni mara tatu ya gharama ya kumsafirisha yeye, mizigo na familia yake. | 204,101,448 |
| 4. | Ubalozi wa Tanzania Ottawa, Canada(Fungu 2012) | Alistaafu tarehe 12 Desemba, 2011 na kupewa mkataba wa miaka miwili uliokwisha 12Desemba, 2013. | 137,513,455 |
| 5. | Ubalozi wa Tanzania Washington DC | Amefanya kazi na ubalozi kwa muda wa miezi mitatu (Februari, 2014 mpaka Aprili 2014 | 30,087,962 |
| **Jumla** | | | **543,796,737** |

Kwa kuwa suala hili linasababishwa na upungufu wa fedha za kuwasafirisha watumishi na mali zao baada ya kustaafu na kuchelewa kwa mamlaka ya uteuzi katika kuteua maafisa wapya baada ya wastaafu kumaliza muda wao, ninaishauri serikali kwamba:

- Badala ya kulipa posho za nje kwa wastaafu,Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa izingatie kutumia fedha hizo kuwasafirisha watumishi wastaafu na mali zao.
- Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuomba Ofisi ya RaisMenejimenti ya Utumishi waUmma kuwaongezea wastaafu muda wa kufanya kazi wakiwa wanasubiriaupatikanaji wa fedhakwa ajili ya malipoya gharama za kuwarudisha nyumbani na mizigo yao.
- Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuandaa taarifa ya watumishi wake ambao watatakiwa kustaafu na mpango wa kuwawezesha maafisa wengine kushika nafasi zitakazo achwa wazi na wastaafu hao.

### 7.3.10Watumishi wa ubalozini hawakulipwa kiinua mgongo TZS.13,263,345

Nilibaini watumishi wazawa katika ubalozi wa Tanzania Cairo Misri hawakulipwa TZS 13,263,435 kama kiinua mgongo. Kati ya kiasichaTZS.13,263,435;kiasi cha TZS7,095,230 zilikuwa kwa kipindi kilichoishia Desemba, 2013 na kiasi cha TZS6,168,115 zilikuwa kwa kipindi kilichoishia Juni,2014.Kiasi hiki chote cha TZS.13,263,345 kilitakiwa kulipwa kwa walengwa 11 kama kiinua mgongo hadi kufikia 31, Januari, 2015.

Ninapendekeza kwamba Serikaliihakikishekuwa inalipa kiinua mgongokwa watumishi wa ubalozi mara muda unapofika wa kulipa ili kuimarisha uwajibikaji naufanisi wa shughuliUbalozini.

# SURA YA NANE

# WAKALA WA SERIKALI NA TAASISI NYINGINE

## 8.0 Utangulizi

Sura hii inaeleza matokeo ya ukaguzi wa Wakala za Serikali thelathini na mbili (32), mifuko maalum ya fedha kumi na mbili (12), taasisi nyingine za Serikali kumi na tatu (13) na vyama vya siasa.

Sura hii inazungumzia masuala maalum ambayo yanahitaji ufuatiliaji wa Serikali, Bunge, Bodi ya Ushauri ya Wizara na Uongozi wa Taasisi husika ili kuleta ufanisi katika uendeshaji wa taasisi.

## 8.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Wakala za Serikali

Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi wa wakala za Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

### 8.1.1 Udhaifu wa Bajeti na Upatikanaji wa Fedha

#### 8.1.1.1 Utegemezi wa Bajeti ya Serikali

Vyanzo vya fedha vya wakala wa Serikali ni pamoja na vyanzo vya ndani na misaada toka serikalini (Kawaida na Maendeleo).Hali halisi ya upatikanaji wa fedha kutoka katika kila moja ya vyanzo hivi una athari juu ya utendaji wa jumla wa bajeti ya wakala.

Kwa mwaka huu wa fedha jumla ya makisio ya mapato ya wakala kutokana na vyanzo vya ndani ilikuwa TZS.1,995,813,296,630; ambapo TZS.1,626,924,694,244 sawa na asilimia 82 ilitegemewa kugharamiwa na ruzuku ya serikali na TZS.368,888,602,386 sawa na asilimia 18 ilitarajiwa igharamiwe na vyanzo vya ndani ya wakala.Angalia **Kiambatisho Na.28**

Wakala kutegemea ruzuku za serikali ni kinyume na Kifungu cha 12(2)(a) cha sheria ya Wakala wa Serikali ya Mwaka 1997 ambayo inataka wakala wa serikali kufanya kazi kwa kutumia kanuni za kibiashara na kuhakikisha kila inapowezekana mapato yake yanatosheleza matumizi. Makisio ya jumla ya vyanzo vya mapato ni zaidi ya mapato halisi yanayokusanywa kuwa na nakisi. Ili

kuboresha vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwa ni pamoja na vyanzo vya ndani ni vema kuhakikisha mapato yanalingana na matumizi.

Katika mwaka wa fedha 2013/2014 jumla ya mapato yalikuwa TZS.1,360,424,225,204 sawa na asilimia 68 ya makisio yaliyoidhinishwa, ikiwa na upungufu TZS. 635,389,071,426 sawa na asilimia 32 ya bajeti yote ya mapato haikukusanywa hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Kielelezo kifuatacho kinaonyesha uhusiano kati ya michango ya serikali kuu na makusanyo toka vyanzo vya ndani kwenye jumla ya mapato ya wakala zote zilizopata ruzuku ya shilingi bilioni tano au zaidi katika mwaka wa fedha wa 2013/2014.

*Kielelezo 22: Mchanganuo wa Mapato ya wakala kutoka Serikalini na Mapato ya Ndani*




Kutokana na kielelezo inaonekana wazi kwamba wakala wa barabara (TANROADS) na Wakala wa Ukaguzi wa madini (TMAA) zinaongoza katika orodha ya taasisi zinazopata ruzuku nyingi kutoka serikalini, zote zikipata zaidi ya asilimia 99 ya mahitaji ya kila moja; kwa upande mwingine TEMESA na GPSA zinaongoza kwa

kuchangia kiasi kikubwa cha fedha kutoka pato la ndani ambapo TEMESA ilichangia asilimia 69 na GPSA asilimia 92.

Kielelezo kifuatacho kinaonyesha uhusiano kati ya michango ya serikali kuu na makusanyo ya ndani yenye jumla ya mapato ya wakala zote zilizopata gawio la chini ya shilingi bilioni tano katika mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Kielelezo 23: Mchango wa Mapato kwenye wakala kutoka Serikalini na Mapato ya Ndani 2013/2014




Katika wakala zilizopata chini ya shilingi bilioni tano katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wakala wa Usafiri wa Mabasi yaendayo kasiDar es Salaam (DART) ulipokea asilimia 100 ya fedha zote kutoka Serikalini, ambapo Wakala wa Huduma za Misitu (TFSA) na Wakala wa Maabara za Serikali (TGLA ) walipata asilimia 100 kutoka vyanzo vya ndani vya mapato. Hivyo, inaonekana wazi kwamba wakala zote kwa kiasi kikubwa bado wanategemea serikali kuu katika kutekeleza shughuli zao kinyume na sheria ya kuanzishwa wakala inayotaka wakala zote za serikali kujiendesha kibiashara kwa mujibu wa kifungu cha 12(2)(a) cha sheria ya wakala wa Serikali ya Mwaka 1997.

Baada ya kuona uhusiano huo hapo juu, na ili wakala ziweze kujiendesha kifedha, napendekeza serikali kutoa uhuru zaidi kwa wakala kubuni vyanzo vipya vya mapato na jinsi ya kukusanya mapato hayo.

Wakala ni lazima kuwa na uwezo wa kutambua vyanzo vya mapato visivyotokana na kodi na kufanya kazi kwa ufanisi na tija na hivyo kupunguza utegemezi serikalini.

#### 8.1.1.2 Upungufu wa Mapato Halisi kutoka vyanzo vya ndani TZS.72,186,497,165

Katika mwaka wa fedha 2013/2014 makusanyo halisi ya mapato kutoka vyanzo vya ndani yalikuwa TZS 296,702,105,221 ikilinganishwa na lengo la makusanyo TZS 368,888,602,386 hivyo kuonyesha mapato pungufu kwa kiwango cha TZS 72,186,497,165 sawa na asilimia 20 ya bajeti ya mapato ya ndani iliyoidhinishwa.

Ruzuku ya serikali kuu kwa wakala zote ilikuwa ni TZS 1,063,722,119,983 ambayo ni asilimia 78 ya mapato yote ikilinganishwa na mapato ya ndani ambayo ni asilimia 22 ya makusanyo yote ya wakala.Hali hii inaonyesha ugumu wa wakala kuweza kugharamiamajukumu ya kifedha na kulipa madeni yanayotokea kwa wakati ikiwa ni pamoja na kushindwa kujitegemea kifedha. Angalia **Kiambatisho Na.29**

Kwa ujumla, wakala haziwezi kujiendesha kwa kutegemea vyanzo vyake vilivyopo, hivyo wigo wa vyanzo vipya unapaswa kubuniwa.

Naishauri Serikali kuweka mikakati ambayo itawezesha taasisi zinazopewa huduma na wakala kuwezeshwa kifedha kupitia bajeti ya serikali ili kuweza kulipa madeni yao kwa wakala kwa wakati, pia itawezesha wakala wa serikali kuboresha huduma zake na kununua teknolojia ya kisasa kwa kutoa huduma bora na kwa ufanisi na tija inayotegemewa.

#### 8.1.1.3 Fedha iliyoidhinishwa na Serikali kwa Matumizi ya Kawaida na Maendeleo haikutolewa TZS 563,202,574,261

Makadirio yaliyoidhinishwa kwa matumizi ya kawaida na maendeleo katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 kwa wakala 32 zilizokaguliwa ilikuwa ni TZS 1,626,924,694,244. Mapitio ya taarifa za fedha za wakala ilibainisha kuwa kwa ujumla TZS 1,063,722,119,983 ilitolewa na serikali, ambapo TZS 505,449,374,902 ilitolewa kwa matumizi ya kawaida na TZ 558,272,745,081 kwa matumizi ya maendeleo, ikiwa ni sawa na asilimia 65 ya makadirio, hivyo kiasi cha TZS 563,202,574,261 au asilimia 35 ya bajeti haikupatikana.

Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 kulikuwa na uhaba mkubwa wa fedha zilizotengwa kwa matumizi ya kawaida na maendeleo, wakala hazikuweza kukidhi gharama za lazima za kazi, hii ina maana kwamba shughuli zilizopangwa kutekekelezwa hazikutekelezwa. Angalia **Kiambatisho Na.30&31**

Kwa sababu ya changamoto hizi, kuna uwezekano kwa Wakala wa serikali kushindwa kufikia malengo waliojiwekea. Kwa misingi hiyo Serikali ina wajibu wa kuendelea kuimarisha usimamizi wa fedha na udhibiti wa bajeti za wakala zote na kuwa na utaratibu wa kufuatilia matumizi.

#### 8.1.1.4 Ucheleweshaji wa Fedha za Miradi toka Serikalini TZS.523,923,237

Ukaguzi uligundua mradi unaotekelezwa na Wakala wa Serikali, Tanzania Global Learning Agency (TGLA) haikutekeleza mradi wa Country Level Knowledge Network (CLK Net) kwa sababu serikali haikutoa kwa wakati mchango wake unaofikia TZS 523,923,237 (USD 316,020). Hata hivyo, mradi ulitekelezwa kwa kiasi kidogo kwani African Capacity Building Foundation (ACBF) walitoa mchango wao unaofikia dola za marekani 500,000.

Ninapendekeza kwamba ili kufanikisha utekelezaji wa miradi kwa kiwango kinachotakiwa, serikali haina budi kutoa fedha kama ilivyokubalika kwenye mikataba na kwa wakati ili kufikia malengo yaliyowekwa na mradi kukamilika.

### 8.1.2 Udhaifu Katika Michakato ya Ununuzi

Mchakato wa manunuzi unahusu kusimamia, kuagiza, kupokea, kupitia na kuidhinisha manunuzi ya bidhaa kutoka kwa watoa huduma, pia kutengeneza na kuimarisha mahusiano na wauzaji au watoa huduma na kuhakikisha huduma nzuri kwa wateja. Yafuatayo ni mapungufu yaliyobainika katika mchakato wa manunuzi:

#### 8.1.2.1 Mapungufu katika Mchakato wa Manunuzi

Upungufu ulijitokeza kwenye manunuzi kwa wakala tatu (3) kushindwa kufuata kikamilifu taratibu zilizoainishwa kwenye Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka, 2011 na kanuni zake kama inavyoonekana kwenye **jedwali Na. 39**hapa chini.

Jedwali 39: Muhtasari wa Mapungufu yaliyojitokeza

| Kigezo | Hoja za Ukaguzi | Jina la Wakala | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|---|
| Kifungu cha 67 cha Sheria ya Manunuzi ya Mwaka, 2011 | Manunuzi yaliyofanyika bila kutangazwa kwenye vyombo vya habari. | RITA | 55,488,800 |
| Kifungu cha 49 cha sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2011, na Kanuni ya 70 ya kanuni za sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2013, pamoja na ukomo wa bajeti ya mwaka 2013. | Manunuzo yaliyofanyika nje ya mpango wa manunuzi | GST | 58,715,660 |
| | | WDMI | 122,644,480 |
| Jumla | | | **236,848,940** |

**Chanzo: Taarifa za Ukaguzi za Wakala 2013/2014**

Ninapendekeza Wakala wafuate sheria ya manunuzi ya umma kama inavyotakiwa ili kupata thamani ya fedha inayotegemewa kutoka kwenye manunuzi na kuepuka uzembeunaoweza kujitokeza katika kutekeleza taratibu za manunuzi.

#### 8.1.2.2 Mikataba haikuwasilishwa kwa Wakaguzi

Katika kupitia nyaraka za mikataba ya wakala, ilibainika kuwa Wakala wa Majengo (TBA) na Wakala wa Barabara (TANROADS) walishindwa kuwasilisha mikataba ya ujenzi wa nyumba za ghorofa kwenye mtaa wa SIDA Kinondoni Dar es Salaam na Arusha yenye jumla ya TZS 4,211,278,740 na mikataba mingine yenye thamani ya TZS.19,079,000,000 (Kituo cha mabasi Ubungo – Kigogo

TZS 11,440,000,000; Barabara ya Kawawa – Bonde la Msimbazi – Makutano ya Twiga TZS 7,639,000,000).

Kwa maana hiyo sikuweza kuthibitisha uhalali wa taratibu za manunuzi na malipo yanayohusu mikataba isiyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Hii inaonyesha kuna udhaifu kwenye usimamizi wa wakala husika katika kutunza nyaraka muhimu. Kukosekana kwa nyaraka kunapunguza mawanda ya ukaguzi.

Tatizo la kutokuwa na nyaraka ni kiashiria cha udhaifu katika mifumo ya usimamizi wa ndani. Hili tatizo limekuwasugu, linajirudia kwa Wakala wa serikalikwa muda mrefu.

Ninawakumbusha Menejimenti za Wakala wa serikali wajibu wao wa msingi wa kuhakikisha kuwa nyaraka muhimu kama mikataba inahifadhiwa ipasavyo na inatolewa pindi inapohitajika kwa ukaguzi.

### 8.1.3 Udhaifu katika Usimamizi wa Mali

Kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika sekta ya Umma IPSAS 17,Mali za Kudumu (PPE) ni raslimali yeyote inayomilikiwa na taasisi, ambapo Menejimenti inatarajia kupata faida ya kiuchumi au kuitumia kwa ajili ya utoaji wa huduma kwa umma kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja. Katika kipindi cha mwaka huu wa fedha, mapungufu yafuatayo yalibainishwa katika usimamizi wa raslimali hizi kama ifuatavyo.

#### 8.1.3.1 Ukosefu wa Daftari la Mali za Kudumu

Uhakiki wa mali za kudumu kwenye wakala saba (7), ulionyesha kuwa hakunadaftari la kudumu kuonyesha mali za kudumu katika wakala zifuatazo:

(a) Wakala wa Majengo Tanzania (TBA),
(b) Wakala wa Vipimo (WMA),
(c) Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo (NHBRA),
(d) Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo(TASUBA),
(e) Wakala wa ya Mafunzo ya Uvuvi Bagamoyo (FETA),
(f) Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA),

(g) Taasisiya Uhasibu Tanzania (TIA).

Daftari la mali za kudumu husaidia kuelezea kiasi cha mali za kudumu kwenye taarifa za fedha za wakala.Kukosekana kwa daftari hilo nilishindwa kuthibitisha kiasi sahihi cha mali na kama mali yote iliyojumuishwa katika daftari la kudumu halikutunzwa na kuhuishwa.

### 8.1.3.2 Kutothaminishwa kwa Mali za kudumu za Wakala

Tathimini iliyofanyika ya utunzaji wa mali za kudumu za wakala ilionyesha mali ambazo zimechakaa na ambazo uchakavu umefanyika hadi kubakia na thamani ya sifuri lakini zikiwa bado kwenye hali nzuri ya matumizi. Hii inaleta mashaka juu ya njia ya kukutoa uchakavu iliyotumika.Hata hivyo, kinyume na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika sekta ya Umma (IPSAS) vinavyohitaji kufanya tathmini kila mwaka. Wakala wa Serikali tano hawajafanya tathmini ya mali zake za kudumu kwa muda mrefu kuonyesha hali halisi kwa sasa kama ilivyo kwenye **jedwali Na. 40** hapa chini.

Jedwali 40: Wakala Wenye Mali zisizothaminiwa

| Na | Jina la Wakala | Maelezo |
|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Ufundi wa Mitambo, Magari na Umeme Tanzania (DART) | Magari |
| 2 | Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) | Mali zilizochukuliwa kutoka serikalini wakala ilipoanza |
| 3 | Wakala wa Mafunzo ya Kimataifa Tanzania (TGLA) | Magari na Samani |
| 4 | Wakala wa Maabara za Serikali Tanzania (GCLA) | Kuwepo kwa aina 564 mbalimbali za mali zenye thamani ya shilingi moja |
| 5 | Wakala wa Mbegu za Kilimo Tanzania (ASA) | 945.98 hecta za Ardhi |

Kutoa taarifa ya Mali za wakala wa serikali bila kuwa na thamani halisi inapunguza au kuongeza thamani ya mali zilizotolewa taarifa za fedha na hazionyeshi thamani halisi ya mali zinazomilikiwa na taasisi mwisho wa mwaka wa fedha.

Wakala wanashauriwa kufanya tathmini ya mali zote za kudumu ili kupata thamani halisi kwa ajili ya kuandaa taarifa za fedha zinazoaminika.

#### 8.1.3.3 Ukosefu wa Hatimiliki za Ardhi na Majengo TZS.7,756,510,071

Wakala wa serikali wanamiliki na kusimamia miundombinumuhimu namali za jamiikama vile barabara,majengo, mitambo navifaakwa ajili ya kutoa huduma kwa jamii. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya wakala wanamiliki mali kama zilivyotajwa hapo juu bila kuwa na nyaraka za umiliki wa mali kama vile hati ya ardhi na majengo.

Jedwali 41: Ardhi na Nyumba zisizo na hati miliki

| Na | Jina la Wakala | Maelezo | Thamani (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) | Ardhi na Majengo hayana hati miliki | 7,733,010,071 |
| 2 | Wakala wa Ufundi wa Mitambo, Magari na Umeme Tanzania (TEMESA) | Ardhi haina hati miliki | 23,500,000 |
| 3 | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo | Ardhi na Majengo hakuna hati miliki | - |
| 4 | Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) | Nyumba hakuna hati miliki | - |
| 5 | Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) | Ekari 12,945.98 za ardhi | - |
| | **Total** | | **7,756,510,071** |

Ninaishauri serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi kuhakikisha kuwa mchakato wa kutoa hati miliki kwa wakala wa serikali unakamilishwa kwa haraka kuwahakikishia umiliki.

#### 8.1.3.4 Mali zisizotumika TZS.697,342,50

Matokeo ya ukaguziwa mali katika taasisi tatu ulibaini kwamba mali ya thamani ya TZS.697,342,500zilinunuliwa na wakala lakini hazitumiki na hivyo kutokuwa na thamani ya fedha. Wakala zilizokuwa na mali zisizotumika ni kama ilivyo katika jedwali **Na.42** hapa chini.

Jedwali 42: Mali zisizotumika

| Na | Jina la Wakala | Maelezo | Kiaisi TZS |
|---|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Uandikishaji wa Vizazi na Vifo Tanzania (RITA) | Uchapishaji wa Vyeti vya Kuzaliwa | 219,000,000 |
| 2 | Wakala wa Maabara za Serikali (GCLA) | Kemikali | 283,305,360 |
| 3 | Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) | Vifaa vya Maabara | 195,037,140 |
| | | **Jumla** | **697,342,500** |

Ninashauri menejimenti ya wakala kuhakikisha Mali zisizotumika ambazo zipo stoo zitumike kama zilivyokusudiwa au kama zimemalizika muda taratibu ya kuzifuta zifanyike ili zisilete madhara au hasara zaidi

### 8.1.3.5Madeni Yasiyokusanywa TZS.245,466,456,485

Madeni yasiyokusanywa hupunguza uwezo wa kutekeleza mipango ya taasisi ikiwa ni pamoja na mipango ya kawaida na maendeleo.Kufikia tarehe 30 Juni, 2014 wakala mbalimbali walikuwa na wadaiwa wenye thamani ya TZS 245,466,456,485. Hali hii ina maana kuwa fedha nyingi za wakala zimefungiwa kwenye madeni ya muda mfupi ambayo hayalipiki.

Kwa mfano, Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (NFRA) ina mamlaka ya kununua na kuhifadhi chakula cha dharura hadi tani 150,000 ambacho kitatosha kwa dharura ya miezi mitatu, kipindi ambacho kinaweza kutosheleza uagizaji wa chakula kutoka nje ya nchi.

Kitengo cha Maafa ya Taifa chini ya ofisi ya Waziri Mkuu ina wajibu wa kusambaza misaada ya chakula kwa maeneo yaliyoathirika wakati mwingine bila malipo au kwa malipo kidogo yaani bei chini ya bei ya soko. Ukaguzi umebaini deni kubwa la Wakala wa Hifadhi ya Chakula wa Taifa (NFRA) linatokana na chakula cha ruzuku kwa Kitengo cha Maafa kuanzia mwaka 2008/2009 hadi 2013/2014.

Mfumo wa kutoa taarifa za fedha unataka Wakala wa Chakula kuonyeshakiasi cha wadaiwa na wadai kila wanapoandaataarifa za mwaka, bila kujali kama chakula kilitolewa kwa kusudi gani.

Urejeshwaji wa fedha za madeni haya niwakutiashaka kwani kiasi hiki ni kikubwa na kimekuwepo kwa muda mrefu bila kulipwa. Orodha ya wadaiwa wa mfuko huu ni kama jedwali**Na 43** linavyoonyesha hapa chini.

Jedwali 43: Orodha ya Madeni Yasiyolipwa TZS.245,466,456,485

| Na | **Wakala** | **Kiasi (TZS)** |
|---|---|---|
| 1. | Wakala wa Kuhifadh Chakula (NFRA) | 163,149,355,176 |
| 2. | Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) | 30,655,085,884 |
| 3. | Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) | 20,468,989,957 |
| 4. | Wakala wa Ufundi wa Mitambo, Magari na Umeme Tanzania (TEMESA) | 17,830,213,267 |
| 5. | Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA) | 3,520,674,967 |
| 6. | Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) | 1,874,723,048 |
| 7. | Wakala wa Usalama na Afya Kazini (OSHA) | 1,793,984,727 |
| 8. | Wakala wa Maabara za Serikali (GCLA) | 1,341,468,725 |
| 9. | Wakala wa Hali ya Hewa Tanzania (TMA) | 1,029,613,482 |
| 10. | Chuo Cha Utumishi wa Umma (TPSC) | 879,868,618 |
| 11. | Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) | 835,010,355 |
| 12. | Wakala Wa Uchimbaji wa Visima na Mabwawa (DDCA) | 747,032,290 |
| 13. | Wakala wa Uandikishaji wa Vizazi na Vifo Tanzania (RITA) | 641,593,437 |
| 14. | Wakala wa Mafunzo ya Kimataifa (TGLA) | 418,014,168 |
| 15. | Wakala wa Huduma za Mitandao Serikalini (E-GA) | 91,811,726 |
| 16. | Wakala wa Maabara za Mifugo Tanzania(TVLA) | 77,764,833 |
| 17. | Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania (NHBRA) | 57,370,570 |
| 18. | Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam (DART) | 29,768,394 |
| 19. | Wakala wa Maendeleo na Usimamizi wa Maji Tanzania (WDMI) | 24,112,861 |
| | **Jumla** | **245,466,456,485** |

*Chanzo: Taaarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti 2013/14*

Madeni makubwa yasiyokusanywa yanaweza kuathiri kiwango cha mtiririko wa fedha na utekelezaji wa shughuli zilizopangwa za wakala hivyo kushindwa kufikia malengo ya msingi kutokana na ukwasi wa fedha.

Ninawasihi wakala wa serikali wote kufuatilia na kuhakikisha kuwa wadaiwa wote wanalipa madeni yao ili kuweza kufikia malengo ya kimkakati waliojiwekea.

Mchanganuo unaonyesha kuwa asilimia 83 ya deni la Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (NFRA) linalofikia zaidi ya bilioni mia thelathini na sita (TZS 136.53 bil) ni deni la Idara ya Kudhibiti Majanga - Ofisi ya Waziri Mkuu, Uongozi wa Wakala unashauriwa kuwasiliana na katibu mkuu wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kukubaliana juu ya utaratibu wa jinsi gani madeni haya yatalipwa au kufutwa. Aidha, mamlaka zote zinazoshughulikia usimamizi wa majanga katika nchi ziimarishwe ili kuboresha uratibu wa taasisi hizi na kuimarisha mahusiano yaliyopo ili kuondokana na tishio la madhara makubwa yanayoweza kutokea.

### 8.1.4 Udhaifu Kwenye Madeni Yasiyolipwa

#### 8.1.4.1Madeni Yasiyolipwa TZS 919,133,767,703

Wakala wa serikali 19 zilizofanyiwa ukaguzi zilibainika kuwa na madeni ya wazabuni yapatayo TZS 919,133,767,703.Kuchelewa kwa fedha kutoka serikali kuu na mapato haba kutoka vyanzo vya ndani kwa baadhi ya wakala, husababisha kwa kiasi kikubwa ucheleweshaji wa mipango ya manunuzi ya Wakala. Fedha hutolewa mwishoni mwa mwaka na kwa kiasi kidogo ukilinganisha na mahitaji halisi ya fedha hivyo kufanya madeni yaliyoiva kushindwa kulipwa kwa wakati.
Kiasi kikubwa cha madeni yanaweza kuathiri vibaya utekelezaji wa mipango ya wakala katika kipindi cha miaka ya mbeleni na pia uaminifu kwa watoa huduma kwa wakala wa serikali unapungua. Wakala wa barabara (TANROADS) una deni kubwa zaidi linalofikia hadi asilimia 95 ya madeni yote.

Orodha ya wakala zenye madeni yasiyolipwa ni kama inavyoonyeshwa kwenye **jedwali Na.44hapa chini**.

**Jedwali 44: Wakala wenye Madeni Yasiyolipwa**

| S/N | Wakala | Kiasi ( TZS) |
|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD) | 877,076,570,588 |
| 2 | Wakala wa Akiba ya Chakula (NFRA) | 18,198,776,258 |
| 3 | Wakala wa Ufundi wa Mitambo, Magari na Umeme Tanzania (TEMESA) | 9,554,507,025 |

| S/N | Wakala | Kiasi ( TZS) |
|---|---|---|
| 4 | Wakala wa Hali ya Hewa Tanzania (TMA) | 3,905,839,997 |
| 5 | Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) | 3,096,672,149 |
| 6 | Wakala wa Utafiti wa Miamba Tanzania (GST) | 2,959,060,616 |
| 7 | Wakala wa Maabara za Serikali Tanzania (GCLA) | 1,097,542,027 |
| 8 | Taasisi ya Maendeleo na Usimamizi wa Maji (WDMI) | 835,874,610 |
| 9 | Wakala wa Uandikishaji wa Vizazi na Vifo Tanzania (RITA) | 694,147,254 |
| 10 | Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) | 429,180,303 |
| 11 | Wakala wa Mafunzo ya Kimataifa (TGLA) | 266,853,093 |
| 12 | Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam (DART) | 250,870,887 |
| 13 | Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) | 233,402,559 |
| 14 | Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA) | 221,417,597 |
| 15 | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TASUBA) | 109,030,900 |
| 16 | Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) | 96,917,777 |
| 17 | Wakala wa Huduma za Mitandao Serikalini (E-GA) | 78,966,062 |
| 18 | Wakala wa Maendeleo na Usimamizi wa Elimu (ADEM) | 19,958,000 |
| 19 | Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania (NHBRA) | 8,180,000 |
| | Total | 919,133,767,702 |

*Chanzo: Taarifa za za Hesabu za Wakala wa Serikali 2013/14*

Kuchelewa kulipa mikataba huambatana na riba ya ucheleweshaji kwenye ankara zilizochelewa ambazo hazikulipwa ndani ya muda uliopangwa. Riba inakubalika kisheria na inaongeza gharama halisi ya mkataba na hivyo kusababisha matumizi mabaya raslimali. Kwa mfano, bajeti ya mwaka 2014/15 kulikuwa na malimbikizo ya madeni yasiyolipwa ambayo yalitakiwa kupatiwa kipaumbele katika bajeti mpya ikimaanisha kuna kuchepusha raslimali kutoka mipango ya mwaka wa fedha 2014/15.

Ninaishauri Serikali kushauriana na maafisa masuuli wa Wakala za Serikali kubainisha sababu ya madeni kuongezeka na kuzuia wakala katika juhudi zake za kufikia malengo yaliyokusudiwa. Serikali ihakikishe kwamba inaongeza fedha kwenye bajeti ya wakala ili kukidhi mahitaji ya wakala kifedha.

#### 8.1.4.2 Kesi za madai dhidi ya wakala TZS 125,328,062,447

Ukaguzi ulibaini kuwa wakala watatu (3) wana kesi kwenye mahakama ambapo jumla ya TZS 125,328,062,447 zinaweza kulipwa na wakala endapo watashindwa kesi. Aidha uwezekano wa wadaiwa kulipa madeni haya ni mdogo kutokana na kuwa mali zilizodhaminiwa hazilingani na kiasi cha madai.Iwapo wakala watashindwa katika kesi hizi kuna uwezekano ukaathiri uendeshaji wa wakala kifedha. Muhtasari wa madeni hayo umeonyeshwa katika **jedwali Na 45**hapa chini.

Jedwali 45: **Madeni Yanayotegemea Maamuzi ya Matukio**

| Na | Jina la Wakala | Kiasi TZS |
|---|---|---|
| 1 | **Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS)** | 51, 461,523,863 |
| 2 | Wakala wa Ufundi wa Mitambo, Magari na Umeme Tanzania (**TEMESA)** | 168,000,000 |
| 3 | **Shirika la Ndege Tanzania (TAA)** | 73,698,538,584 |
| **Jumla** | | **125,328,062,447** |

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi za wakala husika 2013/14

Naishauri serikali kupitia kwa Mwanasheria Mkuu na Wizara ya Katiba na Sheria, kutoa msaada wa kitaalamu na kisheria kuhakikisha kuwa kesi zote zilizoko mahakamani zinakamilika kwa wakati.

Kwa upande mwingine nashauri wakala husika kuhakikisha zinafuata sheria za fedha na manunuzi na pia masharti ya mikataba ili kuepusha migogoro na watoa huduma wa wakala.

### 8.1.5 Usimamizi wa Matumizi ya Serikali

Matatizo makubwa yaliyojitokeza katika usimamizi wa matumizi ya serikali ni kama ifuatavyo.

#### 8.1.5.1 Malipo yasiyokuwa na Viambatisho TZS 1,834,653,623

Kufuatana na kanuni 95 (4) ya Kanuni ya Fedha za Umma, 2001 inataka kila hati ya malipo kuwa na viambatisho vya kutosha na kuongeza kuwa malipo yeyote yasiyokamilika kutokana na kukosekana kwa nyaraka yatahesabika kama hati ya malipo iliyokosekana.

Katika ukaguzi huu, nilibaini kuwa wakala wa serikalikumi (10) zilikuwa na malipo yenye nyaraka pungufu ya kiasi cha TZS 1,834,653,623. Kati ya malipo hayo Wakala wa Misitu Tanzania walikuwa na asilimia 33, ikifuatiwa na Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) asilimia 20, na TEMESA asilimia 19, wakala waliobaki kwa pamoja walikuwa na asilimia 7. Kukosekana kwa nyaraka kulisababisha kupunguza mawanda ya ukaguzi.

Orodha ya wakala waliokuwa na malipo yasiyo na viambatisho ni kama ifuatavyo kwenye **jedwali Na 46**hapa chini:

Jedwali 46: Malipo yasiyokuwa na Viambatisho

| Na | Jina la Wakala | Kiasi TZS |
|---|---|---|
| 1. | Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) | 612,639,600 |
| 2. | Chuo Cha Utumishi wa Umma (TPSC) | 366,231,815 |
| 3. | Wakala wa Ufundi wa Mitambo, Magari na Umeme (TEMESA) | 353,451,015 |
| 4. | Wakala wa Uandikishaji wa Vizazi na Vifo Tanzania(RITA) | 262,267,973 |
| 5. | Wakala wa Utafiti wa Miamba Tanzania (GST) | 136,633,656 |
| 6. | Wakala wa Mafunzo ya Uvuvi Tanzania (FETA) | 47,612,800 |
| 7. | Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa (DDCA) | 35,353,696 |
| 8. | Wakala wa Maabara ya Serikali Tanzania (GCLA) | 12,932,267 |
| 9. | Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam (DART) | 4,509,000 |
| 10. | Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA) | 3,022,600 |
| | **Jumla** | **1,834,654,422** |

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi za Wakala Husika 2013/14

Kutokana na kukosekana kwa nyaraka sikuweza kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika.Ninapendakuwakumbusha menejimenti na uongozi wa wakala zote, kufanya jukumu lao la msingi la kuimarisha mifumo ya udhibit ya ndani na kuhakikishamalipo yanakuwa na nyaraka husika.

### 8.1.5.2 Masurufu Yasiyorejeshwa TZS 724,553,473

Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, nimebaini kuwa wakala za serikali tisa (9) zilikuwa na masurufu yasiyorejeshwa kiasi cha TZS 724,553,473;hadi ukaguzi unakamilika Novemba 2014 masurufu haya yalikuwa hayajarejeshwa kinyume na kanuni 103 (1) ya Kanuni za Fedha ya mwaka 2001 inayotaka masurufu kurejeshwa ndani ya siku 14 baada ya kumalizika kwa kazi iliyopangwa.

Orodha ya wakala ambazo zina masurufu yasiyorejeshwa ni kama ilivyoonyeshwa katika **jedwali 47 hapa** chini:

**Jedwali 47: Orodha ya Wakala walio na Masurufu yasiyorejeshwa**

| Na | Jina la Wakala | Kiasi TZS |
|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa (DDCA) | 397,049,070 |
| 2 | Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania (NHBRA) | 175,381,200 |
| 3 | Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFSA) | 54,936,660 |
| 4 | Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) | 32,539,900 |
| 5 | Wakala wa Ukaguzi wa Madini (TMAA) | 22,124,500 |
| 6 | Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam (DART) | 20,118,985 |
| 7 | Wakala wa Mafunzo ya Uvuvi Tanzania (FETA) | 12,382,280 |
| 8 | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) | 7,652,700 |
| 9 | Wakala wa Utafiti wa Miamba Tanzania (GST) | 2,368,178 |
| | **Total** | **724,553,473** |

**Chanzo: Taarifa za ukaguzi za Wakala 2013/14**

Ninashauri maafisa masuuli wa wakala za serikali kuhakikisha utii wa kanuni na sheria kwa kurejesha masurufu mara baada ya kukamilika kwa kazi husika.

### 8.1.6 Usimamizi wa Rasilimali Watu

Mapungufu yaliyojitokeza katika kukagua mwenendo wa rasilimali watu kwenye wakala wa serikali ni uhaba wa watumishi na nafasi kutokujazwa kwa muda mrefu.

#### 8.1.6.1 Uhaba wawatumishi na nafasi kukaa wazi muda mrefu

Uanzishaji wa wakala wa serikali umefungua nafasi nyingi za ajira, kwa maana hiyo idadi ya wafanyakazi inayohitajika ni kubwa. Katika ukaguzi uliofanyika kwenye wakala za serikalitano (5), imeonekana kuwa idadi ya watumishi waliokuwepo ni ndogo kuliko inayohitajika kwa upungufu wa watumishi 775 kama inavyoonekana kwenye jedwali **Na 48lifuatalo**hapa chini:

Jedwali 48: Wakala wa Serikali walio na Ukosefu wa Watumishi

| Na | Jina la Wakala | Idadi ya Watumishi wanaohitajika | Watumishi waliopo | Tofauti |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa Tanzania(DDCA) | 135 | 99 | 36 |
| 2 | Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) | 529 | 324 | 204 |
| 3 | Wakala wa Ufundi wa Mitambo, Magari na Umeme (TEMESA) | 1167 | 684 | 483 |
| 4 | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TASUBA) | 106 | 54 | 52 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5 | Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) | 304 | 170 | 134 |
| | Jumla | 1,937 | 1,161 | 775 |

Chanzo: Taarifa za ukaguzi za Wakala 2013/14

Uongozi wa Wakala wawasilishe upungufu wa watumishi na wawasiliane kwa wakati mamlaka zinazohusika pamoja na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Inashauriwa kuwa uongozi ushirikiane na mamlaka zinazoshughulikia ajira ili kuhakikisha tatizo la ajira linatafutiwa ufumbuzi kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija katika taasisi.

## 8.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Mifuko Maalum ya Serikali (Ring Fenced Funds)

Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi wa mifuko maalum ya fedha kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

### 8.2.1 Muhtasari wa Matokeo ya Ukaguzi wa Mifuko Maalum ya Fedha

Matokeo ya Ukaguzi katika mifuko maalum yamedhihirishakutozingatiwa kwa sheria ya fedha mbalimb ali. Dosari kadhaa zimeainishwa katika taarifa hii. Dosari hizo ni kama ilivyo katika **jedwali Na 49**lifuatalo hapa chini:

Jedwali 49: Muhtasari wa Makosa yaliyojitokeza – Mifuko Maalum

| Kigezo | Hoja iliyojitokeza | Jina la Mfuko | Kiasi TZS |
|---|---|---|---|
| Kanuni No 24 ya Kanuni za Mashine za za risiti (VAT EFD regulation of 2010) | Kutokufuata kwa Kanuni ya Matumizi ya Mashine Maalum ya kutoa risiti (EFD regulation of 2010) | TFF<br>RFB<br>TWPF | 19,032,632<br>213,759,341<br>91,645,707 |
| **Jumla Ndogo** | | | **324,437,680** |
| Kanuni ya 95(4) ya Kanuni ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001 | Malipo yasiyo na viambatisho sahihi | TFF<br>NRF<br>NFA<br>MDEF<br>RFB<br>TWPF | 24,836,797<br>100,980,450<br>24,317,800<br>266,153,000<br>43,844,508<br>88,950,120 |
| **Jumla Ndogo** | | | **549,082,675** |
| Ukomo wa Bajeti | Manunuzi yasiyo kwenye mpango wa manunuzi | AITF | 43,457,534 |
| | Matumizi ya fedha za barabara kwa shughuli nyingine zisizo za barabara yasiyoidhinishwa | RFB | 42,624,460 |
| **Jumla Ndogo** | | | **86,081,994** |

Kuhusu swala la kutokufuata Kanuni 24ya matumizi ya mashine za risiti za kielekroniki, ninaishauri serikali kutoa maelekezo yatakayozuia Wakala wa serikali na Taasisi nyingine za serikali kufanya biashara na taasisi au watu wasiosajiliwa. Pia serikali kuendelea kutoa elimu kwa umma ili jamii waikubali na kuifuata sheria ya matumizi ya mashine za risiti kwa hiari.

Kuhusu swala la kutokufuatwa kwa kanuni 95(4) ya Sheria ya Fedhaya Umma ya mwaka 2001, malipo yenye nyaraka pungufu ninaishauri serikali kwamba fedha zilizohusika zirejeshwe kwenye mfuko wa serikali kutoka kwa wahusika, na hatua za kisheria zichukuliwe. Pia mifumo ya udhibiti ya ndani iimarishwe kwenye taasisi zote zilizohusika ili kuleta ufanisi unaotarajiwa.

Kuhusu swala la kutokuzingatiwa ukomo wa bajeti na mpango manunuzi, ninashauri wakala wa serikali kuzingatia bajeti iliyopitishwa na bunge pamoja na sheria ya manunuzi ili kuboresha utendaji na kuongeza ufanisi.

## 8.3. Matokeo ya Ukaguzi wa Taasisi nyingine za Serikali

Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi wa taasisi nyingine za umma kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

### 8.3.1 Mikopo kwa Wanafunzi haijalipwa kwa Muda Mrefu TZS 7,583,712,118

Shule ya Sheria ya Tanzania ilikuwa na limbikizo la deni la TZS 7,583,712,118.98 mpaka mwishoni mwa Juni 2014.Deni hili lilitokana na kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Shule ya sheria kwa vitendo bila kufuata sheria na utaratibu maalum. Hata hivyo deni la kuanzia mwaka 2011/2012, serikali iliamua kulichukua na kulibadilisha kuwa ruzuku ya serikali kwa miaka inayofuata.

### 8.3.2 Hati za Malipo Zisizokuwa na Viambatisho TZS 839,855,985

Hati za malipo za Chuo cha Mafunzo ya Serikali za Mitaa Hombolo na Baraza la Wafamasia zenye jumla ya TZS 279,871,280hazikuwa na viambatisho. Pia, risiti za mashine za kielektroniki kwa malipo ya kiasi cha TZS 559,984,705 za Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa hazikuwasilshwa kwa uhakiki.

### 8.3.3 Matatizo Kwenye Ukomo wa Bajeti

Changamoto kubwa kwenye ukaguzi wa bajeti ni tofauti kubwa inayoonekana kati ya bajeti iliyoidhinishwa ya mapato na matumizi halisi, hii inaleta wasiwasi kwamba bajeti inayoandaliwa haina uhalisia wa mahitaji halisi ya taasisi.

### 8.3.4 Wadaiwa Wasiolipa na Madeni Yasiyolipwa

Taasisi nne (4) zilikuwa zinadai wateja wake jumla ya TZS.1,317,814,128kwa mauzo ya bidhaa mbalimbali za taasisi, ambazo ni Taasisi ya Mafunzo yaWanyamapori Pasiansi(PWTI), Nyumbu, Taasisi ya Uongozi wa Sheria Lushoto na Shule ya Sheria Tanzania (law School of Tanzania).
Kwa upande mwingine taasisi hizi zina jumla ya madeni yasiyolipwa (wanadaiwa) yanayofikia TZS 1,509,749,326.

### 8.3.5 Kutozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma

Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM- AIST), Baraza la Taifa la Manesi na Wakunga (TNMC),Tanzania Automotive Technology Centre (TATC - Nyumbu) walikuwa mapungufu ya kutozingatia sheria za manunuzi ya serikali yaliyosababisha manunuzi yaliyofanyika nje ya mpango wa Manunuzi ya mwaka TZS 419,757,141.

Orodha ya Taasisi na Muhtasari wa mambo yaliyojitokeza kwenye taasisi ni kama ilivyo kwenye jedwali **Na 50** hapa chini.

Jedwali 50: Matokeo ya Ukaguzi Katika Taasisi Nyingine

| Na | Kigezo | Hoja ya Ukaguzi | Taasisi Nyingine | Kiasi katika TZS |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kanuni No 24 ya Kanuni za Machine za za risiti (VAT EFD regulation of 2010) | Kutokufuatwa kwa sheria ya mashine za risiti (EFD) kwani malipo haya kuambatanishwa na risiti za mauzo za 'EFD'. | Taasisi ya Mafunzo yaSerikali za Mitaa (Hombolo) | 559,984,705 |
| 2 | Kanuni Na 95(4) ya Kanuni ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001 | Kutokufuatwa kwa sheria ya fedha, malipo bila viambatanisho vya mauzo | Baraza la Wafamasia Tanzania | 256,710,580 |
| | | | Taasisi ya Mafunzo yaSerikali za Mitaa (Hombolo) | 23,160,700 |
| **Jumla Ndogo** | | | | **839,855,985** |

| Na | Kigezo | Hoja ya Ukaguzi | Taasisi Nyingine | Kiasi katika TZS |
|---|---|---|---|---|
| 3 | Ukomo wa bajeti | Manunuzi yaliyofanywa nje ya Mpango wa Manunuzi | Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) | 30,035,460 |
| | | | Chama cha Manesi na Wakunga Tanzania (TNMC) | 364,116,660 |
| | | | Nyumbu (TATC) | 25,605,021 |
| **Jumla Ndogo** | | | | **419,757,141** |
| 7 | Wadaiwa wa muda mrefu | Wadaiwa wasiolipa madeni yao | Taasisi ya Mafunzo ya Wanyama Pori Pasiansi | 26,000,000 |
| | | | Nyumbu (TATC) | 668,165,000 |
| | | | Taasisi ya Uongozi wa Sheria Lushoto (IJA) | 442,259,651 |
| | | | Shule ya Sheria Tanzania (TLS) | 181,389,477 |
| **Jumla Ndogo** | | | | **1,317,814,128** |
| 8 | Madeni/wadai wa muda mrefu | Malimbikizo ya madeni yasiolipwa | Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori Pasiansi | 153,969,880 |
| | | | Nyumbu | 355,150,444 |
| | | | Taasisi ya Uongozi wa Sheria Lushoto | 1,000,629,002 |
| **Jumla Kuu** | | | | **1,509,749,326** |

Kutokana na mapungufu hapo juu ninamapendekezo yafuatayo katika kuboresha utendaji wa taasisi za serikali:

- Wakuu wa Taasisi husika wahakikishe kuwa malipo yote yanaidhinishwa na yanaambatanishwa na nyaraka zote muhimu, hii itaboresha usimamizi wa matumizi na ufuatiliaji ndani ya taasisi husika.

- Wakuu wa Taasisi husika wanapaswa kuhakikisha kuwa wateja wanapewa risiti za mauzo mara tu baada ya mauzo, mapato yanakusanywa na kuingizwa kwenye vitabu vya fedha ili kuhakikisha ukamilifu wa mapato yaliyokusanywa na kuboresha

utunzaji wa fedha taslimu ili kuzuia mianya ya upotevu wa fedha za umma na malimbikizo ya wadaiwa.

- Kuhusu manunuzi yaliyofanywa nje ya mpango wa manunuzi, ninaishauri serikali kuhakikisha utiifu na kuzingatia sheria na kufuata bajeti kama ulivyopangwa.

- Ninashauri mikopo kwa wanafunzi wa chuo iratibiwe na kutolewa kwa kuzingatia urejeshaji wa mikopo. Utaratibu wa urejeshaji uwe wazi ili kudhibiti ucheleweshaji wa mikopo.

## 8.4 Ukaguzi wa Vyama Vya Siasa

Kulingana naKifungu Na. 14(1)(b)(i) ya Sheria ya Vyama vya SiasaNa. 5,1992ikijumuishamarekebisho yaliyotolewana SheriaNa. 7, 2009inahitajikila chama cha siasachenye usajili wa kudumu kuwasilisha kwaMsajili wa vyama vya siasataarifa za fedha za chama ili zikaguliwe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuuwa Hesabu za serikali.

Hata hivyo, vyama (12) kati ya vyama 21 ndivyo vilikaguliwa kwa kipindi cha miaka ya fedha ya 2009/2010 hadi 2012/2013 kama inavyoonyesha hapa chini;

1. Chama cha Mapinduzi (CCM)
2. Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA)
3. Chama cha Wananchi (CUF)
4. Chama cha NCCR-MAGEUZI
5. Chama cha TLP
6. Chama cha NRA
7. Chama cha UMD
8. Chama cha APPT - Maendeleo(APPT-MAENDELEO)
9. Chama cha NLD,
10. Chama cha ADC
11. Chama cha Sauti ya Umma (SAU)
12. Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA)

Vyama tisa vya siasa (9), havikuleta taarifa zao za fedha kama ifutavyo;

1. Chama cha UPDP,
2. Chama cha TADEA,
3. Chama cha(UDP)

4. Chama cha Demokrasia Makini (MAKINI),
5. Chama cha Haki na Ustawi (CHAUSTA),
6. Chama cha DP,
7. Jahazi Asilia,
8. Chama cha AFP
9. Chama cha Kijamii (CCK)

**Maoni ya Ukaguzi yaliyotolewa kwa Vyama vya Siasa**

Maoni ya ukaguzi niliyotoa kwa hesabu za vyama vya siasa ni kama yanavyonekana kwenye **jedwali Na51**

Jedwali 51: Hapa chini ni muhtasari wa aina ya maoni ya ukaguzi niliyotoa kufuatia kaguzi za vyama vya siasa kwa kipindi mwaka ulioishia 30 Juni 2010, 2011, 2012 na 2013.

| Na | Chama | 2009/2010 | 2010/2011 | 2011/2012 | 2012/2013 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | CCM | | | | Hati yenye shaka |
| 2 | CHADEMA | | | Hati yenye Mashaka | Hati yenye shaka |
| 3 | CUF | Hati yenye Mashaka | Hati yenye Mashaka | Hati yenye Mashaka | |
| 4 | NCCR | | | | Hati yenye shaka |
| 5 | TLP | | | | Hati yenye shaka |
| 6 | NRD | Hati mbaya | Hati mbaya | Hati mbaya | Hati mbaya |
| 7 | UMD | Hati mbaya | Hati mbaya | Hati mbaya | Hati mbaya |
| 8 | ADC | | | | Hati mbaya |
| 9 | APPT | Hati mbaya | Hati mbaya | Hati mbaya | Hati mbaya |
| 10 | NLD | Hati mbaya | Hati mbaya | Hati mbaya | Hati mbaya |
| 11 | SAU | | Hati mbaya | Hati mbaya | Hati mbaya |
| 12 | CHAUMMA | | | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |

Kwa mwaka wa fedha2013/2014ukaguzi wataarifa za fedha za vyama vya siasa bado unaendelea, sababu kubwa ni kuchelewa kwavyama vya siasa kuwasilisha taarifa za fedha ndani ya muda ulipangwa kisheria.Ripoti ya ukaguzi itatolewa baada ya kukamilika kwa zoezi la ukaguzi.

Ili kuboresha uwasilishaji wa taarifa za fedha za vyama vya siasa, ninaishauri Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kwa kushirikiana na Mhasibu Mkuu wa Serikali kuandaa mwongozo mzuri wa kuandaa taarifa za hesabu. Hii itawezesha kutoa taarifa za fedha kwa ubora unaotarajiwa.

## SURA YA TISA

## USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA

### 9.0 UTANGULIZI

Sura hii inaonyesha matokeo ya mapitio ya taratibu za manunuzi ya umma na usimamizi wa mikataba kama ilivyoonekana kutokana na kaguzi zaWizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa kwa mwaka huu wa fedha.

### 9.1 Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.7 ya 2011 na Kanuni zake za Mwaka 2013

Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 7 ya mwaka 2011 (PPA, 2011) ilianza rasmi kutumika Desemba 15, 2013 kupitia Tangazo la Serikali GN. No. 445 la tarehe 13 Desemba 2013. Kifungu cha 107 (3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma, 2011 kinaweka mwisho ya matumizi ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 (PPA, 2004) pamoja na Kanuni zake za mwaka 2005.
Hivyo ni muhimu kutambua kwamba kutoka Desemba 15, 2013,taasisi zote za Ummazilitakiwa kutekeleza manunuzi kwa kutumia sheria mpya pamoja na kanuni zake za 2013.

Katika kipindi cha mpito Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) ilitoa waraka wa jinsi ya kushughulikia manunuzi yalioanzishwa na Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 kwa mujibu wa kifungu cha 107 na 108 cha Sheria mpya. Waraka huo ulitoa ufafanuzi juu ya manunuzi yaliyoanzishwa na sheria ambayo imefutwa yatakavyokamilishwa.

Kutokana na waraka huo, manunuzi yote yaliyoanzishwa na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2004 na hadi sheria mpya inapitishwa yatakamilishwa na Sheria ya zamani.

### 9.2 Mapungufu yaliobainika katika ukaguzi wa Manunuzi

Ukilinganisha na ukaguzi wa mwaka jana, inaonekana kuwa manunuzi ya umma yameendelea kuwa ni eneo muhimu sana la

kuzingatiwa ili kupata thamani halisi ya fedha za umma. Serikali imefanya juhudi katikakuimarisha kufuata Sheria ya Manunuzi na Kanuni zake katika sekta ya umma kupitia ushauri niliotoa kwenyeripoti zangu za miaka ya nyuma na za Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA).

Pamoja na juhudi hizo, lakini bado kuna baadhi ya ofisi za Serikali ambazo hazifuati sheria za manunuzi kwa umakini na weledi. Kwa mwaka huu kumekuwana matukio yasiyofuata sheria ya manunuzi na kanuni katika kuhakikisha uwazi, ushindani wa haki na thamani ya fedha.

Katika kuhakikisha wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa zinafuata taratibu za manunuzi, Kifungu cha 48(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011, kinaeleza bayana kumtaka mkaguzi wa hesabu kufanya tathmini kwa kila taasisi ya umma kuona uzingatiaji wa taratibu za manunuzi ikiwa ni sheria na kanuni zake katika kaguzi zake za kawaida.

Yafuatayo ni mapungufu yaliyobainika katika ukaguzi wa mwaka huu:

### 9.2.1 Manunuzi yaliofanyika kinyume na Mpango wa Manunuzi wa Mwaka TZS.204,346,797

Kanuni 69 (3) ya PPR, 2013 inazitaka taasisi za manunuzi kuandaa mpango wa manunuzi wa mwaka kwa kujumuisha manunuzi yote kwa kadiri inavyowezekana kama yalivyoainishwa kwenye mpango kazi wa mwaka na kuwekwa kwenye makisio ya mwaka.

Hata hivyo katika ukaguzi wa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa imebainika kuwa taasisi nne (4) zilifanya manunuzi nje ya mpango kazi wenye thamani ya TZS.204,346,797 ambapo taasisi tatu zilitumia TZS.196,583,061 na ubalozi mmoja TZS. 7,763,736 ambayo hayakuwamo kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka kinyume na kanuni tajwa hapo juu. Manunuzi kinyume na mpango wa manunuzi yameorodheshwa kwenyejedwali Na. 52hapa chini.

Jedwali 52: Taasisi zilizofanya Manunuzi nje ya Mpango wa Manunuzi wa Mwaka

| Fungu | Taasisi | Hoja | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|---|
| 97 | Wizara ya Afrika Mashariki | Manunuzi yaliyofanywa nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka | 96,940,255 |
| 29 | Idara ya Magereza | Manunuzi yaliyofanywa nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka | 63,450,000 |
| 80 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara | Manunuzi ya Mafuta nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka | 36,192,806 |
| 2027 | Ubalozi wa Tanzania nchini Abu Dhabi | Manunuzi yaliyofanywa nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka | 7,763,736 |
| **Jumla** | | | **204,346,797** |

*Chanzo: Ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti 2013/14*

Manunuzi nje ya mpango kazi wa mwaka yamepungua kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na ukaguzi wa mwaka jana ambapo ilibainika manunuzi ya TZS.2,748,883,871 yalifanywa na taasisi tatu bila kufuata mpango wa manunuzi wa mwaka. Kuna kupungua kwa kiasi cha TZS. 2,544,539,074,hii inaonyesha ni kwa jinsi gani serikali inavyotumia juhudi kuhakikisha mapendekezo yangu ya ukaguzi yanafanyiwa kazi.

Nashauri taasisi zote kuzingatia mpango wa manunuzi wa mwaka pamoja na kuboresha usimamizi ili kuhakikisha dhana ya uwazi na uwajibikaji katika manunuzi ya umma unakua na kuzoeleka.

Pia nashauri taasisi zihakikishe zinaandaa mpango wa manunuzi wa mwaka unaoendana na bajeti.

### 9.2.2 Manunuzi yaliyofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni TZS.760,868,514

Taasisi tisa (9) zilizokaguliwa, ikiwa ni Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti zilifanya manunuzi yasiyoidhinishwa na bodi ya zabuni kinyume na kifungu 35 (3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni ya 55 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013. Katika ukaguzi wa mwaka huu taasisi zimeongezeka kutoka moja hadi kumi. Taasisi za serikali kuu ziliingia kwenye mikataba mbalimbali isiyoidhinishwa na bodi za zabuni zenye

thamani ya TZS.760,868,514 kama zilivyoorodheshwa kwenye jedwali Na. 53 hapa chini:

Jedwali 53: Taasisi zilizofanya Manunuzi bila idhini ya Bodi ya Zabuni

| Na. | Fungu | Taasisi | Amount(TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | 94 | Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi | 282,788,898 |
| 2 | 48 | Wizara ya Kazi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | 213,331,441 |
| 3 | 28 | Idara ya Jeshi la Polisi | 85,158,950 |
| 4 | 81 | Sekretariet ya Mkoa wa Mwanza | 52,225,487 |
| 5 | 84 | Sekretariet ya Mkoa wa Singida | 48,712,103 |
| 6 | 36 | Sekretariete ya Mkoa wa Katavi | 44,529,472 |
| 7 | 2015 | Ubalozi wa Tanzania Roma, Italy | 14,089,157 |
| 8 | 77 | Sekretariate ya Mkoa wa Mara | 13,958,006 |
| 9 | 31 | Offisi ya Makamu wa Rais | 6,075,000 |
| | | **Total** | **760,868,514** |

*Chanzo: Ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti 2013/14*

Kuingia mikataba bila idhini ya bodi ya zabuni inaweza kusababisha kutoa zabuni kwa wakandarasi wasio na uwezo hivyo kupelekea kukosekana kwa uwazi, ufanisi na malengo yaliyokusudiwa kutofikiwa.

Kwa mamlaka niliyopewa katika Kifungu 35 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2011, ninaishauri serikali na taasisi zake kuzingatia taratibu za manunuzi kwa kushirikisha bodi za zabuni ili kuondokana na mikataba isiyofaa au manunuzi yasio na tija.

### 9.2.3Manunuzi yaliofanyika bila Ushindani TZS. 144,484,478

Kanuni 163 na 164 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inazitaka taasisi za serikali zinazofanya manunuzi kuzingatia upatikanaji wa nukuu za bei zisizopungua tatu kutoka kwa wazabuni tofauti. Katika ukaguzi wangu niligundua taasisi tatu (3) zilifanya manunuzi yenye thamani ya TZS.144,484,478 moja kwa moja kutoka kwa wazabuni bila kupata nukuu ya bei kinyume na kanuni tajwa hapo juu. Baadhi ya taasisi ambazo hazikufuata kanuni hizi zimeorodheshwa kwenye jedwali Na. 54 hapa chini:

Jedwali 54: Manunuzi yasiyo kuwa na ushindani

| S/N | VT No. | Taasisi | Amount(TZS) |
|---|---|---|---|
| 2 | 39 | Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) | 76,820,000 |
| 3 | 2030 | Ubalozi wa Tanzania Lilongwe,Malawi | 39,914,478 |
| 1 | 88 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dar es Salaam | 27,750,000 |
| | | **Total** | **144,484,478** |

***Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti2013/14***

Kwa ujumla, idadi ya taasisi za serikali kuu zilizofanya manunuzi bila ushindanishi zimepungua kutoka tisa (9) katika ukaguzi wa mwaka 2012/13 hadi kufikia tatu (3) katika ukaguzi wa mwaka huu.

Ili kuhakikisha uwazi na upatikanaji wa thamani ya fedha katika manunuzi ya umma nashauri taasisi za manunuzi za umma kufuata ununuzi unaozingatia ushindanishi kama ilivyoelekezwa kwenye sheria ya manunuzi ya umma.

Ni muhimu pia kuhakikisha kunakuwepo na uwazi na thamani ya fedha katika manunuzi na ushauri wangu ni kwa taasisi za manunuzi kuzingatia manunuzi ya kushindanisha wazabuni.

### 9.2.4 Mapokeziya vifaa na huduma visivyofanyiaUkaguzi TZS 534, 899,396

Kanuni ya 244 na 245 ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 zinawataka maafisa masuuli kuteua kamati ya ukaguzi na mapokezi ya vifaaambavyo zitawajibika kukagua, kuthibitisha ubora wa vifaa au huduma na kupokea pindi zinaponunuliwa kutoka kwa wazabuni.

Wakati wa ukaguzi niligundua taasisi sita (6) za serikali kuu zilizofanya manunuzi ya huduma na vifaavyenye thamani ya TZS 534,899,396 bila kufanyiwa utaratibu wa mapokezi na ukaguzi. Muhtasari wa taarifa ya manunuzi unapatikana kwenye jedwali Na.55 hapa chini.

Jedwali 55: Mapokezi ya vifaa visivyofanyiwa ukaguzi

| S/N | Vote | Taasisi | Maelezo | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 6 | Taasisi ya kusimamia Matokeo Makubwa sasa | Vifaa vilivyonunuliwa na kupokelewa bila kufanyiwa Ukaguzi | 314,884,678 |
| 2 | 29 | Idara ya Magereza | Vifaa zilizonunuliwa na kupokelewa bila kufanyiwa Ukaguzi. | 155,110,000 |
| 3 | 83 | Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga | Vifaa zilizonunuliwa na kupokelewa bila kufanyiwa Ukaguzi. | 23,997,370 |
| 4 | 84 | Sekretarieti ya Mkoa wa Singida | Matengenezo ya Magari ambayo hayakufanyiwa ukaguzi baada ya kukamilika | 17,261,501 |
| 5 | 81 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza | Matengenezo ya Magari ambayo hayakufanyiwa ukaguzi baada ya kukamilika | 16,145,847 |
| 6 | 79 | Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro | Vifaa vilivyonunuliwa na kupokelewa bila kufanyiwa Ukaguzi. | 7,500,000 |
| | | | **Total** | **534,899,396** |

*Chanzo: Ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti 2013/14*

Kupokea Vifaa bila kukaguliwa na kukubaliwa na kamati ya ukaguzi na mapokezi ya vifaa na huduma, kunaweza kukatoa fursa kwa taasisi za umma kununua vifaa na huduma zisizokuwa na viwango au zisizofuata mahitaji ya mnunuzi.

### 9.2.5 Utunzaji Usioridhisha wa Kumbukumbu za Michakato ya Manunuzi

Utunzaji wa kumbukumbu za manunuzi kwa taasisi za umma ni suala la lazima kama ilivyoainishwa kwenye kifungu cha 61(1) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011. Pia kifungu hiki kinazitaka taasisi za manunuzi kutunza kumbukumbu zote za taratibu za manunuzi ikiwa ni pamoja na maamuzi yaliyofikiwa na sababu ya uamuzi huo na kwamba taarifa hizi zitahifadhiwa kwa kipindi kisichopungua miaka mitano kuanzia tarehe mkataba ulipoingiwa na zitakuwa tayari kuwasilishwa zitakapohitajika kwa Waziri wa Fedha au Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kumbukumbu za manunuzi katika mfumo wa kutumia karatasi (hard copy) naelektroniki, ni muhimu katika mchakato wenye ufanisi katika manunuzi. Pia kumbukumbu zinatoa ushahidi kwa maamuzi yaliyofanyika wakati wa mchakato wa manunuzi pia kuonyesha mtiririko wa matukio ikiwemo uwazi, uwajibikaji na kufuata kanuni za manunuzi ya umma.

Katika ukaguzi wa mwaka huu taasisi za serikali kuu kumi (10) zimegundulika kuwa hazikufuata Sheria ya Manunuzi ya Umma katika eneo hili; taasisi hizo zimeorodheshwa kwenye jedwali Na. 56hapa chini:

*Jedwali 56: Utunzaji Usioridhisha wa Kumbukumbu za Manunuzi*

| Fungu | Taasisi | Hoja |
|---|---|---|
| 77 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mara | Utunzaji wa mikataba usioridhisha pamoja kumbukumbu/taarifa za miradi |
| 75 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro | Mpango wa manunuzi wa mwaka hakuandaliwa |
| 35 | Kurugenzi ya Mashtaka ya Umma | Utunzaji usioridhisha wa daftari la mikataba |
| 96 | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo | Utunzaji usioridhisha wa daftari la mikataba |
| 48 | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | Taarifa za manunuzi za kila mwezi hazikuandaliwa |
| 72 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma | Daftari la mikataba halikuandaliwa |
| 2034 | Ubalozi wa Tanzania Moroni, Comoro | Mpango wa manunuzi wa mwaka haukuandaliwa pamoja na taarifa za utekelezaji |
| 2025 | Ubalozi wa Tanzania Pretoria, Afrika ya Kusini | Taarifa za manunuzi hazikuandaliwa |
| 2008 | Ubalozi wa Tanzania Maputo, Msumbiji | Mpango wa manunuzi wa mwaka haukuandaliwa pamoja na taarifa za utekelezaji |
| 2002 | Ubalozi wa Tanzania Berlin, Ujerumani | Taarifa za manunuzi hazikuandaliwa |

Chanzo: Ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti 2013/14

Ufanisi wa usimamizikumbukumbuni muhimu ili kuhakikishaunaleta tija katika kuhifadhi, kuzipata unapozihitaji na kutumikakwa kuzingatiausalama, uadilifu na usiri.Kwa hiyo nashauri nimuhimu kwambashughuli zoteza manunuzilazima zitunzwe vizurina taasisi kwa ajili ya kumbukumbubaadaye.

### 9.2.6Manunuzi ya Vifaa na huduma bila ya Mikataba TZS.134,071,510

Kifungu cha 75 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 kinataka bodi ya zabuni kuidhinisha utolewaji wa zabuni za huduma na Vifaa kama ilivyobainishwakatika nyaraka maalum za zabuni. Lakini wakati wa ukaguzi niligundua kuwa taasisi za serikali kuu zipatazo kumi na moja(11) zilifanya manunzi yenye thamani ya TZS.134,071,510 bila ya kuwepo kwa mikataba kati yao na wazabuni wa huduma na vifaa.Jedwali Na. 57hapa chini linaonyesha manunuzi yaliyofanyika bila ya kuwepo kwa mikataba.

*Jedwali 57: Ununuzi wa bidhaa na huduma bila ya kuwepo kwa Mikataba*

| Na. | Fungu | Taasisi | Maelezo | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 2030 | Ubalozi wa Tanzania Lilongwe, Malawi | Malipo yaliofanyika kupitia mkataba ambao ulishapitwa na wakati | 57,284,539 |
| 2 | 96 | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo | Manunuzi yenye mashaka yaliofanyika bila kuwepo kwa mkataba | 29,778,571 |
| 3 | 27 | Msajili wa vyama vya siasa | Mkataba wa kupangisha uliopitwa na wakati | 14,640,000 |
| 4 | 35 | Kurugenzi ya Mashtaka ya Umma | Upangishaji wa nyumba bila mkataba | 14,288,400 |
| 5 | 57 | Wizara ya Ulinzi | Malipo yalifanyika bila kuwepo mkataba uliosainiwa | 9,080,000 |
| 6 | 63 | Sekretarieti ya Mkoa wa Geita | Kukosekana kwa mkataba wa ukodishaji wa magari kwa ajili ya kusafirsha mitihani ya darasa la saba | 4,700,000 |
| 7 | 35 | Kurugenzi ya Mashtaka ya Umma | Ununuzi wa huduma bila kuwapo kwa mkataba | 4,300,000 |
| | | | **Total** | **134,071,510** |

*Chanzo: Ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti 2013/14*

Ni muhimu manunuzi ya umma yakaambatanishwa na nyaraka za kutosha za mikataba ili kama kutatokea mmoja kushindwa kutimiza makubaliano ziweze kukubalika mbele ya sheria.

Ili kushughulikia mapungufu katika kuvunja Sheria za manunuzi katika taasisi za umma, nashauri taasisi zizingatie sheria ya manunuzi ya umma na kanuni zake kwa kuingia makubiliano ya mikataba inayokubalika mbele ya sheria.

### 9.2.7Manunuzi kwa kutumia Masurufu TZS.65,806,202

Ili kuhakikisha mchakato wa manunuziunafuata kanuni za msingi wauwazi, ushindani, uchumi, ufanisi,usawa nauwajibikaji;Kanuni ya 166 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013inaeleza bayanamanunuzimadogo madogo yanaweza kufanyika moja kwa moja kutokamaduka makubwa yanayotambulika, madukaau stoo za dawa, kama thamani yamanunuzihaizidi kikomokilichowekwa katika jedwali la sabalaKanuni hizi.Taasisi inayofanyamanunuziinaweza kutumia masurufu au kadi ya manunuzikufanya manunuzi madogo madogo.Kikomo cha manunuzi madogokilichoruhusiwa nichini ya TZS.5,000,000.

Ukaguzi ulibaini taasisi nne (4) za serikali kuu kufanya manunuzi yenye thamani ya TZS 65,806,202 kwa njia ya masurufu au maofisa wa taasisi kulipwa fedha taslimu kwa ajili ya manunuzi ya bidhaa na huduma kama ilivyonyeshwa kwenye jedwali Na. 58 kinyume na Kanuni 166 ya kanuni za manunuzi ya umma za mwaka 2013

*Jedwali 58: Manunuzi kwa kutumia Masurufu*

| Na. | Fungu | Taasisi | Hoja | Kiasi(TZS) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 36 | Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi | Manunuzi kwa kutumia fedha taslimu | 24,885,202 |
| 2 | 38 | Jeshi la Wananchi wa Tanzania. | Manunuzi kwa kutumia masurufu | 19,000,000 |
| 3 | 80 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara | Manunuzi kwa kutumia masurufu | 14,430,000 |
| 4 | 86 | Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga | Manunuzi kwa kutumia fedha taslimu | 7,491,000 |
| | **Total** | | | **65,806,202** |

*Chanzo: Ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti 2013/14*

Nashauri taasisi za umma kuzingatia sheria ya manunuzi ya umma ili kuweza kuhakikisha kunakuwepo na uwazi na thamani ya fedha katika manunuzi ya serikali.

### 9.2.8Manunuzi Vifaa na huduma toka kwa wazabuni wasioidhinishwaTZS.519,022,745

Taasisi zipatazo tisa (9) zilikiuka Kanuni Na.131 (5) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 inazozitaka taasisi za umma kununua vifaa na huduma kutoka kwa wazabuni walioidhinishwa. Katika ukaguzi wa mwaka huu niligundua taasisi za serikali kuu

zilifanya manunuzi yenye thamani ya TZS 519,022,745 kutoka kwa wazabuni wasioidhinishwa. Manunuzi haya yanajumuisha madawa na vifaa tiba yenye thamani ya TZS 250,763,634 yaliyonunuliwa bila kuidhinishwa na Bohari ya Madawa (MSD) kinyume na kanuni ya 140 na 142 ya kanuni za manunuzi ya umma za mwaka 2013.

Aidha matengenezo ya magari yenye thamani ya TZS 26,722,737 hayakuidhinishwa na TEMESA kinyume na kanuni Na.137 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013. Muhtasari wake umeonyeshwa kwenye jedwali Na. 59 hapa chini:

*Jedwali 59: Manunuzi bidhaa na huduma toka kwa wazabuni wasioidhinishwa*

| Fungu | Taasisi | Hoja | Kiasi (TZS.) |
|---|---|---|---|
| 85 | Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora | Manunuzi ya madawa na vifaa tiba nje ya bohari kuu ya madawa (MSD) | 152,500,014 |
| 82 | Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma | Manunuzi ya vifaa na huduma kutoka kwa wazabuni wasioidhinishwa | 142,641,152 |
| 81 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza | Manunuzi ya madawa na vifaa tiba nje ya bohari kuu ya madawa (MSD) | 83,387,220 |
| 36 | Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi | Manunuzi ya vifaa na huduma kutoka kwa wazabuni wasioidhinishwa | 65,066,430 |
| 81 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza | Manunuzi ya vifaa na huduma kutoka kwa wazabuni wasioidhinishwa | 33,828,792 |
| 87 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera | Manunuzi ya Madawa kwa wazabuni binafsi bila ya kupata kibali kutoka bohari kuu ya madawa (MSD) | 14,876,400 |
| 63 | Sekretarieti ya Mkoa wa Geita | Matengenezo ya Magari yasioidhinishwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) | 12,814,800 |
| 55 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | Matengenezo ya Magari yasioidhinishwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) | 9,021,578 |
| 41 | Wizara ya Katiba na Sheria | Matengenezo ya Magari yasioidhinishwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) | 4,886,359 |
| **Jumla** | | | **519,022,745** |

*Chanzo: ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti*

Nashauri taasisi za Umma kuzingatia sheria ya manunuzi ya umma ili kuhakikisha kuwepo uwazi na thamani ya fedha katika manunuzi ya umma.

### 9.2.9Vifaana hudumazilizolipiwa hazikupokelewaTZS.857,879,731

Taasisi sita (6) zilizokagua,ziligundulika kuwa na vifaa na huduma zenye thamani ya TZS. 857,879,731zilizoagizwa na kulipiwa lakini hazikupokelewa au kukamilika. Makubaliano katika mikataba yanaonyesha utekelezaji ulitakiwa uwe umekamilika kati ya Aprili na Julai 2014;kinyumechake wakandarasi na wazabuni walishindwa kuzingatiamakubaliano hayo na hadi ukaguziunafanyika Desemba,2014 kazi zilikuwa bado kukamilika kama ilivyo katika jedwali 60 hapa chini:

*Jedwali 60:Bidhaa zilizolipiwa hazikupokelewa*

| Fungu | Taasisi | Hoja | Kiasi (TZS.) |
|---|---|---|---|
| 46 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi | Magari yamelipiwa lakini hayakupokelewa | 443,485,463 |
| 73 | Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa | Fedha zilikatwa kwenye akaunti ya Hospitali ya Rufaa Iringa lakini Bohari Kuu ya madawa (MSD) haikupeleka madawa na vifaa tiba | 150,312,900 |
| 61 | Tume ya Uchaguzi | Vifaa vimelipiwa lakini havikupokelewa | 86,800,000 |
| 40 | Mahakama ya Tanzania | Malipo ya awali yalifanyika kwaa jili ya kulipia vifaa vya kuweka kumbukumbu ya mienendo ya kesi mahakamani lakini vifaa havikupokelewa | 85,111,557 |
| 81 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza | Malipo yalifanyika kwa kazi zisizofanyika kuweka umeme kwenye nyumba ya Mkuu wa Wilaya Nyamagana | 47,169,811 |
| 52 | Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii | Vifaa vimelipiwa lakini havikupokelewa | 45,000,000 |
| **Jumla** | | | **857,879,731** |

***Chanzo:*** *Ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti 2013/14*

Kulikuwa na matukioyasiyofuata makubaliano ya mkataba na wajibukwa upande wawazabuni;kushindwa huko kungeweza kufanya wazabuni watakiwe kulipa tozo ya kuchelewesha kazi au bidhaa.Hata hivyo hakuna tozo iliyodaiwa na taasisi toka kwa wakandarasi.

NashauriMaafisaMasuulikuhakikisha kwambawazabuniwanazingatiavipengele vya mikataba nakukamilisha mikataba yao bila kuchelewazaidi.

### 9.2.10 Mapungufu katika Utekelezaji wa Mikataba na Miradi

Taasisi nyingi za serikali ziliendelea kuwa na taratibu za manunuzi zinazopingana na Sheria za Manunuzi ya Ummakatika utekelezaji wa mikataba na miradi.Katika ukaguzi nilibaini mikataba na miradi (33) kutoka katika taasisi za umma ambayo haikukamilika hadi Juni, 2014 licha ya kwamba miradi hiyo ilitakiwa kutekelezwa katika kipindi cha kati ya miezi miwili (2) na kumi na nane (18).

Kuchelewa kukamilika miradi na mikataba kulichangiwa zaidi na kuchelewa kupatikana fedha kutoka Wizara ya Fedha. Kuendelea kuchelewa kwa miradi hii kunaweza kuongeza gharama za mikataba kutokana na mfumuko wa bei pamoja na kuongezeka kwa gharama za vifaa vya ujenzi.

Aidha niligundua mapungufu katika miradi mitatu (3) ya utoaji malipo ya awali ya mkataba pamoja na wakandarasi kutotozwa kwa ucheleweshaji wa kazi na mikataba kama ilivyo katika vipengele vya mkataba.

Pamoja na hayo miradi tisa (9) ilitekelezwa kwa kukiuka vipengele mbalimbali vilivyoanishwa kwenye mikataba. Taarifa za miradi na mikataba zimeorodheshwa kwenye **Kiambatanisho Na.19**

Nazishauri taasisi kukusanya fedha kutoka kwa wakandarasi zinazotokana na tozo ya ucheleweshaji wa kazi pamoja na malipo ya awali ya kazi.

Aidha, nashauri taasisi kuendelea kufanya juhudi za ufuatiliaji rasilimali fedha kutoka hazina ili kuweza kutekeleza miradi iliyopangwa katika bajeti.Nashauri miradi yenye fedha kidogo itekelezwe kwa hatua ili kurahisisha usimamizi wa miradi na ulipaji wake.Hii itawezesha serikali kuepuka gharama zisizo za lazima zinazotokana na mfumuko wa bei pamoja na kuongezeka kwa gharama za vifaa.

### 9.2.11 Taarifa ya PPRA - Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka, 2011 na Kanuni zake za, 2013

Kutokana na mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 9(1)(i)cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka, 2011 Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) ilifanya ukaguzi wa manunuzi katika Wizara na Idara za Serikali zipatazo 17. Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kubainisha kama taratibu, mfumo na kumbukumbu za kuingia mikataba ilifanyika kufuatana na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2011 na Kanuni zake za 2013 na fomu ya mkataba iliyoidhinishwa na PPRA na kama manunuzi yalifanywa kuzingatia uchumi, ufanisi na tija yaani kuweza kupata thamani ya fedha.

Kutokana na vigezo vilivyowekwa na PPRA, Wizara, Wakala na Idara za serikali zimefanya vizuri katika kufuata Sheria ya manunuzi kutoka asilimia 66 mwaka jana hadi 71 mwaka huu. Hata hivyo, matokeo ya mwaka huu yamekuwa chini ya lengo la asilimia 72 lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

**a) Tathmini ya Uzingatiaji wa Sheria**
Tathmini iliyofanywa katika taasisi mbalimbali ilionyesha kuwa maeneo mawili yalikuwa juu ya lengo kufuata taratibu; maeneo hayo ni:
a) Kuanzishwa kwa kitengo cha manunuzi na utendaji kazi wake asilimia 74;
b) Zabuni kufuata utaratibu asilimia 76.

Hata hivyo, maeneo yafuatayo yalifanyika chini ya kiwango kilichowekwa:

*Jedwali 61: Tathmini ya PPRA Uzingatiaji Sheria na Kanuni za Manunuzi*

| Eneo la tathmini | Asilimia ya Uzingatiaji |
|---|---|
| Uandaaji na utekelezaji wa mpango wa mununzi | 69 |
| Usimamizi na utekelezaji wa mikataba | 63 |
| Usimamizi wa kumbukumbu za manunuzi | 53 |
| Utekelezaji wa mifumo ya manunuzi iliyoandaliwa na PPRA | 23 |

**b) Mfumo wa Utunzaji wa taarifa za Manunuzi kielekroniki (PIMS)**
Mfumo wa mtandao ulianzishwa kurahisisha kuwasilisha taarifa PPRA kutoka taasisi za manunuzi kama vile mpango wa manunuzi wa mwaka na taarifa za kila mwezi za robo mwaka. Hata hivyo katika kaguzi zilizopita bado zinaonyesha kuwa taasisi za serikali

hazifuati mifumo hii katika kuwasilisha taarifa zao kwa PPRA. Kama ilivyokuwa kwa mwaka uliopita, taasisi nyingi bado hazitekelezi mfumo wa uwasilishaji wa taarifa kupitia mfumo PMIS na SCM iliyoanzishwa na Mamlaka.

Tathmini ya ukaguzi wa mwaka huu umeonyesha kumefuatwa kwa asilimia 24 kwa taasisi zilizokaguliwa. Mapungufu yalionekana katika maeneo yafuatayo: Asilimia 39 ya taasisi zilizokaguliwa hazikuwasilisha mpango wa manunuzi wa mwaka kwa PPRA; Asilimia 95 ya taasisi zilizokaguliwa hazikuwasilisha taarifa za kukamilika kwa mikataba; halikadhalika asilimia 90 ya taasisi zilizokaguliwa hazikuwasilisha taarifa za mwezi, asilimia 81hazikuwasilisha taarifa za robo mwaka na asilimia 65 hazikuwasilisha taarifa za mwaka mzima.

Sababu zilizotolewa kushindwa kutumika mfumo huu ni pamoja na hizi zifuatazo; ugumu wa mfumo wenyewe siyo rafiki kwa mtumiaji, upungufu wa watumishi PMU, ukosefu wa mtandao wa intaneti, ukosefu wa kompyuta na kukosekanakwa mafunzo ya kutosha kwa watumiaji.

**c) Mapungufu yaliyojitokeza katika Wizara na Idara za Serikali zilizokaguliwa**

Jedwali Na. 62 linaonyesha mapungufu yaliyoonekana na PPRA wakati wa ukaguzi wa manunuzi katika taasisi zilizokaguliwa:

*Jedwali 62: Mapungufu yaliyojitokeza katika Wizara na Idara za Serikali zilizokaguliwa*

| Taasisi za Manunuzi | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|
| Wizara ya Mambo ya Ndani | Ukaguzi ulibaini kuwa mwenyekiti wa bodi ya Zabuni ni inspekta Jenerali wa Magereza ambaye pia ni mtendaji mkuu wa Magereza.Hii ni kinyume na matakwa ya uhuru wa kazi na majukumu. |
| Wizara ya Maliasili na Utalii | Ilibainika kuwa baadhi ya idara ziliendelea na manunuzi bila kuwashirikisha kitengo cha manunuzi na bodi ya zabuni. Kwa mfano kila manunuzi ya tiketi za ndege yalifanyika kwa mkataba moja kwa moja bila idhini ya bodi ya zabuni kinyume na kifungu cha 31 (1) na (2) ya sheria ya manunuzi 2004. |
| Wizara ya Mambo ya Ndani | Mpango wa manunuzi wa mwaka haukuzingatiwa. Baadhi ya manunuzi yaliyokasimiwa kwenye Idara za Jeshi la Polisi, Magereza, Zima Moto na Uokoaji na |

| Taasisi za Manunuzi | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|
| | Uhamiaji hayakujumuishwa kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka wa Wizara. Mpango wa manunuzi wa wizara nzima ulikuwa ni loti 94 lakini wakati wa utekelezaji idadi iliongezeka na kufika loti 796. Ununuzi wa magari ya Polisi haukuonekana kwenye Mpango wa manunuzi ya wizara kinyume na Kifungu cha 45 (b) ya sheria ya manunuzi na Kanuni, 46 (10), na 49 (1) ya GN No, 97 ya mwaka 2005. |
| Wakala wa Manunuzi ya Serikali (GPSA) | Mapungufu yaliyojitokeza katika tathmini ya zabuni. Wazabuni ambao hawakuwasilisha kinga ya Kisheria wakati wa mchakato wa zabuni walipitishwa na kutakiwa kuwasilisha kabla ya kusainiwa kwa mkataba hii ni kinyume na nyaraka za zabuni ambazo zilieleza bayana kuwa zabuni zilitakiwa kuwasiliswha pamoja na nguvu ya Kisheria. Mfano kampuni yaM/s Afro Stationery Manufacturers Ltd ilipewa zabuni ya ununuzi wa milingoti ya bendera ya taifa bila kuwasilisha nguvu ya kisheria pamoja na kupewa siku 60 badala ya 90 ya muda wa halali wa zabuni.<br>• Mifano ya zabuni ambazo kinga ya kisheria hazikuwasilishwa ni AE/005/HQ/2013/2014/G/05 na. AE/005/HQ/2013/2014/G/08 kwa ajili ya ununuzi wa magari and bajaji |
| Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi | Mkataba Na. RAS - 006/2012 / 2013 / HQ / W / 04 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Ilulu ulitolewa kulingana na makadirio ya mhandisi ambayo hayakuwepo kwenye nyaraka za zabuni. Matokeo yake zabuni alipatiwa Mkandarasi Ntina General Enterprises kwa gharama ya TZS. 52,383,000 ikiwa ni asilimia 2 juu ya makadirio ya Wahandisi ya TZS. 51,359,000.00 badala ya M/s Masaho General Supplies and Construction Company Limited kwa garama ya TZS. 49,101,000.00 ambayo ilikuwa chini ya kadirio la Wahandisi kwa asilimia 5. |
| Tume ya Taifa ya Uchaguzi | Nyaraka za Manunuzi zilizopitishwa na PPRA kwa ajili ya manunuzi yanayozidi kiwango cha TZS 80,000,000 hazikutumiwa badala yake wazabuni waliwasilisha Ankara kifani. |

Uchambuzi wa matokeo ya ukaguzi ulionyeshakuwa Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi ilikuwa na utendaji usioridhisha katika kutekeleza sheria ya manunuzi ya umma na kanuni zake. Ingawa awali ilikuwa ikikaguliwa na mapendekezo ya kusaidia kutekeleza sheria ya manunuzi kutolewa, matokeo ya ukaguzi yalionyesha kuwa

mapendekezo yaliyotolewa yalikuwa yakipuuzwa. Kumbukumbu ya matokeo ya ukaguzi zinaonyesha ufanisi kuwa asilimia 31.07 katika mwaka 2012/2013 na asilimia 50.8 katika mwaka 2013/2014.

**Mapendekezo yaliyotolewa na PPRA**

- Taasisi zote za manunuzi ambazo zimefanya vizuri, zipongezwe kwa kazi zao nzuri; na maafisa Masuuli, wenyeviti wa bodi za zabuni wakuu wa vitengo vya manunuzi ambazo hazikufanya vizuri wanatakiwa kutoa maelezo kwa bodi ya wakurugenzi wa PPRA na kuweka mikakati ya kuondoa mapungufu yaliyoonekana.

- Maafisa masuuli wa taasisi iliyofanya vibaya itakiwe kutoa sababu kwanini mamlaka ya manunuzi ya umma isichukue hatua kwa kuhamishia shughuli za manunuzi kwa taasisi yenye uwezo kutokana na kuendelea kujirudia kuvunja sheria ya manunuzi ya umma na kanuni zake. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 20(1) (d) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011.

- Taasisi zote za manunuzi ambazo zimepata chini ya wastani wa asilimia 72 iliyotarajiwa kufikiwa na taasisi zote, wanatakiwa kuwapatia watumishi mafunzo ya jinsi ya kutumia sheria, kanuni, miongozo na mifumo iliyoandaliwa na Mamlaka. Mafunzo haya yatokane na mahitaji ya taasisi inayohusika kutokana na mapungufu yaliyoonekana katika ukaguzi. Gharama za mafunzo hayo zitalipwa na taasisi husika.

- Maafisa Masuuli wa taasisi watakiwe kuandaa mpango kazi au mpango mkakati ndani ya miezi mitatu ya kuwasilisha taarifa za ukaguzi inayokusudia kuhakikisha kufuata sheria na kanuni za manunuzi.

- Ili kuufanya mfumo wa kutunza taarifa za manunuzi kuwa ni mfumo rafiki kwa watumiaji, PPRA inatakiwa kufanya

uchunguzi na kujua ni vitu gani vya kuongeza katika mfumo wa PIMS ili watumiaji wawe na uwezo wa kuutumia mfumo huo.

Kwa ujumla ili kuepuka mapungufu yaliyoonekana hakuna budi kwa wataalamu wa manunuzi na ugavi kuchangia katika kusimamia matumizi ya raslimali chache tulizo nazo kupunguza umasikini, kuboresha maisha ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

### 9.2.12 Taarifa ya Kurugenzi ya Uhakiki mali za Serikali

**Mapungufu katika manunuzi na utunzaji wa bohari/stoo**

Kwa mujibu wa kanuni Na.239-249 ya Kanuni za Fedha za mwaka 2001,Mhakiki mali wa serikali anatakiwa kufanya uhakiki wa mali katika bohari/stoo za taasisi za umma na kutoa taarifa kutokana na uhakiki huo. Katika mwaka wa fedha husika Mhakiki mali wa serikali alifanya uhakiki wa mali katika Wizara kumi na nne (14), Idara sita (6) na Sektretarieti kumi (10) za Mikoa.

Uhakiki wa Mali katika taasisi hizo ulilenga kubaini kama maafisa masuuli husika wanatimiza wajibu wao katika kusimamia kwa kuweka taarifa sahihi za mali. Nimejumuisha taarifa ya mhakiki mali katika taarifa yangu ya ukaguzi ya mwaka huu kama kanuni Na. 245(3) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka, 2001 kwamba; Mhakiki Mali anatakiwa kuwasilisha nakala moja ya taarifa ya uhakiki mali kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kumbukumbu zake, na pia kumpatia nakalaAfisa Masuuli, katibu Mkuu na Mhasibu Mkuu.

Katika kupitia taarifa hiyo nimebaini kwamba mapungufu yaliojitokeza mwaka huu wa fedha yamepungua ikilinganishwa na ukaguzi wa mwaka jana kutoka TZS. 20,103,289,577 hadi kufikia TZS.7,496,106,586, hii inaonyesha kupungua kwa asilimia 63. Taarifa ya mapungufu kwa ufupi yaliyojitokeza yameanishwa kwenye jedwali Na 64 hapa chini:

*Jedwali 63: Taarifa ya Mhakiki Mali*

| Na | Hoja | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|
| 1 | Vifaa vimegawiwa lakini havikupokelewa | 1,867,408,573.64 |
| 2 | Manunuzi ya Vifaa vya Bohari bila kuhesabiwa | 1,741,881,261.11 |
| 3 | Upokeaji wa Vifaa vya Bohari wenye mapungufu ya | 1,459,237,538.00 |

| Na | Hoja | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|
| 1 | Vifaa vimegawiwa lakini havikupokelewa | 1,867,408,573.64 |
| | nyaraka | |
| 4 | Ugawaji wa Vifaa na mafuta usio na nyaraka za kutosha | 552,857,697.00 |
| 5 | Bakaa ya vifaa isiyohesabiwa | 426,564,160.00 |
| 6 | Mafuta ambayo hayajaingizwa katika leja | 415,277,752.83 |
| 7 | Mapokezi ya Vifaa vya Bohari bila kuhesabiwa | 313,494,449.00 |
| 8 | Ugawaji wa Vifaa bila kuingizwa katika leja | 196,401,131.64 |
| 9 | Vifaa vyenye mapungufu | 137,277,660.00 |
| 10 | Vifaa ambavyo vimekopeshwa | 104,525,530.00 |
| 11 | Manunuzi bila ushindanishi wa bei | 70,152,767.00 |
| 12 | Vifaa vimenunuliwa lakini havijapokelewa | 65,785,420.00 |
| 13 | Ukarabati na matengenezo ya magari ya Serikali kwa Karakana binafsi bila kibali kutoka Idara ya matengenezo | 43,462,572.06 |
| 14 | Vifaa vimegawiwa bila kuhesabiwa | 39,186,874.00 |
| 15 | Vifaa ambavyo vimekwisha muda wake | 30,250,000.00 |
| 16 | Uuzaji wa magari wenye mashaka | 11,600,000.00 |
| 17 | Mapokezi ya vifaa bila kuingizwa katika leja | 10,177,800.00 |
| 18 | Bakaa ya vifaa ambayo haijahamishwa | 6,745,400.00 |
| 19 | Upotevu wa kompyuta haukutolewa taarifa | 2,520,000.00 |
| 20 | Vifaa ambavyo havikuingizwa kwa usahihi kwenye leja | 1,300,000.00 |
| | **Jumla kuu** | **7,496,106,586** |

Kwa maelezo zaidi ya Wizara/Idara na Sektretarieti za Mikoa zilizohusika angalia **kiambatisho 20.**

Ili kupunguza na kuepuka upotevu wa vifaa kwa njia ya wizi, matumizi mabaya na udanganyifu, ninapendekeza kwa maafisa masuuli kuimarisha mfumo waudhibiti wa ndani katika manunuzi ili kupunguza mapungufu yaliyoainishwa na Mhakiki Mali wa Serikali.

## SURA YA KUMI

## USIMAMIZIWAMATUMIZI

### 10.0 UTANGULIZI

Mwaka huu wa ukaguzi kama mwaka uliopita kwa mara nyingine tena nimebaini mapungufu katika usimamizi wa matumizi. Sababu za ujumla zinazopelekea mapungufu ya usimamizi wa matumizi katika Wizara, Idara, Wakala, Balozi na Sekretarieti za mikoa ni pamoja na:

- Uhaba wa ujuzi sahihi wa usimamizi wa fedha ndani ya Wizara / Sekretarieti / Balozi
- Upungufu wa uwajibikaji na usimamizi wa manejimenti za taasisi husika.
- Mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani.

Kwa ujumla, pamoja na njia mbalimbali za kukabili mapungufu tajwa hapo juu nashauri kuwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Mkaguzi Mkuu wa Ndani kutoa mafunzo sahihi kwa watendaji, menejimenti na kamati za usimamizi (Kama kamati ya ukaguzi) ili kuhakikisha uelewa na Usimamizi wa mfumo mzuri wa utawala bora unaongezeka.

### 10.1 Mapungufu katika Usimamizi wa matumizi

Katika sura hii, nimewasilisha mapungufu niliyobaini wakati nilipokagua Usimamizi wa matumizi ya Wizara, Idara, Wakala, Balozi na Sekretarieti za mikoa kwa mwaka wa fedha 2013/14.

### 10.1.1Hati za malipo zenye nyaraka pungufu-TZS.7,154,790,996

Kanuni 95(4) ya fedha za Umma, 2001 inabainisha kuwa hati ya malipo ambayo haijakamilika kwa kukosa viambatisho, itachukuliwa kuwa ni hati ya malipo inayokosekana.

Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu nimebaini malipo ya kiasi cha TZS 7,154,790,996 yaliyofanywa na taasisi 17 za Wizara, Idara, na Wakala na Sekretarieti za mikoa 10 yakiwa hayana viambatisho

vyake kinyume na Kanuni 86 ya fedha za umma ya mwaka 2001. Angalia **Kiambatisho 21**

Nyaraka za viambatisho zikikosekana inakuwa vigumu kuthibitisha pasipo shaka uhalali wa malipo hayo hivyo kufanya mawanda ya ukaguzi kuwa finyu. Muhtasari wa miaka mitatu (4) wa mwenendo wa malipo yaliyo na nyaraka pungufu ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na 23** hapa chini:

*Kielelezo 24: Mwenendo wa malipo yaliyo na nyaraka pungufu*




| Mwaka | 2010/2011 | 2011/2012 | 2012/2013 | 2013/2014 |
|---|---|---|---|---|
| Kiasi (TZS) | 8.08bn | 2.12bn | 14.50bn | 7.15bn |
| Taasisi zilizohusika | 23 | 8 | 29 | 27 |

***Chanzo:Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali***

Kutokana na kielelezo hapo juu, kiasi cha malipo yasiyo na viambatisho kwa mwaka wa fedha 2013/14 yamepungua kwa TZS.7.2Bil kutoka TZS.14.4Bilionhadi TZS.7.2Bil ikilinganishwa na mwaka jana, ambapo taasisi zilizohusika zimepungua kutoka 29 mwaka 2012-13 hadi 27 mwaka huu 2013-14. Hii inamaanisha kuwa mfumo wa udhibiti wa ndani kwa kiasi fulani umeimarika.

Ninashauri kuwa Maafisa Masuuli wa taasisi zinanazohusika kuendelea kuimarisha vitengo vya ukaguzi wa nyarakakabla na baada ya malipo.

### 10.1.2 Kukosekana kwa hati za malipo TZS.125,163,277

Kanuni Na.86 (1) ya kanuni za fedha, 2001 inaagiza malipo yote ya fedha za umma kulipwa kwa kutumia hati za malipo, kinyume chake, hati za malipo ya TZS 125,163,277 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Kutokana na kukosekana kwa hati za malipo na viambatisho vyake, ilipelekea kutoweza kubaini uhalali, uhalisia, aina na madhumuni ya matumizi hayo. Jedwali Na 64lifuatalo linaonesha hati za malipo zilizokosekana kwa kila fungu:

*Jedwali 64: Orodha ya Taasisi zenye hati za malipo zinazokosekana:*

| NA | Fungu | Jina | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | Fungu 81 | Sekretarieti ya Mkoamwanza | 89,142,188 |
| 2 | Fungu 95 | Sekretarieti ya Mkoa-Manyara | 29,522,807 |
| 3 | Fungu 85 | Sekretarieti ya Mkoa-Tabora | 3,498,282 |
| 4 | Fungu 89 | Sekretarieti ya Mkoa-Rukwa | 3,000,000 |
| | | **Jumla** | **125,163,277** |

Muhtasari wa miaka minne (4) wa mwenendo wa malipo yasiyo na nyaraka ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na.24** hapa chini:

*Kielelezo 25: Malipo ambayo Hati za malipo zinakosekana*




| **Mwaka wa fedha** | 2010/2011 | 2011/2012 | 2012/2013 | 2013/2014 |
|---|---|---|---|---|
| **Kiasi (TZS)** | 250.8mil | 923.0mil | 70.2mil | 125.2mil |
| Taasisi zilizohusika | 3 | 2 | 3 | 4 |

Kutokana na kielelezo hapo juu, mwenendo unaonesha kuwa tatizo la hati za malipo kukosekanalimeongezeka kwa mwaka 2013/2014 (TZS 125,163,277) ikilinganishwa na mwaka jana 2012/13 (TZS 70,195,394), pia idadi ya taasisi zimeongezeka kufikia 4 mwaka huu kutoka taasisi 3 mwaka jana.

Hata hivyo, kuendelea kwa mapungufu haya kunaonyesha kuwepo kwa udhaifu katika udhibiti wa ndani, Kwa hiyo napenda kuwakumbusha Maafisa Masuuliwa Wizara na Sekretarieti za Mikoa kwamba ni wajibu wao kimsingi kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani ili kuhakikisha nyaraka za fedha zikiwemo hati za malipo zinatunzwa vyema.

### 10.1.3Kukosekana kwa Risiti za Mashine za Kielectroniki TZS.4,095,224,472

Kanuni Na. 28(1) ya Kanuni za Sheria ya Kodi ya Mapato (Mashine za risiti za Kielektroniki) ya mwaka 2012 zinahitaji kila mnunuzi kudai na kuhifadhi risiti au ankara na kuziwasilisha kwa Kamishna au afisa wa kodi aliyeidhinishwa endapo zitahitajika.

Kinyume na hivyo, baadhi ya Wizara na Sekretarieti za Mikoa hazikudai wala kuhifadhi risiti hizo za kielektroniki kwa kila manunuzi waliyoyafanya kwa mwaka huu wa fedha hivyo wanafanya kosa ambalo likithibitika wanaweza kushtakiwa na kwa mujibu wa Kanuni Na. 24 ya Sheria ya Kodi ya Mapato (Mashine za risiti za Kielektroniki), 2012 na kutatakiwa kulipa mara mbili ya kodi iliyokwepwa.

Aidha, kwa kutokudai risiti hizo za kielektroniki kunamaanisha kuwa taasisi hizo za Serikali zinawasaidia wafanyabiashara kukwepa kodi na hivyo kuisababishia Serikali hasara kwa kupoteza sehemu kubwa ya mapato ya kodi kila mwaka.

Katika kipindi cha mwaka 2013/14, nimebainiSekretarieti 5 za Mikoa na Wizara 7 zilifanya malipo ya kiasi cha TZS.4,095,224,472

bila kuambatisha risiti za kielekroniki kutoka kwa wauzaji mbalimbali kama **Jedwali No.65**linavyoonesha kwa muhtasari hapa chini:

Jedwali 65:Taasisi zilizohusika na kufanya manunuzi bila kudai risiti za kielektroniki

| NA. | Fungu No. | Jina la Taasisi | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | Fungu 61 | Tume ya Uchaguzi | 1,892,166,696 |
| 2 | Fungu 23 | Tume ya Maendeleo ya Ushirika | 1,061,444,795 |
| 3 | Fungu 89 | Sekretarieti ya Mkoa-Rukwa | 317,910,623 |
| 4 | Fungu 56 | Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa | 173,134,675 |
| 5 | Fungu 69 | Wizara ya Maliasili na Utalii | 131,283,467 |
| 6 | Fungu 95 | Sekretarieti ya Mkoa-Manyara | 126,537,614 |
| 7 | Fungu 73 | Sekretarieti ya Mkoa-Iringa | 111,402,702 |
| 8 | Fungu 86 | Sekretarieti ya Mkoa-Tanga | 90,745,647 |
| 9 | Fungu 54 | Sekretarieti ya Mkoa-Njombe | 78,632,406 |
| 10 | Fungu 40 | Bunge la Tanzania | 67,562,047 |
| 11 | Fungu 66 | Ofisi ya Rais-Tume ya Mipango | 44,403,800 |
| | | **Jumla** | **4,095,224,472** |

**Jedwali Na. 67:** *Ulinganisho kwa miaka iliyopita:*

| Mwaka | Kiasi (TZS) | MDA/RS |
|---|---|---|
| 2012/13 | 47,935,509,285 | 13 |
| 2013/14 | 4,095,224,472 | 12 |

Kutoka Jedwali No.67 hapo juu, inaonyesha kwamba malipo yaliyokosa risiti za kielektroniki yamepungua kwa kiasi kikubwa kutoka TZS.47,935,509,285 mpaka TZS.4,095,224,472 upungufu wa kiasi cha TZS.43,840,284,813 sawa na asilimia 91, ninaipongeza Serikali kwa juhudi ilizozifanya kufikia mafanikio haya .

Nashauri Serikali iendelee kutoa elimu juu ya utekelezaji wa hiari kuzingatia Kanuni za Sheria ya Kodi ya Mapato (Electronic Fiscal Devices) za mwaka, 2012 kuhusu matumizi ya hiari ya mashine za EFD ambazo zitachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza mapato ya Serikali kama kila manunuzi ya Serikali yataambatana na Risiti.

Pia, ninapendekeza kwamba serikali isiendelee kufanya biashara na wauzaji ambao hawatumii mashine EFD na kutoa risiti za kielektroniki.

### 10.1.4 Malipo katika vifungu vya bajeti visivyostahili- TZS.1,833,544,597

Katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi, nimebaini kuwa, Wizara kumi na tano (15) na Sekretarieti nane (8) za Mikoa zilifanya malipo ya kiasi cha TZS.1,833,544,597 kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na.22** Yalilipiwa kwa kutumia vifungu vya matumizi visivyostahili bila idhini ya mamlaka stahiki, hii ni kinyume na Kanuni 51 (1-8) Kanuni za fedha za umma za mwaka 2001

Kufanyika kwa matumizi nje ya bajeti iliyoidhinishwa kunaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika bajeti husika. Muhtasari wa miaka mitatu (4) wa mwenendo wa malipo yaliyolipwa katika vifungu visivyostahili ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na.25** hapa chini:

Kielelezo 26: Malipo Katika vifungu visivyostahili




| **Mwaka wa fedha** | 2009/10 | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kiasi (TZS) | 5.30bn | 0.34bn | 6.03bn | 2.40bn | 1.83bn |
| Taasisi zilizohusika | 9 | 13 | | 25 | 23 |

Kwa ujumla kwa ya kipindi cha miaka minne iliyopita malipo ya matumizi nje ya vifungu vya bajeti iliyoidhinishwa yamekuwa yakipungua, hata hivyo ninashauri Maafisa Masuuli katika siku zijazo kujiepusha na kufanya matumizi nje ya vifungu vya bajeti iliyoidhinishwa. Endapo italazimu, basi nashauri uhamisho wa fedha kutoka fungu moja kwenda lingine upate idhini ya mamlaka husika kwa mujibu wa kanuni za fedha za umma za mwaka 2001.

### 10.1.5 Matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa TZS.4,956,081,490

Katika ukaguzi wa hesabu za mwaka huu, nimebaini kwamba, Wizara 16 na Sekretarieti 5 za mikoa zimelipa kiasi cha TZS.4,956,081,490 kwa matumizi mbalimbali. Hata hivyo, matumizi haya yalifanyika nje ya bajeti iliyopitishwa bila kutafuta idhini au kibali kinyume na kanuni Na. 46 (3) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2004. Orodha ya taasisi ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na 23**

Hii ina maana kwamba baadhi ya shughuli zilizopangwa hazikuweza kutekelezwa kama zilivyoidhinishwa kwenye bajeti. Muhtasari wa matokeo ya malipo kufanyika nje ya bajeti iliyopitishwa na uliganisho kwa miaka ya nyuma ni kama inavyoonesha katika **Kielelezo No.26** hapa chini:

*Kielelezo 27: Malipo yaliyofanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa*




| Mwaka wa fedha | 2011/2012 | 2012/2013 | 2013/2014 |
|---|---|---|---|
| Kiasi (TZS) | 2,292,796,070 | 15,785,285,943 | 4,956,081,490 |
| Taasisi zilizohusika | 10 | 29 | 21 |

Uchambuzi kutokana na jedwali hapo juu, unaonesha kwamba, idadi ya Wizara/Idara na Sekretarieti za mikoa zilizofanya malipo nje ya bajeti kwa mwaka huu zimepungua kutoka 29 kwa mwaka 2012-13 mpaka 21 kwa mwaka huu 2013/14 sawa kwa TZS 15.8Bil mpaka TZS 4.9Bil.

Hii inaonyesha kwamba kuna uboreshaji katika udhibiti wa kufanya matumizi kwa kuzingatia bajeti. Hata hivyo, bado ipo nafasi ya kuboresha zaidi ili kuhakikisha kwamba bajeti inaandaliwa na inafuatwa ipasavyo.

### 10.1.6 Masurufu yaliyokaa muda mrefu bila kurejeshwaTZS.291,531,914

Kanuni Na. 103 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka, 2001 inahitaji masurufu yote yarejeshwe mapema pindi tu kusudio la masurufu linapokamilika, kinyume na kanuni hii kwa mwaka unaoishia Juni 30, 2014 kulikuwa na Wizara kumi (10) na Sekretarieti ya Mkoa moja (1) ambayo ilikuwa na masurufu

yaliyokaa muda mrefu bila kurejeshwa ya kiasi cha TZS 291,531,914.

Masurufu yasiyorejesha kwa wakati yanaweza kutumika kwa matumizi yasiyokusudiwa. Wizara na Sekretarieti za mikoa zilizohusika ni kama inavyoonekana kwenye jedwali Na. 66hapa chini:

*Jedwali 66:Taasisi zenye masurufu yasiyorejeshwa kwa muda mrefu*

| NA | Fungu Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | Fungu 42 | Bunge | 85,116,810 |
| 2 | Fungu 97 | WizarayaUshirikianowaAfrikaMashariki | 71,080,779 |
| 3 | Fungu 57 | Wizara ya Ulinzi na JKT | 65,672,727 |
| 4 | Fungu 40 | Mahakama ya Tanzania | 35,102,477 |
| 5 | Fungu 34 | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa | 10,321,160 |
| 6 | Fungu 2019 | Ubalozi wa Tanzania- Brussels-Ubelgiji | 5,802,537 |
| 7 | Fungu 51 | Wizara ya Mambo ya Ndani | 5,791,000 |
| 8 | Fungu 38 | Jeshi la Kujenga Taifa | 5,562,424 |
| 9 | Fungu 83 | Sekretarieti ya Mkoa-Shinyanga | 3,941,400 |
| 10 | Fungu 56 | Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | 3,140,600 |
|  |  | **Jumla** | **291,531,914** |

Mchanganuo kwa miaka minne wa masurufu yaliyokaa muda mrefu bila kurejeshwa ni kama inavyoonekana katika **kielelezo Na 27**hapa chini:

*Kielelezo 28: Masurufu yasiyorejeshwa kwa muda mrefu*




| Mwaka wa fedha | 2010/2011 | 2011/2012 | 2012/2013 | 2013/2014 |
|---|---|---|---|---|
| Kiasi (TZS) | 436,398,424 | 806,437,464 | 154,174,697 | 291,531,914 |
| Taasisi zilizohusika | 8 | 4 | 9 | 11 |

Mwenendo wa masurufu yaliyokaa muda mrefu bila kurejeshwa ikilinganishwa na mwaka jana, inaonyesha tatizo kuongezeka kwa TZS.137,357,217 sawa na 89%, wakati huo huo Idadi ya Wizara/Sekretarieti za mikoa zilizohusika zimeongezeka kutoka 9 hadi 11.

Kwa hiyo, ninapendekeza kwamba Wizara/Sekretarieti za Mikoazihakikishekwamba masurufu yanarejeshwa mara tu baada ya kukamilika kwa shughuli iliyokusudiwa kwa kipinidi kisichozidi siku kumi na nnevinginevyo, marejesho ya masurufu yafanywe kupitia makato kwenye mshahara wa mdaiwa wa masurufu hayo kwa mujibu wa Kanuni 103(2) ya Kanuni za Fedha, za umma za 2001

### 10.1.7 Malipo yaliyolipwa zaidi ya kiwango stahiki-TZS.440,721,740

Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu, nilibaini malipo ya kiasi cha TZS 440,721,740 yaliyolipwa zaidi ya kiwango stahiki yakihusisha Wizara tano (5) na Sekretarieti tatu (3) za mikoa. Fedha zilizolipwa zaidi ya kiasi kinachostahili au kwa kazi ambazo hazijafanyika kunapelekea kutofanikisha kwa shughuli zingine

zenye manufaa kwa umma.Malipo zaidi ya kiasi kilichostahili ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 67**hapa chini:

*Jedwali 67:Malipo zaidi ya kiasi kinachostahili*

| NA. | Fungu no. | Description | Kiasi kilicholipwa zaidi (TZS) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Fungu 78 | Sekretarieti ya Mkoa-Mbeya | 268,356,163 | Malipo ya gharama za usafiri kwa dawa ambazo usafiri umeshalipiwa (dawa za TB, ALU ,malaria, UKIMWI) na wafadhili. |
| 2. | Fungu 41 | Wizara ya Katiba na Sheria | 24,359,633 | Malipo mara mbili katika kununua Gari |
| 3. | Fungu 73 | Sekretarieti ya Mkoa-Iringa | 17,911,155 | Malipo makubwa ya bili za maji kupita gharama halisi |
| 4. | Fungu 56 | Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa | 12,948,545 | » TZS.10,278,045 malipo ya ziada kwa watoa huduma na bidhaa na<br>» TZS.2,670,000 malipo ya posho zaidi ya kiasi stahiki. |
| 5. | Fungu 33 | Ofisi ya Raisi-Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi | 9,470,034 | Malipo zaidi ya bei iliyoko kwenye hati ya madai ya ununuzi wa gari |
| 6. | Sub Fungu 2025 | Ubalozi wa Tanzania Pretoria-Afrika kusini | 9,375,560 | Malipo ya tozo ya bima zaidi ya kiwango stahiki |
| 7. | Fungu 63 | Sekretarieti ya Mkoa-Geita | 6,765,000 | Malipo ya posho na bili za huduma zaidi ya kiwango stahiki. |
| 8. | Fungu 92 | Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) | 5,427,970 | Malipo ya ziada zaidi ya kiwango kilichodaiwa kwenye hati za madai. |
| | **Jumla** | | **440,721,740** | |

Mchanganuo wa malipo zaidi ya kiwango stahiki kwa miaka minne (4) iliyopita uko katika **Kielelezo na. 28** hapa chini:

*Kielelezo 29: Mwenendo wa malipo zaidi ya kiwango stahiki*




| Mwaka wa fedha | 2010/2011 | 2011/2012 | 2012/2013 | 2013/2014 |
|---|---|---|---|---|
| Kiasi (TZS) | 126,495,025 | 90,392,726 | 68,089,906 | 440,721,740 |
| Taasisi zilizohusika | 7 | 2 | 5 | 8 |

Kwa kuwa Mwenendo wa malipo zaidi ya kiwango stahiki yameongezeka kwa kiwango kikubwa mwaka huu 2013-14 ikilinganishwa na miaka mitatu iliyopita, nashauri Maafisa masuuli wa taasisi zilizohusika kufuatilia urejeshwaji wa malipo hayo yaliyolipwa zaidi ya kiwango.

### 10.1.8 Matumiziyasiyokuwanamanufaa – TZS.1,698,741,394

Kama ilivyotafsiriwa katika Kanuni Na. 21 ya Kanuni za Fedha, 2001, matumiziyasiyokuwana manufaanimatumiziambayoyamefanyikabilakupatathamaniyafedha nayasingewezakufanyikaendapotahadhariingechuliwamapema.

Kwa mantiki hiyo, tathmini ya hati za malipo na viambatisho vyake, nimebaini kuwa; Wizara kumi na mbili (12) na Sekretarieti za mikoa mbili (2) ( **Kiambatanisho Na24**) zilihusika na malipo yasiyokuwa na manufaa ya kiasi cha TZS.1,698,741,394 kama **Jedwali Na.68**kwa muhtasari linavyoonesha hapa chini:

*Jedwali 68: Ulinganisha wa matumizi yasiyo na faida kwa miaka miwili*

| Mwaka wa fedha | 2012/2013 | 2013/2014 |
|---|---|---|
| **Kiasi (TZS)** | 687,169,796 | 1,698,741,394 |
| **Taasisi zilizohusika** | 10 | 12 |

Ulinganisho hapo juu unaonesha ongezeko kubwa la malipo ya kiasi cha TZS1,011,571,598 kwa matumiziyasiyokuwa na manufaa kwa mwaka 2013/2014 . Ninapendekeza kuwa Manejimenti za Wizara husika &Sekretarieti za Mikoa waimarishe mifumo yao ya udhibiti wa ndani kukabili changamoto hii.

### 10.1.9 Fedha kutumika kwa shughuli zisizokusudiwa TZS.1,562,946,574

Jumla ya kiasi cha TZS.**1,562,946,574**kama ilivyoanishwa kwenye **Kiambatisho 25**hakikulipwa kwa shughuli zilizokusudiwa kinyume na kanuni Na. 115 ya Kanuni za Fedha, 2001 ambayo inahitaji fedha zilizo katika bajeti kutumika tu kwa malengo yaliyokusudiwa, vinginevyo inaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha hizo na kufanya malengo yaliyokusudiwa yasifikiwe.

Mchanganuo wa malipo yaliyolipwa kwa matumizi yasiyokusudiwa kwa mwaka huu ikilinganishwa na mwaka jana ni kama inavyoonesha kwenye **Jedwali Na.69** hapa chini:

*Jedwali 69: Ulinganifu wa malipo yasiyokusudiwa kwa miaka miwili:*

| Mwaka wa fedha | 2012/13 | 2013/14 |
|---|---|---|
| **Kiasi (TZS)** | 1,770,390,504 | 1,562,946,574 |
| | 17 | 18 |

Kutoka kwenye **Jedwali Na.69**hapo juu, inaonesha kuwa malipo kwa kwa shughuli zisizokusudiwa yamepungua kwa kiasi cha TZS.293,551,610 sawa na asilimia 17 ikilinganishwa na mwaka jana 2012/13.

Hata hivyo, Ili kuhakikisha kwamba fedha zote kama zilivyoidhinishwa na Bunge zinatumika kwa matumizi

yaliyokusudiwa pekee na kwa mujibu wa sheria, ninashauri menejimenti ya taasisi zilizokaguliwa kuimarisha mfumo wa udhibiti wa matumizi kwa mujibu wa bajeti kuanzia maandalizi yake mpaka utekelezaji wake, ukiukwaji wowote utambuliwe na ushughulikiwe ipasavyo.

Hata hivyo, ili shughuli zilizokuwa zimepangwa zifanyike, ninapendekeza kwamba fedha zote zilizotumika kwa ajili ya shughuli zisizotarajiwa zirejeshwe na kutumika kwa malengo yayokusudiwa na kuidhinishwa na bunge.

### 10.1.10 Malipo yasiyokuwa na risiti za mapokezi TZS.27,742,156,492

Katika mwaka huu wa ukaguzi, nimebaini malipo ya kiasi cha TZS.27,742,156,492 yalihusisha Sekretarieti tatu (3) za Mikoana Wizara moja (1).

Hata hivyo, malipo haya hayakuambatishwa na risiti kuthibitisha kuwa yalipokelewa na muhusika sahihi kinyume na kanuni Na. 95(4) ya kanuni za fedha za 2001. Ufafanuzi unaonesha kwenye **Jedwali Na. 72**hapa chini:

**Jedwali Na.72:** *Taasisi zilizofanya malipo yasiyokuwa na risiti za mapokezi*

| NA. | Fungu no. | Jina la Taasisi | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1. | Fungu 57 | WizarayaUlinzi na JKT | 27,698,489,526 |
| 2. | Fungu 73 | Sekretarieti ya Mkoa-Iringa | 34,056,966 |
| 3. | Fungu 86 | Sekretarieti ya Mkoa -Tanga | 3,600,000 |
| 4. | Fungu 87 | Sekretarieti ya Mkoa - Kagera | 3,450,000 |
| 5. | Fungu 80 | Sekretarieti ya Mkoa - Mtwara | 2,560,000 |
| | | **Jumla** | **27,742,156,492** |

Pasipokuwepo na risiti za mapokezi, sio rahisi kuthibitisha kuwa malipo yalipokelewa na mlipwaji aliyestahili.

## SURA YA KUMI NA MOJA

## USIMAMIZI MALI NA MADENI

### 11.0 Utangulizi

Sehemu hii ya ripoti inatarajia kuonyesha muhtasari wa matokeo muhimu ya ukaguzi na mapendekezo husika kutokana na ukaguzi wa usimamizi mali na madeni kwa mwaka 2013/14.

### 11.1 Ukaguzi wa Usimamizi wa Mali

Ukaguzi wa usimamizi mali kwa mwaka 2013/14 ulijikita katika mapitio ya kuwepo kwa mali, kutoa taarifa, utambuzi, uainishaji, haki na wajibu, kuonyesha zinavyotumika na thamani ya fedha ya mali zote zilizoonyeshwa katika taarifa za fedha.

Ufuatao ni muhtasari wa mapungufu yalioonekana wakati wa ukaguzi wa usimamizi mali katika wizara, idara na sekretarieti za mikoa kwa mwaka husika;

#### 11.1.1 Magari na pikipiki ambazo zimeegeshwa bila matengenezo

Katika sampuli zilizochaguliwa za Sekretarieti za mikoa mitano (5), wizara tatu na balozi tatu (3), nilibaini vyombo vya moto 380 ambavyo vimefikia ukomo kutumika na baadhi haziwezi kutengenezwa. Maafisa Masuuli bado hawajafanya taratibu za kuziondoa kwa mujibu wa Kanuni Na.254 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma 2001. **Jedwali Na.70**hapa chini linaonyesha orodha ya taasisi ambazo zina mali ambazo zimeegeshwa bila matengenezo.

*Jedwali 70: Taasisi ambazo zina vyombo vya moto ambavyo zimeegeshwa bila matengenezo.*

| Na. | Fungu | Jina | Idadi ya magari na pikipiki | maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 28 | Idara ya Polisi | 333 | 333 Gari |
| 2. | 86 | Sekretarieti ya mkoa wa Tanga | 16 | Pikipiki 14 na gari 2 |
| 3. | 38 | Jeshi la Ulinzi | 11 | Gari 11 |
| 4. | 72 | Sekretarieti ya mkoa | 5 | Gari |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | waDodoma | | |
| 5. | 89 | Sekretarieti ya mkoa wa Rukwa | 5 | 3 pikipiki na gari 2 |
| 6. | 75 | Sekretarieti ya mkoa wa Kilimanjaro | 4 | Gari |
| 7. | 2015 | Ubalozi wa Tanzania Roma | 2 | Gari |
| 8. | 36 | Sekretarieti ya mkoa wa Katavi | 1 | Gari |
| 9. | 31 | Ofisi ya Makamu wa Rais | 1 | Gari |
| 10. | 2007 | Ubalozi wa Tanzania Lusaka Zambia | 1 | Gari |
| 11. | 2022 | Ubalozi wa Tanzania Harare | 1 | Gari |
| | | **Jumla** | **380** | |

*Chanzo: Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2013/2014*

Kwa kuwa kuna uwezekano wa Serikali kupata hasara ya mali kutokana na wizi wa vifaa au kutelekezwa, ninapendekeza Serikali kuhakikisha mali ambazo zinaonekana zinaweza kutumika zifanyiwe matengenezo na ambazo zina hali mbaya ziondolewe kwa mujibu wa kanuni za fedha ili kuepuka hasara zaidi baadaye.

### 11.1.2 Thamani yaArdhi na Majengo kutotenganishwa kwenye Taarifa za Fedha

Aya ya 17 (74) ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu Katika Sekta ya Umma Na.17 (IPSAs 17) inahitaji ardhi na majengo kutenganishwa wakati wa kuandaa taarifa za fedha kwa sababu ardhi haina ukomo wa matumizi na kwa hiyo thamani yake haipungui wakati majengo yana ukomo wa matumizi na thamani yake inashuka.

Mapitio yaliyofanyika katika taarifa za mali kwa sampuli ya taasisi tatu yalibaini thamani ya ardhi na majengo ambayo iliwekwa kimakosa katika kundi moja kinyume na viwango tajwa hapo juu.**Jedwali Na.71**hapo chini linaonyesha mchanganuo wa sampuli taasisi ambazo hazikutenganisha ardhi na majengo.

*Jedwali 71: Taasisi ambazo hazikutenganisha ardhi na majengo.*

| No. | Fungu | Jina | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | 96 | Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo | 39,109,000,000 |
| 2. | 95 | Sekretarieti ya mkoa wa Manyara | 9,310,318,311 |
| 3. | 92 | Tume ya Kudhibiti Ukimwi | 6,093,591,866 |

*Chanzo: Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2013/2014*

Ninaishauri serikali kuhakikisha kwamba Maafisa Masuuli wanatenganisha na kuonyesha katika taarifa za fedha thamani ya ardhi na majengo.

### 11.1.3 Ongezeko lisilo sahihi la thamani ya mali zisizoshikika TZS.46,751,382,233

Aya ya 16 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu Katika Sekta ya Umma Na.31 (IPSAS 31) inaeleza mali zisizoshikika (intangible assets) kama ni mali zinazotambulika bila umbile. Aya ya 129 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu Katika Sekta ya Umma Na.31 (IPSAS 31) inaruhusu utambuzi wa mali zisizoshikika kuanzia kipindi kilichopita.

Nilibaini kwamba Wizara ya Fedha (Fungu 50) imetoa taarifa za mali zisizoshikika katika taarifa ya fedha (Statement of Financial Position) za gharama ya ushauri zinazohusiana na ufadhili wa miundombinu wa 'Millennium Challenge Cooperation' (MCC) wa kiasi cha TZS.46,751,382,233 ikihusisha miaka iliyopita ikiwa ni pamoja na 2013/2014. Utambuzi uliofanyika haukidhi maana ya mali zisizoshikika na kwa sababu hiyo yanatakiwa kutambulika kama matumizi kufuatana na aya ya 18 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu Katika Sekta ya Umma Na.31 (IPSAS 31).
Kukosekana kwa taarifa kamili ya mali kunasababisha mapungufu katika mali za kudumu na hivyo kiasi cha thamani ya mali kilichoonyeshwa katika taarifa ya fedha kinapotosha watumiaji wa taarifa za fedha. Ninapendekeza serikali kufanya juhudi za kuhakikisha kwamba Maafisa Masuuli wanafuata aya ya 18 na ya 129 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Taasisi za Umma Na.31 (IPSAS 31).

### 11.1.4 Mali ambazo hazikuonyeshwa katika taarifa za fedha.

Nilibaini kwamba Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma (Fungu 74) ilipokea mali kutoka UNDP na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambazo zilikuwa zinasubiri kufanyiwa uthamini ambazo hazikuonyeshwa katika taarifa za fedha. Mchanganuo wa mali hizo ni kama zinavyoonekana katika Jedwali Na.72 hapo chini:

*Jedwali 72: Mali ambazo hazikuonyeshwa katika taarifa za fedha.*

| Na. | mali | Ilipokelewa kutoka |
|---|---|---|
| 1. | Toyota Land Cruiser Station Wagon DFP 3264 | UNDP |
| 2. | Toyota Land Cruiser Station Wagon DFP 3908 | UNDP |
| 3. | Toyota Land Cruiser Station Mark II DFP 7994 | TAMISEMI |
| 4. | Toyota Double Cabin STK 8512 | TAMISEMI |
| 5. | Nissan Patrol STK 6543 | TAMISEMI |

*Chanzo: Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2013/2014*

Katika kupitia Mkakati wa Afya wa Kitaifa (Tanzania National Health Strategy) ambao ulianzishwa ili kubadilisha mfumo wa huduma za afya kwa kuinua uwezo wa teknolojia ya mawasiliano kwa kuboresha Afya na Ustawi wa Jamii kwa ajili ya wananchi wote, nilibaini uwepo wa mifumo sita ya programu za kompyuta inayomilikiwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (Fungu 52) ambayo haikuonyeshwa kama mali isiyoshikika (intangible assets) kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 73**hapo chini:

*Jedwali 73: Mali zisizoshikika ambazo hazikuonyeshwa katika taarifa za fedha*

| Na. | Mfumo | Kazi | Idara |
|---|---|---|---|
| 1 | Mfumo wa Taarifa za Afya za Wilaya (District Health Information System) | Kukusanya taarifa kutoka wilayani(HMIS) | DPP – M & E |
| 2 | Mfumo wa taarifa za Rasilimali watu (Human Resource for Health Information System (HRHIS) | Kukusanya taarifa za rasilimali watu | DHR |
| 3 | Mfumo wa Taarifa za Chuo cha mafunzo (Training Institute Information System (TIIS) | Kukusanya wanafunzi,rasilimali watu na mali kutoka katika vyuo vya afya | DHIR |
| 4 | Usajiri wa Kituo cha Afya ( Health Facility Registry (HFR) | Kukusanya taarifa zote za afya | DCS & ICT |
| 5 | Vifaa vya kielektonikia vya usalama katika kuwafikia wagonjwa (Electronic Integrated Decease | Kukusanya kwa haraka taarifa za afya kutoka katika vituo vya afya | DPS – Epidemiology |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Response Surveillance and Response (Eidsr) | | |
| 6 | Mfumo wa kielektonikia katika kusimamia mpangilio wa taarifa (Electronic Logistic Management Information System (Elmis)) | Kukusanya mpangilio wa dawa kutoka Bohari kuu ya dawa kwenda katika wilaya. | Famasia |

***Chanzo: Mkakati wa Afya wa Kitaifa Julai, 2013 - Juni, 2018***

Kwa kuwa kutokuonyeshwa kwa mali hizi kunasababisha pungufu ya mali, ninapendekeza serikalikuwaelekeza Maafisa Masuuli wote waonyesha thamani za mali zote walizonazo katika taarifa za fedha.

### 11.1.5 Uhamisho wa Fedha kwenda kwenye Taasisi kuonyeshwa visivyo TZS.12,810,825,703

Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta za Umma Na.17(IPSAS 17) kinahitaji majengo, mitambo na vifaa vitambuliwe kama mali kama kuna uhakika wa kupata manufaa ya kiuchumi au huduma yatokanayo na mali husika kwa sasa na kwa siku za usoni yatakuja kwenye taasisi husika na kwamba thamani au gharama ya mali iwe inaweza kupimwa kwa uhakika.

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii(Fungu 52) pamoja na Hazina (Fungu 21) walihamisha fedha kiasi cha TZS.7,865,825,703 na TZS.4,945,000,000 kwa mtiririko huo kwenda katika taasisi zilizo chini yake. Uhamisho wa fedha ulionyeshwa kama majengo, mitambo na vifaa katika taarifa za fedha kinyume na mwongozo tajwa hapo juu.

Kutokana na hili kumeifanya taarifa ya fedha isiwe ya kuaminika na kupotosha watumiaji wa taarifa. Hivyo, ninaishauri serikali kuhakikisha kwamba Maafisa Masuuli wanaondoa mapungufu yaliyoonekana katika taarifa za fedha kwa kutofautisha matumizi ya kawaida na ya maendeleo katika Mfumo wa Epicor ambayo yanaonyeshwa katika taarifa za fedha.

### 11.1.6 Ukosefu wa Nyaraka za Umiliki wa Ardhi na Majengo

Wakati wa ukaguzi wa taasisi saba (7) zilizochaguliwa kama sampuli, niligundua ardhi na majengo vinavyomilikiwa bila ya kuwa na nyaraka za umiliki halali wa mali ambazo zinadhibitisha umiliki wa mali zilizoonyeshwa katika hesabu. Kutokana na ukosefu wa nyaraka zinazodhibitisha umiliki halali wa mali, nimeshindwa kujiridhisha kama mali hizo zinamilikiwa na taasisi husika. Hii inaonyesha kwamba taasisi hizo hazina umiliki wa kisheria wa ardhi na majengo.

Hati miliki za ardhi na majengo yanayomilikiwa na serikali hazijapatikana mpaka sasa ingawa niliishauri serikali kupata hati hizo katika mapendekezo yangu ya miaka iliyopita. **Jedwali Na.74** linaonyesha orodha ya taasisi ambazo hazina nyaraka za umiliki wa ardhi na majengo.

*Jedwali 74:Taasisi ambazo hazina nyaraka za umiliki wa ardhi na majengo.*

| Na. | Fungu | Jina |
|---|---|---|
| 1. | 26 | Ofisi ya Makamu wa Rais |
| 2. | 35 | Kurugenzi ya Mashtaka ya Umma |
| 3. | 55 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora |
| 4. | 59 | Tume ya Marekebisho ya Sheria |
| 5. | 96 | Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo |
| 6. | 85 | Sekretarieti ya mkoa wa Tabora |
| 7. | 86 | Sekretarieti ya mkoa wa Tanga |
| 8. | 2030 | Ubalozi wa Tanzania Lilongwe |

***Chanzo: Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2013/2014***

Serikali inashauriwa kuhakikisha kwamba taasisi zote zinapata nyaraka za umiliki ili kulinda mali za serikali.

### 11.1.7 Rejista ya Mali za Kudumu Kutojazwa kwa wakati

Kanuni Na.265 (2) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 inaelekeza kuweka kumbukumbu sahihi wakati wa kuhamisha mali kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Kumbukumbu hizi ni pamoja na tarehe ya kuhamisha.

Pia, waraka wa uhasibu Na. 3 wa mwaka 2013/2014 kuhusu kufunga hesabu za mwaka 2013/2014 unaelekeza Maafisa Masuuli kuhakikisha kwamba rejista ya mali za kudumu inaonyesha thamani ya mali kama inavyoonekana katika Taarifa za Fedha hasa mizania ya hesabu(Statement of Financial Position).

Hata hivyo, rejista ya mali za kudumu kutoka katika taasisi nne zilizokaguliwa kama zinavyonekana katika **Jedwali Na.75** hapa chini haziaminiki, kwa kuwa taarifa zilizoko kwenye Taarifa za Fedha zinatofautiana na taarifa zilizoko katika rejista ya mali za kudumu.

*Jedwali 75: Taasisi ambazo taarifa zake za mali zinatofautiana na taarifa iliyopo katika rejista ya mali za kudumu*

| **Na.** | **Fungu** | **Jina** | **Mali kama ilivyo katika taarifa za fedha (TZS)** | **Mali kama zinavyoonekana katika rejista ya mali za kudumu (TZS)** | **Tofauti (TZS)** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 92 | Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania | 9,023,570,352 | 9,284,031,877 | 260,461,525 |
| 2. | 37 | Ofisi ya Waziri Mkuu | 31,808,947,203 | 31,747,844,097 | 61,103,106 |
| 3. | 63 | Sekretarieti ya Mkoa wa Geita | 2,012,781,204 | 2,008,947,954 | 3,833,250 |

*Chanzo: Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2013/2014*

Nilibaini zaidi kwamba rejista ya mali za kudumu katika Wizara na idara tisa(9), balozi nane(8) na Sekretarieti za Mikoa miwili(2) hazikuweza kuweka kumbukumbu zake za mali kuendana na wakati kama zinavyoonekaana hapa chini katika **Jedwali Na.76:**

*Jedwali 76: Taasisi ambazo rejista ya mali za kudumu haziendani na wakati*

| **Na.** | **Fungu** | **Jina** |
|---|---|---|
| 1. | 14 | Kitengo cha Zimamoto |
| 2. | 21 | Hazina |
| 3. | 26 | Ofisi ya Makamu wa Rais |
| 4. | 31 | Ofisi ya Makamu wa Rais |
| 5. | 33 | Sekretarieti ya Maadili ya Umma |
| 6. | 50 | Wizara ya Fedha |
| 7. | 52 | Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii |
| 8. | 61 | Tume ya Taifa ya Uchaguzi |
| 9. | 98 | Wizara ya Ujenzi |
| 10. | 72 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma |
| 11. | 83 | Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga |
| 12. | 2002 | Ubalozi wa Tanzania Berlin |

| | | |
|---|---|---|
| 13. | 2003 | Ubalozi wa Tanzania Cairo |
| 14. | 2005 | Ubalozi wa Tanzania Abuja |
| 15. | 2009 | Ubalozi wa Tanzania Moscow |
| 16. | 2013 | Ubalozi wa Tanzania Brasilia |
| 17. | 2014 | Ubalozi wa Tanzania Beijing, China |
| 18. | 2015 | Ubalozi wa Tanzania Roma |
| 19. | 2029 | Ubalozi wa Tanzania Muscat |

*Chanzo: Taarifa za Fedha, rejista ya mali za kudumu kwa mwaka wa fedha 2013/14*

Ninapendekeza serikali kuhakikisha kwamba rejista ya mali za kudumu inalinganishwa mara kwa mara na taarifa za fedha za mali zinazoonyeshwa katika vitabu vya hesabu vinatakiwa kulingana na kiasi kinachonekana katika rejista ya mali za kudumu na Maafisa Masuuli wa taasisi husika kuzingatia Kanuni Na.265 (2) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 katika kuhuisha rejista ya mali za kudumu.

### 11.1.8 Mali za Kudumu ambazo hazina alama za utambulisho TZS.10,614,563,419

Mifumo ya utunzaji wa mali na udhibiti husaidia taasisi kusimamia mitaji yao na kuwaruhusu kufanya maamuzi kutokana na taarifa sahihi kuhusu mali zilizopo. Hii ni kama vile ni wakati gani wa kukarabati au kuzibadilisha mali.Pia husaidia kufuatilia na kuzuia wizi wa mali.

Faida nyingine ya kutumia mfumo wa usimamizi wa mali zikiwa na utambulisho ni pamoja na: kuongeza ufanisi kwa wafanyakazi na mali, kupunguza muda wa kukaa bila kazi kwa vifaa kupitia mipango bora, kuzuia wizi na kuimarisha usalama wa mali na inasaidia kufuata sheria zinazotakiwa.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini Wizara tatu(3), idara mbili(2), balozi tatu (3) na Sekretarieti ya Mkoa mmoja ambazo zilikuwa na mali ambazo hazina utambulisho kama zinavyoonekana katika **Jedwali 77** hapa chini:

*Jedwali 77: Taasisi ambazo rejista ya mali za kudumu haziendani na wakati*

| Na. | Fungu | Jina | Kiasi(TZS) |
|---|---|---|---|
| 1. | 52 | Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii | 9,492,472,682 |
| 2. | 6 | Taasisi ya Rais ya kusimamia matokeo makubwa sasa ( President's Delivery Bureau (PDB) | 621,382,863 |
| 3. | 2034 | Ubalozi wa Tanzania Moroni Moroco | 160,499,237 |
| 4. | 39 | Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii | 125,000,000 |
| 5. | 2025 | Ubalozi wa Tanzania Pretoria Afrika Kusini | 95,748,770 |
| 6. | 16 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu | 51,756,100 |
| 7. | 70 | Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha | 50,540,800 |
| 8. | 2008 | Ubalozi wa Tanzania Maputo Msumbiji | 9,115,367 |
| 9. | 62 | Wizara ya Uchukuzi | 8,047,600 |
| | | **Jumla** | **10,614,563,419** |

*Chanzo: Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2013/2014*

Ninapendekeza serikali kuhakikisha kwamba mali zote zilizopo katika Wizara, Idara, wakala, balozi na Sekretarieti za Mikoa zinapatiwa namba maalumu za utambulisho.

### 11.1.9 Upungufu wa fedha za ukarabati wa majengo ya serikali na kuendeleza viwanja vya serikali katika balozi za Tanzania nje ya nchi.

**a) Upungufu wa fedha za ukarabati wa majengo ya serikali**

Serikali haikutenga fedha za kutosha kukarabati nyumba katika balozi nane(8). Pia, serikali haina mkakati wa ukarabati na matengenezo ya nyumba zake nje ya nchi, hii inasababisha nyumba hizo kuwa katika hatari ya kuchakaa kabisa. Kati ya balozi 34 zilizokaguliwa, nyumba katika balozi nane (8) sawa na asilimia 23 ziko katika hali mbaya na zinahitaji matengenezo kama zinavyoonekana hapo chini katika **Jedwali Na.78:**

*Jedwali 78: Nyumba za serikali ambazo ziko katika hali mbaya*

| Na. | Fungu | Jina | Nyumba ambazo ziko katika hali mbaya |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | 2002 | Ubalozi wa Tanzania Berlin | Nyumba ya Mkuu wa Utawala Ubalozini |
| 2. | 2007 | Ubalozi wa Tanzania Lusaka Zambia | Nyumba Na. 5200 United Nations Avenue; Na. 488A 31 Leopards Close; Na. 3821 Manda Hill; Na. 6829 Katima Mulilo; Na. 10E, 377A Chitemwiko Close; Na. 127 Mwambula Road; Na. 131 barabara ya Mwambula; Na. 126 barabara ya Mwambula ; Na. 130 barabara ya Mwambula |
| 3. | 2008 | Ubalozi wa Tanzania Maputo Msumbiji | Nyumba ya balozi na nyumba ya Mkuu wa Utawala Ubalozini |
| 4. | 2019 | Ubalozi wa Tanzania Brussels Ubeligiji | Jengo la Ofisi ubalozini na nyumba ya balozi |
| 5. | 2022 | Ubalozi wa Tanzania Harare Zimbabwe | 23 Baines Avenue, 13 barabara ya broadlands , 7 barabara ya Chalfont , 6 Allan Wilson,7 Alum Close,8 Glen Helen way,6 Wrentham,91 Churchil Avenue |
| 6. | 2023 | Ubalozi wa Tanzania Nairobi Kenya | Nyumba zinazo milikiwa na ubalozi wa Tanzania Khartoum Sudan : Nyumba ya balozi na nyumba ya Mkuu wa Utawala Ubalozini ambazo zinasimamiwa na Ubalozi wa Tanzania Nairobi Kenya |
| 7. | 2025 | Ubalozi wa Tanzania Pretoria Afrika Kusini | 845 Government Avenue -Arcadia, Pretoria; 147 Nicolete Street, Mayers Park-Pretoria; 846 Thomas Street, Arcadia, Pretoria (SMZ House) and Edenvile - Johannesburg (ATC House) |
| 8. | 2030 | Ubalozi wa Tanzania Lilongwe Malawi | Nyumba ya balozi,nyumba ya mhasibu wa ubalozi na nyumba ya Mkuu wa Utawala Ubalozini |

*Chanzo: Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2013/2014*

Nyumba hizo kama hazitafanyiwa matengenezo haraka utatokea uharibifu zaidi na kupelekea matengenezo makubwa zaidi. Hii itashusha morali wa kufanya kazi na kuathiri ufanisi wa wafanyakazi katika kufanya shughuli zao za kila siku kama wawakilishi wa Tanzania nje ya nchi.

**b) Viwanja vya serikali ambavyo havijaendelezwa nje ya nchi.**

Serikali inamiliki viwanja ambavyo bado havijaendelezwa, ambavyo ni kiwanja Na. 157/1CT Maputo Msumbiji , Kiwanja kwa ajili ya Mkuu wa Utawala katika ubalozi wa Tanzania Lilongwe Malawi na kiwanja Na. 38 A 11 CA cha Ubalozi wa Tanzania Moroni, Comoro.

Serikali inashauriwa kuwa na mpango wa ujenzi wa nyumba zake nchi za nje na kuweka kwenye bajeti ya maendeleo gharama za matengenezo ya nyumba za serikali nchi za nje na kutenga fedha katika bajeti ya maendeleo kwa ajili ya matengenezo makubwa ya nyumba kwenye balozi nje ya nchi.

Pia napendekeza serikali kuviendeleza viwanja vyake nje ya nchi, na kutokana na uhaba wa fedha serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ifikirie kuweka uzio ili kulinda viwanja hivyo.

### 11.1.10 Mali za Kudumu zilizonunuliwa lakini hazitumiki TZS.240,112,734

Taasisi mbili za serikali kuu zilinunua mali za thamani ya TZS.240,112,734 ili kuongeza ufanisi katika kutoa huduma. Hata hivyo, mali hizo hazikutumika baada ya kununuliwa. Mchanganuo wa mali hizo na taasisi zilizokaguliwa ni kama zilivyoelezewa katika **Jedwali Na.79** hapa chini.

*Jedwali 79: Taasisi zilizonunua mali za kudumu ambazo hazitumiki.*

| Fungu | Jina | Maelezo | Kiasi(TZS) |
|---|---|---|---|
| 28 | Idara ya Polisi | Jengo jipya la kituo cha polisi | 92,442,734 |
| 46 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi | mashine ya uchapishaji Kisomo (Press) Mwanza | 73,910,000 |
| 28 | Idara ya Polisi | kamera 73 za kielektroniki | 73,760,000 |
| | | **Jumla** | **240,112,734** |

*Chanzo: Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2013/2014*

Kwa kuwa thamani ya fedha haijaonekana na lengo halijafikiwa, serikali inashauriwa kuhakikisha mali zilizonunuliwa zinatumika ipasavyo.

### 11.1.11 Vifaa vilivyonunuliwa ambavyo havikuingizwa katika vitabu vya stoo TZS.329,406,602

Lengo la serikali katika kusimamia vifaa ni kulinda vitu vilivyohifadhiwa kutokana na hasara, uharibifu, wizi au upotevu

na kusimamia uhamishwaji wa vifaa kwenda kwa watumiaji kwa njia iliyo rahisi na ya haraka.

Hata hivyo, sampuli nane zilihusisha Wizara, idara tano na Sekretarieti za Mikoa mitatu hazikuingiza kwenye vitabu vya stoo manunuzi ya TZS.329,406,602 kinyume na kanuni Na. 198 ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001.

Matokeo ya ukaguzi yalionyesha kutokuwepo kwa usimamizi madhubuti kuhusu vifaa katika Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa ambayo yameongezeka kwa asilimia 123 ikilinganishwa na ukaguzi wa mwaka jana. Kwa matumizi hayo ya kiasi kikubwa cha fedha za umma katika manunuzi ya vifaa, ni muhimu kuzingatia kuingiza kwa wakati kwenye vitabu vya stoo manunuzi yote ya umma na kuwepo na matumizi bora ya rasilimali katika kutoa huduma kwa wakati kwa watumiaji wa vifaa.

Maelezo ya vifaa ambavyo havikuingizwa katika vitabu vya stoo ni kama vinavyoonekana katika **Jedwali Na. 80**hapa chini:

*Jedwali 80: Taasisi zenye vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye vitabu.*

| Na. | Fungu | Jina | maelezo | Kiasi(TZS) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 94 | Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma | Vifaa havikuingizwa vitabuni | 81,766,820 |
| 2 | 29 | Huduma za Magereza | Ukosefu wa kumbukumbu za matumizi na uwajibikaji wa mafuta yaliyonunuliwa. | 80,000,290 |
| 3 | 39 | Jeshi la Kujenga Taifa | Vifaa havikuingizwa vitabuni | 70,226,000 |
| 4 | 2006 | Ubalozi wa Tanzania London | samani na vifaa vilivyonunuliwa ambavyo havikuingizwa katika kumbukumbu ya mali. | 55,108,126 |
| 5 | 73 | Sekretarieti ya mkoa wa Shinyanga | Kumbukumbu za matumizi ya dawa kutolewa kwenye kitengo cha kusambaza dawa ambazo hazikuthibitishwa. | 13,588,700 |
| 6 | 74 | Sekretarieti ya mkoa wa Kigoma | Vifaa vilivyonunuliwa ambavyo havikuingizwa vitabuni | 13,070,600 |
| 7 | 35 | Kurugenzi ya Mashtaka ya Umma | Mafuta yaliyoingia na kutoka ambayo hayakuingizwa katika regista ya mafuta. | 10,850,418 |
| 8 | 83 | Sekretarieti ya mkoa | Mapungufu yaliyobainika katika | 3,429,168 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | wa Shinyanga | manunuzi na matumizi ya shajara. | |
| 9 | 70 | Sekretarieti ya mkoa wa Arusha | Vifaa ambavyo havikuingizwa vitabuni | 1,366,480 |
| | **Jumla** | | | **329,406,602** |

*Chanzo: Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2013/2014*

Ninapendekeza serikali kuhimiza ufuataji wa kanuni tajwa pamoja na uboreshaji wa mifumo ya udhibiti wa ndani katika usimamizi wa vifaa ili kuhakikisha uwajibikaji wa maafisa waliokabidhiwa fedha za umma.

Pia ninapendekeza vifaa vyote ambavyo havikuingizwa katika kumbukumbu, viingizwe katika kumbukumbu hizo ili kulinda mali za serikali.

### 11.1.12 Mapungufu katika usimamizi wa vifaa vilivyo stoo TZS.1,296,926,176

Kwa Wizara, Wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa utaratibu wa utunzaji wa vifaa unafuata Kanuni za Fedha za Umma, 2001 Sehemu ya XIV(vifaa vya umma) ambayo inajumuisha kupokea na kutunza vifaa ,mahitaji ya kuhesabu vifaa na kuviondoa/ kuvifuta visivyofaa.

Ukaguzi ulipitia kazi za usimamizi wa vifaa vya Wizara, wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa katika uwekaji wa kumbukumbu, udhibiti wa ndani,mgawanyo wa kazi, utaratibu wa kupokea vifaa, kutunza vifaa, uidhinishwaji wa vifaa na hati ya kutoa vifaa.

Nilibaini Wizara, idara sita (6) na Sekretarieti za Mikoa mitano (5) zilipata mafuta kutoka stoo. Vifaa vyenye thamani ya TZS.51,086,512 vilitolewa bila kuwa na kumbukumbu katika vitabu vya magari husika, mafuta ya gari yenye thamani ya TZS. 8,778,338 yalitolewa kwa magari binafsi bila ya kibali kutoka kwa Maafisa Masuuli,kulikuwa na matumizi ya kupindukia ya mafuta ya gari yenye thamani ya TZS. 17,520,375.83, mapungufu katika udhibiti wa utoaji mafuta yenye thamani ya TZS.50,443,660, mapungufu katika udhibiti wa kuhamisha fedha kiasi cha

TZS.26,400,000 kwenda Bohari Dodoma na vifaa vyenye thamani ya TZS.1,142,697,291 vilibakia stoo bila kutumika. Maelezo ya mapungufu hayo ni kama yanavyoonekana katika **Jedwali Na.81** hapo chini:

*Jedwali 81: Taasisi ambazo zina mapungufu katika usimamizi wa vifaa*

| Na. | Fungu | Jina | Mapungufu | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| 1) | 32 | Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma | Vifaa kutolewa bila ya kuwa na hati ya kutolea vifaa na vifaa kubakia bila kutumika kwa muda mrefu bila kuvitoa | 1,029,243,969 |
| 2) | 29 | Huduma za Magereza | Vifaa vilivyoacha kwa muda mrefu | 61,596,372 |
| 3) | 66 | Ofisi ya Rais - Tume ya Mipango | Mapungufu katika udhibiti wa utoaji mafuta. | 50,443,660 |
| 4) | 55 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | Manunuzi ya vifaa ambavyo viliachwa bila kutumika. | 42,682,000 |
| 5) | 95 | Sekretarieti ya mkoa wa Manyara | Mafuta yaliyotolewa kwenye vitabu vya hesabu lakini hayakuingizwa kwenye daftali la gari, mafuta yaliyotolewa kwa ajiri ya gari lakini matumizi yake hayakuthibitishwa kwa sababu ya ukosefu wa kitabu cha kumbukumbu za gari na matumizi ya kupindukia ya gari. | 30,209,355 |
| 6) | 87 | Sekretarieti ya mkoa wa Kagera | Matumizi ya mafuta ambayo hayakuthibitishwa kwenye daftali la kumbukumbu za gari. | 29,936,017 |
| 7) | 97 | Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki | mapungufu katika udhibiti wa kuhamisha fedha kwenda Bohari Dodoma | 26,400,000 |
| 8) | 94 | Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma | Vifaa ambavyo havikuonekana | 9,174,950 |
| 9) | 63 | Sekretarieti ya mkoa wa Geita | Mafuta yaliyotolewa kwa gari binafsi bila ya kibali cha Afisa Masuuli. | 8,778,338 |
| 10) | 70 | Sekretarieti ya mkoa wa Arusha | Mafuta yaliyotolewa lakini hayakuingizwa katika daftali la kumbukumbu la gari. | 7,046,015 |
| 11) | 89 | Sekretarieti ya mkoa wa Rukwa | Manunuzi ya mafuta kwa kutumia masurufu ambayo hayakuingizwa katika daftali la kumbukumbu la gari. | 1,415,500 |
| | | | **Jumla** | **1,296,926,176** |

*Chanzo: Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2013/2014*

Ili kupunguza au kuondoa hasara kupitia wizi na matumizi mabaya, ninazishauri menejimenti za taasisi husika kuimarisha udhibiti wa usimamizi juu ya vifaa kwa kuhakikisha vifaa vyote vinaingizwa kwenye vitabu.

## 11.2 Ukaguzi wa madeni kwa mwaka 2013/2014

Kiwango cha Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta za Umma Na.1(IPSAS 1) kinatafasiri kwamba madeni ni wajibu uliopo wa kulipa kwa taasisi utokanao na matukio ya zamani, ambapo malipo yake yanategemea kupunguza fedha kutoka kwenye taasisi ambayo imefaidika kiuchumi au uwezo wa huduma.

Baadhi ya sifa ya madeni ni pamoja na: aina ya mkopo, mapato binafsi yaliyotakiwa kulipwa, wajibu wa kulipa madeni mengine kupitia uhamisho wa mali, na shughuli zilizopita ambazo ni wajibu kwa taasisi husika.

Ufuatao ni muhtasari wa masuala niliyoyabaini katika ukaguzi wa madeni kwa mwaka 2013/2014.

### 11.1.13 Madeni tarajiwa TZS.599,473,932,835

Katika kupitia madeni tarajiwa, nilibaini kwamba katika sampuli ya Wizara na Idara saba (7) na Sekretarieti za Mikoa mitano (5) kuna kesi 83 za kisheria mahakamani dhidi ya makampunimbalimbali na watu binafsi ambazo zilikuwa zinasubiria maamuzi zenye jumla ya TZS. 599,473,932,835. Hizi zitakuwa na athari za kifedha katika uendeshaji wa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa. Baadhi ya kesi zipo katika hatua ya kusikilizwa na nyingine katika hatua ya upatanishi mahakamani.

Pia, nilibaini kesi ambazo zina zaidi ya miaka kumi (10) na hakukuwa na taarifa ya mahakama juu ya tarehe ya kusikilizwa. Wizara ya Nishati na Madini ina kiasi kikubwa cha deni ambacho ni sawa na asilimia 82 ya deni lote, ikifuatiwa na Wizara ya Ujenzi (13%) na ya tatu ni Wizara ya Maliasili na Utalii (4%). Taasisi ambazo zina kesi mahakamani ni kama zinavyoonekana katika **Jedwali Na.82** hapa chini:

*Jedwali 82: Taasisi zenye kesi zinazoendelea*

| Na. | Fungu | Jina | Idadi ya kesi | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| 1) | 58 | Wizara ya Nishati na Madini | 4 | 482,964,399,000 |
| 2) | 98 | Wizara ya Ujenzi | 29 | 79,384,269,062 |
| 3) | 69 | Wizara ya Maliasili na Utalii | 20 | 22,003,214,827 |
| 4) | 43 | Wizara ya Kilimo, chakula na Ushirika | 5 | 9,120,207,722 |
| 5) | 37 | Ofisi ya Waziri Mkuu | 6 | 2,400,000,000 |
| 6) | 50 | Wizara ya Fedha | 12 | 1,580,092,326 |
| 7) | 95 | Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara | 1 | 714,000,000 |
| 8) | 46 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi | 1 | 678,440,898 |
| 9) | 81 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza | 1 | 500,000,000 |
| 10) | 89 | Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa | 2 | 109,000,000 |
| 11) | 75 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro | 1 | 12,900,000 |
| 12) | 70 | Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha | 1 | 7,409,000 |
| | | **Jumla** | **83** | **599,473,932,835** |

*Chanzo: Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2013/2014*

Kuna hatari ya kuingia katika matumizi yasiyo na faida kwa Wizara,Idara na Sekretarieti za Mikoa yatokanayo na faini ambayo itatakiwa kulipwa mahakamani kama Wizara, wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa zitashindwa kesi, kwa kuongezea kuna gharama kubwa ambazo zinaingiwa katika kufuatilia hizi kesi. Ninapendekeza kwa serikali kufanya yafuatayo:

- Kuhakikisha Maafisa Masuuli katika Wizara, Wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa husika wanashirikiana na ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufuatilia kwa karibu kesi ili kuhakikisha kesi zilizopo zinakamilika mapema ili kuepuka au kupunguza gharama zinazoweza kutokea na kuweka katika bajeti fungu ili iweze kuwa na uwezo wa kulipa kama itashindwa kesi.
- Kuepuka kutoa maamuzi ambayo yanaweza kusababisha kuongezeka kwa madeni ambayo yangeweza kuzuilika na kuhakikisha kuwa udhibiti wa madeni.
- kufanya kazi kikamilifu na kujitetea kupitia Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuweza kushinda kesi na kukamilisha kesi mbalimbali ambazo zipo mahakamani.

### 11.1.14 Limbikizo la madeni TZS.772,508,290,161

Mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2014 Wizara, Idara 59 na Sekretarieti za Mikoa 23 zilikuwa na madeni ya kiasi cha TZS.772,508,290,161 ambayo yameongezeka kwa kiasi cha TZS.272,979,513,582 sawa na asilimia 55% ikilinganishwa na mwaka wa ukaguzi uliopita (tarehe 30 Juni, 2013) ambapo madeni yalikuwa ya kiasi cha TZS.499,528,776,579.

Limbikizo la madeni linaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika miaka inayofuata kama fedha zinaweza kutumika kulipia madeni.

Sehemu kubwa ya deni ni kutoka Jeshi la Polisi ambao wana deni sawa na asilimia 21 ya jumla ya deni lote, ya pili ni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ikiwa na asilimia 18 ya jumla ya deni ikifuatiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (Fungu 38) likiwa na asilimia 10 ya jumla ya deni lote.

Kwa namna ya pekee, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilikuwa na kiasi kikubwa cha bili za matibabu kwa serikali kutoka katika hospitali za nchi ya India ambazo serikali inapeleka wagonjwa. Kumbukumbu za hivi karibuni zinaonyesha bili za matibabu ambazo zilizokuwa zinadaiwa hadi kufikia Januari 31, 2015 ni kiasi cha Rupia 605,014,043 sawa na shilingi za kitanzania 16,940,393,204. Orodha ya taasisi ambazo zina madeni ambayo serikali inatakiwa kulipa ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho 26**

Ongezeko kubwa la deni bila ya kuonyesha juhudi za kulilipa linavuruga uhusiano mzuri uliokuwepo kati ya Wizara, wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa na watoa huduma wake na wafanyakazi na inaweza kusababisha utoaji wa huduma kwa umma usioridhisha. Wizara, wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa zinaweza kushitakiwa kwa kosa la kushindwa kulipa deni kwa wakati. Ninapendekeza serikali:

- Kuhakikisha fedha zinatolewa kama zilivyopitishwa na Bunge ili kupunguza limbikizo kubwa la deni ambalo linaweza kusababisha hatari ya kudaiwa na kupunguza uaminifu, kuingiza katika bajeti ya mwaka ufuatao madeni yote ili kuepuka mgogoro na watoa huduma na wadau wengine.

- Kupitia mchakato wa bajeti ili kuhakikisha bajeti halisi inayoandaliwa inaendana na shughuli zilizopangwa na mahitaji yote kwa ujumla.

## SURA YA KUMI NA MBILI

## 12.0 UKAGUZI MAALUM

### 12.1 Utangulizi

Katika sura hii, nitawasilisha mapungufu yaliyobainika katika kaguzi maalum zilizofanyika katika mwaka wa fedha 2013/2014

### 12.2 Kaguzi maalum zilizofanyika kwa mwaka wa fedha 2013/2014

Kaguzi maalum zilifanyika kwa mujibu wa kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 pamoja na kanuni ya 79(1) ya kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009.

Mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya kaguzi maalum nane zilifanyika katika taasisi za serikali. Kaguzi hizo ni :

- Ukaguzi maalum wa mfumo mzima wa manunuzi na usambazaji wa pembejeo za kilimo katika sekta ya kilimo cha tumbaku chini ya WETCU – Tabora
- Ukaguzi maalum wa ujenzi wa jengo la kumbi za watu mashuhuri katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere uliopo Dar es Salaam katika kipindi cha mwaka 2006/2007 hadi 2011/2012
- Ukaguzi maalum kuhusu matatizo yanayozikumba balozi za Tanzania
- Ukaguzi maalum juu ya utekelezaji wa mikataba ya ujenzi wa mradi wa usambazaji maji Chalinze – Awamu ya pili
- Ukaguzi maalum wa fedha zilizotumiwa na Wizara mbalimbali kuchapisha hotuba baada ya kuidhinishwa na bunge la bajeti kwa miaka ya 2011/2012 na 2012/2013.
- Ukaguzi maalum katika fungu 98 – Wizara ya Ujenzi kuhusu uhalali wa fedha TZS 252,975,000 za ujenzi wa miradi maalum ya barabara
- Ukaguzi maalum wa taarifa za fedha zilizotumika katika mkutano wa kimataifa SMART Partnership Dialogue wa mwaka 2013 uliofanyika kuanzia mwezi Julai, 2012 hadi Januari, 2014

- Ukaguzi maalum wa mradi wa manunuzi ya matrekta na zana za kilimo wa SUMA JKT kwa kipindi cha kuanzia julai, 2010 hadi Aprili, 2014

Mambo muhimu yatokanayona kaguzi maalum yameonyeshwa kwa muhtasari katika taarifa hii, hata hivyo taarifa husika za kaguzi maalum zilishapelekwa kwa mamlaka husika kwa mujibu wa kanuni ya 81 ya kanuni za ukaguzi wa umma za mwaka 2009.

## 12.3 Ukaguzi maalum wa mfumo mzima wa manunuzi, uagizaji kutoka nje ya nchi, mapokezi na usambazaji wa pembejeo za kilimo katika sekta ya kilimo cha tumbaku chini ya WETCU - Tabora

Ukaguzi huu maalum ulifanyika katika mfumo mzima wa manunuzi ambayo ni pamoja na; uagizaji, upokeaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo kwa ajili ya sekta ya tumbaku chini ya Chama Kikuu cha Wakulima wa Tumbaku Kanda ya Magharibi kwa miaka ya fedha 2010/2011, 2011/2012 na 2012/2013. Ukaguzi huo ulibaini mapungufu yafuatayo ;

- Mapitio ya mfumo mzima wa usambazaji wa pembejeo za kilimo cha tumbaku yalionyesha kuwa utaratibu wa manunuzi ya wasafirishaji haukuwashindanisha na wala utaratibu wa kuwapata wasafirishaji (wasambazaji) haukuwa wazi. Wasambazaji walipewa zabuni bila kuwasilisha nyaraka za kuombea zabuni na bila kupitishwa na bodi ya zabuni.
- Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) vilivyotembelewa vilibainika kutokuandaa maeneo kwa ajili ya mashamba ya miti, utunzaji usioridhisha wa kumbukumbu na taarifa zenye kuwezesha kujua idadi ya miche iliyohitajika kwa kila chama cha ushirika cha msingi (AMCOS) na kwa kila mkulima, au kiasi gani kilinunuliwa na kusambazwa kwa kila chama cha ushirika cha msingi (AMCOS) na kwa kila mkulima. Hapakuwepo taarifa na kumbukumbu zenye kuonesha idadi ya miti iliyooteshwa na kiasi gani cha mkopo kwa kila chama cha ushirika cha msingi

(AMCOS) na kwa kila mkulima. Pia sehemu kubwa ya miti aliyodaiwa kupandwa haikuonekana.

- Mchakato mzima wa ujenzi wa ghala ikiwa ni pamoja na ununuzi wa zabuni za ukandarasi haukufanyika kwa kufuata sheria ya manunuzi na kanuni zake. Maghala yaliyotembelewa yalibainika kuwa chini ya kiwango na baadhi kuanguka hata kabla ya kutumika.
- Kutopatikana kwa kumbukumbu za kiasi kilicholipwa kwa wakandarasi kwa kila AMCOS na nyaraka za malipo husika.
- Maelekezo ya malipo mengi yaliyofanyika benki yalitolewa na meneja uendeshaji wa WETCU ambaye hakuwa mwidhinishaji malipo na bila uongozi wa WETCU kuwa na taarifa. Aidha vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS) husika ambavyo akaunti zao zilitumika kukamilisha miamala hiyo uongozi wake haukuwa na taarifa.
- Mchakato mzima wa manunuzi ya zabuni za makandarasi yalifanywa na maafisa wa CRDB Tabora ambapo mfanyakazi wa CRDB ambaye pia ni ndugu wa damu wa Mkurugenzi mtendaji wa Kampuni ya Euro services (Mkandarasi) iliyopewa zabuni kwa ajili ya ujenzi wa maghala.Ukaguzi ulibaini kuwa mume wa Msajili Msaidizi alipewa kufanya sehemu ya mkataba (sub-contractor) wa Euro-Services wa ujenzi wa maghala na msajili nsaidizi aliweka saini kwenye mikataba hiyo kama shahidi. Hii inathibitika kutokuwepo na uwazi katika mchakato mzima wa manunuzi ya wakandarasi na pia kuwepo mgongano wa kimaslahi na hivyo kutokuwepo na utawala bora.

**Mapendekezo**

- Nashauri AMCOS zizingatie sheria za manunuzi ya umma na kanuni zake zake kwa manunuziya aina zote,
- Napendekeza serikali iwawajibishe mameneja kwa maamuzi waliyofanya katika mchakato wa manunuzi na CRDB kwa kukubali maelekezo ya kufanya malipo toka kwa mtu asiyekuwa mwidhinishaji malipo,
- Nasisitiza serikali kuweka kiwangocha chini cha elimu kinachohitajika kwa menejimenti za AMCOS kwani hali ya sasa

inaonyesha kuwa viongozi wengi wa AMCOS ni darasa la saba jambo linalotia wasiwasi juu ya uwezo wa kusimamia fedha, mikopo na AMCOS kwa ujumla,

- Nashauri serikali ifanye uchunguzi wa kina kwa kutumia vyombo vya uchunguzi.

## 12.4 Ukaguzi maalum wa ujenzi wa jengo la kumbi za watu mashuhuri katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam katika kipindi cha mwaka 2006/2007 hadi 2011/2012

Mradi wa ujenzi wa Jengo la kumbi za watu mashuhuri (VIP) ulianza mwezi Mei, 2009 na kukamilika mwezi Oktoba, 2010 ambapo mfadhili na mwajiri alikuwa ni M/s China International Fund Limited (CIFL), msimamizi alikuwa M/s Beijing CECD Supervision & Consulting Co. Ltd na mkandarasi alikuwa M/s Beijing Construction Engineering Group Co. Ltd. Gharama za ujenzi wa mradi zilikuwa ni Dola za Kimarekani 7.5 milioni kwa mchanganuo ufuatao; Dola za Kimarekani milioni 6 (CIFL) na Dola za Kimarekani milioni 1.5 (Serikali/Mamlaka)

Mambo muhimu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi maalumu:

- China Sonangol International Limited (CSIL) ilitoa msaada wa dola za Kimarekani 4,102,639 sawa na TZS.5,335,359,318 na siyo dola za Kimarekani 6,000,000 sawa na TZS.9,000,000,000 kama ilivyoelezwa awali. Kiasi hicho cha TZS 3,664,640,682 sawa na 40.7% hakikutolewa na CSIL,
- Gharama za mchango wa Serikali katika jengo la Kumbi za watu Mashuhuri kwa kazi zilizofanyika ambazo hazikuhusika na ujenzi wa jengo lenyewe ulikuwa ni TZS.869,485,164 na sio bilioni tatu (TZS.3,000,000,000). Serikali haikuweza kuchangia TZS 2,130,514,836 ikiwa ni sawa na 71%,
- Sikuweza kupata nyaraka wala vielelezo vyovyote vilivyomo kwenye majalada ya ofisi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) na yale ya Kiwanja cha JNIA (k.m mkataba) kwa ajili ya kumbukumbu zinazoonyesha gharama halisi za ujenzi wa

jengo. Hii inamaanisha kwamba Mkandarasi (M/s Beijing Construction Engineering Group Co. Ltd) pamoja na Mfadhili (M/s China International Fund Limited) hawakukabidhi nyaraka za ujenzi Serikalini na hivyo kushindwa kufahamu gharama halisi iliyolipwa na Mfadhili huyo.

- Kwa mujibu wa taarifa ya utathminikutoka kwa Mthamini Mkuu wa majengo ya Serikali thamani ya jengo hilo hadi Mwezi Mei, 2014 ni TZS.3,072,000,000 ikiwa ni tofauti na ilivyoelezwa awali ya TZS 12,000,000,000 ikisababisha tofauti ya TZS 8,928,000,000. Thamani ya jengo ya TZS 3,072,000,000 iko chini ya kiasi kilichokuwa kimekusudiwa kutolewa na CSIL kwaajili ya ujenzi wa jengo la kumbi za watu mashuhuri kwa TZS 5,335,359,318 (RMB 27,980,000)
- Mamlaka ya viwanja vya ndege imefanya manunuzi ya vifaabila kuwepo ushindani wa bei TZS. 283,803,729 kinyume na Kanuni ya Manunuzi ya Umma Na.68 (4-5) ya mwaka, 2005.
- Pia manunuzi ya vifaa vya TZS 737,240,842 yalifanyika bila kufuata taratibu za Manunuzi.

**Mapendekezo**

Napendekeza kuwa uendelezaji wa aina yoyote katika viwanja vya ndege unahitaji kufanyika kwa uangalifu ili kuwa wa ufanisi. Serikali inatakiwa kuwa na udhibiti wa ndani ulioimara wa mali inazozipata. Mfumo wa uwekaji nyaraka inapaswa uimarishwe ili kuwepo na ukamilifu, uadilifu na upatikanaji wa taarifa.

## 12.5 Ukaguzi maalum kuhusu matatizo yanayozikumba balozi za Tanzania

Wakati wa mapitio ya taarifa ya hesabu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa zikiwamo Balozi mbalimbali, kamati ya hesabu za Serikali(PAC) ilibaini fedha kutotumwa kwa wakati Balozini, udhaifu katika ukusanyaji wa mapato na hali mbaya ya majengo ya serikali yaliyopo Balozini.

kwa kuzingatia changamoto zilizojitokeza, kamati ya hesabu za serikali (PAC) iliamuru ukaguzi maalum ufanyike ili kubaini chanzo cha changamoto zilizokabili Balozi za Tanzania na kuja na njia

bora ya kutatua matatizo yanayoathiri utendaji wa Balozi. Ukaguzi maalum uliofanywa ulibaini changamoto zifuatazo :

- Makisio ya matumizi yamekuwa yakiandaliwa bila kuzingatia mahitaji halisi ya balozi, matokeo yake balozi zimekuwa haziwezi kulipia huduma zote muhimu na hivyo kuwa na madeni na hata hukatiwa baadhi ya huduma muhimu. Ukomo wa bajeti hauzingatii vifungu vya matumizi ya gharama za uendeshaji wa ofisi kama vile umeme, mfumo wa upashaji joto majumbani, mafuta kwaajili ya magari na gharama za usafiri,
- Baadhi ya balozi zimekuwa zikiandaa makisio ya chini ya makusanyo ili yafikiwe bila jitihada za ziada au kutoonyesha uwezo halisi ambao balozi zinao katika kukusanya maduhuli,
- Makusanyo ya maduhuli yamekuwa hayaridhishi kutokana na kukosekana kwa mikakati balozini ya kuitangaza nchi ya Tanzania. Watalii na wageni wanaokuja Tanzania husafiri na kupatiwa viza uwanjani ; Kutofunguliwa kwa balozi za heshima (honorary consulates) kwenye maeneo ambayo yalikwisha kuainishwa kuwa na wageni wanaotembelea Nchi ya Tanzania ; na udhibiti mdogo wa ukusanyaji maduhuli kutokana na kutotumia mashine za viza kwenye balozi,
- Kutofanyika ukarabati kwa muda mrefu na kusababisha wapangaji katika nyumba za ubalozi kuhama,
- Fedha ya maendeleo imekuwa haitoshi na imekuwa haitengwi kwaajili ya ukarabati wa majengo, matengenezo ya magari na ununuzi wa samani. Aidha fedha imekuwa haitolewi kulingana na mahitaji ; Serikali imekuwa ikimiliki viwanja visivyoendelezwa kwenye balozi zake,
- Watumishi walioko ubalozini kutorejea nchini baada ya muda wao wa utumishi kukoma au baada ya kustaafu ; hawa wameendelea kulipwa posho ya huduma kwa watumishi walioko nje ya nchi.

Kwa kawaida balozi huandaa bajeti kulingana na mahitaji na kuziwasilisha Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kila mwaka. Hata hivyo mahitaji haya ya kibajeti

kwa mwaka wa fedha yamekuwa hayatekelezwi kwa sababu Wizara ya Fedha imekuwa ikitoa ukomo wa bajeti ambao kwa kawaida huwa uko chini ya mahitaji halisi.

**Mapendekezo**

- Balozi zinakabiriwa na changamoto za fedha kutokana na changamoto katika utoaji wa fedha. Napendekeza kuwa ni wakati muafaka sasa kutenga fedha zitakazotosheleza mahitaji ya balozi kupitia fungu maalum litakayoitwa fungu la balozi,
- Serikali ihakikishe kwamba fedha inayotengwa katika bajeti kwaajili ya balozi inatoshereza mahitaji ya kifedha ya balozi

**12.6 Ukaguzi maalum juu ya utekelezaji wa mikataba ya ujenzi wa mradi wa usambazaji maji Chalinze – Awamu ya pili**

Ukaguzi huu maalum unatokana na ombi la serikali kupitia barua yake yenye kumbukumbu namba CAB446/626/01/36 ya tarehe 24 Novemba, 2012 naCAB 446/626/01/63ya tarehe 16 Januari, 2014 baada ya kubainika kwa mapungufu katika utekelezaji wa mikataba ya ujenzi kama ilivyoonyeshwa katika taarifa ya mamlaka ya manunuzi ya umma.
Ukaguzi huu maalum umelenga kuangalia kama Sheria ya manunuzi ya umma na kanuni zake zilizingatiwa wakati wa utekelezaji wa mikataba ya ujenzi

Mikataba ya ujenzi wa wa mradi wa usambazaji maji Chalinze – Awamu ya pili ulikuwa na vipande tisa; Kipande F&H, Kipande 1 hadi 6 na J.Muhtasari wa mapungufu yaliyobainika ni;

**a) Mikataba kutokamilika katika muda uliopangwa**

Kutokuwa na usimamizi wa kutosha wa mikataba na hivyo kupelekea mradi kuchelewa kukamilika kwa kati ya miezi kumi na nane (18) na miezi (36) na kusababisha kusitishwa kwa mikataba.

**b) Kutokuwepo kwa taarifa ya upembuzi yakinifu**

Kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi wa maji Chalinze kulitakiwa kufanyike upembuzi yakinifu. Taarifa hiyo ya upembuzi yakinifu haikuweza kupatikana wakati wakati wa ukaguzi na hivyo kusababisha kushindwa kuthibitisha iwapo utekelezaji wa mradi ulifuata upembuzi yakinifu uliokuwa ufanyika.

**c) Kasoro mbalimbali katika usanifu na michoro wa mradi**
Nilipokagua taarifa za usanifu na michoro iliyotayarishwa na mhandisi mshauri nilibaini kuwa kazi ilikuwa imefanyika chini ya kiwango na hivyo kupelekea kuwa na marekebisho mengi yaliyosababisha nyongeza za mkataba wa awali na kupelekea ongezeko la mara kwa mara la gharama ya mkataba

**d) Udhaifu uliobainika kwa Mkandarasi Mshauri**
Mhandisi mshauri ambaye pia alikuwa msimamizi wa mkandarasi wa ujenzi wa vipande H na F alikuwa na madhaifu yaliyohusisha; kutokuwa eneo la mradi kwa kipindi kirefu, kutoandaa taarifa ya mwezi ya maendeleo ya mradi na kuziwasilisha kwa mwajiri (Wizara ya Maji) kulingana na matakwa ya mkataba, kukubali mabomba ya kupitishia maji kuwa ya plastiki badala ya chuma kinyume na matakwa ya mkataba pia kushindwa kuchukua hatua stahiki kwa wakati ikiwa ni pamoja na kumshauri mwajiri ipasavyo kuhusiana na utendaji usioridhisha wa mkandarasi (Mega Builders Limited) ambaye hakuwa na sifa zayakufanya kandarasi kubwa kama ile kulingana na viwango vilivyowekwa na Bodi ya usajiri wa wakandarasi.

**e) Mapungufu yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa kipande F na H**
Vipande hivi viwili, H na F pamoja na kuwa vilikuwa tofauti vyote vilitolewa kwa mkataba mmoja na. MTB/Tender N.ME-011/2005-01/W/02 iliosainiwa tarehe 14 Agosti 2009 na mkandarasi kukabidhiwa mradi tarehe 29 Septemba, 2009 na ulipaswa kuwa umekamilika kabla ya mwezi machi 2011 kitu ambacho hakikufanyika.

Muda wa mkataba uliongezwa kwa kipindi kingine cha miezi sita hata hivyo kandarasi hii haikuweza kukamilika kwa wakati na hata mindo mbinu ilikuwa chini ya kiwango kitendo kilichopelekea kuvunjwa kwa mkataba mkataba na Wizara ya Maji tarehe 19 February, 2013 na kazi iliyobaki kupewa mkandarasi mwengine Badra East African Enterprise Ltd kwa mkataba na. 011/2008/2009/W/02 kwa TZS 5,843,395,800

Mkataba ulitiwa saini tarehe 5 Novemba, 2013 na ulitarajiwa kukamilika mwezi Mei 2014. Kandarasi hii haikuweza kukamilika kwa muda uliopangwa na mkandarasi alishawasilisha nyongeza ya mkataba wa TZS 2,872,324,078 kwa kazi za ziada sawa na asilimia 49 ya mkataba wa mwanzo.

Hii inadhihilisha udhaifu wa uandaaji na uchambuzi wa kazi za mkataba na gharama zake.

**f) Hati za madai za makandarasi kulipwa bila kuonyesha kazi iliyofanyika**

Nilibaini kuwa hati za madai za mkandarasi zilikuwa zikilipwa ingawa zilikuwa hazionyeshi uchambuzi wa gharama kwa kuoanisha na kazi zilizofanyika kwa kufuata mchanganuo wa gharama kwa kuoanisha na kazi zilizofanyika kwa kufuata mchanganuo wa gharama za ujenzi (BOQ) na ziliidhinishwa na mkandarasi mshauri. Hati hizi za madai za mkandarasi ni za thamani ya dola za kimarekani 5,255,842 (sawa na TZS 6,832,594,600)

**g) Miundombinu ya maji kukabidhiwa bila kufanyiwa majaribio**

Miundombinu ya maji kipande J na Na. 6 imekamilika na kukabidhiwa kwa Wizara ya Maji lakini haikufanyiwa majaribio ili kuona ubora wake kutokana na ukosefu wa nyumba ya kuhifadhia mashine ya kusukuma maji,nyumba ya genereta, na pia ununuzi na ufungwaji wa mashine za kusukuma maji na jenereta katika vituo vya ubenazomozi na Mbwewe ambapo kila kituo pamejengwa tanki la kuhifadhia maji lenye ukubwa wa mita za ujazo 450 kila moja.

**h) Riba kwa kuchelewesha malipo kwa makandarasi TZS.3,897,283,923**

Mshauri (Mhandisi msimamizi) Seureca Newt aliwasilisha makadirio ya riba ya kiasi cha TZS.3,897,283,923 sawa na dola za kimarekani milioni 2.8 zilizotokana na ucheleweshaji wa malipo ya makandarasi kwa zaidi ya siku 307 kwaajili ya kipande Na. 1 hadi Na. 6

**Mapendekezo**

- Serikali itoe kazi kwa makandarasi wa ujenzi kulingana na uwezo wao. Uwezo wao ni kwa mujibu wa madaraja waliosajiliwa na bodi ya usajili wa wakandarasi (CRB). Hii itasaidia taasisi zinazofanya manunuzi kuepuka kazi zisizo na ubora, hivyo kuepusha hasara kwa serikali.
- Usanifu wa miundombinu ya maji kwa miradi kama Mradi wa usambazaji maji Chalinze ipitiwe na wataalam kabla kukaribisha maombi ya zabuni kutoka kwa wakandarasi,hii itasaidia taasisi zinazofanya manunuzi kutofanya mabadiliko makubwa ya gharama za mikataba, hivyo kutoathili utekelezaji wa miradi kwasababu ya ufinyu wa bajeti kuweza kukabili mabadiliko ya mara kwa mara ya usanifu.
- Taasisi zinazofanya manunuzi ziimarishe ufuatiliaji ili kuhakikisha wahandisi washauri wanafuatiliwa na wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa makubaliano.Hatua za haraka zichukuliwe dhidi ya wahandisi washauri ambao hawawajibiki ipasavyo kwa mujibu wa mkataba na matarajio ya mwajiri.
- Taasisi zinazofanya manunuzi zihakikishezinakuwa na uhakika wa upatikanaji wa fedha kabla hazijaingia katika mikataba ya ujenzi.Hii itasaidia taasisi zinazofanya manunuzi kufanya malipo kwa wakati na kuepuka riba ambayo ni adhabu ya kuchelewesha malipo, hivyo kuwa na gharama za ziada kwa mradi

### 12.7 Ukaguzi maalum wa fedha zilizotumiwa na Wizara mbalimbali kuchapisha hotuba za bajeti za Wizara baada ya kuidhinishwa na bunge la bajeti kwa miaka ya 2011/2012 na 2012/2013.

ukaguzi huu umefanyika kufuatia barua yenye kumbukumbu Na. BC.50/188/01 ya tarehe 9 Octoba, 2013 kutoka Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum ili kujua kiasi cha fedha kilichotumiwa na serikali kutangaza hotuba ya bajeti ya Wizara mbalimbali kwa miaka ya 2011/12 na 2012/13. Matokeo ya ukaguzi ni kama ifuatavyo;

- Nimebaini kiasi cha TZS 2,545,517,367 kilitumika kutangaza hotuba ya bajeti iliyoidhinishwa kwa Wizara 21 na taasisi 5 kwa mwaka wa fedha 2011/12 na 2012/13, ambapo kiasi kilichotumika kutangaza bajeti ya mwaka wa fedha 2011/2012 ni TZS 1,131,608,828 na mwaka wa fedha 2012/2013 ni TZS 1,413,908,539,kiasi kilichotumika mwaka 2012/2013 ni zaidi kwa 25% ukilinganisha nakiasi kilichotumika mwaka 2011/2012,
- Ukosefu wa sheria zinazosimamia uchapishaji wa bajeti katika magazeti,
- Orodha ya vyombo vya habari vilivyo idhinishwa na kupewa kibali kutangaza bajeti za Wizara haikuwasilishwa kwaajili ya uhakiki,
- Nilibaini kuwa hakuna mwongozo wala waraka unaotoa ukomo wa matangazo kuhusu wakati gani, mara ngapi bajeti itangazwe, vyombo vingapi vya matangazo vitumike na kiasi gani kitumike

**Mapendekezo**
Naishauri serikali kuandaa mwongozo ambao utatoa maelekezo juu ya uchapishaji wa bajeti kwenye magazeti

## 12.8 Ukaguzi maalum katika fungu 98 – Wizara ya Ujenzi kuhusu uhalali wa fedha TZS 252,975,000 za ujenzi wa miradi maalum ya barabara

Ukaguzi maalum wa Wizara ya Ujenzi (Fungu 98) ulilenga kuhakiki TZS 252,975,000,000 zilizoidhinishwa kwaajili ya miradi maalum ya barabara ambazo zilitumika kulipia madeni ya makandarasi na wahandisi washauri. Yafuatayo ni mambo muhimu yaliyojitokeza;

- Taarifa iliyotolewa bungeni kuhusu miradi maalum ya ujenzi wa barabara Na. 4168 yenyethamani ya TZS 252,975,000,000 haikuwa sahihi kwani fedha hizo zilitumika kulipia madeni ya makandarasi na wakandarasi washauri,
- Wakala wa barabara Tanzania (TANROADS) ilibadilisha fedha zilizopokelewa kutoka Wizara ya ujenzi bila kuijulisha Wizara na nyaraka zilizotumika kufanya mabadiliko hayo kutowasilishwa kwaajili ya mapitio,

- Jumla ya TZS 175,279,428,818 zilihamishwa kwenda akaunti ya maendeleo ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS). Hata hivyo, kati ya kiasi hicho TANROADS ilifanya matumizi ya TZS 3,048,365,229 ambacho maelezo na nyaraka hazikuwasilishwa kwaajili ya mapitio,
- Jumla ya TZS 13,385,089,124 zilitumika katika matengenezo ya barabara za wilaya ambazo hupokea mgao wa fedha kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara. Pia, nimebaini baadhi ya Miradi ambayo haikuwepo kwenye bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka 2010/2011 na miradi mengine ililipwa naTANROADS zaidi ya kiasi kilichotengwa bila kuonyesha chanzo cha fedha,
- Jumla ya TZS 6,596,312,084 zilionyeshwa kwenye taarifa ya madeni yaliyowasilishwa Wizara ya Ujenzi na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), lakini madeni hayo yalikuwa tayari yamelipwa na Ofisi za mkoa za Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS),
- Meneja wa mkoa wa Morogoro alilipa jumla ya TZS 1,116,010,174 kulipia madeni ya kimkataba yanayotokana na ujenzi wa daraja la makutano linalomilikiwa na kampuni binafsi ya miwa. hata hivyo daraja hilo halitumiki,
- Nilibaini kuwa mahitaji ya bajeti ya Wizara ya ujenzi hayakufikiwa na serikali kwani Wizara ya fedha hutoa ukomo wa juu wa bajeti ambao ni mdogo zaidi ya mahitaji halisi.

**Mapendekezo**

- Naishauri serikali kuendelea kusaini mikataba mipya ya ujenzi wa barabara na baada ya kutathmini uwezo wa kulipa madeni yaliyopo ya wakandarasi ili kuepuka ukuaji wa madeni hayo katika siku zijazo na kuwa mzigo kwa taifa .
- Naishauri Serikali kuzingatia mikataba iliyoingia kati yake na makandarasi ili kuepuka malipo ya riba endapo makandarasi watachukua hatua za kisheria kutokana na kukiuka masharti yaliyowekwa katika mikataba,
- Zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara mpya uende sambamba na fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha

husika na kama ilivyo katika mpango wa manunuzi wa mwaka husika,

- Nashauri Wizara pamoja na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) waboreshe vitengo vya uhasibu na kuhakikisha rejesta ya wadeni inaandaliwa ili kuwa na uwezo wa kujua madeni yote ya makandarasi na washauri,
- Nashauri Wizara na TANROADS wahakikishe taarifa za malipo zilizopo kwenye nyaraka za Wahandisi wa miradi, ripoti za maendeleo ya miradi za mwezi, rejista za madeni na hati za malipo zinafanyiwa usuluhishi.

**12.9 Ukaguzi maalum wa taarifa za fedha zilizotumika katika mkutano wa kimataifa wa "SMART Partnership Dialogue" wa mwaka 2013 kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2012 hadi Januari, 2014**

Nilifanya ukaguzi maalum wa taarifa za fedha za mkutano wa kimataifa wa "Smart Partnership Dialogue" wa mwaka 2013 ambapo Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ilikuwa mwenyeji.Ukaguzi ulikuwa nikwa kipindi cha miezi kumi na nane kuanzia Julai 2012 hadi Januari 2014.

Ukaguzi huu maalum wa mkutano wa kimataifa wa Smart Partnership Dialogue wa mwaka 2013 umefanyika kufuatia ombi kutoka serikalini. Muhtasari wa matokeo ya ukaguzi maalum ni kama ifuatavyo:

- Malipo ya TZS.187,478,000 yalifanywa kwa M/S Simply Computers Tanzania Ltd kwaajili ya manunuzi ya vifaa vya ofisi.vifaa hivyo vilipokelewa tarehe 9 Septemba, 2013 baada ya kukamilika kwa mkutano huo.Mkutano wa kimataifa wa Smart Partnership Dialogue wa mwaka 2013 ulifanyika kuanzia 28 Juni hadi 31 Julai, 2013.
- Kutozingatiwa kwa bajeti iliyoidhinishwa kwaajili ya manunuzi ya tiketi za usafiri wa ndege.Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya tiketi za usafiri wa ndege ilikuwa TZS 21,000,000 lakini kiasi halisi kilichotumika kwa tiketi hizo ni TZS.186,998,268; hivyo kupelekea matumizi zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa kwa TZS.165,998,268.

- Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ilipanga na kuidhinisha manunuzi ya vifaa na huduma zenye thamani ya TZS.974,054,600,hata hivyo ukaguzi maalum ulibaini manunuzi yenye thamani ya TZS.614,626,341 yalifanyika nje ya mpango wa manunuzi uliopitishwa.

**Mapendekezo**

- Nashauri taasisi zinazofanya manunuzi kutambua ushiriki wao katika kazi kubwa katika uchumi wa taifa kwani kiasi kikubwa cha fedha za serikali zinatumika kufanya manunuzi ya bidhaa na huduma
- Matumizi ya mpango wa manunuzi yahamasishwe ili kuwe na matumizi bora ya raslimali na kupunguza matumizi ya fedha yasiyokuwa na tija kwa taifa.

### 12.10 Ukaguzi maalum wa mradi wa manunuzi ya matrekta na zana za kilimo wa SUMA JKT kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2010 hadi Aprili, 2014

Ukaguzi maalum wa mradi wa manunuzi ya matrekta na zana za kilimo ilifanyika kufuatia ombi la Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Muhtasari wa matokeo ya ukaguzi ni kama ifuatavyo;

- Mzabuni M/S ESCORT LTD alishinda zabuni ya kusambaza matrekta, mashine za kusukumia maji, zana za kilimo na huduma nyingine kwa gharama ya USD 40,000,000. Mzabuni huyu aliomba zabuni kwa USD 35,526,412 na kusababisha tofauti ya USD 4,473,589 bila maelezo
- Nilibaini mapungufu katika manunuzi ya matrekta 1846 na zana za kilimo 4,450 kutokana na kukosekana kwa nyaraka za matangazo ya zabuni, muhtasari wa kikao cha ufunguzi wa zabuni, muhtasari za vikao vya bodi ya manunuzi,
- SUMA JKT ilifanya manunuzi ya matrekta 268 kwa thamani ya USD 4,334,560 sawa na TZS 7,082,78,800 kutoka kwa Lucky Export bila ya kuwa na mkataba wa maandishi. Hii ni kinyume na Sheria na kanuni za manunuzi ya umma,

- Udhaifu katika utekelezaji wa mkataba kati ya SUMA JKT na ESCORT LTD kuhusu manunuzi ya matrekta 1846 na zana za kilimo 4,450, na kupelekea karakana ya kuunganisha matrekta ya thamani ya USD 883,362 kutojengwa TACT Nyumbu,
- Hakuna nyaraka zilizowasilishwa kuonyesha kuwa kiasi cha USD 1,102,800 kilitumika kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa SUMA JKT na Nyumbu (TACT) kuhusiana na jinsi ya kuunganisha na kukarabati matrekta, mashine za kusukumia maji na zana za kilimo kwa mujibu wa kifungu cha 2.3(a) na (b) cha mkataba,
- Ukosefu wa eneo maalum au ghala kwaajili ya kuhifadhia matrekta na zana za kilimo hivyo kupelekea uharibifu wa zana za kilimo kutokana na mvua na jua na kusababisha kutu. Mashine za umwagiliaji 31 zenye thamani ya TZS 177,181,242 ziliungua kwa moto,
- Hasara ya jumla ya TZS 261,029,531 iliyosababishwa na kuchomolewa kwa sehemu za matrekta matano zenye thamani ya TZS 125,989,531 na sehemu za matrekta madogo(Power Tiller) kumi na sita zenye thamani ya TZS 135,040,000,
- Afisa Masuuli hakuteua kamati ya mapokezi na kukubali vifaa hivyo kupelekea vipuri vya vifaa visivyokuwa na viwango vya USD 88,728 sawa na TZS 149,507,000 kuletwa na mzabuni M/S ESCORT Company,
- Mapato yanayotokana na mauzo ya matrekta na zana za kilimo ya TZS 6,676,711,168 kwa mkopo kwa wateja 117 ilikuwa bado haijakusanywa kwa zaidi ya miaka mitatu,
- Hasara ya jumla ya TZS 19,652,138 ilibainika kutokana na mauzo ya matrekta na zana za kilimo chini ya bei iliyoidhinishwa; trekta moja liliuzwa kwa TZS 1,000,000 badala ya TZS 16,480,952 na mashine ya kupandia iliyotakiwa kuuzwa kwa TZS 5,171,186 badala yake iliuzwa kwa TZS 1,000,000,
- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga taifa ilipokea TZS 5,171,325,331 kutoka Hazina kwaajili ya mradi wa matrekta na zana za kilimo wa SUMA JKT. Nilibaini kuwa, katika kiasi hiki nyaraka za matumizi ya TZS 498,920,299 hazikuwasilishwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa,

- Mradi ulikuwa na matumizi yenye nyaraka pungufu kiasi cha TZS 3,265,740,402,
- Utekelezaji wa mradi unakabiliwa na changamoto nyingi kuhusu maandalizi ya mradi na usimamizi wa mradi. Hatahivyo, SUMA JKT ilishindwa kufanya maandalizi ya jinsi ya kuutekeleza mradi. Uibuaji na maandalizi ya mradi na hatua muhimu za kuweka viwango na vigezo vya kuutekeleza, kuutathmini na kuufuatilia mradi vyote hivyo havikufanyika kwa umakini.

**Mapendekezo**

- Uongozi wa mradi wa matrekta uliopo chini ya SUMA JKT unapaswa kufuatilia mchakato wa kutathmini zabuni na kutoa taarifa ambazo hazikutolewa kwaajili ya uhakiki na kudai malipo ya ziada yaliyofanyika bila kuwa na maelezo ya kiasi cha USZ 4,473,588.52 alicholipwa M/S ESCORT LTD,
- Uongozi wa SUMA JKT uimarishe mfumo wa udhibiti wa ndani katika manunuzi ya bidhaa na huduma ili kuhakikisha uzingatiaji wa sheria na kanuni za manunuzi ya umma. Zaidi ya hayo, uongozi unapaswa kuchukua hatua zinazostahili dhidi ya wahusika waliosababisha mapungufu katika manunuzi ya matrekta 2,114 na zana za kilimo 4,450,
- Menejimenti ya SUMA JKT iimarishe usimamizi na na ufuatiliaji wa shughuli za mradi wa matrekta na kuhakikisha ujenzi wa karakana ya kuunganisha matrekta na eneo la kuhifadhia matrekta na zana za kilimo unafanyika Nyumbu (TACT),
- Afisa Masuuli aanzishe kamati ya kukagua na kupokea bidhaa, na kuchukua hatua stahiki kwa watendaji waliosababisha hasara ya TZS 261,029,531 iliyosababishwa na kunyofolewa kwa sehemu za matrekta
- Menejimenti ianzishe mfumo wa kihasibu wa ki-kompyuta (computerized accounting system) na kuandaa mwongozo wa kukusanya madeni na mkakati wa ukusanyaji mapato. Pia, menejimenti ifuatilie wadaiwa.

## SURA YA KUMI NA TATU

## HITIMISHO NA MJUMUISHO WA MAPENDEKEZO

### 13.0 Utangulizi

Katika taarifa hii nimejumuisha matokeo ya ukaguzi nilioufanya kwenye Wizara, Idara na Wakala wa serikali; na Sekretarieti ya Mikoa kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014. Masuala yote yaliyoelezewa kwenye taarifa hii yamewasilishwa pia kwa Maafisa Masuuli husika kwa ajili ya utekelezaji. Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara, Wakala wa serikali, na Sekretarieti ya Mikoa wanatakiwa kuandaa majibu ya hoja na mpango kazi wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali na kuyapeleka kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali kama Sheria ya ukaguzi wa umma Na. 11 ya mwaka 2008 inavyoagiza.

Nikirejea katika matokeo ya ukaguzi wa mwaka huu 2013-14, kwa ujumla, nimeziona jitihada za serikali za kuongeza juhudi kushughulikia hoja za ukaguzi kama inavyoonyeshwa na kuongezeka kwa taarifa zenye hati safi za ukaguzi kama ilivyo onyeshwa kwenye sura ya pili ya taarifa hii.

Hata hivyo, pamoja na maboresho yaliyopelekea kuongeza idadi ya hati zinazoridhisha, matokeo ya ukaguzi kwa mwaka huu wa fedha yanaonesha kuendelea kuwepo kwa mapungufu ambayo nimeyaelezea kwenye sura zilizotangulia za taarifa hii ambayo yanawahitaji maafisa masuuli kuchukua hatuaza kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani. Kwa mantiki hiyo, katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2013/2014 ninapendekeza yafuatayo.

### 13.1 Kutotekelezwa kwa baadhi ya mapendekezo yangu ya mwaka uliopita

Katika ripoti yangu ya ukaguzi ya mwaka uliopita kulikuwa na masuala muhimu baadhi yalitekelezwa na baadhi hayakutekelezwa kabisa ambayo yameelezewa katika Sura ya tatu.

**Mapendekezo**

Maafisa Masuuli wa taasisi zinazohusika pamoja na Bodi za Ushauri zilizoko chini ya Wizara zinapaswa kuongeza jitihada ili kuhakikisha mapendekezo ya ripoti za ukaguzi za miaka iliyopita yanatekelezwa kwa wakati ili kuleta tija katika uendeshaji wa Wizara/Idara/Balozi zetu.

## 13.2 Mamlaka ya Mapato Tanzania

### 13.2.1 Mapungufu katika mifumo wa misamaha ya kodi na ufuatiliaji wake

Katika ukaguzi huu nimebaini mapungufu katika utoaji wa misamaha ya kodi na matumizi yake, ushuru wa forodha na mfumo wa ukadiriaji wa kodi nchini.

Kulikuwa na matukio kadhaa ambapo wasiostahili misamaha ya kodi walipata misamaha ikiwemo ya usajili wa magari mbali na waagizaji halisi. Matukio hayo yamekuwa ya kawaida katika sekta ya utalii na mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo yanaashiria kuwepo kwa udanganyifu baina ya maafisa kutoka mamlaka husika.

Matukio mengine ni ukwepeshaji wa bidhaa zilizosamehewa kodi kwa matumizi mengine aidha kwa kutumiwa na makampuni yasiyostahili msamaha, haya yalibainika katika sekta ya madini, mafuta na gesi, Maduka yasiyotoza kodi na kwa wawekezaji wenye cheti cha uwekezaji.Hivyo basi, tathmini za misamaha ya kodi zinakabiliwa udanganyifu na pia ni chanzo kimojawapo cha upotevu wa mapato ya Serikali.

**Mapendekezo**

Ninashauri Serikali ifanye ifuatayo:

- Kuanzisha kitengo cha ufuatiliaji misamaha ambacho kitakuwa na wajibu wa udhibiti na kuhakikisha kuwa utoaji wa misamaha ya kodi unanakidhi matakwa ya kisheria na kufanya ufuatiliaji wa matumizi ya misamaha hiyo ya kodi pamoja na kushirikiana na mamlaka zinazohusika na utoaji wa misamaha hiyo.

- Kufanya mapitio ya sheria za misamaha ya kodi kwa lengo la kupunguza mianya katika misamaha ya kodi. Aidha, serikali ihakikisha kwamba misamaha ya kodi haizidi 1% ya Pato la Taifa au 5% ya mapato ya kodi yaliyokusanywa.

### 13.2.2 Kuchelewa katika kushughulikia rufaa za kodi

Ukaguzi wangu umebaini mapungufu namna ambavyo kesi za rufaa za kodi zinavyoshughulikiwa kwani kumekuwepo na kiasi kikubwa cha kodi hakilipwi kutokana na kutoamuliwa mapema kwa kesi nyingi zilizoko Bodi ya Rufaa za Kodi na Mahakama ya Rufaa ya Tanzania chenye thamani ya trilioni TZS.1.7 hadi wakati wa kuandika taarifa hii, Januari, 2015.

Kwa maoni yangu, kiasi cha kodi kinachosubiria uamuzi wa mahakama ni kikubwa mno, hivyo basi kuzidi kuchelewa kwa namna yoyote katika kutatua kesi hizo kunaitwisha mzigo serikali katika suala la gharama za uendeshaji wa kesi na upotevu wa mapato iwapo itatokea mkata rufaa amefilisika kabla ya kesi haijaisha.

**Mapendekezo**

Ninapendekeza Serikali kuongeza kasi ya kushughulikia rufaa hizo kwa kuzingatia umuhimu wa kodi katika uchumi wa nchi.

### 13.2.3 Udhaifu katika usimamizi wa mapato

Tathmini yangu imeonesha kwamba usimamizi wa makusanyo ya kodi kuwa si madhubuti na wa kutosha. Mamlaka ya mapato Tanzania ilipoteza mapato katika maeneo yafuatayo; ushuru wa forodha kutoka Makampuni ya gesi na mafuta, unafuu wa kodi ulitolewa mara mbili kwa hati moja ya maombi, mapungufu kwenye ukadiriaji wa kodi inayopaswa kulipwa, tozo na faini zilizopaswa kukusanywa na bidhaa zilizopata kibali cha kuingia nchini kwa muda kuwa baadae kusafirishwa nje ya nchi, hakuna ushahidi kwamba zilisafirishwa kama ilivyokusudiwa. Hivyo, udhaifu katika usimamizi na ukusanyaji wa mapato katika maeneo hayo kumeikosesha serikali mapato yake halali.

**Mapendekezo**

Kwa mantiki hii, ninapendekeza Mamlaka ya Mapato (TRA) kuyafanyia uchunguzi wa kina makampuni yote ya mafuta na gesi ikiwa ni pamoja na makampuni kuchimba madini kutathmini kiwango cha ushuru wa forodha ambacho hakijalipwa na kuchukua hatua ili kilipwe, pia, katika siku zijazo, mamlaka ihakikishe ushuru huo unalipwa na makampuni yote yanayopaswa kulipa.

## 13.3 Kujumuishwa kwa Taasisi za Umma zenye Vipindi na Kanuni Tofauti za Uhasibu katika Hesabu Jumuifu

Mapitio ya Hesabu za Majumuisho(consolidated accounts) yamebaini kwamba taasisi za umma kama vile BRELA, SUMA JKT hazikujumuishwa katika hesabu. Vilevile, nimebaini ujumuishwaji wa taasisi za umma zenye kuandaa hesabu zake kwa kutumia tarehe (vipindi) tofauti na ile ya serikali, yaani tarehe 30 Juni, 2014. Taasisi hizo zimekuwa zikijumuishwa katika Hesabu za Majumuisho ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pasipo kuzingatia tofauti ya tarehe za ufungaji wa mahesabu.

Ni maoni yangu kwamba, kwa serikali kushindwa kujumuisha hesabu za taasisi zake zote, na pia kushindwa kusuluhisha hesabu za taasisi zenye vipindi tofauti vya ufungaji wa mahesabu inapelekea kuleta uwalakini katika kueleza hali halisi ya Hesabu za Jamhuri.

**Mapendekezo**

Nashauri Serikali ifanye yafuatayo:

- Mifumo ya uhasibu ya taasisi zinazomilikiwa na serikali iwianishwe pamoja na kuendana sambamba na mfumo wa uandaaji hesabu wa kimataifa usio wa taslimu (IPSAS Accrual).
- Taasisi zote zinazomilikiwa na serikali zijumuishwe kwenye hesabu za taasisi miliki ili hesabu za taasisi hiyo zioneshe uhalisia na kuendana na viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu.

## 13.4 Deni la Taifa

### 13.4.1 Ukosefu wa Uwiano Sawia wa Ukomo katika Dhamana za Serikali

Muundo wa Dhamana za Serikali katika Deni la Ndani umegubikwa na wingi wa dhamana za muda mfupi. Kulingana na Mpango wa Utoaji wa Dhamana za Serikali wa mwaka 2013/2014 ulioandaliwa na Kamati ya Maendeleo ya Masoko ya Dhamana, serikali ilipanga kuuza dhamana za muda mrefu. Nia hasa ilikuwa kuiwezesha serikali kuleta uwiano sawia wa muundo wa dhamana zake katika soko na hivyo kuipunguzia gharama za kulipa dhamana hizo katika vipindi vya pamoja.

Hata hivyo, nimebaini kwamba serikali iliuza zaidi Hati fungani pamoja na Dhamana za muda mfupi, miaka 2, na hivyo kuendelea kuiongezea serikali gharama za ulipaji katika vipindi vifupi. Hali hii ni kinyume na Mpango wa Utoaji wa Dhamana za Serikali na pia kinyume na Mkakati wa Taifa wa Deni, 2002 (National Debt Strategy, 2002).

**Mapendekezo**

Napenda kuishauri serikali kuongeza ushindani katika soko la ndani la dhamana za serikali na hivyo kuongeza ushawishi wa ununuzi wa dhamana za muda mrefu.

### 13.4.2 Kutokuwepo Taarifa ya Hesabu za Udhamani wa Serikali ndani ya Deni la Taifa

Ukaguzi wangu umebaini kwamba madeni ya udhamini wa Serikali kwenye taasisi za kijamii zinazotegemea ruzuku kutoka serikalinikama vile Mamlaka ya Vitambulisho (NIDA), na Chuo Kikuu cha Dodoma hayakuingizwa katika hesabu za deni la Taifa. Vile vile, kulikuwepo na madeni ambayo yametokana na taasisi za umma kushindwa kumudu masharti ya udhamini na hivyo kuipelekea serikali kuanza kuyalipa pasipo kujumuishwa kwenye deni la taifa. Kimsingi, madeni haya yatokanayo na udhamini yanastahili kutambuliwa kama sehemu ya deni la taifa na hivyo yarekodiwe kwenye hesabu za Fungu 22 – Deni la Taifa.

**Mapendekezo**

Napenda kuishauri serikali kuzingatia utendaji bora na hivyo kuingiza madeni yanayotokana na udhamini wa Taasisi za kijamii katika Deni la Taifa. Pia, nashauri serikali kumteua Kamishina na wasaidizi wake katika ofisi mpya ya kusimamia deni la taifa (Debt Management Division) ili madeni na udhaminiviweze kusimamiwa vyema.

**13.5 Usimamizi Usiotosheleza Kwenye Uwekezaji waSerikali na Vipaumbele Vyake**

Nimebaini kudorora kwa usimamizi wa kutosha kwenye uwekezaji wa serikali na vipaumbele vyake ndani ya makampuni mbalimbali. Hali hii inapelekea wakati mwingine hisa za serikali zimekuwa zikipungua na hata wakati mwingine kuisha kabisa. Hii inatokana na serikali kuchelea kuongeza mtaji wakati ilipohitajika kufanya hivyo katika hisa za Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Biashara (NBC Ltd.). Mashirika mengine ambayo yamegubikwa na kusuasua kwa usimamizi wa uwekezaji wa serikali ni pamoja na Shirika la Ndege (ATCL), TAZARA, Shirika la Reli (TRL) ambayo yote kwa namna moja au nyingine yana changamoto za mitaji na hivyo kuendelea kutegemea ruzuku toka serikalini.

Kukosekana kwa Mfuko wa Uwekezaji imekuwa ni changamoto kwa mashirika niliyoyabainisha hapo awali hasa inapotokea uhitaji wa kuongeza mtaji. Kwa mwenenendo huu, wahitaji wengine katika makampuni wanaweza kushawishika kuongeza mitaji(recapitalization) na hali wakijua serikali inakabiliwa na uhaba wa fedha na hivyo kupelekea hisa za serikali kupungua, na hata kuisha kabisa kwenye umiliki ndani ya mashirika.

**Mapendekezo**

Hivyo, naishauri serikali kuandaa Mfuko wa Uwekezaji utakaowezeshwa kutoka kwenye gawio na mapato mbalimbali ili kunusuru hisa za serikali, na pia kuiwezesha serikali kuwekeza katika sekta zingine ambazo itaona zinahitaji ushiriki wake.

Mwisho, naishauri serikali kupitia mara kwa mara ufanisi wa uwekezaji wake na malengo yake katika makampuni ambayo inamiliki hisa chache.

## 13.6 Ucheleweshwaji wa Fedha na Kutolewa kwa Fedha Pungufu

Fedha zinazotolewa na Serikali kupitia Hazina zimekua zikitolewa kwa kuchelewa na pengine zimekua zinachelewa kupokelewa kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hii imesababisha kuchelewa kwa utekelezaji au kutotekelezwa kabisa kwa miradi iliyokusudiwa kwa wakati na kupelekea kuongezeka kwa gharama za miradi na kubaki kwa kiasi kikubwa cha fedha mwishoni mwa mwaka ambazo hazijatumika.

Katika kipindi cha mwaka uliomalizika, fedha za maendeleo kiasi cha TZS.1,888,911,542,533 hakikutolewa, wakati kiasi cha TZS.19,229,865,085 cha fedha zilizotolewa kwa ajili ya maendeleo hazikutumika. Kiasi cha TZS.400,259,001,766 za akaunti ya matumizi ya kawaida hazikutolewa wakati kiasi cha TZS.8,279,275,815 cha fedha kwa matumizi ya kawaida hazikutumika.

Fedha za maendeleo kiasi cha TZS.1,259,031,558,670 sawa na 40% ya fedha iliyotolewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo za Wizara na Sekretarieti za Mikoa na fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya kiasi cha TZS.2,187,509,171,733 sawa na 23% ya fedha iliyotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Wizara na Sekretarieti za Mikoa ilitolewa katika robo ya nne ya fedha mwaka.Maelezo zaidi yanapatikana katika sura ya nne ya ripoti hii.

**Mapendekezo**

Ili kukabiliana na changamoto ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kutolewa kwa kuchelewa, nashauri Serikali kuandaa makisio yake ya mwaka yanayoshabihiana na makusanyo ya mapato ili kuepuka kutolewa kwa kiasi kikubwa cha fedha mwishoni mwa mwaka wa

fedha. Kwa kufanya hivyo, inatarajiwa kwamba shughuli zilizopangwa zitatekelezwa kama zilivyopangwa.

Ili Serikali kupunguza utegemezi katika misaada kutoka nje kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Taifa, nashauri Serikali kuchunguza vyanzo mbadala vya mapato vya ndani.

### 13.7 Mapungufu katika Usimamizi wa rasilimali watu na malipo ya mishahara

Mapitio ya usimamizi wa rasilimaliwatu yamebaini mapungufu katika baadhi ya Wizara/Idara/Balozi kama vile ukosefu wa taarifa sahihi za watumishi, Malipo kwa watumishi ambao hawapo kwenye utumishi, watumishi wenye sifa kutothibitishwa kwa wakati, makato ya mishahara zaidi ya kiwango kinachokubalika kisheria, Ukosefu wa fedha za kusafirisha watumishi wa ubalozi waliostaafu na mali zao, marejesho ya mishahara kwenye akaunti isiyo sahihi.

**Mapendekezo**

- Kutokana na mapungufu niliyobaini katika usimamizi wa rasilimaliwatu, Maafisa Masuuli wanashauriwa kutumia kwa ufanisi mfumo wa kompyuta wa Lawson na kuhakikisha kwamba kumbukumbu sahihi za wafanyakazi zinatunzwa ,na wakati huohuo maafisa waliostaafu wanafutwa kwenye mfumo huo kwa wakati, pia kuhakikisha kuwa mtumishi haidhinishiwi mkopo mpya kabla ya kulipa na kumaliza uliotangulia.

- Ninashauri kuwa, Menejimenti ya wizara ya mambo ya nje na ushirikiano wa kimataifa kusitisha mara moja malipo ya posho na kodi kwa watumishi waliostaafu walioko nje ya nchi na kufanya utaratibu kwa ajili ya kuwarejesha maafisa husika nyumbani mara tu muda utumishi wao unapokoma.

### 13.8 Mapungufu katika Usimamizi wa mali

Ukaguzi wa usimamizi mali kwa mwaka 2013/14 ulijikita katika mapitio ya kuwepo kwa mali, kutoa taarifa, utambuzi, uainishaji, haki na wajibu, kuonyesha zinavyotumika na thamani ya fedha ya

mali zote zilizoonyeshwa katika taarifa za fedha.

Changamoto za usimamizi wa mali umeonyeshwa kwa kina katika sura ya kumi na moja ya taarifa hii. Changamoto hizo ni magari na pikipiki zilizoegeshwa ambazo zimefikia muda wake wa mwisho wa kutumika na hazitengenezeki; Ardhi na majengo kutotenganishwa wakati wa kuandaa taarifa za fedha kwa mujibu wa aya ya 17(74) ya IPSASs; Ukosefu wa nyaraka za umiliki wa ardhi na majengo na Rejista ya mali za kudumu kutokwendana na wakati.

**Mapendekezo**

- Kwakuwa kasi ya kutathimini mali za kudumu, uandaaji wa rejista ya mali za kudumu na kuweka alama za utambulisho wa mali linaonekana kuwa ndogo, nashauri Mlipaji Mkuu wa Serikali aharakishe mchakato huo na ahakikishe changamoto zote zilizobainikazinashughulikiwa kabla ya mwaka 2016/2017 ambapo serikali inatakiwa iwe inatekeleza IPSAS kikamilifu,
- Mbali na mafunzo ambayo yamefanyika, nashauri Mlipaji Mkuu wa Serikali kutoa mwongozo wa namna ya kuweka kumbukumbu katika rejista ya mali za kudumu, msisitizo uwe katika jinsi ya kutathimini mali, kiwango cha uchakavu, kuweka alama za utambulisho na uboreshaji wa taarifa mara kwa mara katika rejista ya mali za kudumu,
- Nashauri serikali kuzingatia matumizi ya mifumo ya kompyuta ambayo inaendana na kuingiliana na mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS) kwaajili ya kusimamia mali za serikali ili kuepuka uandaaji wa taarifa nyingi na vihatarishi vinavyotokana na kuhamisha taarifa kutoka mfumo mmoja kwenda mwingine,
- Naishauri serikali kuhakikisha taarifa za kihasibu za Maafisa masuhuli zinatenganisha ardhi na majengo ili kupata thamani ya ardhi na kutoza uchakavu kwenye mali zinazochakaa. Pia, nashauri serikali ihakikishe Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za mikoa zinapata hati miliki ili kulinda mali zake,

- Nashauri serikali ichukue hatua stahiki kuweza kufuta ambazo zimechakaa na hazitengenezeki kwa mujibu wa kanuni za fedha za mwaka 2001.

## 13.9 Menejimenti ya Wakala za Serikali.

Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 nimetoa taarifa maalum inayohusu utendaji wa Wakala za Serikali, Mifuko Maalum ya fedha na taasisi nyingine za serikali.

Matokeo ya ukaguzi katika wakala wa serikali umeonyesha kuwepo kwa makosa katika kufuta sheria mbalimbali za fedha kama ilivyoonyeshwa kwenye sura ya nane ya taarifa hii.

Vilevile imeonekana kuwa Wakala Kuu wa serikali bado wanaitegeme Serikali katika kuendesha maswala yao kama vile kulipa mishahara ya wafanyakazi na fedha nyingine za matumizi ya kawaida na maendeleo kinyume na sheria ya kuanzishwa kwa wakala.

**Mapendekezo**

- Kuhusu ukusanyaji wa mapato ninazishauri wakala zote kuweka mikakati ya kutafuta vyanzo vipya vya mapato na kuandaa sera na miongozo itakayosaidia kuhakikisha kuwa mapato yanakusanywa kama ilivyotegemewa.
- Kwa sababu wadaiwa wengi ni Idara za serikali, ninamshauri Mlipaji mkuu wa serikali kuhakikisha kuwa miongozo inatolewa kwa wakala ili waweze kulipa madeni husika.

## 13.10 Limbikizo la Madeni

Matokeo ya ukaguzi ya mwaka huu wa fedha yanaonyesha kuongezeka kwa madeni kwa zaidi ya asilimia 50, kiasi hiki ni kikubwa na kinahitaji ufuatiliaji wa haraka. Nina maoni kuwa mfumo taslimu wa bajeti(Cash based budgeting) ni sababu mojawapo ya kuongezeka kwa limbikizo la deni hili.Ninaishauri serikali kuhakikisha kuwa mfumo wa bajeti ya taslimu unabuniwa upya ili kuhakikisha utaondoa udhaifu wake na kuimarisha ubora

wake wa kuoanisha (Performance budgeting) bajeti na MTEF.

Nimeona kutokuingizwa kwa malimbikizo ya madeni kwenye bajeti inayofuata ya serikali kuu, inasababisha kuendelea kuongezeka kwa madeni kwa sababu bajeti ya sasa itatumika kulipa madeni ya nyuma. Katika kiasi kilichotolewa taarifa TZS 1,691,751,088,761, kiasi cha TZS 1,076,686,798,505 ni madeni ambayo yana zaidi ya siku 90.

Iwapo juhudi hazitafanywa kulipa madeni haya , basi wazabuni na watoa huduma watakosa imani na taasisi za Serikali , na hivyo kutokuendelea kutoa huduma serikalini, jambo ambalo litadumaza ubora wa huduma zitolewazo.

**Mapendekezo**

Ninaishauri serikali kuongeza makusanyo ya mapato, kupunguza matumizi ya serikali na hatimaye kutumia baki ya fedha kulipa madeni, zaidi ya hayo ninaishauri serikali kulipa umuhimu wa kipekee swala la kulipa madeni ya huduma za afya nje ya nchi.

## 13.11 Madeni yanayotegemea Matukio(Contingent Liabilities)

Katika kupitia taarifa za fedha za taasisi kumi (10) za Serikali kuu, na Mikoa mitano (5) nimeona kuna kesi 83 zinazosubili hukumu za mahakama na ambazo zina athari kubwa za kifedha kwa taasisi husika.

**Mapendekezo**

Kufuatana na kesi zilizoko mahakamani na ambazo zina athari za kifedha kwenye taasisi za Serikali kuu (MDAs na RAS) ninawashauri Maafisa Masuuli kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha kuwa ufuatiliaji wa Karibu unafanyika ili kesi hizi zihitimishwe kwa mujibu wa sheria zilizopo na hivyo kuondoa gharama kubwa za ufuatiliaji.

## 13.12 Ukaguzi maalum

Sura ya kumi na mbili inazungumzia matokeo ya kaguzi Maalum nane zilizofanyika katika mwaka wa fedha 2013/2014. Yafuatayo ni Majumuisho na mapendekezo yatokanayo na ukaguzi maalum;

### 13.12.1 Ukaguzi maalum wa mradi wa manunuzi ya matrekta na zana za kilimo wa SUMA JKT kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2010 hadi Aprili, 2014

Utekelezaji wa mradi huu umekuwa na changamoto kadhaa katika usimamizi wa mradi zilizosababishwa na utekelezaji wa mradi bila kuzingatia andiko la mradi;awali matrekta yalikuwa yanauzwa kwa fedha taslim na baadaye kwa mkopo bila kuzingatia gharama ya ukusanyaji wa madeni katika bei ya kuuzia matrekta hayo. Pia, ukaguzi umegundua udhaifu kadhaa katika manunuzi ya matrekta hayo.

**Mapendekezo**

- Serikali inapaswa kutathmini uwezo wa kifedha wa mradi, uwezo wa rasilimali watu na uwezo wa kiufundi ili kujua udhaifu uliopo na hatimaye kutoa msaada ipasavyo.
- Usimamizi wa mradi wa matrekta chini ya SUMA JKT uhakikishe mradi unatekelezwa kwa kufuata sheria na kanuni za husika za manunuzi ili kuhakikisha pande zote mbili katika mkataba zinatekeleza mkataba ipasavyo,majukumu yote ya kimkataba ambayo hayajatekelezwa inapaswa yatekelezwe au gharama husika zake kurejeshwa kwa mwajiri

### 13.12.2 Ukaguzi maalum wa mfumo mzima wa manunuzi wa pembejeo za kilimo katika sekta ya kilimo cha tumbaku chini ya WETCO – Tabora

Mchakato wa kuwapata wazabuni uligubikwa kukosekana kwa utawala bora na mgongano wa kimaslahi, ulipelekea wasambazaji kupewa zabuni bila kuwasilisha maombi ya zabuni na bila kibali cha kutoka bodi ya zabuni

Mchakato mzima wa ujenzi wa maghara ikiwa ni pamoja na jinsi ya kuwapata wakandarasi haukufanyika kwa kwa mujibu sheria na kanuni za manunuzi. Maghara yaliyotembelewa yalikuwa chini ya kiwango na baadhi kuanguka kabla ya kutumika

**Mapendekezo**

- Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika inapaswa kuimarisha jukumu la usimamizi ili kuhakikisha kunakuwepo wa utawala bora katika uendeshaji wa vyama vya ushirika,
- Naishauri Serikali kuweka sifa za chini za viongozi wavyama vya msingi vya ushirika (AMCOS) kutokana na hali ya sasa ilivyo, viongozi wengi wa vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS) wana viwango vya chini vya elimu hivyo uwezo wao unaleta mashaka kama wanaweza kusimamia vyama, fedha na mikopo ya vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS).Pia, napendekeza sheria ya manunuzi ifuatwe.

### 13.12.3 Ukaguzi maalum wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu changamoto inayozikabili balozi za Tanzania katika mwaka wa fedha 2010/11, 2011/12 na 2012/13

Ukaguzi maalum uliofanyika umebaini kuwa bajeti iliyoandaliwa haikuwa na uhalisia kwasababu bajeti iliandaliwa bila kuzingatia mahitaji halisi ya balozi. Baadhi ya vifungu vya matumizi havikuwekwa kwenye bajeti, vifungu hivyo ni vya matengenezo ya magari, ununuzi wa mafuta, maji na gharama za umeme. Hivyo, kuathiri utekelezaji wa malengo ya balozi.

**Mapendekezo**

- Balozi zinakabiriwa na changamoto za fedha kutokana na urasimu katika utoaji wa fedha. Napendekeza kuwa ni wakati muafaka sasa kutenga fedha zitakazotosheleza mahitaji ya balozi kupitia fungu maalum itakayoitwa fungu la balozi,
- Serikali ihakikishe kwamba fedha inayotengwa katika bajeti kwa ajili ya balozi inatosheleza mahitaji ya kifedha ya balozi

### 13.12.4 Ukaguzi maalum juu ya utekelezaji wa mikataba ya ujenzi wa mradi wa usambazaji maji Chalinze – Awamu ya pili

Mapungufu yaliyobainika ni pamoja naMikataba kutokamilika katika muda uliopangwa, ripoti ya upembuzi yakinifu iliombwa lakini haikuwasilishwa kwa wakaguzi.

Kasoro mbalimbali katika usanifu wa mradi na michoro, Utendaji duni wa mshauri hivyo kushindwa kuchukua hatua stahiki kwa wakati ikiwa ni pamoja na kumshauri mwajiri ipasavyo juu ya utendaji usioridhisha wa mkandarasi (Mega Builders Limited) ambaye hakuwa na sifa za kufanya kandarasi kubwa kutokana na viwango vilivyowekwa na bodi ya kusajili makandarasi, mkandarasi alisajiriwa katika daraja sita wakati kazi ilihitaji wakandarasi wa daraja la IV, III, II na I.

Pia, nilibaini malipo yalifanyika kwa mkandarasi bila kuwepo kwa hati ya kuonyesha kazi imekamilika, miundombinu ya maji ilikabidhiwa bila kufanyiwa majaribio, riba ya TZS 3,897,283,923 kutokana na kuchelewesha malipo kwa wakandarasi

**Mapendekezo**

- Wazabuni wapewe mikataba ya kazi inayolingana na uwezo wao na daraja la mkandarasi kwa mujibu wa Bodi ya Usajili wa wakandarasi (CRB)
- Usanifu wa miradi kama wa usambazaji wa maji Chalinze ni vema ukapitiwa kwa umakini kabla ya kutangazwa kwa zabuni,
- Taasisi zinazofanya manunuzi zinapaswa kuimarisha ufuatiliaji ili kuhakikisha makandarasi wanafuatiliwa na wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa mkataba.Taasisi zinazofanya manunuzi zinatakiwa kuwa na hakika wa upatikanaji wa fedha kabla ya kuingia katika mikataba ili kuepuka gharama za ziada kama tozo zinazosababishwa na ucheleweshaji wa malipo.

### 13.12.5 Ukaguzi maalum katika Wizara ya Ujenzi kuhusu uhalali wa fedha TZS 252,975,000,000 za ujenzi wa barabara kutumika kulipia madeni nje ya utaratibu

Ukaguzi maalum wa Wizara ya Ujenzi (fungu 98) ulilenga kufanya uhakiki wa fedha kiasi cha TZS. 252,975,000,000 kilichoidhinishwa kwaajili ya mradi wa ujenzi wa barabara maalum kilitumika kulipa madeni ya wakandarasi na washauri.

Taarifa iliyowasilishwa bungeni juu ya mradi wa ujenzi wa barabara maalum na. 4168 kwa TZS. 252,975,000,000 haikuwa sahihi kwani fedha hizo zilitumika kulipia madeni ya wakandarasi na washauri.

Ilibainika kuwa bajeti inayohitajika kwaajili ya Wizara ya Ujenzi haikuweza kufikiwa na serikali kwani Wizara ya Fedha ilitoa ukomo wa juu wa bajeti ambao ni mdogo ukilinganisha na mahitaji halisi.

**Mapendekezo**

- Bajeti inapaswa iandaliwe kwa kuzingatia mahitaji halisi.
- Serikali isaini mikataba mipya ya ujenzi wa barabara baada ya kupima uwezo iliona wa kulipa madeni ya wakandarasi waliopo ili kuzuia kukua kwa madeni katika siku zijazo

### 13.12.6 Ukaguzi maalum wa taarifa za fedha zilizotumika katika mkutano wa kimataifa wa SMART Partnership Dialogue (SPD) wa mwaka 2013 uliofanyika kwa miezi kumi na nane kuanzia Julai, 2012 hadi Januari, 2914

Ukaguzi maalum ulibaini Kutozingatiwa kwa bajeti iliyoidhinishwa kwaajili ya manunuzi ya tiketi ya usafiri wa ndege.Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya tiketi za ndege ilikuwa TZS 21,000,000 lakini kiasi halisi kilichotumika ya tiketi hizo ni TZS.186,998,268; hivyo kupelekea matumizi zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa kwa TZS.165,998,268.Pia, manunuzi yenye thamani ya TZS.614,626,341 yalifanywa nje ya mpango wa manunuzi uliopitishwa.

**Mapendekezo**

Nashauri taasisi zinazofanya manunuzi ya vifaa, huduma na ujenzi zihakikishe manunuzi yote yanawekwa na kufanyika kwa mujibu wa mpango wa manunuzi. Taasisi zifanye manunuzi yenye tija kwa taifa kwani kiasi kikubwa cha fedha za serikali zinatumika katika kufanya manunuzi.

## 13.13 Mapungufu katika usimamizi wa manunuzi

Katika ukaguzi wangu nimebaini bado kuna mapungufu katika uzingatiaji wa Sheria manunuzi ya umma ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013.

Wizara, Idara, Wakara na Sekretarieti za mikoa nyingi bado zinafanya manunuzi ya bidhaa, huduma na ujenzi bila kuzingatia mpango wa manunuzi, zinaingia katika mikataba bila kuwepo ushindanishaji wa zabuni na mchakato wa tathmini, bidhaa na huduma zinanunuliwa bila idhini ya bodi ta manunuzi na bidhaa zinapokelewa bila kukaguliwa.

Kwa ujumla Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za mikoa hazina mfumo mzuri wa ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa manunuzi na mchakato wa kuingia katika mikataba ya bidhaa na huduma yanaleta thamani ya fedha na kufikiwa kwa malengo yaliyopangwa.

**Mapendekezo**

Kwa kuzingatia muhtasari wa mapungufu niliyoyataja kwenye taarifa hii, kwa ujumla ninapendekeza kwamba menejimenti za Wizara/Sekretarieti za mikoa zinapaswa kuhakikisha kuwa sheria ya manunuzi ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013 zinazingatia kikamilifu. Pia, mapendekezo yaliyotolewa na PPRA na Mhakiki mali ni muhimu yatekelezwe.

## 13.14 Usimamizi wa bajeti usioridhisha

Mwenendo wa ukuaji wa bajeti ya Taifa unaonesha kwa miaka kadhaa unaonesha kukua katika mapato na matumizi.Hata hivyo,ikilinganishwa na ukuaji wa makusanyo na ukuaji wa matumizi inaonesha ukuaji wa ukusanyaji wa mapato haundeni na ukuaji wa bajeti ya matumizi

Kutokana na kutofautiana kati ya rasilimali chache zilizopo na haja ya ukuaji kiuchumi kwa haraka, taifa limejikuta na changamoto ya kujiendesha na bajeti isiyo na uhalisia kila mwaka. Kwa ujumla kwa miaka mingi Serikali imejikuta inashindwa kuziba pengo la hilo. Kutofikiwa kwa bajeti kunapelekea kugharamia matumizi yenye kipaumbele kulingana na fedha iliyopatikana badala ya fedha iliyoidhishwa na bajeti. Kuchelewa kwa kutolewa fedha kutoka wizara ya fedha kunacheleweshа mipango ya manunuzi pamoja na malipo yake.

Bajeti ya maendeleo ina ufanisi mdogo ukilinganisha na bajeti ya matumizi.Hii imesababishwa na kuchelewa kwa utekelezaji na kukamilika kwa miradi ya maendeleo katika ngazi ya kitaifa na kimkoa kupelekea ongezeko zaidi la gharama ya utekelezaji wake ikilinganishwa na ilivyopangwa hapo awali. Pia nimebaini kuwa baada ya bajeti kupitishwa na kuidhinishwa baadae kumekuwepo na marekebisho kadha kutokana na makusanyo halisi kuwa ya chini ikilinganishwa na gharama zilizokisiwa.

**Mapendekezo**

- Ukomo wa bajeti unapaswa kuwa wa uhalisia na unapaswa kurejewa/kupitiwa mara kwa mara. Hatua zichukuliwe ili kupunguza ucheleweshaji katika utoaji wa fedha kutoka Wizara ya Fedha.
- Miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya mipya wakati wa utengaji na ugawaji wa fedha.
- Kukuza ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa kuongeza ulipaji kodi kwa hiari ili kukuza mapato, kuongeza vyanzo na kupanua wigo wa kodi.

- Nashauri Serikali kutumia hati za manunuzi kutokana na mfumo wa EPICOR kuepuka kuwalipa wazabuni nje ya bajeti na kutoa kipaumbele kwa miradi inayoendelea na kuhakikisha uwepo wa fedha kabla ya kusaini mikataba.
- Serikali ianzishe utaratibu kutunza kumbukumbu za madeni mwishoni mwa mwaka na kuhakikisha kuwa malimbikizo hayo yanabajetiwa katika bajeti ya mwaka unaofuata. Mbinu hii itapunguza ukuaji wa madeni.

## 13.15 Usimamizi wa madeni

Mapitio niliyofanya kwenye Usimamizi wa matumizi nimebaini kuwa, baadhi ya Wizara/Idara/Balozi zina mfumo dhaifu wa Usimamizi wa matumizi ambayo umeplekea baadhi ya malipo kufanywa bila kuidhinishwa, malipo yasiyo na viambatisho vya kutosha, kukosekana kwa hati za malipo, Malipo zaidi ya kiwango stahiki, Malipo yasiyo na tija, na malipo ambayo hayajaambatishwa na risiti za kukiri mapokezi, risiti za kielechroniki. Mapungufu haya yamejadiliwa kwa kina kwenye sura ya Kumi ya taarifa hii.

**Mapendekezo**

Maafisa masuhuli wa Wizara/Sekretarieti za Mikoa/Balozi wanahimizwa kuendelea kuboresha udhibiti wa ndani ikiwemo kuwajengea uwezo kupitia mafunzo.

## 13.16 Kutotumika kwa Mashine za kielektroniki za EFD

Tathmini yangu juu ya matumizi ya mashine za EFD nimebaini kuwa makampuni na wafanyabiashara wengi bado hawatumii mashine za EFD kutoa risiti. Mapungufu haya yamebainika baada ya Mamlaka ya Mapato kutoza tozo linalofikia TZS 440,793,600 kwa wafanyabiashara kwa kushindwa kutoa risiti za kielektroniki kwa kutumia mashine za EFD. Hata hivyo, ni kiasi cha TZS 71, 893, 600 pekee ambacho kimelipwa waliokiuka sharia na kupelekea salio la kiasi cha TZS 368,900,000 hakijalipwa. Hata hivyo, Malipo yanayofikia kiasi cha TZS 4,419,662,152 yalikosa risiti za EFD.

**Mapendekezo**

Kutokana na kutozingatia Kanuni Na. 24 ya Kanuni za Mapato (EFD) Kanuni za 2012, ninapendekeza serikali kutoa maelekezo kwa taasisi zote za serikali kutojihusisha na wauzaji ambao hawatumii mashine za EFD. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya kodi nashauri elimu ya ulipaji kodi bila shuruti iendelee kutolewa mara kwa mara.

## VIAMBATANISHO

### Kiambatisho 1: Hati za Ukaguzi kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 zilizotolewa kwa Mafungu ya Serikali kuu (Votes)

| S/N | Fungu | Jina la Taasisi | Hati iliyotolewa |
|---|---|---|---|
| 1 | 6 | Ofisi ya Raisi usimamizi na Ufuatiliaji wa Miradi ya Kipaumbele | Hati inayoridhisha |
| 2 | 7 | Msajili wa Hazina | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 3 | 8 | Tume ya Mabadiliko ya Katiba | Hati inayoridhisha |
| 4 | 9 | Ofisi ya Rais-Bodi ya Mishahara | Hati inayoridhisha |
| 5 | 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | Hati inayoridhisha |
| 6 | 12 | Tume ya Huduma za Mahakama | Hati inayoridhisha |
| 7 | 13 | Kitengo cha uchunguzi wa Fedha | Hati inayoridhisha |
| 8 | 14 | Kikosi cha Zimamoto | Hati inayoridhisha |
| 9 | 15 | Tume ya usuluhishi | Hati inayoridhisha |
| 10 | 16 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu | Hati inayoridhisha |
| 11 | 20 | Ofisi ya Rais Ikulu | Hati inayoridhisha |
| 12 | 21 | Idara ya Hazina | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 13 | 22 | Idara ya Madeni ya Taifa | Hati yenye shaka |
| 14 | 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu | Hati inayoridhisha |
| 15 | 24 | Tume ya Maendeleo ya Ushirika | Hati inayoridhisha |
| 16 | 25 | Ofisi ya Waziri Mkuu | Hati inayoridhisha |
| 17 | 26 | Ofisi ya Makamu wa Rais | Hati inayoridhisha |
| 18 | 27 | Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | Hati inayoridhisha |
| 19 | 28 | Idara ya Polisi | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 20 | 29 | Idara ya Huduma za Magereza | Hati inayoridhisha na |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | masuala ya msisitizo |
| 21 | 30 | Ofisi ya Rais- Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri | Hati inayoridhisha |
| 22 | 31 | Ofisi ya Makamu wa Rais | Hati inayoridhisha |
| 23 | 32 | Ofisi ya Rais -Menejimenti ya Utumishi | Hati inayoridhisha |
| 24 | 33 | Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili | Hati inayoridhisha |
| 25 | 34 | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa | Hati inayoridhisha |
| 26 | 35 | Mkurugenzi Mwendesha Mashitaka | Hati inayoridhisha |
| 27 | 36 | Sekretarieti ya Mkoa-Katavi | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 28 | 37 | Ofisi ya Waziri Mkuu | Hati inayoridhisha |
| 29 | 38 | Jeshi la wananchi wa Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 30 | 39 | National Service (JKT) | Hati inayoridhisha |
| 31 | 40 | Mfuko wa Mahakama | Hati inayoridhisha |
| 32 | 41 | Wizara ya Katiba na Sheria | Hati inayoridhisha |
| 33 | 42 | Bunge | Hati inayoridhisha |
| 34 | 43 | Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 35 | 44 | Wizara ya Viwanda na Biashara | Hati inayoridhisha |
| 36 | 46 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi stadi | Hati inayoridhisha |
| 37 | 47 | Sekretarieti ya Mkoa -Simiyu | Hati inayoridhisha |
| 38 | 48 | Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi | Hati inayoridhisha |
| 39 | 49 | Wizra ya Maji na Umwagiliaji | Hati inayoridhisha |
| 40 | 50 | Wizara ya Fedha | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 41 | 51 | Wizara ya Mambo ya Ndani | Hati yenye shaka |
| 42 | 52 | Wizra ya Afya na Usitawi wa Jamii | Hati yenye shaka |
| 43 | 53 | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto | Hati inayoridhisha |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 44 | 54 | Sekretarieti ya Mkoa-Njombe | Hati inayoridhisha |
| 45 | 55 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | Hati inayoridhisha |
| 46 | 56 | Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | Hati inayoridhisha |
| 47 | 57 | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 48 | 58 | Wizara ya Madini na Nishati | Hati inayoridhisha |
| 49 | 59 | Tume ya Marekebisho ya Sheria Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 50 | 61 | Tume ya Uchaguzi ya Taifa | Hati inayoridhisha |
| 51 | 62 | Wizara ya Uchukuzi | Hati inayoridhisha |
| 52 | 63 | Sekretarieti ya Mkoa Geita | Hati yenye shaka |
| 53 | 65 | Wizara ya Kazi na Ajira | Hati inayoridhisha |
| 54 | 66 | Ofisi ya Rais Tume ya Mipango | Hati inayoridhisha |
| 55 | 67 | Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira Utumishi Wa Umma | Hati inayoridhisha |
| 56 | 68 | Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia | Hati inayoridhisha |
| 57 | 69 | Wizara ya Maliasili na Utalii | Hati inayoridhisha |
| 58 | 70 | Sekretarieti ya Mkoa Arusha | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 59 | 71 | Sekretarieti ya MkoaPwani | Hati inayoridhisha |
| 60 | 72 | Sekretarieti ya Mkoa Dodoma | Hati inayoridhisha |
| 61 | 73 | Sekretarieti ya Mkoa Iringa | Hati yenye shaka |
| 62 | 74 | Sekretarieti ya Mkoa Kigoma | Hati inayoridhisha |
| 63 | 75 | Sekretarieti ya Mkoa Kilimanjaro | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 64 | 76 | Sekretarieti ya Mkoa Lindi | Hati inayoridhisha |
| 65 | 77 | Sekretarieti ya Mkoa Mara | Hati inayoridhisha |
| 66 | 78 | Sekretarieti ya Mkoa Mbeya | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 67 | 79 | Sekretarieti ya Mkoa Morogoro | Hati inayoridhisha na |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | masuala ya msisitizo |
| 68 | 80 | Sekretarieti ya Mkoa Mtwara | Hati inayoridhisha |
| 69 | 81 | Sekretarieti ya Mkoa Mwanza | Hati yeney shaka |
| 70 | 82 | Sekretarieti ya Mkoa Ruvuma | Hati inayoridhisha |
| 71 | 83 | Sekretarieti ya Mkoa Shinyanga | Hati inayoridhisha |
| 72 | 84 | Sekretarieti ya Mkoa Singida | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 73 | 85 | Sekretarieti ya Mkoa Tabora | Hati inayoridhisha |
| 74 | 86 | Sekretarieti ya Mkoa Tanga | Hati inayoridhisha |
| 75 | 87 | Sekretarieti ya Mkoa Kagera | Hati yenye shaka |
| 76 | 88 | Sekretarieti ya Mkoa Dar es Salaam | Hati inayoridhisha |
| 77 | 89 | Sekretarieti ya Mkoa Rukwa | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 78 | 91 | Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya | Hati inayoridhisha |
| 79 | 92 | Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 80 | 93 | Idara ya huduma za Uhamiaji | Hati inayoridhisha |
| 81 | 94 | Public Service Commission | Hati inayoridhisha |
| 82 | 95 | Sekretarieti ya Mkoa Manyara | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 83 | 96 | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo | Hati inayoridhisha |
| 84 | 97 | Wizara ya Ushirikiano Afrika Mashariki | Hati inayoridhisha |
| 85 | 98 | Wizara ya Ujenzi | Hati inayoridhisha |
| 86 | 99 | Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi | Hati inayoridhisha |
| 87 | | Hesabu Jumuifu za Taifa | Hati isiyoridhisha |

## Kiambatisho 2: Hata za Ukaguzi kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 zilizotolewa kwa Wakala wa Serikali(Agencies)

| | Jina la wakala wa serikali | Aina ya hati iliyotolewa |
|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Serikali Huduma za Mtandao serikalini | Hati inayoridhisha |

| | | |
|---|---|---|
| 2 | Wakala wa usajili wa vifo na Vizazi, Ufilisi (RITA) | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 3 | Wakala wa huduma za misitu Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 4 | Wakala wa Mafunzo ya Kimataifa | Hati inayoridhisha |
| 5 | Chuo cha Utumishi wa Umma | Hati inayoridhisha |
| 6 | Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 7 | Wakala wa Mbegu za Kilimo | Hati inayoridhisha |
| 8 | Wakala Wa Uchimbaji wa Visima na Mabwawa | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 9 | Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo | Hati inayoridhisha |
| 10 | Wakala wa Utafiti wa Miamba | Hati inayoridhisha |
| 11 | Taasisi ya mafunzo ya mifugo | Hati inayoridhisha |
| 12 | Wakala wa Chakula cha Akiba Taifa | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 13 | Mamlaka ya viwanja vya ndege Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 14 | Wakala wa Majengo Tanzania | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 15 | Wakala wa Ufundi wa Mitambo, Magari na Umeme Tanzania | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 16 | Wakal wa ndege za Serikali Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 17 | Wakala wa Utabiri wa Hali ya Hewa Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 18 | Wakala wa barabarabtanzania (TANROAD) | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 19 | Wakala wa Maabara ya Mifugo Tanzania | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 20 | Taasisi ya Maendeleo ya Rasilimali ya Maji | Hati inayoridhisha |
| 21 | Wakala wa Vipimo Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 22 | Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 23 | Wakala wa Maendeleo na Usimamizi wa Elimu | Hati inayoridhisha |
| 24 | Wakala wa Maabara za Serikali | Hati inayoridhisha |

| | | |
|---|---|---|
| 25 | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo | Hati inayoridhisha |
| 26 | Wakala wa Usalama na Afya Kazini (OSHA) | Hati inayoridhisha |
| 27 | Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 28 | Wakala wa ukaguzi wa madini Tanzania Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 29 | Wakala wa magari ya mwendo kasi DSar es salaam (DART) | Hati inayoridhisha |
| 30 | Wakala wa huduma za ugavi na manunuzi (GPSA) | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 31 | Wakala wa Chakula na Dawa Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 32 | Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) | Hati inayoridhisha |

**Kiambatisho 3: Hati za Ukaguzi kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 zilizotolewa kwa Taasisi nyingine (Other Institutions)**

| Na. | JINA LA TAASISI | AINA YA HATI ILIYOTOLEWA |
|---|---|---|
| 1 | Mpango Kukuza Uuchumi na urasimishaji Mali Tanzania (MKURABITA) | Hati inayoridhisha |
| 2 | Chuo cha uongozi wa Mahakama | Hati inayoridhisha |
| 3 | Shule ya Sheria Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 4 | Mfuko wa taifa wa mambo ya kale | Hati inayoridhisha |
| 5 | Chuo cha Wanyamapori Pasiansi | Hati yenye shaka |
| 6 | Mfuko wa Misitu Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 7 | Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori | Hati inayoridhisha |
| 8 | Taasisi ya Uongozi | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 9 | Mfuko wa Pembejeo za Kilimo | Hati inayoridhisha |
| 10 | Mfuko wa Ukaguzi na Usimamizi wa Ushirika | Hati inayoridhisha |
| 11 | Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo | Qualified Audit Opinion |
| 12 | Bodi ya Mfuko wa Barabara | Hati inayoridhisha |

| | | |
|---|---|---|
| 13 | African Peer Review Mechanism | Hati inayoridhisha |
| 14 | Office of the Constituent Assembly | Hati inayoridhisha |
| 15 | Taasisi ya Mafunzo Serikali za Mitaa Hombolo | Hati inayoridhisha |
| 16 | Kituo cha Teknolojia ya Uundaji magari Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 17 | Mfuko wa Kupambana na Majanga Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 18 | Baraza la Famasia Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 19 | Baraza la Wakunga na Wauguzi Tanzania | Hati inayoridhisha |
| 20 | Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru | Hati inayoridhisha |
| 21 | Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake | Hati inayoridhisha |
| 23 | Mfuko wa Maendeleo na Uwezeshaji Kuchimba Madini | Hati inayoridhisha |

## Kiambatisho 4: Hati za Ukaguzi kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 zilizotolewa kwa Ofisi za Balozi

| S/No. | Fungu No. | Balozi | Hati iliyotolewa |
|---|---|---|---|
| 1 | 2001 | Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa, Ethiopia | Hati inayoridhisha |
| 2 | 2002 | Ubalozi wa Tanzania Berlin, Germany | Hati inayoridhisha |
| 3 | 2003 | Ubalozi wa Tanzania Cairo, Misri | Hati inayoridhisha |
| 4 | 2004 | Ubalozi wa Tanzania Kinshasa, Congo- | Hati inayoridhisha |
| 5 | 2005 | Ubalozi wa Tanzania - Abuja | Hati inayoridhisha |
| 6 | 2006 | Ubalozi wa Tanzania – London, Uingereza | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 7 | 2007 | Ubalozi wa Tanzania - Lusaka | Hati inayoridhisha |
| 8 | 2008 | Ubalozi wa Tanzania Maputo, Mozambique | Hati inayoridhisha |
| 9 | 2009 | Ubalozi wa Tanzania Moscow, Russia | Hati inayoridhisha |
| 10 | 2010 | Ubalozi wa Tanzania - New Delhi, India | Hati inayoridhisha |
| 11 | 2011 | Ubalozi wa Tanzania umoja wa Mataifa - New York | Hati inayoridhisha |
| 12 | 2012 | Ubalozi wa Tanzania - Ottawa, Kanada | Hati inayoridhisha |
| 13 | 2013 | Ubalozi wa Tanzania Paris, Ufaransa | Hati inayoridhisha |
| 14 | 2014 | Ubalozi wa Tanzania Beijing, China | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 15 | 2015 | Ubalozi wa Tanzania Rome, Italy | Hati inayoridhisha |
| 16 | 2016 | Ubalozi wa Tanzania Stockholm, Sweden | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 17 | 2017 | Ubalozi wa Tanzania Tokyo, Japan | Hati inayoridhisha |
| 18 | 2018 | Ubalozi wa Tanzania Washington D.C., United States | Hati inayoridhisha |
| 19 | 2019 | Ubalozi wa Tanzania Brussels, Belgium | Hati inayoridhisha |
| 20 | 2020 | Ubalozi wa Tanzania UN - Geneva | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 21 | 2021 | Ubalozi wa Tanzania Kampala, Uganda | Hati inayoridhisha |
| 22 | 2022 | Ubalozi wa Tanzania - Harare | Hati inayoridhisha |
| 23 | 2023 | Ubalozi wa Tanzania Nairobi, Kenya | Hati inayoridhisha |
| 24 | 2024 | Ubalozi wa Tanzania Riyadh, Saudi Arabia | Hati inayoridhisha |
| 25 | 2025 | Ubalozi wa Tanzania Pretoria, South Africa | Hati inayoridhisha na masuala ya msisitizo |
| 26 | 2026 | Ubalozi wa Tanzania Kigali, Rwanda | Hati inayoridhisha |
| 27 | 2027 | Ubalozi wa Tanzania Abu Dhabi | Hati inayoridhisha |
| 28 | 2028 | Ubalozi wa Tanzania Bujumbura | Hati inayoridhisha |
| 29 | 2029 | Ubalozi wa Tanzania Hague | Hati inayoridhisha |
| 30 | 2030 | Ubalozi wa Tanzania Lilongwe | Hati inayoridhisha |
| 31 | 2031 | Ubalozi wa Tanzania - Kuala Lumpar | Hati inayoridhisha |
| 32 | 2032 | Ubalozi wa Tanzania Brasilia | Hati inayoridhisha |
| 33 | 2033 | Ubalozi wa Tanzania, uholanzi | Hati inayoridhisha |
| 34 | 2034 | Ubalozi wa Tanzania Moroni, Comoro | Hati inayoridhisha |

## Kiambatisho 5: Hoja zilizosalia

| Na | Fungu | | Shilingi | Fedha za kigeni |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 36 | Sekretarieti za Mikoa - Katavi | 142,172,994.49 | - |
| 2 | 47 | Sekretarieti za Mikoa - Simiyu | 8,205,000.00 | - |
| 3 | 63 | Sekretarieti za Mikoa - Geita | 379,321,946.00 | - |
| 4 | 70 | Sekretarieti za Mikoa - Arusha | 1,179,122,475.45 | - |
| 5 | 71 | Sekretarieti za Mikoa - Pwani | 600,725,706.00 | - |
| 6 | 72 | Sekretarieti za Mikoa - Dodoma | 9,991,961,854.00 | - |
| 7 | 73 | Sekretarieti za Mikoa - Iringa | 1,683,576,113.25 | - |
| 8 | 74 | Sekretarieti za Mikoa - Kigoma | 4,532,848,072.00 | - |
| 9 | 76 | Sekretarieti za Mikoa - Lindi | 700,178,009.00 | - |
| 10 | 77 | Sekretarieti za Mikoa - Mara | 17,447,020.80 | - |
| 11 | 78 | Sekretarieti za Mikoa - Mbeya | 713,227,108.00 | - |
| 12 | 79 | Sekretarieti za Mikoa - Morogoro | 139,549,247.00 | |
| 13 | 80 | Sekretarieti za Mikoa - Mtwara | 777,679,822.00 | - |
| 14 | 81 | Sekretarieti za Mikoa - Mwanza | 7,723,013,004.80 | - |
| 15 | 82 | Sekretarieti za Mikoa - Ruvuma | 1,106,262,285.00 | - |
| 16 | 83 | Sekretarieti za Mikoa - Shinyanga | 675,498,001.24 | - |
| 17 | 84 | Sekretarieti za Mikoa - Singida | 357,981,591.00 | - |
| 18 | 85 | Sekretarieti za Mikoa - Tabora | 1,171,131,799.51 | - |
| 19 | 86 | Sekretarieti za Mikoa - Tanga | 184,294,057.00 | - |
| 20 | 87 | Sekretarieti za Mikoa - Kagera | 1,085,128,853.00 | - |

| Na | Fungu | | Shilingi | Fedha za kigeni |
|---|---|---|---|---|
| 21 | 88 | Sekretarieti za Mikoa - Dar es Salaam | 114,000,000.00 | - |
| 22 | 89 | Sekretarieti za Mikoa - Rukwa | 480,173,253.69 | - |
| 23 | 95 | Sekretarieti za Mikoa - Manyara | 732,501,940.85 | - |
| 24 | 7 | Msajili wa Hazina | 2,644,223,645.00 | USD 496,598.98 |
| 25 | 21 | Hazina | 7,560,000,000.00 | JPY 17,089,499,858.00 |
| 26 | 23 | Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 12,040,000.00 | - |
| 27 | 25 | Ofisi ya Waziri Mkuu – Ofisi ya waziri Mkuu | 121,069,211.76 | - |
| 28 | 27 | Msajili wa vyama vya siasa | 27,742,098.00 | - |
| 29 | 28 | Idara ya Polisi | 768,568,294.00 | - |
| 30 | 29 | Idara ya Magereza | 6,981,570,087.92 | - |
| 31 | 32 | Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma | 124,273,914.00 | - |
| 32 | 34 | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa | 2,047,923.00 | - |
| 33 | 37 | Ofisi ya Waziri Mkuu | 157,047,276.00 | - |
| 34 | 38 | Jeshi la Wananchi wa Tanzania | 2,921,254,811.72 | - |
| 35 | 40 | Mahakama ya Tanzania | 65,892,630.70 | - |
| 36 | 43 | Wizara ya kilimo, Chakula na Ushirika | 1,338,905,336.21 | - |
| 37 | 46 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi | 92,437,331,068.00 | - |
| 38 | 49 | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | 132,598,919 | - |
| 39 | 50 | Wizara ya Fedha | 193,965,881.00 | - |
| 40 | 51 | Wizara ya Mambo ya | 93,469,100.00 | - |

| Na | Fungu | | Shilingi | Fedha za kigeni |
|---|---|---|---|---|
| | | Ndani | | |
| 41 | 52 | Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii | 34,998,099,144.00 | - |
| 42 | 56 | Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI | 1,091,845,009.00 | - |
| 43 | 57 | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Taifa | 113,660,032,542.00 | - |
| 44 | 61 | Tume ya Uchaguzi ya Taifa | 5,656,393.00 | - |
| 45 | 65 | Wizara ya Kazi na Ajira | 568,939,707.00 | - |
| 46 | 69 | Wizara ya Maliasili na Utalii | 478,659,185.80 | USD 903,862.40 |
| 47 | 92 | Tume ya kudhibiti Ukimwi | 80,278,917.00 | - |
| 48 | 93 | Idara ya Uhamiaji | 83,344,000.00 | USD 75,580 |
| 49 | 94 | Ofisi ya Rais – Tume ya Utumishi wa umma | 5,541,400 | - |
| 50 | 96 | Wizara Habari, Vijana na Utamaduni | 308,328,471.00 | - |
| 51 | 99 | Wizara ya maendeleo ya mifugo na Uvuvi | 3,572,628,565.99 | - |
| 52 | 034-2001 | Ubalozi wa Tanzania - Addis Ababa | 38,989,755.00 | - |
| 53 | 034-2002 | Ubalozi wa Tanzania - Berlin | 2,379,829,593.66 | EURO 6,528 |
| 54 | 034-2003 | Ubalozi wa Tanzania - Cairo | - | EURO 158,185.49 |
| 55 | 034-2005 | Ubalozi wa Tanzania - Abuja | 1,289,501,459.90 | - |
| 56 | 034-2006 | Ubalozi wa Tanzania - London | 1,859,723,419.00 | PAUND 79,567.82 |
| 57 | 034-2007 | Ubalozi wa Tanzania - Lusaka | 116,742,480.21 | - |
| 58 | 034-2009 | Ubalozi wa Tanzania - Moscow | 447,226,310.95 | - |
| 59 | 034-2010 | Ubalozi wa Tanzania - New Delhi | 252,920,000.00 | - |
| 60 | 034-2013 | Ubalozi wa Tanzania - Paris | 1,686,112,998.13 | - |
| 61 | 034- | Ubalozi wa Tanzania - | | |

| Na | Fungu | | Shilingi | Fedha za kigeni |
|---|---|---|---|---|
| | 2014 | Beijing | 3,654,946,427.18 | - |
| 62 | 034-2015 | Ubalozi wa Tanzania - Rome | 1,944,381,641.80 | EURO 3,000 |
| 63 | 034-2016 | Ubalozi wa Tanzania - Stockholm | 1,217,893,521.00 | - |
| 64 | 034-2017 | Ubalozi wa Tanzania - Tokyo | 2,449,562,114.00 | - |
| 65 | 034-2018 | Ubalozi wa Tanzania - Washington | 298,438,338.74 | - |
| 66 | 034-2021 | Ubalozi wa Tanzania - Kampala | 95,183,992 | - |
| 67 | 034-2022 | Ubalozi wa Tanzania - Harare | 117,950,657 | - |
| 68 | 034-2023 | Ubalozi wa Tanzania - Nairobi | 1,560,528.00 | - |
| 69 | 034-2024 | Ubalozi wa Tanzania - Riyath | 97,722,020.00 | - |
| 70 | 034-2025 | Ubalozi wa Tanzania - Pretoria | 207,885,201.00 | - |
| 71 | 034-2027 | Ubalozi wa Tanzania - Abu dhabi | 210,310,084.28 | - |
| 72 | 034-2029 | Ubalozi wa Tanzania - Muscat | 787,100,717.95 | - |
| 73 | 034-2030 | Ubalozi wa Tanzania - Lilongwe | 716,669,070.00 | - |
| 74 | 034-2031 | Ubalozi wa Tanzania - Brasilia | 396,491,837.00 | - |
| 75 | 98 | Wizara ya Ujenzi | 29,402,371.00 | €54,254.00 |
| 76 | | Mamlaka ya Mapato Tanzania | 967,171,880,376 | USD 56,186,207 |
| | | | **1,237,636,636,278.90** | **USD57,662,248.38** |
| | | | | **£ 79,567.82** |
| | | | | **€ 221,967.49** |
| | | | | **JP¥ 17,089,499,858** |

**Kiambatisho 6: Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya taarifa ya jumla ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali**

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | **2006/2007** | | |
| 1 | **Mapungufu katika usimamizi wa dhamana za serikali**<br><br>Wizara inashauriwa kupitia Sheriana Kanuni kwa kufanyamarekebishokwenye sheria ya dhamana na Kanuni zake ili kuendana na hali ya sasa | | Marekebishoya sheria ya mikopoya Serikali,dhamana na ruzuku Na.3 ya mwaka 1974 (iliyorekebishwa 2004) na mapitio ya Mkakati wa Deni la Taifa(NDS) yanasubiriwa |
| 2 | **Fedha zilizotolewa kuagiza bidhaa nje yanchi ambazo hazijarudishwa Serikalini.**<br><br>Tunaendelea kusisitiza kwamba Wizara ifanye juhudi ikishirikiana na mkusanyaji wa madeni ya Serikali kusisitiza makusanyo ya kiasi kilichobaki cha JPY 16,699,499,858 na kuwasilisha maendeleo yaliyofikiwa kwa ajiri ya ukaguzi. | | Haijatekelezwa kikamilifu |
| | **2008/2009** | | |
| 3 | **Kutoandika kwa usahihi mikopo iliyotolewa na serikali kama dhamana** | Makubaliano hayo yaliofikiwa baina ya Serikali na Makampuni | unaendeleautekelezaji |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | Mlipaji Mkuu wa Serikali kuwasilishamakubaliano hayo yaliofikiwa baina ya Serikali ya Tanzania na Makampuni hayo ya maua, ratiba ulipaji mikopo pamoja na vielelezo vingine vinavyoonyesha kuanza kulipwa kwa mkopo. | hayo ya maua pamoja na vielelezo vingine vya msingi viwasilishwe ofisi ya ukaguzi kwa ajili ya uhakiki. | |
| | **2010/2011** | | |
| 4 | **Madeni na Mihadi**<br><br>Mamlaka ya mapato Tanzania inatakiwa kuongeza ukusanyaji wa mapato na Hazina kuhakikisha kuwa fedha zinatolewa kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji washughuli zilizopangwa kwenye bajeti | • Serikali itaongeza juhudi ili kuboresha mikakati ya ukusanyaji wa mapato kuwezesha utekelezaji washughuli zilizopangwa,kupitia, Mwendelezo wakurasimishasekta isiyo rasmiilikuingizakatikawigo wa kodi.<br><br>• Taasisi za Umma, Wakala za Serikali naMamlakaambazohukusanya mapatoyasiyo yakodi kupeleka mapato yote iliyokusanya kupitia mpango wa mabakizo | Hoja ipo kwenye utekelezaji.<br><br>Ufuatiliaji utafanyika juu ya utekeleza wa menejimenti |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | | (retention schemes) kwenye Mfuko Mkuu waSerikali. Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa, Manispaa, Halmashauri ya Jiji,Wakala na Mamlaka ambazo zinakusanya ada na ushuru zimeamuliwa kuanzisha mashine za EFD ili kupunguza upotevu wa mapato.Wakala wa Serikali ulioanzishwa chini ya sheria ya Wakala wa Serikali, shirika la umma lililoanzishwa chini yaSheria yaMashirika ya Umma, mamlaka ya ummaau taasisi ya umma itawasilisha bajeti ya mapato na matumizi kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uchunguzina kibali. | |
| 5 | **Mali zisizoingizwa katika daftari la kudumu la mali**<br><br>Mlipaji Mkuu wa Serikali anatakiwa kuonyesha hatua (ratiba) za utekelezaji wa ushauri huu. Daftari la mali za kudumu linatakiwa kuwa tayari kabla ya mwaka 2016/2017 ambapo | Programu ya usimamizi wa mali (Assets Management (Tracking Software - SAGE) imewekwa kama chombo cha kuthibitisha na uboreshaji. Mafunzo kwa ajili yahiyo yamefanyika na uboreshaji wa daftari la kudumu la mali | Ninamshauri Mlipaji Mkuu wa Serikali kuongeza kasi ya kuaandaa daftari la kudumu la mali na kuhakikisha kwamba daftari litakuwa tayari limekamilika kabla ya |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | serikali itakuwa inatumia viwango vya kufunga Hesabu vya kimataifa (IPSAS) | utaanza mwaka 2014/2015 | 2016/2017 ambapo viwango vya kufunga Hesabu vya kimataifa (IPSAS) vitakuwa vinatumika kwa ukamilifu (baada ya kuisha kipindi cha mpito) |
| | **2011/2012** | | |
| 6 | **Deni la Shirika la ndege (ATCL)**<br><br>• Ninapendekeza hatua za kinidhamu kuchukuliwa dhidi ya waliohusika katika kuiingiza serikali katika biashara zisozaa matunda ambazo zimesababisha serikali kudaiwa limbikizo la deni la dola za Marekani 41,466,177.16 kuanzia 26/10/2012; na<br><br>• Kuanzia tarehe 26/10/2012 deni limekuwa likiongezeka mpaka kufikia dola za Marekani41,466,177.16 kutoka dola 39,000,000 Serikali inapaswakujadili hilideni na kampuni ya Wallis kama kuna uwezekano wa kulifuta kwa vigezo kwamba serikali | | uchunguzi unafanywa na Taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa (TAKUKURU) |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | haikufaidika na biashara hiyo. | | |
| 7 | **Malipo ya matibabu nje ya nchi yasio na nyaraka za viambatanisho kiasi cha Sh. 448,144,343**<br><br>Afisa Masuuli katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii<br>anatakiwa kuboresha udhibiti wa ndani katika matumizi ya wizara na kuhakikisha kwamba nyaraka zote zilizotakiwa zinazohusiana na matibabu ya nje zinawasilishwa kwa ukaguzi. | | Hoja ipo kwenye utekelezaji. |
| | **2012/2013** | | |
| 8 | **Usimamizi wa manunuzi**<br>Ukaguzi ulibaini mapungufu yanayojirudia katikashughuliza manunuzi.Hivyoninapendekeza:<br><br>• Serikali kupitiaMamlaka ya udhibiti wa manunuzi ya umma(PPRA)<br>kuendesha semina kadhaakwa lengo la kujengauwezo kwaenye kitengo cha manunuzi, Bodi ya Zabuni, Maafisa Masuuli na Idarambalimbali juu ya umuhimu wa | | Hoja ipo kwenye utekelezaji.<br>Hii ni ya muda mrefu ikiwashirikisha wadau wote. |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | kutekeleza Sheria ya Manunuzina kanuni zake<br>• Pia ni muhimu kuwa na mfumo wa usimamizi wa taarifa za manunuzi katika kufanikisha shughuli za manunuzi. Mfumo huu unasimamiwa na Mamlaka ya udhibiti wa manunuzi ya umma. Mamlaka hii inatakiwa kuhakikisha kwamba mfumo huu ni rafiki kwa watumiaji wa mwisho ili kwamba Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa watumie mfumo huu kwa urahisi katika kuboresha shughuli za manunuzi. | | |
| 9 | **Kutofanyiwa kazi kwa changamoto ya upungufu wa Wafanyakazi nguvukazi katika Wizara na Sekretarieti za Mikoa**<br><br>Ukaguzi ulibaini upungufu mkubwa wa wafanyakazi ikilinganishwa na ikama ya watumishi katika taasisi.Kwa hiyo ninapendekeza:<br>• Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO- PSM) ipitie upya ikama za Wizara, Idara za Serikali na Tawala za Mikoa na kuja na mapendekezo halisi ya idadi ya watumishi wanaohitajika. | | Haijatekelezwa kikamilifu |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | • Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara za Serikali na Tawala za Mikoa wanapaswa kuhakikisha kwamba wana idadi yakutosha ya watumishi wenye sifa stahiki. Uhaba wa watumishi unapaswa kutolewa taarifa kwa mamlaka husika ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO- PSM). | | |
| 10 | **Malipo ya mishahara kwa watumishi hewa**<br><br>Baada ya kubaini uwepo wa mishahara iliyolipwa kwa watumishi hewa ,napendekeza kwa serikali kwamba:<br>• Ili kuepuka upotevu kama huu katika siku zijazo, Maafisa Masuuli katika Wizara,Idara na Mikoa husika wanapaswa kuangalia taarifa za mishahara ya watumishi wao mara kwa mara na kuthibitisha uhalali wa watumishi wote kabla ya malipo. Mawasiliano pia lazima kuimarishwa ili kuhakikisha kwamba majina ya wastaafu, watoro/walioacha kazi au walioachishwa kazi yanafutwa katika taarifa za wafanyakazi mara moja.<br>• Mbali na hayo, Maafisa Masuuli | | Serikali inafanya juhudi za kuwaondoa kwa wakati katika taarifa za mishahara watumishi waliositisha ajira mara ajira inapositishwa.<br><br>Ninaamini kwamba mapungufu yatakoma katika kipindi kifupi kijacho. |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | wanatakiwa kuhakikisha mishahara isiyolipwa kwa watumishi ambao muda wao wa utumishi umekoma kwa sababu moja au nyingine inarudishwa Hazina kwa wakati kulingana na maagizo.<br>• Zaidi ya hayo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuhakikisha kuwa Mfumo wa kutunza taarifa za watumishi (HCMIS-LAWSON) unafanya kazi na unatumika kikamilifu ili kupata thamani ya fedha tarajiwa. | | |
| 11 | **Usimamizi wa Matumizi**<br>Baada yakubaini mapungufu mbalimbali katika<br>usimamizi wa matumizi ya fedha za umma, ninapendekeza kwamba:<br><br>Maafisa Masuuli wa Wizara/Idara, Mikoa na Balozi wanapaswa kuhakiki malipo yote na kuyathibitisha kuwa halali na yana nyaraka sahihi kama matakwa ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001, Kanuni ya 95 (4) inavyosema. Uangalizi wa ndani unahitaji kuboreshwa ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa awali wa ndani | | Haijatekelezwa kikamilifu |
| 12 | **Utendaji katika Balozi**<br>Mapungufu mbalimbali yalionekana katika | | Haijatekelezwa kikamilifu |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | shughuli za balozi nje ya nchi. Kwa hivyo ninapendekeza kwamba:<br><br>• Balozi husika zikishirikiana na Wizara ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa Kimataifa (MFAIC) zinatakiwa kusitisha malipo ya posho kwa maafisa wastaafu na kufanya utaratibu wa kuwarudisha nyumbani haraka pindi utumishi wao unapokoma. Napendekeza mamlaka husika kuangalia ni jinsi gani zitakavyoweza kurudisha fedha zilizolipwa maafisa wasiostahili wa Balozi.<br>• Menejimenti ya Balozi iwasiliane na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa ajili ya kuwarejesha majumbani watumishi waliomaliza utumishi wao ambao bado wanaendelea kuishi ubalozini na wale ambao wamekaa kituo kimoja muda mrefu wabadilishwe. Hii itakuwa ni chachu katika utoaji wa huduma kwa balozi zetu.<br>• Menejimenti ya Wizara ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa Kimataifa ione uwezekano wa kuanzisha mfuko katika bajeti yake kwa ajili ya kufanya shughuli | | |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | za diplomasia ya kiuchumi na kukuza vivutio vya utalii, kwa kuzingatia kwamba hii ni kazi muhimu kwa uchumi wa nchi. | | |
| 13 | **Uendeshaji wa Hospitali Teule na Hospitali za Rufaa**<br>Wakati wa ukaguzi maalum, nilibaini mapungufu kadhaa za kiutendaji katika hospitali teule na rufaa, kwa hivyo ninapendekeza kwamba:<br>• Wizara ya Afya inapaswa kuhakikisha kuwa fedha zote zinapohamishwa kwenda hospitali mbalimbali zinaambatana na mchanganuo wa matumizi yake badala ya utaratibu wa sasa usioainisha malengo ya fedha hizo kama ilivyodhihirika wakati wa ukaguzi.<br>• Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Hazina ni muhimu waboreshe mawasiliano na menejimenti za Hospitali husika kuhakikisha kuwa watumishi hewa wanafutwa kwa wakati katika mfumo wa ajira serikalini<br>• Nasisitiza Hospitali teule kuzingatia | Wizara imewasiliana na hospitali zote teule nchini kwa barua yenye kumbukumbu Na. HC.209/320/01 ya tarehe 30 Octoba, 2013 na kuwataka kurejesha Wizara ya fedha mishahara yote haikustaili kulipwa. | Natambua hatua ambazo Serikali imezichukua juu ya suala hili. Uhakiki wa Serikali katika suala hili unaendelea. |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | makubaliano ya mkataba kati yao na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii<br>• Ninapendekeza Wizara ya Afya kwa kushirikiana na menejimenti za Hospitali husika kuhakikisha ya kwamba, wanafungua akaunti ya benki inayojitegemea mahususi kwa ajili ya fedha za ruzuku za Serikali badala ya hali ya sasa ya kuchanganya fedha hizi za Serikali na fedha za matumizi mengine ya hospitali. Aidha, Menejimenti za hospitali zinapaswa kuwajibika kutoa taarifa za mara kwa mara za matumizi ya fedha hizo kwa Wizara husika. | | |
| 14 | **Vocha za Pembejeo za Kilimo (NAIVS)**<br>Kufuatia changamoto nilizozibaini wakati wa ukaguzi, ninapendekeza uboreshaji wa mpango huu wa NAIVS katika maeneo yafuatayo;<br>• KuwashirikishaMaafisauganiwakilimo,mawakalawaMbegunaTaasisizautafitiwaKilimokupitiaupyanakutathminiainazambegunamboleazinazosambazwanchini,piakudhibitimbegu na mbolea bandia | | Suala hili liko katika Utekelezaji |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | • Kuhakikishakwambaununuzinausambazajiwavochaunafanyikakwawakatimuafaka. Utafitiwakutoshawaainazaudongounafanyikakwanzakablayautoajiwahatizamboleailikuhakikishapembejeozinazotolewazinaendana na aina yaudongo wa mahalihusika.<br>• Kubunimwongozokazirahisiwanamnayautekelezajiwampangohuu(ukiwakatikalughayaKiswahili)ukianishavizurinakuelezeanamnanzuriyautunzajiwanyaraka,nautoajiwataarifazamarakwamarazilizofanyiwausuluhishi(reconciliation)nataarifanyinginembalimbali.Wakulima wakumbushwe nawapewetaarifazakutoshajinsi mfumowa vocha unavyofanyakazinafaidazakekatikakuhimizamatumiziyambeguboranambolea. | | |
| 15 | **Ununuzi wa Kivuko cha Misungwi**<br>Mapungufu kadhaa yalibainika katika maalum wa ununuzi wa kivuko cha Misungwi;Napendekeza<br><br>Hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya maafisa wa umma walioshindwa kusimamia utekelezaji wa | • Hatua zimeshachuliwa dhidi ya maafisa wa umma ambao walishindwa kusimamia utekelezaji wa mkataba wa ununuzi wa kivuko cha Misungwi,<br>• Wizara ya Ujenzi kupitia | Natambua hatua ambazo Serikali imezichukua katika kushughulikia suala hili. Ufuatiliaji katika suala hili unaendelea. |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | mkataba wa ununuzi kivuko cha Misungwi na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya mzabuni M/S Sinnautic international ambaye alishindwa kutekeleza kazi zote za kuleta vipuri vya thamani ya Euro 41,140 zakivuko cha Misungwi kwa mujibu wa mkataba. | barua yake yenye kumbukumbu namba AB 13/179/07/42 ya tarehe 16 Mei, 2014,<br>• The Ministry of Works, via a letter with Ref. AB 13/179/07/42 of 16th May 2014, ilitoa taarifa kwa mkandarasi, M.S Sinnautic International, ikimwagiza ailipe Wizara, kiasi cha Euro 41,140 ikiwa ni thamani ya vipuri na vifaa ambavyo havikuletwa katika mkataba wa ununuzi wa kivuko. Wizara ikishirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaangalia utaratibu wa kuchukua hatua zaidi za kisheria dhidi ya Mkandarasi | |
| 16 | **kituo cha mafunzo ya uuguzi Mkomaindo**<br>Kutokana na Ukaguzi maalum uliofanywa katika kituo cha mafunzo ya uuguzi Mkomaindo, nashahuri uongozi wa kituo kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani ikiwa | | Suala hili liko katika utekelezaji |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | ni pamoja na kuboresha utunzaji wa kumbukumbu. | | |
| 17 | **Utayari wa Serikali katika utekelezaji wa IPSAS yaani Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Taasisi za Umma**<br>• Kutengarasilimalifedhanawatuzakutosha katikakurahisishautendajiusiona vikwazowa zoezi hili,<br>• NinashauriSerikalikuzingatiakikamilifuIPS AS 25(MafaoyaWafanyakaziyanayofadhiliway otenamwajiri)inayohitajikufanyikatathmi niyauwezowamfukoilikubainikiwangocha denilawanalodaiwastaafulitakaoingizwak atikataarifazahesabuzamwaka,<br>• Kuanzishakamatiyakitaifayakuratibuutek elezajiwaIPSASambayoitashirikishawataa lamnawadaumbalimbaliambaowatakuwa wasimamiziwajukumuhilikwamiakamitan oilikuhakikishakilahatuainatekelezwakwa umakininakwawakati.Hadisasamwakamm oja umepita naimebaki miaka mine, | • Katika mwaka wa fedha 2014/2015 kamati ya kitaifa ya IPSAS itaanzishwa na itakuwa na jukumu ya kusimamia na kuimarisha utekelezaji wa mpango kazi wa IPSAS<br>• Kikosi kazi kitatumika kutenganisha thamani ya ardhi na majengo katika makundi mawili tofauti kama IPSAS inavyohitaji<br>• Kitengo cha kuendeleza mifumo (SDU) ya uhasibu na bajeti chini ya usimamizi wa mkandarasi mshauri wanafanya kazi ya kusanifu mfumo wa e-by Epicor ili kuwezesha mfumo kutengeneza na kutoa taarifa | Natambua hatua ambazo Serikali imezichukua katika kushughulikia suala hili. Uhakiki wa jibu Serikali utafanyika katika kaguzi zijazo |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | • MhakikimaliwaSerikalianapaswakufanyakazikwakaribunawadauilikuhakikishautekelezajiwampangowakuhamiaIPSASisiyotaslimuunazingatiaIPSAS17,piakufanyamabadilikomuhimukatikataarifazafedhayanayohusukutenganishaardhinamajengomakundimawilitofauti,<br>• SerikaliinashauriwakuanzishamchakatowakutengenezaripotiyafedhayamwakailiyounganishataarifazafedhazataasisizakezotezikiwemoSerikalizaMitaana vyombovinginevilivyochiniyake,<br>• KuuboreshamfumowaEPICORnawabajetiiliuwezekumudukutengenezaripotizamwakazinazokidhimatakwaya viwango vya uhasibu vya kimataifa visivyo vya taslimu,<br>• Mlipaji Mkuu wa Serikali ahakikishe Sheria ya Fedha ya Umma iliyorekebishwa inaanza kutumika,<br>• Serikali ihakikishe hati miliki za ardhi na majengo yanayomilikiwa na wizara, idara, wakara na sekretarieti za mikoa zinafuatiliwa mara moja ilikuwa na ushahidi wa umiliki wa mali hizo,<br>• Napendekeza kwamba menejimenti za | za fedha kadri IPSASs inavyohitaji<br>• Serikali inatarajia kujumuisha taarifa za fedha za Serikali za Mitaa katika mwaka wa fedha 2013/2014, na taasisi za serikali zinazofanya biashara (GBEs) na taasisi nyinginezo zitajumuishwa katika mwaka wa fedha 2014/2015,<br>• Zoezi la kuthaminisha majengo ya Serikali za Mitaa linasubiri Sheria ya Fedha za Umma(PFA) ifanyiwe marekebisho na kutoa mamlaka ya kisheria kwa Idara ya usimamiaji mali za serikali (GAMD) kusimamia mali za umma ikiwa ni pamoja na mali za serikali za mitaa ikiwemo kuzithaminisha mali hizo,<br>• Wizara ya Fedha ipo katika mchakato wa kuandaa juhudi za pamoja na Wizara ya | |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za mikoa kwa kushirikiana na Hazina ihakikishe kwamba modules zote za IFMS zinarekebishwa na zinatumika kikamilifu. Na pia mafunzo yafanyike pale inapohitajika haswa wakati kuna waajiriwa wapya na kunapokuwa na maboresho mapya katika mfumo wa kihasibu,<br>• Serikali itoe mafunzo jinsi ya kutumia EPICOR 9.05 na viwango vya uhasibu vya kimataifa visivyo vya taslimu,<br>• Kuanza kutumika kwa viwango vya uhasibu vya kimataifa visivyo vya taslimu kabla ya marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Umma Na. 6 ya 2001 (iliyolekebishwa 2004), hivyo Sheria ya Fedha ya Umma inakinzana na falsafa ya viwango vya uhasibu vya kimataifa visivyo vya taslimu | Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Ujenzi kupitia kitengo cha Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ili kuandaa hati miliki za majengo ya Wizara, Idara, Wakala, Balozi na Sekretarieti za Mikoa,<br>• Serikali ina nia ya kuhakikisha kuwa modules zote za IFMS zinafanya kazi kama inavyotakiwa,<br>• Kwa sasa Serikali inakamilisha marekebisho ya mfumo wa IFMS/EPICOR ili kukidhi mahitaji ya mfumo wakihasibu kwa misingi isiyokuwa ya fedha taslim.(Accrual basisi of Accounting) Pia ni lengo la Serikali kuhuisha *modules* zilizobakia kwenye mfumo kama vile *modules* za mali za kudumu na mali zilizobaaki mwisho wa mwaka | |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | | *(Inventory*),<br>• Mafunzo ya EPICOR 9.05 yameshafanyika kwa Wahasibu Wakuu, Wahasibu wa Mikoa, Wakuu wa Vitengo vya Hazina Ndogo, wafanyakazi wanaoingiza taarifa (Data Entries), na waandaaji wa taarifa za fedha wa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa. Hata hivyo mafunzo ni zoezi endelevu<br>• Mafunzo ya EPICOR 9.05 juu ya *module* ya kusimamia mali yanatarajiwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2014/2015,<br>• Serikali iliendelea kufanya mageuzi ya kifedha ambayo yalipelekea kupitiwa kwa Sheria ya Fedha ya Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) ili iweze kuondoa changamoto zilizopelekea kufanyika kwa mageuzi hayo | |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | | • Kwa sasa rasimu ya pili ya sheria mpya imetolewa kwa mamlaka ya juu kwa mapitio na mapendekezo. Hata hivyo, kifungu cha 38 kinazungumzia mabadiliko yaliyoletwa na viwango vya hesabu vya kimataifa katika misingi isiyo ya fedha taslim (IPSAS accrual),<br>• Serikali ilianza kutumia viwango vya uhasibu vya kimataifa visivyo vya taslimu *(IPSAS accrual)* kwa mara ya kwanza katika mwaka wa fedha 2012/2013, kwasasa bado ipo katika kipindi cha mpito,<br>• Serikali imeandaa mpango kazi wa miaka mitano wa kutekeleza IPSASs ambapo uthaminishaji wa mali na madeni ya serikali utafanyika. | |
| 18 | **Ufuatiliaji na tathmini ya miradi inayotekelezwa kwa fedha za mikopo** | | Haijatekelezwa |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | Kuna ongezeka la mikopo ya miradi ya maendeleo ambayo ni kipaumbele cha Taifa hivyo<br>Naishauri Serikali kuanzisha utaratibu maalum wa ufuatiliaji na kutathmini miradi ambayo imetekelezwa na inayotekelezwa kwa kutumia fedha za mikopo. Hali hii itasaidia kufanya tathmini ya matokeo ya miradi kadiri inavyoendelea.Hii itasaidia kupunguza hali ya sintofahamu kati ya wadau na serikali | | |
| 19 | **Kukosekana kwa Ofisi ya Usimamizi wa Madeni**<br><br>Haja ya kuanzisha ofisi ya Usimamizi wa Madeni ni moja ya suala muhimu ambalo nilizungumzia katika mwaka wa fedha 2010/2011. Nashauri Serikali kutilia mkazo uanzishwajiwa Ofisi ya Usimamizi wa Madeni (DMO) ili kuweza kukabiliana kimamilifu na kwa ufanisi kuratibu shughuli za usimamizi wa madeni. | • Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa taarifa Na. 494 ya tarehe17 Desemba2010. Rais aliunda Wizara ya Fedha ambayomiongoni mwa mambo mengineilipewa mamlaka ya kusimamia mikoponasera za mikopo nautekelezajiwake.<br>Wizara ya Fedha iliweza kuanzisha Idara ya usimamizi wa madeni. Idara itachukua kazi zote za usimamizi wa madeni yaliyotawanyika kutokawadau | uanzishwajina utendaji waidara yausimamizi wa madeni itafanyiwa tathminikatika ukaguziujao |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | | mbalimbali.Idaraitaanzishamfumo fanisi wa usimamizi wa madeninchini.Aidha,Idara itaunga mkono kwa ujumla juhudi katikakuimarisha utawalakwa kuboresha uwazi nauwajibikaji katika usimamizi waDeni la Umma.<br><br>• Tarehe 19 Mei, 2014Rais alipitisha mapendekezo ya kazi naMuundo waWizara ya FedhaambaoIdara ya Usimamizi wa Madeni imeanzishwana itakuwainashughulikia masuala ya Madeni ya Umma.Wakati huo huoKamatiya ushauri ya Wizara inafanya kazi bila kuchoka ili kuhakikisha kwamba shughuliiliyowekwachini ya mpangowa mageuzina kujenga uwezo | |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | | zinatekelezwa kwa wakati muafaka. | |
| 20 | **Kubadilisha Hati za Ukwasi(Liquidity Papers) kugharamia nakisi ya bajeti**<br><br>Nashauri Serikali kujiepusha na kubadili hati za ukwasi ili kuepuka uwezekano wa kuwa na deni kubwa siku za usoni lisilolipika. Iko haja ya Serikali kuchukua hatua za makusudi ikiwa ni pamoja na kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Serikali kupitia mamlaka ya mapato Tanzania (TRA), kupunguza matumizi, na makadirio ya bajeti yenye ufanisi. | | Haijatekelezwa |
| 21 | **Kutolewa migao ya fedha mwishoni mwa mwaka wa fedha**<br><br>Ili kukabiliana na changamoto ya fedha zilizoidhinishwa kutotolewa kwa wakati, Nashauri Serikali kutengeneza makisio yake ya mwaka yakishabihiana na makusanyo ya | Fedha zilizotolewa zinategemea ukusanyaji wa mapato kwa kuwa bajeti ya serikaliinafanya kazi chini yamisingi ya fedha taslimu, hivyo katika siku zijazoSerikali itahakikisha fedha zitakazotolewa zitaendana na bajeti | Utekelezaji wamapendekezo yangu utahakikiwakatika ukaguziijayo. |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | mapato ili kuzuia kutolewa kwa kiasi kikubwa cha fedha mwishoni mwa mwaka wa fedha. Kwa kufanya hivyo, inatarajiwa kwamba shughuli zilizopangwa zitatekelezwa kama mpango kazi ulivyo | namakusanyo ya mapato. | |
| 22 | **Usimamizi wa Forodha na maghala ya mali (customs bonded warehouses) ambazo hazijalipiwa kodi**<br><br>Nilibaini mapungufu mbalimbali katika usimamizi wa forodha na maghala ya mali.<br><br>Hivyo, ninaishauri Serikali kuhakikisha udhibiti wa kutosha kwenye uendeshaji wa maghala ya ushuru wa Forodha ili kukusanya madeni yote yatokanayo na kutokusanywa kwa ushuru wa forodha. Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania inapewa wito wa kuzingatia na kutekeleza sheria zilizopo. | | Haijatekelezwa kikamilifu |
| 23 | **Tathmini ya Wakala wa Serikali**<br><br>Ukaguzi ulibaini mapungufu mbalimbali katika shughuli za Wakala wa Serikali. Hivyo ninapendekeza kwamba: | | Haijatekelezwa kikamilifu |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | • Wakala zote za serikali ambazo zimeanzishwa kwa lengo la kutoa huduma kwa umma na wanapata mapato kulitokana na huduma wanazotoa, niwakati muafaka kwao kushindana katikaulimwenguwa kibiashara kwa kuwawabunifu zaidi nakuongeza uborana kiwango cha huduma. Hii itaboresha makusanyo yao na kupunguza utegemezi kutokaserikali kuu katika suala la fedha.<br>• Wakala ambazo zimeanzishwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa idadi kubwa ya wateja inapaswa kuzingatia faida ya kuwa na wateja wengi kama msingi wa kuongeza makusanyo yao.<br>• Ili kutoa huduma bora ni muhimu kuwa na wafanyakazi wenye taaluma na vifaa vya kufanyia kazi. Wizara mama ikishirikiana na Tumeya Utumishi wa Umma zihakikishe wakala zao zina zinajitosheleza kwa wafanyakazi wenye uwezo na vifaa nyenzo muhimu za kufanyia kazi ambazo zitasaidia kuongeza kiwango cha huduma nakuboresha utoaji | | |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | wa hudumazaokwa umma<br>• Kutokana hali ya sasa ya serikali ya upungufu wa fedha serikali ni lazima kuacha kuunda wakala nyingine mpaka hapo hali ya kifedha itakapoboreshwa. | | |
| 24 | **10.2 Ulipaji wa kodi ya kupanga ofisi Sh. 7,895,872,337**<br>Kuna umuhimu wa Serikali kuwekeza katika ujenzi wa majengo yake yenyewe. Ninaishauri Serikali kuwa na mpango endelevu wa kujenga majengo kwa ajili ya ofisi za Serikali. Serikali inaweza kufanya yafuatayo ili kufanikisha jambo hili.<br>• Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi kwa kushirikiana na Wakala wa majengo ya Tanzania (TBA) watafute maeneo ambayo Serikali inaweza kujenga ofisi za wizara, idara na wakala wake.<br>• Serikali ifanye majadiliano na Mifuko ya hifadhi ya Jamii ili waweze kupata mkopo kwa ajili ya kugharamia miradi yaujenzi wa majengo ya Serikali.<br>• Serikali pia ifanye mazungumzo na washirika wa maendeleo kama vile Benki | • Serikali kupitia wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya makazi na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu imeanza kugawa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya serikali mjini Dodoma,<br>• Serikali kupitia Wizara ya Fedha itaanzisha mazungumzo na taasisi za fedha na mifuko ya ustawi wa jamii ili iweze kutoa mikopo kwaajili ya ujenzi wa majengo ya serikali,<br>• Serikali itaendelea kununua majengo na viwanja kwaajili ya ujenzi wa majengo ya balozi zetu nje ya nchi. Majengo ambayo yameshanunuliwa ni pamoja | Natambua juhudi ambazo serikali imezichukua katika kushughulikia suala hili. Nitafuatilia kwa karibu utekelezaji wa mapendekezo yangu. |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | ya Maendeleo ya Africa (AfDB) na Benki ya Dunia ili waweze kupata mikopo/misaada kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa Ofisi hizo.<br>• Kwa zile wizara, idara na wakala za Serikali ambazo zinakusanya mapato kutokana na shughuli zao, nashauri watumie mapato ya ndani ya wizara kuanza kujenga ofisi zao binafsi. | na jengo lililonunuliwa Amerika na viwanja vilivyonunuliwa Kenya, Saudi Arabia na Qatar. | |
| 25 | **Changamoto zinazokabili huduma ya magereza Tanzania**<br>Kutokana na changamoto inayoikabili idara ya huduma ya magereza ya Tanzania ninapendekeza yafuatayo kwa Serikali na kwa idara ya huduma ya Magereza yenyewe.<br>• Mahakama ya Tanzania iharakishe kutoa maamuzi juu ya kesi zilizopo. Kuna idadi kubwa ya mahabusu katika magereza ambao wanasubiri kesi zao kusikilizwa na haki kutolewa na mahakama. Kwa kukamilisha kesi zinazowakabili mahabusu kutasaidia kupunguza idadi ya mahabusu katika magereza,<br>• Serikali inaweza kuchagua kutumia njia nyingine ya kuwaadhibu wafungwa baada ya kupatikana na hatia. Serikali inaweza | | Pendekezo bado halijatekelezwa |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | kuchagua kutumia njia mbadala kama wafungwa kutumikia kifungo cha nje cha kuanzia mwaka mmoja mpaka miwili chini ya uangalizi wa mkuu wa wilaya au mkoa huku akijushughulisha na shughuli za jamii kama usafi maofisini bila malipo (extra Mural labour), kifungo cha nje chini ya uangalizi cha miaka minne na kuendelea kutokana na makosa madogo madogo kwa wafungwa ambao tayari wametumikia theluthi moja(1/3) ya kifungo chao gerezani huku wakishughulika na huduma za jamii bila malipo(Parole). Hii kwa kiasi kikubwa itapunguza idadi ya mahabusu na wafungwa katika magereza,<br>• Kwa ajili ya wahalifu wadogo na wanaokiuka sheria ni bora kulipa faini na kama wao wakishindwa kulipa faini, wanapaswa kupelekwa kwa uongozi wa miji yao, au wilaya na kupewa kazi za jamii (communal based labour),<br>• Kuwahudumia mahabusu na wafungwa kunasababisha gharama kubwa kwa Serikali. Kuwalisha, kuwapa mavazi na matibabu ni ghali. Uongozi wa idara ya | | |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | huduma ya magereza unashauriwa kuboresha shughuli zao za uzalishaji kama useremala, shughuli za kilimo, ushonaji, ujenzi wa nyumba na mafundi mitambo na magari. Baada ya hapo watafute soko la bidhaa zao na hii itawawezesha kuwa na uwezo wa kujilisha na kujinunulia mavazi wenyewe,<br>• Idara ya huduma ya Magereza inahamasishwa kuandika juu ya mapendekezo kadhaa ya maendeleo na kutafuta wahisani mbalimbali kama Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), nk ambayo watatoa fedha kwa ajiri ya kupanua na kuboresha magereza,<br>• Uongozi wa idara ya huduma ya magereza unashauriwa kutoa wito kwa wajumbe wa kamati ya bunge ya Serikali kuu (PAC) na viongozi wengine wa Serikali kutembelea magereza na kuona hali halisi katika magereza. Hii itawasaidia kufanya maamuzi sahihi juu ya mgao wa rasilimali. | | |
| 26 | **Miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP)** | • Tunakubaliana na mapendekezo ya ukaguzi. Na | Nitafuatilia hatua zitakazochukuliwa na |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | Pamoja na faida ambayo inaweza kupatikana kutokana na mipango ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi, kuna baadhi ya hatari zinazohusiana na ubia ambayo ni muhimu zaidi kwa Serikali kuingilia kati. Ubia unaweza kuongeza gharama za uendeshaji, kutoa huduma chini ya kiwango, madhara katika maslahi ya umma, na kuanzisha fursa mpya kwa udanganyifu, kula njama, na rushwa.Ili kukabiliana na hatari hizi, napendekeza;<br>• Serikali inapaswa kubuni kupitia mchakato wa manunuzi na tathmini ambao utapima utegemezi na uadilifu wa washirika wenye uwezo.Tathmini hiyo inapaswa kuzingatia uchaguzi wa mshirika mwenye rekodi zilizothibitishwa katika maendeleo ya mradi kwa njia ya mchakato wa ushindani wa zabuni,<br>• Kwa kutambua umuhimu wa upembuzi yakinifu ili maslahi kwa pande zote mbili yaweze kutumika na mafanikio kupatikana, Serikali inapaswa kuunda Mfuko wa fedha za uwezeshaji wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) ili kuwezesha upembuzi yakinifu juu ya | tunatoa maelezo yafuatayo kuonyesha namna mbili tunazotumia tunazuia viatarishi vilivyopo kwenye miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP):<br>1) Mchakato wa kutathmini endapo upembuzi yakinifu ulifanyika na masuala ya kiufundi, kisheria, kiuchumi, kimazingira, kibiashara na kifedha yamezingatiwa na<br>2) Kuangalia kama mchakato wa kutoa idhini ulizingatia awamu zote za mzunguko wa PPP. Ikiwa ni pamoja na upembuzi yakinifu unaofanywa na Wizara ya fedha, kuidhinishwa kwa ombi la kupendekezo PPP, kuidhinisha muundo wa kifedha wa PPP na mkataba wa PPP | Serikali katika kutekeleza pendekezo hili. |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | miradi muhimu ya utekelezaji. Pamoja na hayo, Serikali inahimizwa kuzindua juhudi kamili za uhamasishaji ili kushirikisha kikamilifu sekta binafsi katika miradi ya taifa yenye vipaumbele vinavyotambulika. Kuendelea kukosekana kwa fedha katika kufanya utafiti wa upembuzi yakinifu kunaweza kusababisha jambo lenye gharama kubwa sana,<br>• Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa masuala ya kugawana faida (ikiwa ni pamoja na uwezekano wa faida kwa siku zijazo kutokana na mauzo ya mali au uwekezaji) yanawekwa wazi katika makubaliano ya ushirikiano. Ni lazima pia kuhakikisha kwamba maslahi ya nchi yanalindwa wakati mali zilizochangiwa zinaondolewa katika ushirikiano (kwa mfano kuhakikisha Serikali inapata sehemu ya mapato). Serikali pia inapaswa kuwa na uwezo wa kuthibitisha jumla ya gharama zilizoingizwa katika mradi ambayo zinatarajiwa kurudi wakati wa uhai wa mradi huo,<br>• Naishauri Serikali kwamba inapaswa | Na mbinu hizo zimeshatumika katika utekelezaji wa miradi mipya ya PPP<br>• Masuala ya kugawana na faida ni jambo moja muhimu katika PPP hasa katika ubia. kwa miradi iliyotekelezwa baada ya kutungwa kwa sheria ya PPP mwaka 2010, mikataba imeeleza wazi namna ya kugawana faida na hasara katika ubia | |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | kufikiria kama mali zenye umuhimu wa kitaifa zinaweza kukodishwa kwa sekta binafsi badala ya kuhamishwa kabisa. Makubaliano ya ushirikiano wana namna hii yanaweza kutoa fursa kwa sekta ya umma kuingilia kati katika tukio kubwa la kushindwa katika utoaji wa huduma au kufilisika kwa mbia,<br>• Serikali inapaswa kutathmini kama gharama zote na ya kushiriki ni halali. Uchambuzi makinini lazima ulenge kushughulikia mgao sahihi wa athari zinazoweza kutokea katika mradi huo kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kuhusiana na mradi huo.Katika mipangilio yote ya ubia (PPP), chombo cha umma kinapaswa kuangalia athari zinazoweza kutokea na kuhakikisha kwamba zinaweza kudhibitiwa ipasavyo,<br>• Serikali inapaswa kuwa makini katika ubunifu wa mkataba na majadiliano ili kuhakikisha kwamba athari yoyote kutokana na matukio yasiyoonekana inagawanywa kati ya pande zote mbili na kwa mujibu wa viwango vya athari hiyo | | |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | kulingana na makubaliano,<br>• Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa makubaliano yanaruhusu habari ya utendaji kuwa zinatolewa, kulingana na mahitaji, kwa mbia wa sekta ya umma. Wakati Serikali inakuwa kama taasisi ya kutoa mkopo au mdhamini ni lazima kuomba taarifa za ziada kutoka kwenye upande inayoshirikiana nayo ili kuhakikisha usalama wa mkopo wake,<br>• Katika uchambuzi wa vihatarishi kabla ya kuingia katika ushirikiano, Serikali inapaswa kufikiria kwa makini na kuweka vifungu kwenye masharti ya mkataba (mfano kifungu kinachohusu uwezo wa kujitoa inapotokea utendaji mbovu bila upotevu wa fedha kama fidia) au kifungu kinachoruhusu kuwepo kwa mipango ya dharura (mfano kuuza hisa),<br>• Serikali inapaswa kulinganisha malipo ya mikataba na mafanikio ambayo yalikubalika kufikiwa na kiwango chahuduma zinazotolewa. | | |
| 27 | **Sheria ya Miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi haimpi Mdhibiti na Mkaguzi** | | Pendekezo bado halijatekelezwa |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | **Mkuu wa Serikali uwezo wa taarifa za miradi hiyo**<br>• Sheria inapaswa kuhakikisha kuwa mkataba wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) na makubalianao ya kushirikiana katika uzalishaji(PSAs) yanamwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupata rekodi za fedha na taarifa nyingine za mbia binafsi au kampuni iliyo katika mpango wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP),<br>• Pamoja na hayo, Serikali inapaswa kusaidia na kumpatia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu taarifa zote muhimu za mkataba wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) katika maisha yote ya mradi tokea mchakato wa zabuni, kupewa rasmi mkataba na awamu ya uendeshaji wa mradi. Mwongozo Na. 3 wa Viwango vya Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs) 5220 inasema kwamba, kuchunguza mradi na Taasisi kuu ya Ukaguzi (SAI) katika hatua zote za mradi inafaida zake endapo udhaifu wowote ukigundulika unaweza kurekebishwa kabla | | |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
| --- | --- | --- | --- |
| | ya mkataba haujasainiwa na matatizo mabaya zaidi kuepukwa katika hatua ya baadaye,<br>• Serikali pia inapaswa kutoa taarifa mara kwa mara juu ya utendaji wa mradi kuonyesha wazi wazi kama mbia binafsi anatekeleza majukumu yake kwa mbia wa sekta ya umma ili hatari yoyote ya hasara itambulike mapema iwezekanavyo, kuwezesha Serikali/mbia wa sekta ya umma kufikiria namna bora ya kulinda maslahi yake. | | |
| 28 | **Ukaguzi wa hesabu za Vyama vya Siasa**<br>Kutokana na changamoto zilizojitokeza wakati wa ukaguzi wa vyama vya siasa napendekeza;<br>• Ili kuboresha utoaji wa taarifa, uwasilishwaji na ulinganifu wa utendaji wa vyama vya siasa, vyama vinatakiwa kuandaa taarifa za hesabu kwa mujibu wa viwango vya uhasibu vya kimataifa. Kuanza kutumika kwa mfumo mmoja wa taarifa za kihasibu utasababisha kufanana kwa taarifa za hesabu za vyama vya siasa. Hii inawezekana pale ambapo Msajili wa vyama vya siasa akishirikiana na Mhasibu | | Pendekezo bado halijatekelezwa |

| Na. | Mapendekezo ya ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) | Maoni ya Ukaguzi juu ya majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) |
|---|---|---|---|
| | Mkuu wakitoa mwongozo wa aina ya muundo wa taarifa za fedha utakaotumiwa na vyama vya siasa,<br>• Napendekeza Serikali irekebishe sheria ya vyama vya siasa Na. 5 ya mwaka 1992 ili kutatua changamoto zilizopo. | | |

**Kiambatisho 7: Utekelezaji wa mapendekezo ya kamata ya kudumu ya bunge ya hesabu za serikali**

| Na | Mapendekezo ya Kamati(PAC) | Majibu ya Serikali | Maoni ya ukaguzi |
|---|---|---|---|
| **2011/2012** | | | |
| 1 | **Usimamizi wa kesi za madai ya kodi zilizopo mahakamani**<br>• Hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya wafanyakazi waliosababisha kesi hizo<br>• Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ifanye kazi kwa uadilifu na umakini katika kuitetea serikali ili iweze kushinda kesi | | itafuatilia uamuzi wa mahakama katika kesi zilizosalia |
| 2 | **Mkatabawenyeutata wakutengenezaLeseni zaudereva Tanzania**<br>• Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato ihakikishe inapitia upya mkataba huo na vipengele vyenye mapungufu virekebishwe,<br>• Vilevile, TRA naJeshi la Polisiwahakikishemfumo waleseniza uderevaunatumika kwa asilimia 100 ili kuongeza mapato ya Serikali,<br>• Mdhibiti naMkaguziMkuuwaHesabuzaSerikalikufanyaukaguzimaalumwalesenihizina kuwasilishaTaarifa yakekwenyeKamati,<br>• Aidha, Kamatiinapendekezakuwa mikatabaambayoitahusishautoaji wamisamahayakodiiweinapitiwanaMwanasheriaMkuuwaSerikalikablayakusainiwa. | | Ripoti ya ukaguzi maalum inayohusu leseni za udereve imeshatolewa |
| 3 | **Kutotolewa fedha za kutosha kwa Wakala wa umeme vijijini (REA)**<br>Kamati ya kudumu ya bunge ya hesabu za serikali katika mwaka wa fedha 2014/2015 imependekeza kuwa serikali inapaswa kutoa fedha kwa Wakala wa umeme vijijini (REA) kutoka vyanzo vyake yenyewe ili kuwezesha upelekwaji wa umeme vijijini | | Ufuatiliaji wa swala hili utafanyika katika ukaguzi wa mwaka |

| Na | Mapendekezo ya Kamati(PAC) | Majibu ya Serikali | Maoni ya ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | | | 2014/2015 |
| | **Ulipaji usioridhisha wa deni ambalo Serikali inadaiwa na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF)**<br>• Serikali iendelee kutenga fedha na kulipa kila mwaka TZS. 71 bilioni kwenda PSPF ili kuwezesha mfuko huo kuendelea **kutoa pensheni** kwa wastaafu bila vikwazo;<br>• PSPF ihakikishe inafanya uwekezaji na kutoa mikopo kwa Taasisi mbalimbali kwa kuzingatia uwezo wake wa kifedha ili isiendelee kuingia katika hatari ya mfuko kushindwa kujiendesha na kuathiri watumishi na wastaafu mbalimbali;<br>• Mamlaka ya Usimamizina Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) iwe makini katika kusimamia kiwango cha Uwekezaji na mikopo inayotolewa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kiwe kinalingana na uwezo wa Mifuko hiyo husussan kutoathiri uwezo wa mifuko hiyo kulipa pensheni za wastaafu. | | Hadi sasa Serikali imeshalipa TZS bilioni 50 kwa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF) katika mwaka wa fedha 2013/2014<br><br>Serikali ihakikishe inalipa kiasi kilichosalia |
| 5 | **Bajeti finyu na ucheleweshaji wa kutuma fedha balozini**<br>• Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya nje na Uhusiano wa Kimataifa inatakiwa kuhakikisha kuwa Mashine zote za kutolea Stika za VIZA zinafanya kazi na zinafanyiwa matengenezokila mara,<br>• Wizara hii pia inatakiwakuhakikisha kuwa Mfumo wa udhibiti matumizi ya fedha (IFMS-EPICOR) unafanya kazi kwa ufanisi wake ili kuepuka kuingia hasara,<br>• Pia Wizara hii kwa kushirikiana na wizara ya Fedha kwa pamoja zinashauriwa kuangalia ni jinsi gani wanaweza kupunguza gharama ya kuendesha Mfumo wa kuthibiti matumizi ya fedha (IFMS) katika balozi zetu. | | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ameshatoa ripoti inayohusu matatizo yanayokabili balozi za Tanzania |

| Na | Mapendekezo ya Kamati(PAC) | Majibu ya Serikali | Maoni ya ukaguzi |
|---|---|---|---|
| 6 | **Mwenendo wa makusanyo ya maduhuli yanayofanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**<br>• Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ihakikishe inaimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani wa ukusanyaji wa maduhuli,<br>• Kwa lengo la kuongeza ukusanyaji wa maduhuli, Wizara pamoja na kuwa na mfumo wa Land Rent Management System (LRMS), ianze kutumia mfumo wa kieletroniki (EFD), katika kukusanya maduhuli ya Serikali,<br>• Mfumo huo wakieletronikiuambatane nanamba ya utambulisho wamlipakodi(TIN)ilikujua takwimusahihi za walipakodi pamoja nakupunguzamigogoro yaugawaji waardhi.<br>• Wizara itafute utaratibu maalum utakao hakikisha kuwa kodi ambazo hazijalipwa katika viwanja mbalimbali zinalipwa mapema iwezekanavyo. | | Mapendekezo ya kamati hayatekelezwa kikamilifu |
| **2012/2013** | | | |
| 7 | **Misamaha ya Kodi**<br>• Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuanzisha kitengo cha kusimamia misamaha ya kodi ambacho kitakuwa na jukumu la kufuatilia matumizi ya misamaha ya kodi na kuwasiliana na Mamlaka zingine zenye jukumu la kutoa misamaha ya kodi,<br>• Mamlaka ya Mapato ianzishe utaratibu wa kuzikagua (inspection and monitoring visits) mara kwa mara kampuni zilizopewa misamaha ya kodi kwa lengo la kuhakikisha kampuni hizo zinatekeleza matakwa ya Sheria na kuepusha hasara inayotokana na matumizi mabaya ya misamaha ya kodi. Aidha, TRA ihakikishe inaokoa kodi yenye thamani ya TZS 22,325,178,728 iliyopotea kutokana na kukosekana kwa udhibiti na usimamizi mzuri wa matumizi ya misamaha ya kodi kwa kuitaka kampuni ya Geita Goldmines kulipa fedha hiyo pamoja na adhabu kali, | • Mamlaka ya Mapato Tanzania imekuwa inalishughulikia suala hili na tayari imeshachukua hatua kadhaa. Ukaguzi ilifanyika kwenye baadhi ya makampuni ya madini na kubaimi kuwa baadhi ya makampuni haya ikiwemo Geita Gold | Natambua juhudi ambazo serikali imezichukua katika kushughulikia suala hili. Ufuatili |

| Na | Mapendekezo ya Kamati(PAC) | Majibu ya Serikali | Maoni ya ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | • Mamlaka ya Mapato iongeze udhibiti wa misamaha ya kodi inayotolewa kwa waagizaji wa magari ikiwa ni pamoja na kuhakikisha gari lililosamehewa kodi linasajiliwa kwa jina la muagizaji (Importer). Aidha, TRA ihakikishe kampuni ya Kiliwarrior Expeditions Ltd na Kampuni ya Kilemakyaro Mountain Lodge Limited zinarudisha haraka iwezekanavyo mapato yaliyopotea ya TZS 392,701,602 na TZS 53,399,565 sawia kutokana na udanganyifu uliofanyika katika uingizaji wa magari na Kampuni hizo zifutiwe mara moja msamaha wa kuingiza magari nchini,<br>• Menejimenti ya Mamlaka ya Mapato ihakikishe inafanya uchunguzi na makampuni yanayodaiwa kodi kutokana na kutumia vibaya misamaha ya kodi yarudishe fedha hiyo na Maafisa wa Mamlaka ya mapato walioshiriki katika udanganyifu huo wachukuliwe hatua za kinidhamu na za kisheria,<br>• Mamlaka ya Mapato ihakikishe maduka ya bidhaa zilizosamehewa kodi na makampuni yanayodaiwa kodi yarudishe fedha hiyo na Maafisa wa Mamlaka ya Mapato walioshiriki katika udanganyifu huo wachukuliwe hatua za kinidhamu na za kisheria,<br>• Mamlaka ya Mapato ihakikishe maduka ya bidhaa zilizosamehewa kodi na makampuni yenye misamaha ya kodi yanawasilisha hesabu zake zinazohusu misamaha ya kodi kabla ya kufunga biashara. Aidha, TRA ifanye uchunguzi kuhusiana na matumizi ya msamaha wa kodi uliotolewa kwa M/S Conti-Africa Ltd kabla na baada ya kufunga biashara yake na kuhakikisha mapato yaliyopotea ya TZS 3,824,547,526 yanarudishwa na kampuni hiyo,<br>• Mamlaka ya Mapato ihakikishe maombi yote ya misamaha ya kodi hayashughulikiwi mpaka ziwasilishwe nyaraka sahihi zinazohitajika kisheria,<br>• Menejimenti ya kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ianzishe mchakato wa kurekebisha Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 ili kuondoa | Mine yalitoa mafuta yaliyosamehewa kodi kwa wakandarasi. TRA ilikadiria kodi na kuidai kampuni ya Geita Gold Mine jumla ya TZS bilioni 5.1. Hata hivyo Geita Gold Mine ilikata rufaa kwenye Bodi ya Rufaa za Kodi (Kesi na 5 ya mwaka 2012), ambapo Bodi ilitoa amri ya kutokusanya kodi kutoka kwa makampuni ya madini tarehe 3/10/2012. Hatimaye, Bodi iliondoa zuio hilo tarehe 22 Julai 2014.<br>• TRA inaendelea na juhudi za | aji wa utekelezaji wa mapendekezo ya kamati unaendelea |

| Na | Mapendekezo ya Kamati(PAC) | Majibu ya Serikali | Maoni ya ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | misamaha ya kodi kwa ukarabati au upanuzi wa miradi ya makampuni yaliofaidika na misamaha hapoawali wakati wa uanzishaji wake . | kukusanya kodi kutoka kwa makampuni haya ambapo katika mwaka wa fedha 2012/2012 na 2012/2013 TRA tayari ilikuwa imeshakusanya TZS bilioni 16.7 kutoka kwenye mafuta kutoka makampuni ya geita Gold Mine na Resolute ambao waliwapa wakandarasi bila kodi. Wakandarasi hawa ni pamoja na Ausdiril, AECL, Capital drill, falcon, hilcon, Ako, CASCCO, Moolman, orica, Panaf, Mantra, SGS, Rhino, Caspian Construction, mansons Mines Log Ltd, CSL, Epson na Polisi. Mamlaka | |

| Na | Mapendekezo ya Kamati(PAC) | Majibu ya Serikali | Maoni ya ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | | inaendelea na utaratibu wa kufanya usuluhishi wa takwimu za matumizi ya mafuta yaliyochukuliwa na makampuni ya madini kila mwezi na kukusanya kodi husika,<br>• Katika mfumo wa usajili wa magari, TRA inaendelea na utaratibu wa kuwafungulia kesi za jinai wahusika wote waliohusika na uhalifu huu kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola,<br>• TRA imefanya uchunguzi katika kampuni ya Kilemakyaro Mountain Lodge Ltd ambayo ilipewa | |

| Na | Mapendekezo ya Kamati(PAC) | Majibu ya Serikali | Maoni ya ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | | msamaha wa kuagiza magari. Mamlaka ya mapato Tanzania inafanya usuluhishi wa takwimu (reconciliations) na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika wote,<br>• Serikali kupitia Sheria ya Uwekezaji Tanzania, sura 38, imekuwa inatoa misamaha ya kodi kwa wawekezaji kwenye sekta maalum ikiwa ni pamoja na ukarabati na upanuzi wa miradi yao. Dhamira ya Serikali katika vivutio hivi ni kukuza na kuendeleza uwekezaji hapa | |

| Na | Mapendekezo ya Kamati(PAC) | Majibu ya Serikali | Maoni ya ukaguzi |
| --- | --- | --- | --- |
| | | nchini, hata hivyo vivutio vya kodi katika upanuzi na ukarabati wa miradi imekuwa ikisababisha upotevu wa mapato kwa kiwango kikubwa. Katika Sheria ya Fedha ya mwaka 2014, sehemu ya kumi kifungu cha 48 Ibara "d", Serikali imeondoa msamaha huu,<br>• Serikali inatambua umuhimu wa kuzingatia taratibu katika utoaji misamaha ya kodi. Mamlaka ya Mapato imechukua hatua kadhaa za kuimarisha usimamizi wa utoaji misamaha na kuhakikisha kuwa | |

| Na | Mapendekezo ya Kamati(PAC) | Majibu ya Serikali | Maoni ya ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | | katika utoaji wa misamaha yoyote taratibu zote zinafuatwa kikamilifu kama kamati ilivyoelekeza. | |
| 8 | **Ujenzi wa jengo la kumbi za Watu Mashuhuri katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere-2006/2007-2011/12**<br>Serikali kupitia vyombo vyake vya dola ikiwemo TAKUKURU kufanya uchunguzi wa jinai kwa walioshiriki kuipotezea Serikali zaidi ya shilingi bilioni tisa na wahusika wachukuliwe hatua kisheria haraka iwezekanavyo | • Ujenzi wa jengo la kumbi za watu mashuhuri haukuwa miongoni mwa miradi iliyokuwa itekelezwe kwa mujibu wa kibali kilichotolewa na Baraza la Mawaziri. Chimbuko la ujenzi huo ni Makamu Mwenyekiti wa CSIL ambaye katika moja ya safari zake hapa nchini mwaka 2008, alipokewa katika chumba cha iliyokuwa "VIP Lounge" ndani ya jengo la pili la abiria. Mgeni huyo alionekana | Natambua hatua ambazo serikali imezichukua juu ya suala hili. Suala hili litafuatiliwa pindi serikali itakapotoa majibu. |

| Na | Mapendekezo ya Kamati(PAC) | Majibu ya Serikali | Maoni ya ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | | kutoridhika na hadhi ya chumba cha VIP,<br>• Kutokana na hali hiyo mwenyekiti huyo wa CSIL aliahidi kujenga Jengo jipya la VIP kama msaada kwa Serikali ya Tanzania kwa kuzingatia uhusiano na urafiki uliopo kati ya Tanzania na China. Hatua hiyo ilifuatiwa na Mfadhili kuanza kutoa msaada alioahidi na hatimaye kusaini mkataba mdogo (offer of Grant for VIP Lounge) kwaajili ya ujenzi wa jingo hilo. | |
| 9 | **Gharama za matumizi ya Wizara na Taasisi zake kutangaza hotuba za bajeti.**<br>Kuanzia mwaka ujao wa fedha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, atoe kipaumbele maalum cha ukaguzi kukagua matumizi husika na | | Utekelezaji wa pendekezo la |

| Na | Mapendekezo ya Kamati(PAC) | Majibu ya Serikali | Maoni ya ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | pia Maafisa masuhuli waagizwe kupunguza matumizi hayo yasiokuwa ya lazima kabla hatua kali hazijachukuliwa dhidi yao. | | Kamati yatafua tiliwa katika ukaguzi ujao. |

**Kiambatisho 8: Fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa kwa Wizara, idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa dhidi ya bajeti iliyoidhinishwa**

| FUNGU | WIZARA | Makisio yaliyoidhinishwa (TZS) | Fedha zilizotolewa (TZS) | (Pungufu)/Zaidi ya fedha zilizotolewa (TZS) | Fedha zilizotolewa ambazo hazikutumika (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|
| 31 | Ofisi ya Makamu wa Rais | 72,529,306,453 | 71,305,323,120 | (1,223,983,333) | 11,263,697 |
| 34 | Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa | 172,386,871,817 | 161,076,558,238 | (11,310,313,579) | 1,541,635,040 |
| 37 | Ofisi ya Waziri Mkuu | 38,497,902,944 | 23,684,600,760 | (14,813,302,184) | 38,614,665 |
| 41 | Mambo ya Sheria na Katiba | 12,592,760,040 | 7,483,135,461 | (5,109,624,579) | - |
| 43 | Kilimo, Chakula na Ushirika | 197,829,670,669 | 189,523,738,382 | (8,305,932,288) | 77,347,520 |
| 44 | Viwanda na Biashara | 34,092,172,463 | 30,071,044,252 | (4,021,128,211) | 5,660,868 |
| 46 | Elimu na Mafunzo ya Ufundi | 653,660,829,827 | 626,200,629,105 | (27,460,200,722) | 111,072,008 |
| 48 | Ardhi na Maendeleo | 39,376,932,263 | 38,967,452,873 | (409,479,390) | 993,036,126 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | ya Makazi | | | | |
| 49 | Maji na Umwagiliaji | 30,767,565,055 | 21,268,194,284 | (9,499,370,771) | 35,833,762 |
| 50 | Fedha | 65,028,837,914 | 57,406,750,659 | (7,622,087,255) | 303,166,589 |
| 51 | Mambo ya Ndani | 5,187,057,000 | 4,608,380,381 | (578,676,619) | 1,911,560 |
| 52 | Afya na Ustawi wa Jamii | 300,978,622,933 | 282,439,413,575 | (18,539,209,358) | 48,342,489 |
| 53 | Maendeleo ya Jamii, Jinsia & Watoto | 15,833,711,000 | 12,274,243,700 | (3,559,467,300) | 122,186,977 |
| 56 | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | 211,673,600,337 | 207,910,685,233 | (3,762,915,104) | - |
| 57 | Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa | 19,310,495,000 | 15,915,793,393 | (3,394,701,607) | - |
| 58 | Nishati na Madini | 112,429,504,160 | 84,722,741,029 | (27,706,763,131) | 85,066,884 |
| 62 | Usafirishaji | 112,167,086,823 | 88,860,378,605 | (23,306,708,218) | 17,945,039 |
| 65 | Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana | 13,349,129,586 | 9,910,426,005 | (3,438,703,581) | 1,079,298 |
| 68 | Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia | 32,244,928,547 | 29,143,653,462 | (3,101,275,085) | 221,434 |

